*NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA SABA

## Kikao cha Ishirini na Sita – Tarehe 16 Mei, 2017

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Mwenyekiti (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Tukae, Katibu.

**NDG. THEONEST RUHILABAKE – KATIBU MEZANI:**

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:**

Randama ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

**MHE. KIBERA J. KISHIMBA (K.n.y. MHE. ADADI M. RAJAB - MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA):**

Taarifa ya Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM (K.n.y. MHE. JUMA HAMAD OMAR - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KUHUSU WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA):**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Katibu.

**NDG. THEONEST RUHILABAKE – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na Ofisi ya Rais (TAMISEMI) na swali linaulizwa na Mheshimiwa Dkt. Pudenciana Wilfred Kikwembe.

Na. 209

### Dhana ya Ugatuaji Madaraka kwa Wananchi

**MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE** aliuliza:-

Serikali imekuwa na dhana ya ugatuaji madaraka kwa wananchi ili kuharakisha maendeleo, hususan katika sekta za afya na elimu:-

Je, Serikali inasema nini kuhusu mfumo huo kutokuwa na tija endelevu katika sekta hizo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI), naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Pudenciana Wilfred Kikwembe, Mbunge wa Kavuu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dhana ya Ugatuaji wa Madaraka kwa Wananchi *(Decentralisation by Devolution)* inatokana na Ibara ya 145 na Ibara 146 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. Madhumuni ya kupeleka madaraka kwa umma yakiwemo madaraka ya kisiasa, kifedha na kiutawala ni kusogeza madaraka ya kufanya maamuzi kwa wananchi ili kuboresha, kuimarisha utoaji wa huduma kulingana na matakwa yao ya kuboresha maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeweza kupata mafanikio katika sekta ya afya na elimu kwa kuwashirikisha wananchi katika kutekeleza Mipango ya Maendeleo ya Elimu ya Msingi na Sekondari (MMEM na MMES) na Mpango wa Maendeleo wa Afya ya Msingi (MMAM). Kupitia utekelezaji wa hiyo fursa ya elimu ya msingi na sekondari zimeweza kuongezeka kutokana na ujenzi wa miundombinu ya elimu na kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia. Vilevile huduma za afya zimeimarishwa kwa kuratibiwa kwa karibu na Mamlaka ya Serikali za Mitaa kuanzia ngazi ya zahanati, vituo vya afya pamoja na hospitali ya wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo wa ugatuaji wa madaraka kwa wananchi bado ni dhana muhimu kwa nchi yetu kwani ndio mfumo unaotoa fursa kwa wananchi kuweza kushiriki katika maamuzi na utekelezaji wa vipaumbele vyao katika mchakato mzima wa maendeleo yao na Taifa kwa ujumla.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Kikwembe.

**MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kunipatia nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza. Kwanza kabisa, napenda nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, suala hili ni la kikatiba kwa maana ya kwamba linahusisha Serikali ya wananchi kwa maana ya Serikali za Vijiji. Kwa kuwa wananchi wamekuwa wakichangia takribani 20% ya maendeleo katika maeneo yao ya vijiji. Je, Serikali sasa inafikiria nini kupeleka pesa za maendeleo kwa wakati ili wananchi hawa waweze kujua sasa ile miradi ni mali yao? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli dhana hii inapeleka fursa kwa wananchi na ni kweli tumeshuhudia wananchi katika maeneo mbalimbali wakishiriki vyema katika kutekeleza dhana hii kwa kujitolea katika miradi mbalimbali ya maendeleo. Hata hivyo, naomba nilihakikishie Bunge lako Tukufu kwamba Serikali kwa kipindi cha sasa na nina maana itakapofika mwezi wa Sita mtaona jinsi gani imepeleka nguvu kubwa sana katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano katika sekta ya afya mwaka huu peke yake fedha tulizopeleka katika mifuko mbalimbali ikiwepo *Basket Fund* ni zaidi ya shilingi bilioni 79 na sasa hivi tumeshapeleka fedha za *quarter* ya nne ambapo tunaenda kukamilisha shilingi bilioni 106, hii ni sekta ya afya peke yake. Tumefanya hivyo pia katika sekta ya elimu na maeneo mbalimbali na juzi juzi hapa tumenunua vifaa vya maabara katika maabara zote zaidi ya 1,000 ambapo vyote vilikuwa vinagharimu shilingi bilioni 16.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kuna fedha nyingine za *LDGD* ambazo zimeenda moja kwa moja ambazo hazina ukakasi katika kuzitoa kwake. Serikali

imepeleka hela za kutosha na ni mara ya kwanza baada ya miaka minne iliyopita tulikuwa hatufanyi hivyo. Kwa hiyo, Serikali itaendelea kuweka nguvu kubwa ya kutosha, lengo kubwa ikiwa ni kuwawezesha wananchi kutekeleza miradi yao.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Gekul na Mheshimiwa Chumi.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Mpango wa Afya ya Msingi (MMAM) muda wake ilikuwa uishe mwaka huu 2017 lakini fedha hizo haziji kwa muda mrefu, takribani kama miaka mitatu nyuma fedha haziji. Ni kwa nini mpango huu wa MMAM ambao ulikuwa unasaidia kujenga zahanati zetu umekwama na anawaambiaje Watanzania kwa sababu maboma/zahanati nyingi bado hazikajamilishwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema hapa sio suala la maboma ya afya peke yake hata maboma ya nyumba za Walimu halikadhalika madarasa. Kipindi fulani hapa takribani miaka mitatu, minne fedha hizi zilikuwa haziendi. Ndiyo maana nimesema kupitia Mfuko ule wa *LDGD* ambapo kwa sasa mwaka huu kwa mara ya kwanza, namshukuru Mheshimiwa Waziri wangu alilisimamia kwa karibu sana, ndiyo maana hivi sasa Wabunge kama tumepitia katika Kamati zetu za Fedha katika Halmashauri zetu tunaona kuna fedha nyingi zimekuja ambazo zimesaidia kwa kiwango kimoja au kingine kuweza kuhakikisha maboma mengi sana yameweza kujengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeshuhudia hili kwani nilipopita maeneo mbalimbali nilikuwa nikipata taarifa mbalimbali kutoka kwa Wakurugenzi jinsi gani fedha hizi sasa

wameweza kuzielekeza katika kuhakikisha zile nguvu za wananchi ambazo wamezitoa hazipotei kwa kukamilisha viporo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, naomba tushirikiane kwa pamoja. Lengo kubwa ni kutekeleza mpango wa *D-by-D* kama alivyosema Mheshimiwa Dkt. Kikwembe, tufanye hili kwa ajili ya mustakabali mzuri kwa kuunganisha nguvu za wananchi katika kuhakikisha Taifa hili linaenda mbele.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waziri wa Afya.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nataka tu kumfahamisha Mheshimiwa Gekul kwamba tayari tumeshaanza kuufanyia mapitio Mpango wa Afya ya Msingi (MMAM). Kwa hiyo, tunategemea kabla ya mwisho wa mwaka tutakuwa tumetoa mpango wa pili ambao utatueleza kama, je, ni lazima tuwe na zahanati kila kijiji wakati sasa hivi barabara zinapitika? Je, ni lazima tuwe na kituo cha afya kila kata? Kwa hiyo, hayo maeneo yote tutayaangalia kwa upana wake. Lengo letu ni kuhakikisha tunasogeza huduma bora kwa wananchi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Chumi.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kuniona. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri na jitihada za Serikali kupeleka fedha za maendeleo, ugatuaji lazima uende sambamba na upelekaji wa *resources* hususan fedha za *OC.* Fedha za *OC* zimekuwa haziendi kwa kiwango kinachokusudiwa matokeo yake imekuwa inaathiri mipango inayopangwa na Halmashauri kwa kutekelezwa kutokana na makusanyo ya ndani. Matokeo yake fedha za makusanyo ya ndani sasa zinatumika kuendeshea ofisi badala ya kuelekezwa kwenye

shughuli za maendeleo kama inavyoelekeza ile 50%, ikiwepo 5% ya vijana na wanawake. Je, Serikali imejipangaje kuhakikisha kwamba inapeleka fedha za *OC* ipasavyo ili kusudi makusanyo ya ndani yasiathiri utekelezaji wa shughuli za maendeleo, kama ambavyo zimepangwa na Halmashauri zetu? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli na nakumbuka kwamba tulipokuwa katika kikao chetu cha *ALAT* kule Musoma, *concern* kubwa ilikuwa siyo fedha za *OC* peke yake hata pesa za maendeleo. Waheshimiwa Wenyeviti wa Halmashauri na Wakurugenzi wali-*raise* jambo hili katika ofisi yetu na ndiyo maana katika kipindi cha katikati baada ya harakati hizi kufanyika mmeona tumepeleka fedha nyingi sana za maendeleo na pesa za *OC.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kama ambavyo Mheshimiwa Waziri wangu siku zote amekuwa akisema *definition* ya *OC* maana yake ni *Own Source plus* zile fedha nyingine zinazotoka Serikali Kuu. Kwa hiyo, sisi Serikali tutajitahidi kwa kadiri iwezekanavyo *OC* iweze kwenda, lakini niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge katika maeneo yetu vilevile tuhakikishe makusanyo ya ndani haya yanaimarika kwa kiwango kikubwa kwa sababu tumeshuhudia hivi sasa kuna Halmashauri zingine zimefanya vizuri lakini nyingine zinasuasua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hili ni jambo letu sisi sote. Upande wa Serikali tutajitahidi kufanya kila liwezekanalo kuziwezesha Halmashauri zetu ziweze kufanya kazi vizuri kwa sababu bila ya hivyo maana yake utekelezaji wa Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi utakuwa una matatizo. Kwa hiyo, naomba niwahakikishie kwamba Serikali itafanya kila liwezekanalo, tutakusanya mapato lakini tutayapeleka katika Halmashauri zetu ili miradi iweze kutekelezeka vizuri.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali la Wizara hiyo hiyo la Mheshimiwa Nditiye.

Na. 210

**Hitaji la Mganga wa Meno – Hospitali ya Wilaya ya Kibondo**

**MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE** aliuliza:-

Kwa muda wa zaidi ya miaka miwili, Hospitali ya Wilaya ya Kibondo haina mganga wa meno licha ya hospitali hiyo kuhudumia wagonjwa wengi kwa sasa ikiwemo wakimbizi kutoka nchini jirani ya Burundi:-

Je, ni lini Serikali itapeleka mtaalam wa meno katika hospitali hiyo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI), naomba kujibu swali la Mheshimiwa Injinia Atashasta Justus Nditiye, Mbunge wa Muhambwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekwishapeleka mtaalam wa meno (Daktari Msaidizi wa Meno) tangu tarehe 12/4/2016. Kwa sasa yupo katika Hospitali ya Wilaya ya Kibondo na anaendelea kutoa huduma kwa wagonjwa.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Nditiye.

**MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, nina maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwa kuwa Hospitali ya Wilaya ya Kibondo ndiyo hospitali vilevile inayotumika kama Hospitali ya Rufaa kwa Wilaya ya Kakonko, lakini inatumika kama Hospitali ya Rufaa kwa wakazi kutoka nchini Burundi, kwa maana ya wakimbizi wapatao laki mbili. Serikali

ina mpango gani wa kuongeza majengo kwenye hospitali hiyo ambayo hayajawahi kuongezwa kutoka mwaka 1971?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Kwa sababu hiyo hiyo Serikali ina mpango gani wa kuongeza mgawo wa dawa ili kuweza kukidhi mahitaji ya wananchi wa Wilaya ya Kibondo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli hospitali ya Mheshimiwa Mbunge ya kama Kibondo, ni kweli na mimi nilifika tulienda kukagua hospitali ile, kuna changamoto ya miundombinu pale na hata wenzetu wa Kakonko kwa mwalimu wangu pale, mara nyingi sana wanatumia kama ndio *referral hospital* yao katika eneo lile, changamoto hizo tumeziona. Siku ile nilivyokuwa pale *site* niliwaambia waangalie upungufu uliokuwepo *(needs assessment)* maana hata vifaa tiba na *X-Ray* lilikuwa ni changamoto na nilitoa maelekezo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, imani yangu ni kwamba wenzetu pale Halmashauri watafanya hiyo *needs assessment* ambapo mchakato utaanza katika vikao vya Halmashauri, tutaangalia nini kwa pamoja kitafanyika kwa ajili ya kuboresha hospitali ile kwa sababu idadi ya wagonjwa niliyoikuta pale ni kubwa sana na ni kweli anachosema Mheshimiwa Mbunge. Kwa hiyo, Serikali inasubiri jinsi gani michakato itawekwa katika kipaumbele cha Halmashauri yenyewe na sisi tutaweka nguvu kwa kadri iwezekanavyo ili hospitali ile iweze kutoa huduma vizuri.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Genzabuke.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mkoa wa Kigoma kwa muda mrefu umekuwa haupati watumishi kwa sababu upo pembezoni lakini pia wakimbizi wameingia kwa wingi katika Mkoa wa Kigoma pamoja na kwamba wana hospitali zao kwenye makambi lakini kutokana na binadamu wasivyoweza kuzuiliwa wanaingia kwa wingi katika miji yetu hali inayosababisha wagonjwa kuwa wengi kwenye hospitali zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Ummy alipofanya ziara Mkoa wa Kigoma...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa uliza swali.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Ummy alipofanya ziara Mkoa wa Kigoma alikumbana na tatizo la ukosefu wa waganga katika hospitali zetu. Ni lini sasa Mkoa wa Kigoma utapewa kipaumbele cha kupatiwa waganga wa kutosha? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kulikuwa na suala la *concern* ya dawa katika Hospitali ya Kibondo ambalo mwanzo nilili-*skip.* Hata nilivyofika pale *site* Kibondo nilitoa maelekezo kuhusu matumizi mazuri ya *Basket Fund.* Maeneo yote nilikopita nimekuta kwamba japokuwa tumepeleka fedha za kutosha kwenye *Basket Fund,* lakini Waganga wetu wa Wilaya wameshindwa kuhakikisha zile fedha zinatumika kwa ajili ya kuwasaidia wananchi wetu. Ndiyo maana nimetoa maelekezo kwamba itakapofika mwezi wa Sita, Halmashauri yoyote ambayo Serikali imepeleka fedha lakini zile fedha zimeshindwa kununua dawa na vifaa tiba kuwasaidia wananchi, tutasema kwamba, ma-*DMO* wao hawatoshi katika maeneo yetu hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini suala la watumishi, japokuwa tatizo la watumishi ni tatizo kubwa sana, lakini ukiangalia katika mgawanyo wa Madaktari, Kigoma

tumepeleka madaktari 10 lakini mikoa mingine imepata madaktari watano. Tunajua japokuwa Madaktari kumi wameenda katika Mkoa mzima wa Kigoma, bado hawatoshi, lakini tutakapokuja katika ajira mpya Mkoa wa Kigoma tutaupa kipaumbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba muelewe ndugu zangu, Kibondo pale kwa ndugu yangu Mheshimiwa Nditiye tumepeleka Madaktari watatu, Kasulu tumepeleka Madaktari wawili, halikadhalika Uvinza tumepeleka Madaktari na *RAS* Kigoma tumepeleka takribani Madaktari wanne. Lengo letu ni kuhakikisha Mkoa wa Kigoma na mikoa mingine ya pembeni iweze kupata...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa jibu kwa kifupi tu sababu swali lake la nyongeza yeye kadandia, mjibu kwa kifupi tu. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tutawapa kipaumbele watu wa Kigoma kupata Madaktari wa kutosha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Almas na Mheshimiwa Paresso.

**MHE. ALMASI A. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru sana kuniruhusu kuuliza swali. Kituo cha Afya cha Upuge ndiyo peke yake Hospitali ya Wilaya Jimboni kwangu, hakuna hospitali kabisa isipokuwa Kituo kile cha Upuge na hakina wataalam wa dawa za usingizi, wanaitwa *anesthesia* kitaaluma, kwa hiyo, hatuwezi kufanya operesheni. Je, Serikali inafikiria nini kupeleka mtaalam wa dawa za usingizi ili operesheni zifanyike? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa kifupi, watu ni wengi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kituo cha Afya cha mtani wangu pale, katika idadi ya wataalam

ambao tutawaajiri hapa katikati kutokana na nafasi nyingi zilizotolewa na Mheshimiwa Rais tutaangalia mahitaji halisi ya kituo hiki *then* tutawapa kipaumbele ili mradi wampate mtaalam huyo wa usingizi.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Paresso.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Kumekuwa na tishio kubwa la ugonjwa wa sukari hapa nchini ambao umekuwa ukiwakumba watu wa rika mbalimbali na hatuna wataalam wa kutosha katika hospitali zetu. Vilevile hata dawa wanazopewa ikifikia hatua mgongwa wa sukari anatakiwa apate *insulin* dawa hizo zimekuwa zikiuzwa ghali, watu hawawezi ku-*afford.* Je, Serikali inatoa kauli gani kuhusiana na tatizo hili?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Afya najua ukijibu utapata tabu bora ukae waseme hawa halafu ndiyo ujibu, mimi *style* yangu ni tofauti kidogo. Mheshimiwa Mwijage, maana utakuwa unasimama kila saa hapa.

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa kuwa matatizo ya Kibondo ya Madaktari wa meno ni sawasawa na matatizo ya Wilaya ya Bukoba Vijijini ya Izimbya - Katekana hawana Daktari wa meno hata mmoja wakipata tatizo la ugonjwa mpaka waende Bukoba Mjini na ni mbali sana kutoka pale kwenda Bukoba Mjini. Ni lini Serikali itaona umuhimu wa kuwaletea Madaktari wa meno wa kuwasaidia hao watu wa Bukoba Vijijini?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Sasa Mheshimiwa Waziri wa Afya, yajibu yote.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Cecilia Paresso kuhusu upatikanaji wa dawa za kisukari na ongezeko la wagonjwa wa kisukari nchini. Ni kweli sasa hivi tunashuhudia ongezeko la wagonjwa wa kisukari lakini kwa sababu kwanza ya

mfumo wa maisha ambao watu wanaishi, watu hawafanyi mazoezi, wanakula vyakula bila kuzingatia lishe lakini bila ku-*check* afya zao mara kwa mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kubwa badala ya kujikita kwenye kutibu tumejikita kwenye kuzuia Watanzania wengi wasipate maradhi ya ugonjwa wa kisukari. Pale ambapo Mtanzania ana ugonjwa wa kisukari kwa mujibu wa Sera ya Afya dawa ya mgonjwa wa kisukari inatakiwa kupatikana kwa bei nafuu. Kwa hiyo, tunawaelekeza Waganga Wakuu wa Mikoa na Wilaya wanapoandaa maoteo ya dawa basi wahakikishe pia wana-*orde*r dawa za kutosha kwa ajili ya wagonjwa wa kisukari. Kama hawawezi ku-*order* za kutosha sisi hatuwezi kuwapelekea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili la uhaba wa Madaktari wa Meno, kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri na hata wakati wa bajeti ya Mheshimiwa Waziri wa Utumishi alitoa maelezo kwamba Mheshimiwa Rais ameridhia kuajiri watumishi wa Serikali takriban 52,000 na kati ya hao tunategemea kupata watumishi wa sekta ya afya. Kwa hiyo, Mheshimiwa Savelina Mwijage tutakapopata kibali tutawapanga pia kwa ajili ya hospitali za Mkoa za Kagera. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Daniel Edward Mtuka.

Na. 211

## Ujenzi wa Kituo cha Ukaguzi wa Mizigo Muhulala Manyoni

**MHE. DANIEL E. MTUKA** aliuliza:-

Eneo la Muhalala katika Wilaya ya Manyoni ni moja ya maeneo matatu yaliyoteuliwa na Serikali kujenga vituo vya ukaguzi wa mizigo katika barabara ya kati; maeneo mengine ni Vigwaza Pwani na maeneo mawili yameshajengwa kimebaki kituo cha Muhalala tu:-

(a) Je, ni lini wananchi ambao maeneo yao yametwaliwa tangu mwaka 2012 watalipwa fidia?

(b) Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa Kituo cha Ukaguzi wa Mizigo Muhalala baada ya kituo cha Vigwaza kukamilika?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Daniel Mtuka, Mbunge wa Manyoni Mashariki, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Serikali imeamua kujenga vituo vya pamoja vya ukaguzi wa mizigo inayokwenda nje ya nchi katika barabara ya Ukanda wa Kati na Ukanda wa Dar es Salaam. Katika Ukanda wa Kati vituo vitajengwa Muhalala, Mkoani Singida na Nyakanazi Mkoani Kagera chini ya ufadhili wa Umoja wa Ulaya. Aidha, katika Ukanda wa Dar-es Salaam, vituo vitajengwa Vigwaza, Mkoani Pwani, Ruaha-Mbuyuni, Mkoani Morogoro, Makambako, Mkoani Njombe na Iboya - Mpemba Mkoani Mbeya chini ya ufadhili wa Benki ya Dunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2016/2017, Serikali ilitenga fedha kiasi cha shilingi bilioni 5.86 kwa ajili ya malipo ya fidia kwa watu watakaoathirika na ujenzi wa vituo hivyo. Tathmini ya maeneo ya watu walioathirika na ujenzi huo katika Ukanda wa Kati yaani (Muhalala - Manyoni na Nyakanazi - Kagera) imefanyika na malipo kwa waadhirika wa ujenzi wa vituo hivyo yamefanyika na kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, mkataba wa ujenzi wa vituo vilivyopo Ukanda wa Kati ulisainiwa tarehe 16 Disemba, 2016 kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na mkandarasi M/s *IMPRESA DI CONSTRUZIONI ING E. MANTOVANI* wa Italia. Mpaka sasa mkandarasi yupo

katika eneo la kazi na yupo katika hatua za awali za ujenzi wa vituo hivyo. Mradi huu unatarajiwa kukamilika Septemba, 2018.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mtuka.

**MHE. DANIEL E. MTUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri. Niipongeze pia Serikali ni kweli majuzi tumepokea ugeni na shughuli hiyo imeanza mara moja. Hiyo ndiyo Serikali ya Awamu ya Tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, kuna nyumba zinatakiwa kubomolewa maeneo ya Kintinku, Chikuyu, Maweni barabara kuu zimewekewa alama ya kijani tangu 2013 na kijani maana yake ni kwamba kuna malipo ya fidia, lakini hawajalipwa fidia, Serikali inasema nini? Ni lini wananchi hawa watalipwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**MHE. DANIEL E. MTUKA:** Samahani Mwenyekiti, swali la pili.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri subiri tumpe fursa.

**MHE. DANIEL E. MTUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu 2013 tuliomba barabara inayoanzia Chikuyu – Chibumagwa - Mpandagani - Ikasi ambayo ina urefu wa kilomita 84 ipandishwe daraja lakini tangu kipindi hicho naona ni kimya Serikali haijaleta majibu. Hata hivyo, tarehe 17/3/2015 wataalam kutoka Wizara husika walikuja kukagua barabara hii. Tulitegemea majibu yatoke lakini mpaka sasa hivi ni kimya. Ni lini sasa Serikali itapandisha hadhi barabara hii?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ya Kintinku - Chikuyu na Maweni ambayo yapo katika barabara kuu yamewekewa alama ya 'X' ya kijani kama ambavyo tumeweka alama za 'X' za kijani na nyekundu katika barabara nyingi sana humu Tanzania tokea Sheria ile ya 2007 ilipopitishwa na Kanuni ya 2013 ilipopitishwa. Maana ya zile 'X' ni kwamba tunakujulisha eneo hilo liko ndani ya hifadhi ya barabara kwa mujibu wa Sheria mpya ya mwaka 2007 lakini eneo lako liko kati ya mita 22.5 ambayo ni hifadhi ya barabara kwa sheria ya zamani na mita 30 kwa sheria ya sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu upanuzi huu umefanyika wakati wewe tayari ulishajenga unastahili kulipwa fidia lakini unachotakiwa kufanya ni kuhakikisha kwamba huongezi maendeleo yoyote katika eneo hilo, hiyo ndiyo maana yake. Sasa fidia inakuja wakati eneo hilo linapohitajika. Eneo hilo linapohitajika kupanua barabara tunawalipa fidia kabla hatujaanza kazi ya upanuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kama ambavyo yeye alisimama na mimi nikasimama, barabara inayoanzia Chikuyu - Chibumagwa na kuendelea ombi la kwamba ipandishwe hadhi nimwombe tu avute subira majibu yatolewa. Tuna maombi mengi tu yamekuja na mara yatakapokamilika tutatoa taarifa barabara zipi zimepandishwa hadhi na zipi hazikupandishwa hadhi kutokana na vigezo ambavyo tumejiwekea wenyewe kwa mujibu wa sheria.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mpakate.

**MHE. MPAKATE D. IDDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba niulize swali la nyongeza, kama ifuatavyo. Tatizo la Manyoni linafanana kabisa na mazingira ya tatizo la barabara ya Mtwaro - Pachani - Lusewa - Mchoteka - Nalasi - Mbesa - Tunduru Mjini ambayo iliwekewa alama za 'X' zaidi ya miaka saba iliyopita. Je, ni lini ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami utaanza?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naona Mheshimiwa Mbunge ameanza kutaja maeneo ambayo yako katika Jimbo langu katika kuongeza umuhimu wa swali lake. Naomba tu niseme masuala ya fidia ni ya Kitaifa na wakati ambapo tutaanza kujenga na sasa hivi siwezi kusema tunaanza lini kwa sababu fedha zilizotengwa kwa sasa ni za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa sababu kazi hiyo bado haijakamilika. Naomba kwanza tuikamilishe kazi upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kabla hatujaanza kutafuta fedha za kujenga hiyo barabara.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Mussa Bakari Mbarouk.

Na. 212

**Ukarabati wa Bandari ya Tanga**

**MHE. MUSSA B. MBAROUK** aliuliza:-

Bandari ya Tanga siku hadi siku inafanya kazi chini ya kiwango:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza kina, kuipanua na kuifanya bandari ya kisasa ili kuvutia wafanyabiashara kushusha mizigo yao na wasikimbilie Mombasa Kenya?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mussa Bakari Mbarouk, Mbunge wa Tanga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuvutia wafanyabiashara kushusha mizigo yao na kutokukimbilia bandari ya nchi jirani, Serikali kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania *(TPA)* ina mpango wa muda mfupi na wa kati wa kuboresha bandari ya Tanga kwa kutekeleza mradi wa kuimarisha gati namba mbili (2).

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa kuboresha Bandari ya Tanga ulianza Februari, 2016 na unatarajiwa kukamilika Juni, 2017. Mradi huu unatekelezwa na Kampuni ya Ukandarasi ya *COMARCO* kutoka Kenya. Maboresho ya bandari yanayofanyika katika mradi huu ni pamoja na kuongeza kina cha gati kwa kuchimba (*dredging*) kiasi cha mita 1 na kufanya kina cha gati kufikia mita 4.5; kuimarisha gati na kuweka mfumo wa kuzuia kutu katika nguzo (*cathodic protection).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu ukikamilika utasaidia kuongeza uwezo wa bandari kuhudumia meli zenye wastani wa ukubwa wa tani 1,200 kuingia bandarini. Aidha, Serikali kupitia *TPA* ina mpango wa muda mrefu wa kujenga bandari katika eneo la Mwambani ambayo ina kina kirefu na uwezo wa kuhudumia meli kubwa. *TPA* tayari inamiliki ardhi yenye ukubwa wa hekta 92 katika eneo la Mwambani.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mbarouk.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na bandari iliyokuwepo Serikali ilipata uwezekezaji wa ujenzi wa bandari mpya ya Mwambani na kama sikosei ilikuwa ni Serikali ya Uganda na Serikali ya Kuwait. Swali la kwanza, kwa kuwa *feasibility study* pia ilikwishafanyika, je, ujenzi huu wa bandari mpya wa Mwambani nao umefikia hatua gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, zipo *systems* za *FIFO na LIFO method, First In First Out* na *Last In First Out,* kwa nini naambiwa kwamba itaanza kujengwa bandari ya Bagamoyo katika siku za karibuni isianze kujengwa ile bandari ya Tanga? Nataka kujua hilo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu, anataka kujua kwa nini tu, sasa usimzungushezungushe.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bandari ya Mwambani kama ilivyo bandari ya Bagamoyo tulikuwa tunatarajia ijengwe kwa njia ya *PPP.* Unapokwenda kwenye masuala ya *PPP* inategemea na yule aliyeonesha nia ya kujenga. Wapo watu wameonesha nia Bagamoyo na Tanga pia lakini tatizo lililotokea kwa Mwambani ni kwamba upembuzi yakinifu na usanifu wa kina uliofanyika ulionesha kwamba bandari ile haina faida. Sababu yake hawakufikiria mizigo ambayo italetwa na reli inatokea Musoma hadi Tanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sasa tumeanza kazi upya ya kuipitia hiyo taarifa ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ili waunganishe na uwekezaji mpya uliojitokeza pale Tanga ili hatimaye bandari ile ya Mwambani ionekane ina faida kuijenga. Kwa hiyo, ni kweli kuna huo utaratibu wa *FIFO* na kadhalika lakini hatimaye kwa sababu unatumia *PPP* ni lazima ufuate wale wateja wako wanaotaka kuwekeza pale unaendana nao vipi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa swali la pili, nalo nadhani nimelijibu wakati najibu hili kwa kirefu kwa sababu hoja ni ileile. Nakushuruku sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Saumu na Mheshimiwa Kakoso.

**MH. SAUMU H. SAKALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Pangani kama zilivyo wilaya nyingine zilizoko pembezoni mwa bahari ina bandari bubu nyingi. Bandari hizi zinatumika kuingiza mizigo ambayo ni halali na ambayo pia siyo halali kama vile madawa ya kulevya, wahamiaji haramu hata na bangi kitu ambacho kinasababisha bandari hizi zinakuwa ni chanzo

kikubwa cha rushwa. Je, Serikali haioni umuhimu wa kuzitambua bandari hizi ili zile zenye vigezo ziweze kurasimishwa na kutambulika rasmi ikiwa ni pamoja na kuzikarabati na zile ambazo hazifai zifungwe kwa maslahi ya Taifa na watu Pangani? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, anayoyasema ni sahihi na nadhani anafahamu kwamba ndicho tunachotekeleza ndani ya Serikali kwa sababu tuna timu ya Wakuu wa Mikoa yote iliyoko kwenye mwambao na upande wa Zanzibar wanakutana kila wakati kuhakikisha wanapitia zile bandari bubu kuona zipi zinaweza zikaendelezwa na kurasimishwa na zipi ambazo zinatakiwa kufungwa inasimamiwa kufungwa. Nadhani ni kitu ambacho anafahamu tunakitekeleza na nimushukuru sana kwa sababu kwa kuuuliza hivyo maana yake anaunga mkono hatua tunayoichukua.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Kakoso.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru kunipa nafasi ya kuuliza swali ndogo la nyongeza. Serikali iliazimia kufanya marekebisho ya kuziboresha bandari za Maziwa Makuu kwa maana ya Ziwa Victoria, Nyasa na Lake Tanganyika. Serikali iliazimia kujenga bandari ya Kalema ili iweze kuunganisha na nchi jirani ya *DRC.* Ni lini bandari ya Kalema itakamilika kama Serikali ilivyokuwa imetoa hoja ya kujenga bandari hiyo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Kakos, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu, kwa namna anavyofuatilia maendeleo ya bandari za Mwambao wa Ziwa Tanganyika. Amekuwa mstari wa mbele sana katika kulihangaikia hilo

na sisi tunamuunga mkono katika hilo, tutahakikisha dhamira yake ya kuwatumikia watu wa Mwambao wa Ziwa Tanganyika inatimia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie tu kwamba kazi inayofanyika sasa ni kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa reli na bandari, reli kutoka Kaliua mpaka Kalema pamoja na bandari yake ili hatimaye tujenge reli na bandari tuweze kuhudumia mizigo mingi kutoka Kalemie upande wenzetu wa *DRC* Kongo. Nimwombe akubali kwamba yale ambayo tunakubaliana katika Kamati ndiyo Serikali itakayoyatekeleza. Ahsanteni sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na swali na Mheshimiwa Dkt. Ndugulile, kwa niaba yake Mheshimiwa Dkt. Chegeni.

Na. 213

**Mtambo wa Kudhibiti Takwimu za Mawasiliano ya Simu**

**MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI (K.n.y. MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE)** aliuza:-

Katika Kamati ya Bunge la Kumi Serikali iliahidi kufunga mtambo kwa lengo la kudhibiti takwimu za simu za nje na ndani ili kudhibiti mapato ya Serikali:-

(a) Je, utekelezaji wa suala hilo umefikia wapi?

(b) Je, ni kiasi gani Serikali imekusanya tangu utaratibu huo uanze na kabla yake mapato yalikuwaje?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la

Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile, Mbunge wa Kigamboni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania iliweza kusimika mtambo wa kuhakiki na kusimamia huduma za mawasiliano yaani *TTMS* hapa nchini mwishoni mwa mwaka 2013. Mtambo huu umeisaidia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (*TCRA)* kuongeza ufanisi katika kusimamia sekta ya mawasiliano pamoja na kwenda sambamba na kasi ya mabadiliko yanayotokea katika sekta ya mawasiliano duniani kote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa mtambo wa *TTMS* umeiwezesha *TCRA* kuwa na uwezo wa kusimamia mawasiliano ya simu za kimataifa na zile za mwingiliano; kudhibiti mawasiliano ya simu za ulaghai za kimataifa; kusimamia ubora wa mitandao katika kutoa huduma bora kwa wananchi; kudhibiti namba tambulishi za vifaa vya mawasiliano nchini pamoja na usimamiaji wa miamala ya fedha inayopita katika mitandao ya simu hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio hayo, jitihada za kuboresha zaidi mfumo huu ili kuweza kubaini na kujiridhisha juu ya mapato yote yaani *revenue assurance* yatokanayo na huduma za mawasiliano kwa maana ya simu za sauti, *data* na *SMS* yanakidhi mahitaji ya Mamlaka ya Mapato Tanzania *TRA*, Benki Kuu ya Tanzania *(BOT)* na *TCRA* yanaendelea. Kwa vile vifungu vya mkataba wa *TTMS* vinamtaka mkandarasi kuweka mfumo wa kubaini na kujiridhisha juu ya mapato yote *(Revenue Assurance System),* Serikali kupitia *TCRA* imemwagiza mkandarasi aweke mfumo huo bila gharama za ziada kwa Serikali. Mkandarasi hatimaye amekubali kuweka mfumo wa *Telecom Revenue Assurance* ambapo unategemewa kukamilika mwishoni mwa mwezi Agosti, 2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuanzia Oktoba, 2013 hadi Februari, 2017 kiasi cha sh.63,015,450,230.40 zilipatikana na katika hizo sh.56,987,368,631.08 zimewasilishwa Hazina na sh.6,028,081,599.41 zimewasilishwa Tume ya Sayansi na

Teknolojia *(COSTECH)* kwa ajili ya kugharamia tafiti mbalimbali zenye manufaa kwa nchi yetu. Kabla ya mfumo huu, mapato haya hayakuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kuwajengea uwezo wataalam wa *TCRA* ili waweze kuendana na kasi ya ukuaji wa teknolojia ya habari na mawasiliano hususan katika eneo hili la kuchakata taarifa mbalimbali za huduma za mawasiliano zinazopatikana kutoka kwa watoa huduma ili kuweza kubaini na kujiridhisha juu ya mapato yote.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Chegeni.

**MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, nina swali moja dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa baadhi ya makampuni haya kwa muda mrefu sana yamekuwa yakifanya udanganyifu na hasa katika miamala ya simu pamoja na muda wa maongezi kwa wateja na kwa kuwa Serikali tayari imeshaanza kudhibiti suala hili. Je, Serikali haioni kwamba ni busara na ni vyema kuendelea kudhibiti makampuni yote haya ya simu yaweze kulipa kipato sahihi na kutokuwanyonya wananchi katika suala la miamala ya simu pamoja na muda wa maongezi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana naye na ndivyo tunavyotaka kufanya na tunavyoEndelea kufanya kwa kutumia huu mtambo wa *TTMS* na makampuni yote hatutaacha hata moja tutayaingiza katika mfumo huu na kuhakikisha mapato yao yote yanayopatikana tunayafahamu na tunapata haki yetu.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Martha Mlata, Mheshimiwa Haonga na Mheshimiwa Selasini.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Napenda kujua kama mfumo anaosema Mheshimiwa Naibu Waziri unasaidia pia kukusanya *data* za malipo ya nyimbo za wasanii ambazo zinatumika kama miito kwa sababu ni mara nyingi wamekuwa wakidhulumiwa na kutokujua ni kiasi gani wameuza? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hatujaanza kulifuatilia eneo hilo, lakini tukishakamilisha mfumo huu wa *Total Revenue Assurance,* nina uhakika tutaingia huko. Kikubwa hapa ni mikataba kati ya wasanii na hawa watoa huduma. Ni kazi ya sisi kupitia huu mtambo kuhakikisha tunasimamia mikataba yao na hatimaye tunawanufaisha wasanii. Hilo nadhani litaweza kufanyika, ngoja tusubiri mtambo huu ukamilike katika mfumo wake wa *Total Revenue Assurance.*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Haonga.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na wizi unaofanywa na baadhi ya makampuni ya simu, yanakata fedha za wateja yakidai kwamba tumekuunganisha na huduma fulani ambayo mteja hakuomba. Je, Serikali imejipanga vipi kudhibiti hali hii ya wizi unaofanywa na makampuni haya? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo ni namna tunavyotumia simu hizi. Mara nyingi sana huwa tunaulizwa maswali fulani na tunapojibu tunahalalisha makato bila wenyewe kujijua au unapobonyeza baadhi ya *button* unajikuta unakubali ukatwe bila mwenyewe kujua. Kwa hiyo, tumewataka watu wa *TCRA* wahakikishe wanatoa elimu ya

kutosha ili wananchi wasifike mahali fedha zao zinakwenda bila ridhaa yao wakati wao wana utaalam wa kuwajulisha wananchi na wakatuelewesha ni namna gani tuzitumie hizi *gadgets* hasa hizi za *android* za siku hizi...

**MWENYEKITI:** Ahsante. Ameshakuelewa, Mheshimiwa Selasini.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nauliza swali hili nadhani ni mara ya saba tangu nimekuwa hapa Bungeni. Makampuni ya simu ya nchi jirani kwa mfano *MTN* ya Zambia na *Safaricom* ya Kenya yana nguvu kiasi kwamba ukiwa Tunduma huwezi kupata mitandao kutoka kwenye makampuni ya hapa kwetu na ukiwa kule Rombo karibu nusu ya eneo la Rombo *Safaricom* ndiyo inayosikika na mbaya zaidi hata Redio yetu ya Taifa haisikiki*. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa inaonekana kama wananchi wa mipakani tumetengwa fulani hivi na huduma hizi za simu pamoja na Redio ya Taifa. Naomba hii iwe mara ya mwisho, ni lini Serikali itarekebisha tatizo hili ili kutoingiza wananchi wanaokaa mipakani kwenye *roaming facility* na hivyo kuibiwa muda wao wa maongezi bila wao wenyewe kutaka? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani wakati tunapitisha bajeti ya Wizara ya Habari mtakumbuka kwamba tuliongelea sana uimarishaji wa *TBC.* Tatizo ni kwamba mitambo yetu hatujaifikisha katika maeneo ya mipakani kwa kiwango cha kutosha. Tukishaifikisha mitambo yetu katika maeneo ya mipakani *frequency* haziwezi kuingiliana, uki-*tune TBC* utapata *TBC,* ingawa bado ukitaka ku-*tune* ya upande wa pili nayo utaisikia kwa sababu wenyewe watakuwa wapo kwenye *frequency* tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tutahakikisha tunaimarisha ile miundombinu ya *TBC* ili isikike vizuri maeneo yote ya mipakani. Vilevile wenzetu wanaotoa huduma za mawasiliano ya simu na *internet* nao wakiimarisha huduma zao tatizo hili litakwisha. Kwa hiyo, tupo katika mazingira hayo ya kuimarisha na nadhani atakumbuka tulichokubaliana au tulichopitisha kwenye bajeti ile ya Wizara ya Habari. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na swali linaulizwa na Mheshimiwa Frank Mwakajoka.

Na. 214

**Uhitaji wa Chuo cha VETA Tunduma**

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA** aliuliza:-

Mji wa Tunduma una vijana wengi wanaohitimu kidato cha nne lakini wanakosa nafasi za kuendelea na masomo ya juu:-

Je, Serikali inasema nini kuhusu kujenga Chuo cha Ufundi *VETA* ili vijana wengi waweze kupata ujuzi na kujiajiri na kuongeza kipato chao?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Frank George Mwakajoka, Mbunge wa Tunduma, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali haitaweza kujenga Chuo cha *VETA* katika Halmashauri ya Tunduma kwa sasa kwa sababu ya ukosefu wa fedha. Wakati juhudi mbalimbali zinaendelea za kutafuta vyanzo vya ufadhili wa kujenga Vyuo vya Ufundi Stadi kupitia *VETA,* wananchi wa Mji wa Tunduma

waendelee kutumia vyuo vilivyopo katika mikoa jirani hususan Mkoa wa Mbeya wenye Chuo cha *VETA* cha Mkoa na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi *(FDCs)* vya Nzovwe kilichopo katika Manispaa ya Mbeya na Katumba katika Wilaya ya Rungwe. Aidha, wananchi wanashauriwa kuendelea kutumia vyuo vingine vilivyosajiliwa na Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi *(VETA)* katika mikoa mbalimbali nchini ili kupata mafunzo ya ufundi stadi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Frank.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kutokana na majibu ya Mheshimiwa Waziri, naomba niulize maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kauli mbiu ya Serikali sasa ni viwanda, lakini viwanda havitakuwepo katika nchi hii kama hatutoweza kuzalisha mafundi mchundo wengi ili waweze kutekeleza majukumu mbalimbali ndani ya viwanda hivyo. Je, Serikali haioni kwamba inapoteza muda wa kutamka kwamba itakuwa ni Serikali ya viwanda wakati haitaki kuzalisha mafundi mchundo wengi ili waweze kutekeleza wajibu wao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, katika hali halisi ya majibu ya Mheshimiwa Waziri jana wakati anajibu hoja mbalimbali za Waheshimiwa Wabunge alisema kwamba Serikali imejipanga kujenga Vyuo vya *VETA* nchi nzima na maeneo mbalimbali katika Taifa hili. Leo katika majibu yake anatuambia kwamba Serikali haina mpango wa kujenga Chuo cha *VETA* katika Mji wa Tunduma. Je, jana alikuwa akiwadanganya Wabunge katika majibu yake ya msingi aliyokuwa akiyatoa ndani ya Bunge hili? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa kifupi, ajiandae Mheshimiwa Mbatia, Mheshimiwa Chuachua, Mheshimiwa Halima Bulembo na Mheshimiwa Esther Matiko.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi Serikali inatambua juu ya

umuhimu huo wa kuendelea kuzalisha mafundi sanifu na mafundi mchundo pamoja na wahandisi, lakini njia za kuzalisha mafundi hao haziko tu kupitia *VETA,* zipo pia kupitia vyuo binafsi lakini pia kupitia mafunzo ya muda mfupi ambayo wanafundishwa na kuweza hata kujitegemea katika viwanda vidogo vidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango huo upo, kwa mfano mwaka huu, kuna mafunzo ya vijana wapatao 23,000 ambayo yanaendeshwa na *VETA* ambayo ipo chini ya Wizara yetu lakini pia kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Ajira, Vijana na watu Wenye Ulemavu kuhakikisha kwamba vijana wengi wanapata fursa hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili kuhusiana na majibu yangu kwamba jana nimesema tutajenga vyuo nchi nzima. Kwanza naomba nipende kuliomba Bunge lako Tukufu, naona kuanzia jana hiyo kama ulivyosema na pengine siku zote Waheshimiwa Wabunge pengine huwa hawanisikilizi vizuri ninapotoa majibu yangu kiasi kwamba wameanza kuniwekea maneno ambayo sijazungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachosema ni hivi Serikali ina dhamira ya kujenga Vyuo vya *VETA* katika kila Wilaya lakini vilevile kuhakikisha kwamba inaimarisha Vyuo vya Wananchi kila mahali vilipo ambapo vipo 55. Hata hivyo, kwa sasa kutokana na hali halisi ya kibajeti tumesema tutaimarisha kwanza vyuo vilivyopo na vile ambavyo vilishakuwa vimeanza mchakato wa kuanza kuvijenga. Kwa hiyo, sio kwamba tutajenga tu kila mahali bila utaratibu au bila fedha, naomba nieleweke hivyo tafadhali. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Chuachua, wajiandae Mheshimiwa Mbatia, Mheshimiwa Halima Bulembo na Mheshimiwa Esther Matiko.

**MHE. RASHID M. CHUACHUA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa kuwa hali iliyoelezwa Tunduma inafanana sana na hali iliyopo katika Wilaya ya Masasi. Serikali ina mpango gani sasa wa kuhakikisha kwamba kutakuwa

na Chuo cha *VETA* ambacho kitahudumia karibu asilimia 54 ya watu wa Mkoa wa Mtwara pamoja na wale wanaotokea katika Wilaya ya Nanyumbu? Majibu ya Naibu Waziri hayaoneshi ni lini sasa mpango huo utaanza. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachohitajika ni wananchi kupata mafunzo na mafunzo sio majengo peke yake. Kwa hiyo, kwa upande wa Masasi au Nanyumbu tunacho Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Masasi ambacho tayari kimo katika mpango wa kukiboresha kwa kukifanyia ukarabati wa zaidi na kukiongezea uwezo ili kiweze kutoa mafunzo ambayo yanafanana pia na yale yanayotolewa *VETA.* Vilevile kuna Chuo cha Ndanda, naomba pia wananchi waweze kutumia chuo hicho ili kuweza kupata mafunzo yanayostahili.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mbatia.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Swali la msingi linaulizia kupata ujuzi na kujiajiri na ifikapo mwaka 2030 kwenye Maendeleo Endelevu ya Dunia, Lengo la Nne ni elimu bora sawa kwa wote. Je, Serikali imejipangaje kuwa na uendelevu wa kutoa masomo kwenye sekondari zetu yaani kwenye mitaala ya sayansi, biashara na kilimo badala ya kulazimisha watoto kuchukua sayansi tu ili iweze ikawa ni endelevu watoto wakaweza kujikita kwenye uelewa wao na stadi ambazo wanazipenda zaidi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi, wajiandae Mheshimiwa Bulembo na Mheshimiwa Esther Matiko.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru pia kwa swali zuri. Kimsingi hata sasa hivi kwenye baadhi ya maeneo tunazo shule hata za msingi ambazo zinatoa pia mafunzo ya ufundi, lakini vilevile tunaona kwamba kuna haja ya kuwapandikiza

watoto wetu ujuzi kuanzia katika ngazi za elimu za msingi, sekondari na kuendelea ikiwemo masuala yanayohusiana na sayansi na mazingira au kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninachokiona tu ni kwamba, kuna ugumu wa kusema kwamba kila jambo tunalolihitaji litawekwa kwenye mtaala kwa ajili ya huyo mwanafunzi. Kupitia vipindi vyetu vya elimu ya kujitegemea na mafunzo nje ya vipindi vya kawaida bado hawa wanafunzi wanaweza wakapata pia mafunzo kama hayo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima Bulembo.

**MHE. HALIMA A. BULEMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Ilani ya Chama cha Mapinduzi moja ya ahadi kubwa iliyotolewa ilikuwa ni kujenga *VETA* katika kila Wilaya Tanzania nzima. Kwa kuwa Mkoa wa Kagera unaongoza kwa idadi kubwa ya wanafunzi wanaomaliza darasa la saba na kidato cha nne lakini wanashindwa kujiendeleza kutokana na ukosefu wa vyuo hivyo. Je, ni lini sasa Serikali itahakikisha vijana hawa wanajengewa vyuo hivyo angalau hata katika Wilaya tatu za Mkoa wao? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ni lini?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa Mkoa wa Kagera ni kweli kuna uhitaji wa fursa hizo, lakini tayari kuna Chuo cha *VETA* pale Makao Makuu ya Mkoa. Vilevile kuna Chuo cha Wananchi Karagwe *(KVTC)* ambacho tunaendelea kukifanyia ukarabati na sasa hivi tayari tupo kwenye hatua za mwisho ili kiweze kuchukua wanafunzi wengi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna Chuo cha Maendeleo ya Wananchi cha Gera ambacho nacho kilikuwa katika hali mbaya sasa hivi kimeshafanyiwa ukarabati na tutaendelea kukiboresha ili kiweze kuchukua wanafunzi wengi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa niseme kwamba, kwa Mkoa wa Kagera kuna fursa kubwa ambapo tuna chuo tunategemea kukijenga kule Muhengele ambacho kitakuwa kinatoa mafunzo ya ujuzi wa juu zaidi kidogo kulingana na mahitaji ya soko kwa kushirikiana na ndugu zetu wa China.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Chuo Cha Maendeleo ya Wananchi Tarime miundombinu yake ni mibovu sana na haina hadhi ya kuwa Chuo cha Maendeleo ya Wananchi. Kwa bajeti ya mwaka jana 2016/2017, Serikali iliahidi hapa kwamba Vyuo vyote vya Wananchi vitapandishwa hadhi na kuwa *VETA.* Napenda kujua sasa ni lini Serikali itaenda kutimiza azma yake ya kupandisha Vyuo hivi vya Wananchi kuwa *VETA* kwa kuanzia na Chuo cha Wananchi cha Tarime? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba kuna dhana ya kufikiria kwamba labda mafunzo yanayotolewa na *VETA* ni bora zaidi kuliko yale yanayotolewa na Chuo cha Wananchi. Nitake tu kusema kwamba Vyuo vya Wananchi vina uwezo mzuri na mkubwa sana katika kutoa mafunzo isipokuwa kwa muda mrefu vilikuwa havijapewa haki yake ya kuendelezwa na kufanyiwa ukarabati unaostahili pamoja na kuwekewa miundombinu na vitendea kazi vya kufundishia kama inavyostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka huu Wizara imetenga jumla ya shilingi bilioni 12 kwa ajili ya kufuatilia vyuo hivyo na kuvirekebisha. Kwa hali hiyo, tutafuatilia pia Chuo cha Tarime kama alivyoeleza Mheshimiwa Mbunge ili kiweze kusaidiwa.

**MWENYEKITI:** Ahsante Waheshimiwa. Tunaendelea na Wizara ya Nishati na Mheshimiwa Ester Mmasi aulize swali lake.

Na. 215

**Mradi wa Bomba la Mafuta Mkoani Tanga**

**MHE. ESTER M. MMASI** aliuliza:-

Kupitia fursa ya ujenzi wa bomba la mafuta Mkoani Tanga, ni dhahiri kwamba vijana takribani 15,000 watapata ajira kwenye mradi kwa upande wa Tanzania:-

(a) Je, Serikali imejipangaje kuona kuwa vijana wa Kitanzania wanapata ajira katika soko la Tanzania kupitia fursa hii ya uwekezaji?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuingiza mtaala wa mafuta na gesi katika mitaala ya *VETA* ili kuwajengea uwezo, maarifa na ujuzi vijana wa Kitanzania katika sekta hiyo muhimu?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ester Michael Mmasi, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa ujenzi wa bomba la kusafirisha mafuta ghafi kutoka Hoima (Uganda) hadi Bandari ya Tanga (Tanzania) uko katika hatua ya majadiliano ya jinsi mradi huo utakavyotekelezwa. Katika majadiliano hayo, suala la ajira kwa Watanzania litazingatiwa ili Watanzania wanufaike na ajira kupitia ujenzi na uendelezaji wa mradi huo. Mradi unatarajiwa kutoa ajira 10,000 wakati wa ujenzi na ajira kwa watu 1,000 wakati wa uendeshaji.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2012 na 2013 Wizara ya Nishati na Madini kwa kushirikiana na Kampuni ya *Petrobras* ya Brazili, iliendesha mafunzo maalum ya ufundi wa *plumbing,* uchomeaji, upakaji rangi pamoja na mambo mengine katika Chuo cha *VETA* huko Mtwara na Lindi. Mafunzo hayo yalilenga kuwaongezea weledi wanafunzi wapatao 350 wa *VETA* ambao wamepatiwa vyeti vya kimataifa na wanaweza kuajiriwa ndani ya nchi na nje ya nchi. Gharama za mafunzo yote ni Dola za Marekani milioni nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kushirikiana na Serikali ya Norway, chini ya Mradi wa Mafuta kwa Maendeleo *(Oil for Development)* imekamilisha taratibu za kuingiza mtaala wa mafuta na gesi katika vyuo vya *VETA* hapa nchini. Mtaala huu utaanza kutumika katika baadhi ya vyuo vya *VETA* hapa nchini mwaka 2018. Utekelezaji wa mpango huu utagharimu Dola za Marekani milioni 20.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mmasi ajiandae Mheshimiwa Shekilindi.

**MHE. ESTER M. MMASI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mradi wa bomba la mafuta kutoka Hoima (Uganda) kuja Bandari ya Tanga nchini Tanzania ulitarajiwa kuanza mwezi Juni, 2017. Kwa kuwa pia majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri ni kwamba Serikali itakuwa tayari kuwaandaa vijana wetu kupitia mitaala ya *oil and gas* kwenye Vyuo vya *VETA* mnamo mwaka 2018. Je, Serikali kwa kufanya hivi haioni ni sawa kabisa na kuweka rehani ajira ya kijana wa Kitanzania hususan vijana wanaotoka katika Mkoa wa Tanga?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, mchakato wa uchimbaji, uchanjuaji na uchakataji wa zao la *oil and gas* Mikoani Lindi na Mtwara ulitarajia kuanza mwaka 2013, lakini hakuanza kutokana na sababu za ndani ya Serikali na kubwa ikiwa ni ukamilishwaji wa *local content policy* pamoja na msamaha wa kodi. Nini kauli ya Serikali kwa vijana wahitimu

kwa nchi ya Tanzania hasa ukiangalia kwamba vijana wengi wanahangaika kutafuta kazi pasipokuwa na imani yoyote? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nimpongeze Mheshimiwa Mmasi, tumekuwa na yeye tangu mwaka 2013 katika jitihada za kufungua mafunzo kwa *VETA* kwa wanafunzi wa *oil and gas.* Kwa hiyo hongera sana Mheshimiwa Mmasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na maswali yake haya mawili, la kwanza, Serikali haioni kwamba ni muhimu sasa kuwapatia mafunzo hasa wanafunzi wa *VETA* kwa *oil and gas.* Ni kweli kabisa upo umuhimu na mwaka 2012/2013 kama nilivyosema, tulianza kutoa mafunzo hayo kwa ajili ya kuwafundisha vijana wetu wa *VETA* Lindi na Mtwara kwa ajili ya uchomeleaji, ufundi sanifu pamoja na *theories* za kawaida za utafiti wa kuchimba na kutafiti mafuta na gesi hapa nchini. Kwa hiyo, tunaona umuhimu Mheshimiwa Mmasi na tumeshafika hatua nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, matarajio ya mpango wa Serikali, kweli kabisa mwaka 2018 tunatarajia taratibu zote za taaluma ili kuingiza sasa mtaala katika Vyuo vya *VETA* kwa upande wa mafuta na gesi itafika sasa muda muafaka hasa kwa *VETA* ambavyo ni vyuo vipya ukiondoa vile vyuo ambavyo vimeshaanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninavyowasiliana na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, tumefika hatua nzuri, Serikali ya Norway pamoja na Serikali yetu itatenga shilingi milioni 20 kwa ajili ya kukamilisha hatua hii. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mmasi, tutakapofika katika hatua hiyo tutashirikiana pamoja tuone namna ya kuwapatia vijana wetu mafunzo haya ambayo ni muhimu sana kwa ustawi wa nchi yetu.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Shekilindi, ajiandae Mheshimiwa Khadija.

**MHE. SHAABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona ili niweze kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa bomba hili la mafuta ghafi linaishia Bandari ya Tanga, je, Serikali imejipangaje kuona kuwa vijana wa Kitanzania hasa vijana wa Mkoa wa Tanga wanapata ajira hii katika soko la Kitanzania kupitia fursa hii ya uwekezaji?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Shekilindi, hongera, tumekuona unabeba mawe unasafisha barabara. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nimhakikishie Mheshimiwa Shekilindi, hili bomba la mafuta kutoka Hoima (Uganda) kuja Tanga (Tanzania) lina urefu mpana sana, lina jumla ya kilometa 1,443, lakini sehemu kubwa ya bomba hilo ambayo ni urefu wa kilometa 1,047 ni za hapa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, bomba hilo litapita karibu mikoa sita ya Kagera, Geita, Shinyanga, Dodoma hadi Tanga, kwa hiyo ni manufaa makubwa sana. Hivyo basi, ipo fursa kubwa sana kwa bomba hili kutoa ajira kubwa kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Shekilindi na wananchi wa Tanga kwamba ajira na fursa nyingi sana za kazi zitapatikana. Sambamba na hayo, tunawasiliana kwa karibu sana na Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji ili kutoa fursa nzuri sasa kwa Watanzania kuwekeza kwa kutumia fursa hiyo ya bomba la Hoima hadi Bandari ya Tanga.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Khadija.

**MHE. KHADIJA NASSIR ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwa kuwa ajira hizi zimekuwa zikitajwa kwa

ujumla wake, je, ni lini Serikali itatengeneza mchanganuo ili kupata uwakilishi mzuri kwa pande zote mbili za Muungano?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ni lini, kinachofanyika sasa tupo katika hatua ya pili, hatua ya kwanza tumekamilisha utambuzi wa eneo ambapo bomba litapita. Hatua ya pili, tunakamilisha mazungumzo ili kuainisha maeneo na fursa muhimu kwa nchi zetu mbili lakini pia kwa nafasi za Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar kwa masuala ya mafuta. Kwa sababu suala la ajira siyo la Muungano lakini fursa ziko palepale, utaratibu utakamilika baada ya majadiliano ndani ya mwaka huu lakini hatua ya pili itakuwa kuainisha fursa. Kwa hiyo, tutakapofikia hatua hiyo Mheshimiwa Mbunge tutawasiliana ili tuone namna ya kukamilisha na kuzinufaisha pande zote za Muungano.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Profesa Norman Adamson.

Na. 216

**Ujenzi wa Bwawa la Maji kwa ajili ya Kuzalisha Umeme**

**MHE. PROF. NORMAN A. S. KING** aliuliza:-

Utafiti uliofanywa na Serikali unaonesha kuwa Mto Lumakali unaozalisha maji katika Wilaya ya Makete unaweza kuzalisha *megawatts* 640 za umeme na hasa ikizingatiwa kuwa Wilaya ya Makete inapata mvua kwa miezi nane (8) kwa mwaka:-

Je, ni lini ujenzi wa bwawa ambao ni mpango wa Serikali wa tangu mwaka 2005 utaanza ili kusaidia kujenga uchumi wa kudumu huko Makete, Mkoa wa Njombe na Mbeya kwa ujumla?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Profesa Norman Adamson Sigalla King, Mbunge wa Makete, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, upembuzi yakinifu uliofanyika mwaka 2012 kupitia Shirika la Umeme Tanzania *(TANESCO)* ulibainisha kuwepo uwezekano wa kuzalisha umeme wa nguvu za maji wa megawati 222 katika eneo la Mwakauta kwenye Maporomoko ya Mto Rumakali. Juhudi mbalimbali zimefanywa na Serikali ikiwemo kuingia mikataba mbalimbali ya Makubaliano ya Awali ya uendelezaji wa Mradi huu kwa kushirikisha Kampuni mbalimbali za nje za *JSC* ya Urusi pamoja na kampuni ya China. Kampuni hizo hazikuweza kutekeleza mradi huo kutokana na gharama kuwa kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea na taratibu za kumpata mshauri mwelekezi kwa ajili ya kuandaa makabrasha ya zabuni kwa ajili ya kumpata mbia wa ujenzi wa mradi huo. Kazi ya kumpata mbia itakamilika mwezi Juni mwaka huu wa 2017 na ujenzi wa mradi unatarajiwa kuanza mwaka 2019 na utakamilika mwaka 2026. Gharama za mradi huu ni Dola za Marekani milioni 936.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Profesa.

**MHE. PROF. NORMAN A. S. KING:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu ya Naibu Waziri yanayoleta matumaini. Hata hivyo, nina maswali madogo ya nyongeza. Kwa kuwa mradi huu ulitegemewa kuzalisha umeme na wananchi wote wa Tanzania kunufaika, ni lini sasa Serikali itapeleka umeme kwenye vijiji 76 ambavyo havina umeme Wilaya ya Makete? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, ni lini Serikali itakamilisha upelekaji wa umeme kwenye vitongoji ambavyo havikupata umeme Awamu ya Kwanza ya *REA? (Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Profesa anavyotupa ushirikiano katika jimbo lake na awali ya yote nimhakikishie vijiji vyake 76 vitapata umeme kwenye Awamu ya Tatu ya *REA* inayoanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini sasa vijiji vilivyobaki vitapelekewa umeme, katika majibu yetu ya kila siku tumekuwa tukisema Mradi wa *REA* Awamu ya Tatu umeanza tangu mwezi Machi, 2017 na vijiji vyote vilivyosalia pamoja na vya Mheshimiwa Profesa King vya Makete pamoja na maeneo mengine vitapelekewa umeme kati ya mwaka huu wa 2017 hadi 2020. Kwa hiyo, Mheshimiwa Profesa, vijiji vyake vyote vitapata umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua sana Kata za Mang'oto, Lupende, Kambata na Mabacha pamoja na maeneo mengine ambayo anayataja yatapatiwa umeme katika awamu hii. Vilevile vitongoji na taasisi zake za umma vitapatiwa umeme na mradi huo ni mmoja umeshaanza, tumezindua kwa Mkoa wa Iringa na Njombe kwa Mheshimiwa Mbunge wa Kilolo na kwake wameshaanza, naambiwa wiki ijayo watafika kwa Mheshimiwa Profesa.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea, Mheshimiwa Susane Maselle kwa niaba yake Mheshimiwa Mgonukulima.

Na. 217

**Vijana Walionyang'anywa Ajira Machimbo ya Ishokelahela**

**MHE. SUZANA C. MGONUKULIMA (K.n.y. MHE. SUSANE P. MASELLE)** aliuliza:-

Je, kwa nini Serikali imewanyang'anya ajira vijana waliokuwa wamejiajiri kwenye Machimbo ya Ishokelahela na baadaye ikaamua kubadili umiliki wa leseni kwa siri?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Susane Peter Maselle, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, wachimbaji wadogo waliokuwa wanachimba Ishokelahela hawakuwa na leseni ya uchimbaji bali walikuwa wanachimba katika eneo la utafiti la leseni ya Kampuni ya *Carlton Kitongo Tanzania Limited.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, mwaka 2014, Serikali ilifanya mazungumzo na kampuni hiyo na kuwapatia wachimbaji wadogo hao leseni mbili za uchimbaji zenye jumla ya hekta 20. Wananchi hao waliweza kuunda kampuni yao inaitwa *Isinka Federation Miners Co-operative Limited.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2015 kikundi kiliamua kubadilisha leseni zake mbili za uchimbaji mdogo na kuzifanya kuwa leseni moja ya mgodi wa uchimbaji wa kati lakini chini ya Kampuni yao ya *Isinka Federation Miners Co-operative Limited.* Umiliki wa leseni hizo haujabadilishwa hadi leo upo chini ya umiliki wa wachimbaji hao wadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia mwezi Machi, 2017, mgodi ulikuwa umeshakusanya tani 35,000 za mbale *(ore)* kwa njia ya ubia wa Kampuni ya *Busolwa Mining* pamoja na wachimbaji hao na waliweza kutoa fursa za ajira 164 za moja kwa moja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Suzana.

**MHE. SUZANA C. MGONUKULIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitauliza maswali mawili ya nyongeza kwa niaba ya Mheshimiwa Susane Maselle, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, kutokana na majibu ya Naibu Waziri kuwa wachimbaji hawa wadogo

walipata leseni, je, Serikali inatoa kauli gani juu ya Jeshi la Polisi lililotumia nguvu kupiga mabomu wachimbaji hao wadogo na kuwanyanyasa wenyewe na familia zao na kufanyiwa vitendo vya unyanyasaji wa kijinsia wanawake na watoto? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, je, Naibu Waziri yupo tayari kuongozana na Mheshimiwa Susane Maselle kwenda eneo hilo kuongea na wananchi hao kuhusu vitendo walivyofanyiwa na Jeshi la Polisi kuwa hawakufanyiwa kiusahihi kwa sababu walikuwa na leseni? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi sana.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na swali la pili, niko tayari kufuatana na Mheshimiwa Susane na kwa ridhaa yako kama itapendeza basi nitafuatana naye, nitembelee maeneo yale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na wachimbaji hao kupigwa mabomu pamoja na kufanyiwa *harassment* ni suala ambalo linatakiwa litazamwe kwa kina sana unaweza usiwe na jibu la moja kwa moja. Ninachoweza kusema ni kwamba pale inapotokea kunakuwa na vurugu katika maeneo ya uchimbaji kazi ya Jeshi la Polisi ni kutuliza ghasia ili kuhakikisha kwamba kunakuwa na amani na utulivu katika maeneo yale. Inawezekana ilifanyika katika hatua hiyo, lakini Mheshimiwa Mbunge tutakaa pamoja tuone ni hatua gani zilichukuliwa ili tushirikiane na wenzetu wa Mambo ya Ndani tuone nini cha kufanya zaidi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rhoda Kunchela na Mheshimiwa Msabaha.

**MHE. RHODA E. KUNCHELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nami nataka niulize swali la nyongeza. Kwa wachimbaji wadogowadogo waliopo katika Mkoa wa Katavi hususan katika Machimbo ya Ibindi na Kapanda, vijana hawa wamekuwa na changamoto kubwa nyingi mno

ikiwepo gharama kubwa ya kukata leseni za uchimbaji lakini pia gharama kubwa ya dawa za kusafishia dhahabu wanazopata na gharama za umeme pia ziko juu. Je, nini mkakati wa Serikali kuhakikisha sasa inawasaidia hawa vijana kupunguziwa gharama hizi ambazo ni kero? Tamko la Serikali linasema nini ili kuwasaidia vijana kupata mikopo ili wajiendeleze kiuchumi na kupata kipato?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, wewe ni mtaalam, lijibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, ni kweli kabisa maeneo ya uchimbaji maarufu sana kwa maeneo ya Mpanda ni pamoja na Ibindi, Kapanda pamoja na Dilifu. Hata hivyo, nimtaarifa Mheshimiwa Mbunge kwamba hatua ambazo Serikali imechukua, la kwanza kabisa ni kurasimisha maeneo hayo ambayo nimeyataja kuwa maeneo maalum kwa ajili ya wachimbaji wadogo na wapo wachimbaji wadogo wazuri sana kwenye eneo lako ikiwa ni pamoja na Mheshimiwa Kapufi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili kuhusu mkakati ambao tunafanya...

**MWENYEKITI:** Swali moja tu unajibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Niseme tu, tumetoa ruzuku mwaka juzi kwa wachimbaji wa Ibindi na Kapanda na bado tunawapatia elimu na uwezeshaji kwa ajili ya uchimbaji mzuri kwa wachimbaji hawa wadogo.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Msabaha.

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nami naomba kumuuliza Naibu Waziri swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa kuna migodi ambayo inakuwa imeshafungwa na inakuwa si salama kwa wachimbaji wadogowadogo na hawa wachimbaji

wadogowadogo wamekuwa wakikiuka sheria na kuvamia migodi hii na kuhatarisha maisha yao. Je, Serikali ina mikakati gani kuhakikisha uvamizi huu wa wachimbaji wadogowadogo unakwisha na kuchukulia hatua za kisheria?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi sana.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, kwa mujibu wa Sheria ya Madini ya 2010, hairuhusiwi kufanya uchimbaji wowote bila leseni na kwa hiyo uvamizi kwa hali ya kawaida hauruhusiwi. Hata hivyo, yapo mazingira ambapo wananchi wamekuwa wakivamia maeneo na hasa ambao wao wameanza kuchimba mapema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu na mkakati wa Serikali, kwanza ni kufanya mazungumzo na hao wachimbaji wadogo kuwaelewesha lakini hata wale wenye leseni ambao wameyashikilia bila kuyaendeleza nao kuzungumza nao. Tunachofanya sasa, maeneo ambayo yanachukuliwa na watafiti bila kuyaendeleza Serikali inayachukua na kuwagawia wachimbaji maalum wadogo kwa utaratibu wa kisheria ili kufanya uchimbaji huu uwe wa manufaa kwa wachimbaji wadogo pamoja na wachimbaji wakubwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Wabunge, muda wetu umekwisha tunaendelea na Wizara ya Maji na Umwagiliaji.

Na. 218

### Tatizo Kubwa la Maji – Mkoa wa Simiyu

**MHE. ESTHER L. MIDIMU** aliuliza:-

Kumekuwa na tatizo kubwa sana la ukosefu wa maji safi na salama katika Mkoa wa Simiyu pamoja na Wilaya zake ambao ni Bariadi, Itilima, Busega, Maswa na Meatu:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia maji wananchi wa Mkoa wa Simiyu?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Esther Lukago Midimu, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeshaanza utekelezaji wa mradi wa majisafi kutoka Ziwa Victoria katika Mkoa wa Simiyu kwa miji mikuu ya Wilaya za Bariadi, Maswa, Meatu, Itilima, Busega na vijiji 253 vilivyopo umbali wa kilometa 12 kandokando ya bomba kuu. Tayari Mtaalam Mshauri anakamilisha upembuzi yakinifu, usanifu na uandaaji wa makabrasha ya zabuni. Gharama za utekelezaji wa mradi mzima zinakadiriwa kuwa kiasi cha *Euro* milioni 313. Mradi huu utawanufaisha wakazi wapatao 834,204 na unatarajiwa kutekelezwa katika awamu mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awamu ya kwanza itahusisha kufikisha maji katika Wilaya ya Bariadi, Itilima na Busega pamoja na vijiji vilivyopo kando kando ya bomba kuu ambapo Benki ya Maendeleo ya Ujerumani imeahidi kutoa Euro milioni 25 na tayari mkataba wa fedha *(financial agreement)* umesainiwa. Fedha zingine kiasi cha Euro milioni 80 zitatolewa na *Global Climate Fund* na ujenzi wa mradi huu unatarajiwa kuanza katika mwaka wa fedha 2017/2018 na utachukua miaka miwili hadi kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awamu ya pili ya mradi itafikisha maji katika Wilaya za Meatu, Mji wa Mwanhuzi na Maswa kwa gharama ya Euro milioni 208. Fedha hizi pia zinatarajiwa kutoka katika *Global Climate Fund.*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Midimu.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Kwanza kabisa, namshukuru Naibu Waziri kwa majibu mazuri

yanayotia moyo. Kwa kuwa mradi wa maji wa Ziwa Victoria utachukua muda mrefu ili kuwezesha Wilaya zote za Mkoa wa Simiyu kupata maji, je, Serikali ina mpango gani wa dharura wa kuwapatia maji ya uhakika wananchi wa Mkoa wa Simiyu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa Mji wa Maswa sasa hivi una matatizo makubwa ya maji, wanakunywa maji machafu na kuna mradi wa chujio ambao ni wa muda mrefu. Je, ni lini Serikali itakamilisha ili wananchi wa Maswa wapate maji safi na salama? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza amesema kwa sababu mradi huu utachukua muda mrefu, je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha sasa wananchi wanapata huduma ya maji? Kupitia mpango wa uendelezaji wa hii sekta ya maji, tayari tumeshatekeleza miradi mbalimbali katika Mkoa wa Simiyu na kuna maeneo ambayo kwa mfano, Nyangili, Mwamanyili, Bukapile, Bulima, Lamadi, Lukugu, Manara, kuna ambayo imekamilika na mingine inaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia juzi tumepitisha bajeti na katika Mkoa wa Simiyu tumeweka shilingi bilioni tisa ili Halmashauri ziendelee kutekeleza miradi ya maji kuhakikisha kwamba wakati tunasubiri ule mradi mkubwa, lakini wananchi wanaendelea kupata huduma ya maji. Vilevile Bariadi kuna huu mradi wa visima vya Misri tumechimba visima pale na nimeenda mwenyewe Simiyu maji yanapatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Maswa, ni kweli ukiangalia ule mradi hata utakapoanza eneo la mwisho utakwenda Maswa. Kutokana na hilo, hata jana tulikuwa na kikao, tayari tumeagiza *KASHWASA* washirikiane na Halmashauri ya Maswa ili tuweze kuona uwezekano wa kutoa maji kutoka bomba lile pale Shinyanga kupeleka maji kwa muda pale Maswa wakati tunasubiri mradi mkubwa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tumeshatumia dakika 25 za mijadala ambapo tumeshavuka kile kiwango kilichotakiwa. Nampa Mheshimiwa Mulugo peke yake, wengine nakushauri Waziri wa Maji hili suala la maji ni zito ukae na Wabunge wote hawa ujaribu kuyamaliza, Mheshimiwa Mulugo.

**MHE. PHILLIPO A. MULUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa upendeleo wa kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Songwe lina uhaba mkubwa sana wa maji lakini niongelee Kata moja inaitwa Totowe ambapo mimi mwenyewe kwa juhudi za Mbunge niliomba mradi wa Mheshimiwa Sabodo nikachimba kisima kikubwa sana na kisima hicho mpaka ninavyosema hivi bomba hilo linatoa maji kutoka mwaka 2012 mpaka leo yanatiririka na yamesambaa pale kijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimejaribu kuomba pale Halmashauri angalau watupe fedha hata shilingi milioni 50 tuweze kujenga tanki la kutunzia maji yale angalau yaweze kusambaa vizuri kwa kujenga mabomba kwa wananchi wa Totowe na maeneo ya Namambu. Je, Serikali inanisaidiaje mimi kama Mbunge nimefanya juhudi kutafuta maji halafu maji yanatiririka bila kujengewa tanki ili angalau wanipe fedha nikajenge tanki maji yaweze kuenea pale Totowe? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mweyekiti, alichokisema ni kweli. Baada ya kumaliza Bunge mwezi wa Julai, nitamwomba Mheshimiwa Waziri nianze na Mkoa wa Songwe kwa sababu Halmashauri za Mkoa wa Songwe katika suala la utekelezaji wa miradi ya maji hawakufanya vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Katibu Mkuu anaongea nao kule Morogoro ili kuona hizi Halmashauri ambazo hazikuperform vizuri zina matatizo gani wakati tulitoa maelekezo baada ya bajeti wanatakiwa kufanya manunuzi, lakini hawakufanya manunuzi kabisa. Nitakapokuwa nimekwenda tutaliangalia hili na Mheshimiwa Mbunge ili tuweze kuweka utaratibu wa kwenda haraka wananchi wapate maji. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Nakumbusha tena *rulling* ya Kiti ya kuwa Waziri wa Maji atakapoitwa kwenye Kamati ya Bajeti wadau wa maji wote waalikwe waende wakazungumzie hoja za maji kwenye Majimbo yao.

Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha. Tuna wageni waliopo Bungeni asubuhi hii.

Kuna wageni sita wa Naibu Spika wa Bunge, Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, kutoka Shirika la Kimataifa Lisilo la Kiserikali linalotekeleza miradi mbalimbali ya afya hapa nchini ya kuzuia vifo visivyo vya lazima kwa wanawake na wanafamilia, uzazi wa mama na mtoto pamoja na UKIMWI lijulikanalo kana *Jhpiego* ambao ni Dkt. Leslie Mancuso-Rais na Mtendaji Mkuu wa *Jhpiego* wa Dunia; Dkt. Alain Damiba-Makamu wa Rais Mwandamizi; Dkt. Jeremie Zoungrana-Mkurugenzi wa *Jhpiego* Tanzania; Dkt. Dustan Bishanga-Mkuu wa Mradi wa *USAID* wa Boresha wa Afya; Dkt. Albert Komba – Mkuu wa Mradi wa SAUTI wa *Jhpiego* na Ndugu Owen Mwandumbya-Meneja Mawasiliano na Ushirikishaji Wadau. *(Makofi)*

Tunao wageni 19 wa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la kujenga Taifa, Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi kutoka Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa wakiongozwa na Dkt. Florens Turuka-Katibu Mkuu; Ndugu Immaculate Ngwale-Naibu Katibu Mkuu; Jenerali Venance Mabeyo-Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama, Luteni Jenerali James Mwakibolwa-Mnadhimu Mkuu wa Jeshi; Meja Jenerali Michael Isamuyo-Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa; Meja Jenerali Simon Mumwi-Mkuu wa Mipango na Maendeleo Jeshini; Meja

Jenerali Harrison Masebo-Mkuu wa Utumishi Jeshini; Meja Jenerali E. Athanas-Mkuu wa Jeshi la Akiba; Ndugu Egbert Ndauka-Kamishina wa Sera na Mipango pia wamo Mabrigedia Jenerali na Makanali. Wameambatana na Wakurugenzi, Wakuu wa Taasisi, Idara, Vitengo na Maafisa mbalimbali waliopo chini ya Wizara hiyo. *(Makofi)*

Pia tunao wageni mbalimbali wa Waheshimiwa Wabunge pamoja na wanafunzi waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo Bungeni na Madiwani ambao wanatoka kwenye Jimbo la Mheshimiwa Mulugo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, Katibu.

**MWONGOZO WA SPIKA**

**WABUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika.

**MWENYEKITI:** Subiri Katibu, Waheshimiwa Kiti kikishatoa maelekezo kwa Katibu, ninyi mnachelewa kama una mwongozo si unasema mapema?

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mapema ndiyo hii.

**MWENYEKITI:** Msibishe.

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mapema ndiyo hii.

**MWENYEKITI:** Msibishe itakula kwenu. Haya Mheshimiwa Bilago. *(Kicheko)*

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Bobali.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Haonga.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Bobali.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bobali. Mheshimiwa Haonga endelea.

**WABUNGE FULANI:** Ditopile.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako kwa Kanuni ya 68(7) lakini pia naomba iweze kusomwa na Kanuni ya 101(4). Naomba niisome Kanuni ya 101(4) ambayo inasema:-

*"Kwa kuzingatia masharti ya fasili ya (3), Kamati za Vyama zitawasilisha kwa Spika majina ya Wabunge watakaoomba kupata ufafanuzi wa suala mahususi la sera, na Spika atatoa nafasi kwa Wabunge kwa kuzingatia uwiano."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku ya jana kuna jambo limejitokeza hapa Bungeni ambalo wako Wabunge mbalimbali waliosimama kwa ajili ya kuweza kuomba ufafanuzi wakati tunajadili Wizara ya Elimu. Walisimama Wabunge mbalimbali ambao ulikuwa umewasoma kwa majina ambapo upande wa CHADEMA alisimama Mheshimiwa Susan ambaye ni Waziri Kivuli lakini pia kwa upande wa CCM wapo pia waliosimama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lililotokea kwa kweli lilishangaza sana. Tunaomba kujua kama hili suala linaruhusiwa hapa Bungeni na wakati huo tuone kwa mujibu wa Kanuni hii ya 101(4) kama uwiano ulizingatiwa jana kwa wale Wabunge waliokuwa wamesimama. Kwa hiyo, suala hili kidogo limeleta shida na sintofahamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tulikuwa tunaomba kama kuna uwezekano kulingana na uwiano uliotajwa hapa, akiomba mmoja labda Mbunge kutoka CCM aje wa CHADEMA, aje wa *CUF* mmoja *then* turudi kwa wengine kuliko kuchukua wa upande mmoja wote wanne halafu baadaye ukasema muda umeisha. Suala hili kwa kweli tunaomba

ufafanuzi kwa sababu limelete sintofahamu na siyo jana tu na siku nyingi za nyuma kidogo limeweza kujitokeza. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante nimeshakuelewa. Mheshimiwa Bobali.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nasimama kwa Kanuni ya 68(7) pamoja na 69 ikikupendeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimboni kwangu Mchinga hivi sasa ninapoongea kuna tembo 18 wamevamia kwenye vijiji wanakula mashamba ya wakulima lakini lililo baya usiku wa kuamkia leo wamevamia kijiji na wamevunja nyumba za wananchi bahati ni kwamba hawakuua raia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili nimeshawahi kumwambia Waziri mara nyingi, jana usiku nikampigia simu hakupokea, nikamtumia na meseji, hatua hazichukuliwi na Jimbo la Mchinga halipakani na mbuga yoyote, ni tembo wanaopotea kama hawa ambao walipotea wakaja hapa *UDOM.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa suala hili la tembo...

**WABUNGE FULANI:** Ndovu.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Sawa ndovu ili mwelewe, kuvamia vijiji na kula vyakula vya wakulima katika kipindi hiki ambacho mavuno yenyewe siyo mazuri, mwaka jana zililiwa hekari 183 hakuna hata mkulima mmoja amelipwa wala kupewa kifuta jasho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako, kama Waziri ameshindwa kusimamia hii Wizara aseme kwa sababu kero za namna hii ziko katika Majimbo mengi lakini pia nataka kujua hawa wakulima watafidiwaje. Naomba mwongozo wako.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Bobali umeshaeleweka. Mheshimiwa Bilago.

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako kwa Kanuni ya 68(7) nisiisome lakini ni jambo ambalo limetokea eneo la Masaki jana mapema tu ambapo Askari Polisi ametumia risasi tisa kumdhibiti Adam Malima aliyekuwa Naibu Waziri wa Fedha kwa sababu ya gari tu lililokuwa limepakiwa vibaya *(wrong parking).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi ya risasi tisa ambazo ni fedha za walipa kodi bila sababu yoyote ya msingi na Malima hakuwa adui wala na silaha yoyote na vitendo hivi tumevisema muda mrefu, matukio kama haya yanaendelea kuimarika nchi hii. Tulianza na *TV* ya *Clouds* ikatekwa, akatekwa Mheshimiwa Nape na bastola sasa Malima ametekwa na risasi tisa zimetumika. Naomba mwongozo wako...

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Tunakoipeleka nchi hii...

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Ndiyo huku tulikokuwa tunajivunia?

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Bilago umeshaeleweka.

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Naam.

**MWENYEKITI:** Tumeshakuelewa.

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nimeombwa miongozo mitatu, miongozo yote, mwongozo wa Mheshimiwa Haonga mambo yaliyotokea jana leo hayahusiki lakini nitakusaidia. Kanuni zetu ziko *very clear*, Kanuni ya 5(4) kama Kiti kinafanya kitu hakikuridhishi ni wajibu wako kuandika barua kwa Katibu na mimi nitaitwa kwa Katibu na wewe utaitwa tutaelezana vizuri tu utaratibu wa Bunge linavyoendeshwa. Kwa hiyo, nakushauri kama unaona Kiti hakijakutendea haki, tumia Kanuni ya 5(4), hiyo ndiyo *rulling* yangu.

Mheshimiwa Bobali mambo ya tembo, hizi Kanuni zetu ziko *very clear*, Kanuni ya 67 ni jambo lililotokea mapema Bungeni, lakini naelewa masuala haya yanawagusa Wabunge kwenye Majimbo yao na sehemu ya kilio chao ni humu ndani. Kwa hiyo, Waziri wa Maliasili na Utalii utakaa na Mbunge ili mtazame ni namna gani mtalimaliza tatizo hili na kusaidia wananchi wake wasipate matatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Bilago suala la Mheshimiwa Malima, vilevile Kanuni zetu haziruhusu lakini pia Bunge hatuna taarifa rasmi juu ya suala hili na ili mradi umelisema Serikali ipo wamelisikia, watalifanyia kazi, watatupa maelekezo. Katibu.

**NDG. THEONEST RUHILABAKE - KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa Fedha 2017/2018 - Waziri wa Ulinzi na Jeshi la kujenga Taifa

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, naomba kutoa

hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea, kujadili na kupitisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, kwa kuniwezesha kuwasilisha hotuba yangu ya bajeti kwa mwaka huu wa 2017/2018 mbele ya Bunge lako Tukufu. Pili, namshukuru kwa dhati Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, kwa kuniamini kuendelea kuiongoza Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee nachukua fursa hii kuungana na Watanzania kwa ujumla kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kuchaguliwa kwake kwa kishindo kuwa Mwenyekiti wa Tano wa Chama cha Mapinduzi kufuatia Uchaguzi wa Viongozi wa Chama uliofanyika tarehe 23 Julai, 2016 mjini Dodoma. Watanzania wana matumaini makubwa na safu ya uongozi wa chama chini ya Mwenyekiti wake ambaye pia ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, napenda kuwashukuru Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan na Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa kwa miongozo na maelekezo wanayonipatia katika kutekeleza majukumu ya Wizara yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahadi yangu kwa Mheshimiwa Rais, kwenu Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wenzangu ni kuwa, nitaendelea kutekeleza majukumu niliyokabidhiwa kwa uadilifu na uaminifu mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uongozi wa Awamu ya Tano chini ya Mheshimiwa Rais na Wasaidizi wake Wakuu katika kipindi cha takriban mwaka mmoja na nusu tangu uingie madarakani umekuwa ni mfano wa kuigwa na umeweka historia ya kipekee nchini kwa kuendelea kutekeleza kwa kasi na ufanisi mkubwa ahadi zilizomo kwenye Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie fursa hii pia kumpongeza Jenerali Venance Mabeyo kwa kuteuliwa kuwa Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi. Aidha, nimpongeze Luteni Jenerali James Mwakibolwa kwa kuteuliwa kuwa Mnadhimu Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi. Kipekee, napenda kumshukuru Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi Mstaafu Jenerali Davis Mwamunyange kwa utumishi wake uliotukuka na kwa namna tulivyoshirikiana katika kuliongoza Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania kwa mafanikio makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Spika wa Bunge hili Mheshimiwa Job Ndugai; Naibu Spika, Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson; pamoja na Wenyeviti wa Bunge kwa kuendesha vizuri shughuli za Bunge. Namwomba Mwenyezi Mungu azidi kuwapa maarifa, hekima, busara na nguvu za kuendelea kuongoza Bunge hili katika kutekeleza majukumu yake mazito na nyeti.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, napenda kutumia nafasi hii kuwashukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama Mheshimiwa Balozi Adadi Rajabu, Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Kanali Mstaafu Ally Khamis Masoud na Wajumbe wote wa Kamati hii Tukufu kwa kuendelea kunipa ushirikiano mkubwa katika kuiongoza Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. *(Makofi)*

Kamati hii imetupatia ushauri mzuri wakati wa kuchambua mapendekezo ya makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara yangu kwa mwaka 2017/2018. Maoni na mapendekezo yao yametusaidia sana katika kuandaa mpango na bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kuwapongeza Waheshimiwa wafuatao: Alhaji Abdallah Bulembo, Profesa Palamagamba Kabudi, Mheshimiwa Anne Killango Malecela, Mama Salma Rashidi Kikwete, Dkt. Getrude Lwakatare na Mheshimiwa Catherine Ruge kwa kuteuliwa kuwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri la Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Juma Ali Juma kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Dimani. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Profesa Palamagamba Kabudi kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kutoa salamu za pole kwako Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote kwa kuondokewa na mpendwa wetu Mheshimiwa Samwel Sitta, Mbunge Mstaafu wa Jimbo la Urambo Mashariki na Spika wa Bunge la Tisa la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pia natoa pole kwa Mheshimiwa Spika kufuatia kifo cha Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Dimani Zanzibar kilichotokea tarehe 11 Novemba, 2016 na Mheshimiwa Dkt. Elly Marko Macha aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum kilichotokea tarehe 31 Machi, 2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naungana na wenzangu wote waliotangulia kuwapa pole wale waliopatwa na majanga, pamoja na kufiwa na ndugu, jamaa na wapendwa wao katika matukio mbalimbali yaliyotokea nchini yakiwemo tetemeko la ardhi lililotokea Kagera tarehe 10 Septemba, 2016 na ajali mbalimbali za vyombo vya usafiri yakiwemo mabasi ya abiria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee natumia fursa hii kuwapa pole Wazazi, Walimu na Watanzania wote kutokana na vifo vya wanafunzi 32, Walimu wawili na Dereva wa shule ya Msingi *Lucky Vincent* ya Mjini Arusha vilivyotokana na ajali ya basi iliyotokea tarehe 6 Mei, 2017, katika eneo la Rhotia Wilayani Karatu. Naomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi na kuwajalia majeruhi wote kupona haraka na kurejea katika masomo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, napenda sasa kuchukua fursa hii kuwasilisha hotuba yangu ambayo kiujumla imejikita katika maeneo makuu yafuatayo:-

Malengo na majukumu ya Wizara; Hali ya Usalama wa Mipaka katika mwaka 2016/2017; Utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama; Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya mwaka 2016/2017 na Mpango na Makadirio ya Bajeti kwa mwaka 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malengo na majukumu ya Wizara; kama ilivyo katika Dira ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Wizara imeendelea kuwa Taasisi iliyotukuka ya kulinda na kudumisha amani na usalama wa Taifa letu. Vivyo hivyo, dhima ya Wizara ni kuendelea kulinda Jamhuri ya Muungano wa Tanzania dhidi ya adui wa aina yoyote kutoka ndani na nje ya nchi na kuhakikisha kuwa mamlaka na maslahi ya nchi yetu yanakuwa salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti*,* katika kufanikisha dhima yake, malengo ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa yameendelea kuwa kama ifuatavyo:-

(i) Kuwa na Jeshi dogo na mahiri la Ulinzi wa Nchi lenye weledi, zana bora, vifaa vya kisasa na mawasiliano salama;

(ii) Kuendelea kuwajengea vijana wa Kitanzania moyo wa uzalendo, ukakamavu, maadili mema, utaifa na kuwafundisha stadi za kazi;

(iii) Kuendeleza utafiti na kujenga uwezo katika teknolojia za kijeshi;

(iv) Kuimarisha Jeshi la Akiba;

(v) Kusaidia mamlaka za Kiraia katika kukabiliana

na athari za majanga na matukio yanayoweza kuhatarisha maisha amani na utulivu wa nchi; na

(vi) kudumisha amani na usalama kwa kushirikiana na nchi nyingine duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kufikia malengo yaliyoainishwa, Wizara itaendelea kusimamia utekelezaji wa majukumu yafuatayo:-

(i) Kuandikisha Wanajeshi wenye sifa stahiki kwa lengo la kuwa na Jeshi dogo, mahiri kwa ajili ya Ulinzi wa Taifa na kuwapatia mafunzo na mazoezi ya kinadharia na kivitendo;

(ii) Kuwapatia wanajeshi makazi bora, zana, vifaa na vitendea kazi bora na vya kisasa pamoja na kusimamia matumizi na matunzo yake;

(iii) Kuendesha mafunzo na mazoezi ya Mgambo;

(iv) Kuboresha mitaala ya mafunzo ya JKT kwa vijana ili kuwaandaa kuwa wakakamavu, wenye nidhamu na kuwajengea moyo wa uzalendo na mshikamano wa Kitaifa na kutekeleza shughuli za kujitegemea;

(v) Kuendeleza utafiti na uhawilishaji wa teknolojia za Kijeshi kupitia Mashirika ya Mzinga na Nyumbu;

(vi) Kuwezesha Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Kujenga Taifa (SUMAJKT); kuwa na tija na faida itakayochangia katika uendeshaji wa shughuli za Jeshi la Kujenga Taifa.

(vii) Kushirikiana na Mamlaka za Kiraia katika kukabiliana na majanga na dharura za Kitaifa pale inapohitajika kufanya hivyo; na

(viii) Kuimarisha ushirikiano na nchi nyingine katika nyanja za Kijeshi na kiulinzi kupitia Jumuiya za Kimataifa,

Kikanda na ushirikiano na nchi moja moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama. Wakati Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje Ulinzi na Usalama ilipokaa na kujadili Makadirio ya Mapato, Mpango na Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa fedha 2016/2017 ilitoa maoni, ushauri na maelekezo kadhaa kwa Wizara hii yaliyolenga kuboresha utendaji na utekelezaji wa majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa maoni, ushauri na maelekezo yaliyotolewa yamefanyiwa kazi na hoja mbalimbali zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge wakati wa mjadala huo pia zimezingatiwa katika mpango wa bajeti ya mwaka wa fedha 2017/2018 inayowasilishwa leo hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya Ulinzi na Usalama wa mipaka ya nchi yetu kwa ujumla ni shwari. Hata hivyo, kumekuwa na changamoto ya kutotengamaa kwa hali ya usalama kwenye baadhi ya nchi za Ukanda wa Afrika Mashariki, Maziwa Makuu na Pembe ya Afrika ikiwa ni pamoja na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Burundi, Somalia na Sudan Kusini. Aidha, uwepo wa hali ya matishio ya ugaidi wa Kimataifa umevilazimu vyombo vya Ulinzi na Usalama kwa kushirikiana na nchi jirani na raia wake kuendelea kuwa katika hali ya tahadhari na umakini endapo kutajitokeza dalili yoyote inayotishia usalama, hatua stahiki ziweze kuchukuliwa haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya mipaka ya nchi yetu yenye jumla ya urefu wa kilomita 5,390 ambayo inahusisha eneo la nchi kavu na eneo la maji imeendelea kuwa shwari. Vyombo vyetu vya Ulinzi na Usalama kwa kushirikiana na wananchi vimeendeleza jitihada za kuimarisha usalama wa mipaka hiyo hatua ambayo imechangia kudhibiti na kupunguza matukio na vitendo vyenye kutishia usalama kama vile, ugaidi, biashara ya dawa za kulevya, usafirishaji

haramu wa binadamu, uhamiaji haramu na ujambazi. Hali ya mipaka yetu katika kipindi kinachopitiwa imekuwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpaka wa Mashariki; katika mpaka huu ambao una urefu wa kilomita 1,413, nchi yetu inapakana na Bahari ya Hindi na pia nchi za Kenya, Visiwa vya Ushelisheli, Comoro na Msumbiji. Kwa ujumla hali ya usalama katika mpaka huu imeendelea kuwa shwari kutokana na kudhibitiwa kwa vitendo vya uharamia ambapo kumeambatana na kuongezeka kwa doria katika Bahari ya Hindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpaka wa Kaskazini; kwenye eneo la mpaka huu Tanzania imepakana na nchi za Kenya na Uganda. Hali ya usalama katika mpaka huu wenye urefu wa kilomita 1,221 kwa ujumla ilikuwa shwari licha ya tatizo la uingiaji wa wahamiaji haramu kutoka nchi za Ethiopia, Eritrea na Somalia ambao hujipenyeza kuingia nchini wakiwa safarini kuelekea maeneo ya Kusini mwa Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpaka wa Magharibi; mpaka huu wenye urefu wa kilomita 1,220 ambako Tanzania imepakana na nchi za Burundi, Rwanda na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo *(DRC)* pamoja na kuwa shwari kwa ujumla umekuwa pia na changamoto kadhaa. Mojawapo ya changamoto hizo ni kutokukamilika kwa mazungumzo ya upatanishi ya pande zinazosigana nchini Burundi hali inayosababisha hali ya kiusalama kutotengamaa. Aidha, uwepo wa vikundi vya waasi vyenye silaha vinavyoendesha harakati za kimapigano dhidi ya Majeshi ya *DRC* na Majeshi ya Umoja wa Mataifa *(MONUSCO)* ambako kunasababisha ongezeko la wakimbizi hali ambayo inahatarisha usalama kwenye eneo la mpaka huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpaka wa Kusini; kwenye mpaka wa Kusini ambao una urefu wa kilomita 1,536 Tanzania inapakana na nchi za Msumbiji, Malawi na Zambia. Pamoja na hatua zinazoendelea za usuluhishi wa mgogoro wa mpaka uliopo baina ya Tanzania na Malawi, kwa ujumla

hali ya mpaka huu imeendelea kuwa shwari na wananchi wanaendelea na shughuli zao kama kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Mwaka 2016/2017. Katika mwaka wa fedha wa 2016/2017, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ilikadiria kukusanya mapato ya jumla ya sh.68,406,000.00 kupitia mafungu yake matatu ya 38-NGOME, 39- JKT na 57-Wizara. Kufikia mwezi Aprili, 2017 Mafungu hayo yalifanikiwa kukusanya mapato ya jumla ya sh.43,516,561.80 sawa na asilimia 63.6 ya makadirio. Chanzo kikuu cha makusanyo hayo ni mauzo ya nyaraka za zabuni ambayo yameendelea kupungua kwa kuwa utangazaji wa zabuni sasa unafanywa pia na Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini *(GPSA).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti ya mwaka wa fedha 2016/2017, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa iliidhinishiwa na Bunge lako Tukufu jumla ya sh.1,736,578,102,510.00 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo kwa mafungu yake matatu. Kati ya fedha hizo, bajeti ya kawaida inayojumuisha mishahara na matumizi mengineyo ni sh.1,488,578,102,510.00 na bajeti kwa ajili ya shughuli za maendeleo ni sh. 248,000,000,000.00. Mchanganuo wa bajeti kwa kila Fungu umeoneshwa katika Jedwali Na. 1.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia mwezi Aprili, 2017 Wizara ilikuwa imepokea jumla ya sh.1,199,292,622,613.00 sawa na asilimia 69.1 ya bajeti yake yote. Kati ya fedha hizo, sh.1,163,392,622,613.00 sawa na asilimia 78.2 ya bajeti iliyoidhinishwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida zilipokelewa. Fedha hizo zimetumika kutekeleza majukumu na mipango ya kazi, kulipia mishahara na posho mbalimbali muhimu ikiwa ni pamoja na kugharamia huduma mbalimbali zikiwemo stahili za Wanajeshi na Watumishi wa Umma, uendeshaji wa Ofisi na kulipa madeni ya Wazabuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa matumizi ya maendeleo, fedha zilizopokelewa ni sh.35,900,000,000.00 sawa na asilimia 14.5 ya fedha zote zilizoidhinishwa kwa ajili

ya matumizi hayo. Fedha hizo zimetumika kulipia madeni ya kimkataba, ujenzi wa miundombinu ya maji safi na maji taka vikosini, kuingiza huduma ya maji na umeme katika baadhi ya nyumba 6,064 zilizojengwa kwa makazi ya Wanajeshi na uingizaji umeme katika minara ya mawasiliano iliyosimikwa katika Mikoa ya Morogoro na Dodoma. Kuendeleza ukarabati wa maghala ya silaha na milipuko na ukarabati wa kambi mpya tano za Milundikwa na Luwa (Rukwa), Itaka (Songwe), Mpwapwa (Dodoma) na Makuyuni (Arusha). Mchanganuo wa fedha zilizopokewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo hadi mwezi Aprili, 2017 umeoneshwa katika Kiambatisho Na. 1**.**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuangalia mchanganuo wa fedha zilizopokelewa hadi kufikia mwezi Aprili, 2017, mwenendo wa upatikanaji wa fedha kwa ajili ya matumizi ya kawaida kwa mafungu yote matatu ya Wizara hususan fedha za mishahara na chakula kwa Wanajeshi katika kipindi hicho ulikuwa ni wa kuridhisha. Fedha kwa ajili ya mishahara na marupurupu zilipokelewa kulingana na makisio ya bajeti. Kwa upande wa fedha za shughuli za maendeleo, fedha zilizopokelewa hazikuweza kukidhi mahitaji na hivyo kuathiri utekelezaji wa shughuli za maendeleo ikiwa ni pamoja na ulipaji wa madeni ya kimikataba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mafanikio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Mwaka Wa Fedha 2016/2017. Matumizi ya shughuli za kawaida; katika mwaka wa fedha 2016/2017, Wizara imefanikiwa kulipia mahitaji na huduma muhimu kwa Maafisa, Askari, Vijana wa Jeshi la Kujenga Taifa na Watumishi wa Umma. Aidha, kwa kutumia fedha hizi majukumu mbalimbali ya kiulinzi yaliyotekelezwa ni pamoja na kufanya mafunzo na mazoezi ya Kijeshi, mafunzo ya Mgambo, ushirikiano wa kiulinzi na kijeshi na nchi nyingine, ushirikiano na Jumuiya za Kikanda na Kimataifa, ushirikiano wa Jeshi na Mamlaka za Kiraia na Mafunzo ya JKT.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mafunzo na Mazoezi ya Kijeshi; katika mwaka 2016/2017, Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania, limeendelea kutoa mafunzo na mazoezi kwa

Wanajeshi wake ili kujiimarisha kiulinzi. Jeshi letu lilifanikiwa kufanya mazoezi mbalimbali ya kimataifa na ya ndani yafuatayo: *"Exercise Eastern Accord"* ililofanyika Tanzania kuanzia tarehe 10 hadi 12 Julai 2016, *Exercise Amphibious Landing*" lililofanyika Bagamoyo kuanzia tarehe 19 Agosti, 2016 hadi tarehe 5 Septemba, 2016 ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya sherehe za miaka 52 ya JWTZ; "*Exercise* - Ushirikiano Imara" lililofanyika Mombasa nchini Kenya kuanzia tarehe 17 - 19 Novemba, 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Jeshi liliendelea kutoa mafunzo kwa Maafisa na Askari kwenye vyuo, shule na vituo mbalimbali vya mafunzo kwa wanajeshi katika ngazi mbalimbali ndani na nje ya nchi. Mazoezi na mafunzo haya yalilenga kuwajengea Wanajeshi wetu uwezo, weledi na umahiri wa kiutendaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mafunzo ya Mgambo; mafunzo ya Mgambo kwa wananchi yameendelea kutolewa na Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania. Katika kipindi cha mwaka 2016/2017, JWTZ kwa kushirikiana na Vyombo vya Usalama limeendesha mafunzo katika ngazi mbalimbali ambapo jumla ya wananchi 13,997 walifuzu. Hili ni ongezeko la wahitimu 7,241 sawa na asilimia 51.7 ikilinganishwa na wananchi 6,756 waliopata mafunzo hayo mwaka 2015/2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea kutoa wito kwa Viongozi wa ngazi mbalimbali kuhamasisha wananchi kushiriki katika mafunzo ya Mgambo. Kwa maagizo ya Mheshimiwa Rais, jumla ya Askari Mgambo 48 walioshiriki katika *"Exercise*- Onesha Uwezo wa Medani" lililofanyika katika Mkoa wa Arusha na *"Exercise - Amphibious Landing"* lililofanyika katika Mikoa ya Dar es Salaam na Pwani waliandikishwa katika Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Huduma za Afya na Tiba; katika kipindi husika, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imeendelea kutoa huduma za matibabu kwa Maafisa, Askari,

Watumishi wa Umma, familia zao na wananchi kwa ujumla. Huduma hizo zimekuwa zikitolewa katika hospitali na vituo vya tiba vya Jeshi hapa nchini. Katika kipindi hicho jumla ya wananchi 217,887 walipata matibabu katika zahanati, vituo vya afya na hospitali za Jeshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Wizara imeendelea na maboresho ya huduma za matibabu kwa Wanajeshi na familia zao, ambapo mchakato wa kuanzisha Mfuko wa Bima ya Afya kwa ajili ya Wanajeshi ulioanza mwaka wa fedha 2015/2016 umeendelea kufanyiwa kazi. Hati Maalum *(instrument)* ya mapendekezo ya uanzishwaji wa Mfuko huo na mabadiliko ya Kanuni Namba 26 na 27 ya Juzuu ya Kwanza (I) Utawala vimeandaliwa ili viweze kuwasilishwa kwa Mheshimiwa Rais na Amiri Jeshi Mkuu kwa ajili ya kuridhiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ushirikiano wa Kiulinzi na Kijeshi na Nchi nyingine;ushirikiano kati ya nchi yetu na nchi nyingine katika nyanja za Kijeshi ni suala muhimu katika mustakabali wa ulinzi na usalama. Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania limeendelea kuwa na ushirikiano mzuri na Majeshi ya nchi nyingine hususan katika eneo linalohusu nafasi za mafunzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka fedha wa 2016/2017 Maafisa na Askari zaidi ya 350 wamekwenda kusoma kozi mbalimbali katika nchi rafiki zikiwemo Afrika Kusini, Burundi, Canada, China, Falme za Kiarabu, India, Kenya, Marekani, Misri, Morocco, Rwanda, Uganda, Uingereza, Ujerumani, Urusi na Zambia. Aidha, Maafisa kutoka katika baadhi ya nchi hizi wapo hapa nchini katika vyuo vyetu vya Kijeshi kwa mafunzo. Vyuo hivyo ni Chuo cha Maafisa Monduli, Chuo cha Ukamanda na Unadhimu Arusha na Chuo cha Ulinzi wa Taifa - Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ushirikiano na Jumuiya za Kikanda na Kimataifa; Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania, limeendelea kushiriki katika operesheni za ulinzi wa amani chini ya Umoja wa Nchi za Afrika *(African Union)* na Umoja wa Mataifa. Nchi yetu imeendelea kuwa na vikosi vyake

Darfur nchini Sudan maeneo ya Khor-Abeche; Shangli Tobayi na Menawash chini ya *UNAMID*. Aidha, Jeshi letu limeendelea kuwepo Mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo kama sehemu ya *MONUSCO “Force Intervention Brigade”.* Pia, Kombania mbili za Polisi Jeshi zipo nchini Lebanon kwa majukumu kama hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kikosi na Maafisa wa JWTZ waliopo kwenye Operesheni za Ulinzi wa Amani katika maeneo hayo wote wanaendelea vizuri na utekelezaji wa majukumu yao. Vilevile, katika kudumisha mahusiano na kuzuia matishio ya utekaji wa meli katika Bahari ya Hindi, tumeendelea kushirikiana na nchi mbalimbali zikiwemo, nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika, Afrika Kusini, Australia, Bangladesh, China, Hispania, India, Iran, Italia, Pakistan, Ufaransa, Netherlands, Uingereza na Urusi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ushirikiano wa Jeshi na Mamlaka za Kiraia; katika kudhihirisha utayari wa Jeshi letu kushikiri katika shughuli mbalimbali za kiraia na utoaji wa huduma na misaada wakati wowote inapohitajika, katika mwaka wa fedha 2016/2017, Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania limeshiriki katika kutoa misaada kwenye maafa ya tetemeko la ardhi lililotokea Mkoani Kagera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, misaada hiyo imehusisha kurejesha miundombinu iliyoharibika, ujenzi wa majengo ya Taasisi za Serikali pamoja na kusaidia wananchi. Aidha, Wizara ilichangia sh.76,125,000.00 kwa waathirika wa tetemeko hilo. Nachukua fursa hii kuzipongeza Mamlaka za Kiraia na Taasisi zote kwa kutoa ushirikiano mzuri kwa Jeshi wakati wa kutekeleza majukumu hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukabiliana na vitendo vya kihalifu, Wizara, kupitia JWTZ, imeendelea kushirikiana na Vyombo vingine vya Usalama na Mataifa mengine katika kupambana na matishio ya kiusalama yakiwemo ugaidi, uharamia na biashara haramu ya dawa za kulevya. Aidha, JWTZ limeshiriki katika Operesheni Amboni

Mkoani Tanga iliyoanza mwezi Mei, 2016 na kufungwa rasmi mwezi Desemba, 2016 ambapo wahalifu hao walidhibitiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imekuwa mstari wa mbele katika kutekeleza agizo la Mheshimiwa Rais la kutatua tatizo la uhaba wa madawati katika shule za Serikali za msingi na sekondari. Aidha, kupitia taasisi za Mashirika yake Wizara ilipewa jukumu la kutengeneza madawati 60,000. Kazi hiyo ilifanyika kwa ufanisi na weledi mkubwa. Katika zoezi hilo, JKT ilichangia madawati ya ziada 5,005. Wizara kupitia JWTZ imesimamia ujenzi wa shule ya Sekondari Ihumwa iliyopo Dodoma na inaendelea kusimamia ujenzi wa shule ya Sekondari ya Ihungo iliyopo Kagera iliyoathirika na tetemeko la ardhi mwaka 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa kwa vijana yameendelea kutolewa kwa vijana wa kujitolea na wale wa mujibu wa sheria kwa lengo la kujenga uzalendo, ukakamavu, maadili mema, utaifa pamoja na kutoa stadi za kazi. Katika mwaka 2016/2017, Jeshi la Kujenga Taifa limefanikiwa kuendesha mafunzo kwa vijana 14,748 kwa mujibu wa sheria, ambapo kati yao Wavulana walikuwa 10,863 na Wasichana 3,885 waliohitimu Kidato cha Sita mwaka 2016. Idadi hiyo ni sawa na asilimia 73.7 ya lengo la kuchukua vijana 20,000. Pia, JKT limefanikiwa kuchukua vijana wapya wa kujitolea 9,848 kwa ajili ya mafunzo, kati yao Wavulana ni 7,154 na Wasichana ni 2,694. Idadi hiyo ni sawa na asilimia 98.5 ya lengo la kuchukua vijana 10,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa kuandikisha vijana wa kujitolea kwa ajili ya kujiunga na mafunzo hayo, hutakiwa kujaza na kusaini fomu maalum ya mkataba yenye masharti kwamba kijana awe tayari kurudi nyumbani mara amalizapo mkataba wake. Pamoja na dhamira ya Serikali ya kutoa ajira kwa vijana wanaohitimu mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa, siyo vijana wote wanaohitimu mafunzo hayo wanaweza kupata ajira katika vyombo vya Ulinzi, Usalama au Taasisi zake. Hivyo, napenda kutoa rai kwa vijana wanaopata mafunzo ya JKT wazingatie maarifa na ujuzi

wanaoupata hususan wa stadi za kazi ili waweze kujiajiri na kuweza kujitegemea na hata kuajiri wao wenyewe.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi ya shughuli za maendeleo; fedha zilizopokelewa hadi mwezi Machi katika mwaka wa fedha 2016/2017, kwa Mafungu yote matatu ilikuwa sawa na takribani asilimia 14.5 ya bajeti iliyoidhinishwa. Wizara imeweza kutekeleza miradi ifuatayo:-

Kukamilisha mradi wa ujenzi wa nyumba 6,064 awamu ya kwanza kwa ajili ya makazi ya Wanajeshi; kulipia sehemu ya madeni ya kimkataba; kukarabati majengo pamoja na kuboresha mazingira ya kufanyia kazi na makazi katika makambi na vikosi vya JKT; ukarabati wa zana za ulinzi wa anga; ujenzi wa bwalo la Maafisa katika shule ya Kijeshi ya Ulinzi wa Anga Tanga; kuweka umeme katika baadhi ya minara ya mawasiliano salama Jeshini katika mikoa ya Morogoro na Dodoma. Aidha, kupitia ushirikiano baina ya Tanzania na China, ujenzi wa uwanja wa ndege vita Ngerengere umekamilika na kituo cha mafunzo maalum ya kijeshi Mapinga Bagamoyo ili kukabiliana na matishio mapya ya kiusalama kinaendelea kujengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa nyumba, maghala na miundombinu mbalimbali. Wizara imeendelea kutekeleza mradi wa ujenzi wa nyumba 6,064 ambapo katika mwaka wa fedha 2016/2017, huduma za maji na umeme katika nyumba hizo zimepelekwa na hivyo kuwezesha kuanza kutumika kwa nyumba hizo katika kambi zilizopo Mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Kagera, Kaskazini Pemba, Kigoma, Morogoro, Pwani na Tanga. Juhudi za kupata fedha za kukamilisha ujenzi wa nyumba 3,936 ili kufikia lengo la ujenzi wa nyumba 10,000 katika kambi zilizobaki zinaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, Wizara inaendelea na ujenzi wa maghala ya kuhifadhia milipuko, ambapo maghala 12 yamejengwa Makambako-Njombe na maghala Sita yamejengwa Dunga- Zanzibar. Aidha, katika kipindi hicho, upanuzi wa uwanja wa ndege vita Ngerengere ulikamilika na kuzinduliwa rasmi na Rais na Amiri Jeshi Mkuu

Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli tarehe 6 Machi, 2017. Mradi wa ujenzi wa kituo maalum cha mafunzo *Comprehensive Training Centre* nao unaendelea vizuri na hadi sasa ujenzi umefikia asilimia 30.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ununuzi wa zana na vifaa vya kijeshi; katika juhudi za kuliongezea uwezo wa kiutendaji na kuimarisha mazingira ya kufanyia kazi Serikali imeendelea kulipatia Jeshi zana na vifaa mbalimbali. Katika mwaka wa fedha wa 2016/2017, Jeshi limepokea zana na vifaa mbalimbali kwa ajili ya ulinzi wa nchi kavu, anga na majini. Kupatikana kwa zana na vifaa hivyo kumeongeza uwezo wa Jeshi kutekeleza majukumu yake ya msingi ya kiulinzi. Mpango wa ununuzi wa zana na vifaa vya kisasa na bora pamoja na mafunzo ya namna ya kutumia na kutunza zana na vifaa hivyo utakuwa endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Uzalishaji Mali la SUMAJKT. SUMAJKT limeendelea kutekeleza shughuli zake katika misingi ya kibiashara kupitia Kampuni Tanzu, Idara na miradi yake ifuatayo:-

Kampuni ya Ulinzi SUMA JKT *Guard Limited;* Kampuni ya Ujenzi *National Service Construction Department*; Kampuni ya Ubia; Idara ya Kilimo, Uvuvi na Mifugo; Idara ya Viwanda na mradi wa matrekta. SUMA JKT kupitia kampuni yake ya Ulinzi SUMA JKT *Guard Limited,* inaendesha shughuli za ulinzi katika Ofisi za Serikali, Mashirika ya Umma na sekta binafsi, zikiwemo Benki na Migodi. Kwa mwaka 2016/2017, imefanikiwa kuongeza huduma za ulinzi kwa wafuatao:-

Wakala wa Serikali Mtandao, Air Tanzania *Corporation Limited* Julius Nyerere *International Airport*, Mamlaka ya Chakula na Dawa, *Local Authority Pension Fund*, Wakala wa Ndege za Serikali, *Medical Stores Department, Tanzania Insurance Regulatory Authority*, Wakala wa Nishati Vijijini, *TANROADS*, *Procurement and Supplies Profession Technician* Board, Tanzania *Forests Services*, *Bank of Africa*, *BOT* –Dodoma, *FINCA, DCB Bank*, Dar es Salaam *Maritine Institute* na *KUDU Resources Limited.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kampuni SUMA *Guard* imetoa mchango kwa Serikali kwa kupunguza tatizo la ajira nchini kwa kuajiri vijana 4,150. Kupitia Bunge lako Tukufu natoa rai kwa Kampuni zinazodaiwa kulipa madeni yao mapema iwezekanavyo ili kuwezesha *SUMA JKT Seeds Company Limited* kufikia malengo yake na kuendelea kuzalisha mbegu bora kwa faida ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Mzinga; katika mwaka wa fedha wa 2016/2017, Shirika hili limeendelea na utekelezaji wa majukumu yake ya msingi ya kufanya utafiti wa kuwezesha uzalishaji wa mazao ya kijeshi kwa kutumia malighafi zinazopatikana hapa nchini na kufanya matengenezo na ukarabati wa zana za Kijeshi. Pamoja na changamoto ya upatikanaji wa fedha za maendeleo, shirika limeendelea kupanua uzalishaji wa mazao ya Kijeshi kwa gharama nafuu ikilinganishwa na kuagiza bidhaa hizo kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Mweyekiti, katika kutekeleza azma ya Serikali ya kuwa na uchumi wa viwanda, na pia kukabiliana na changamoto za upatikaji wa malighafi za kistratejia na mtaji, shirika limeendelea kuchukua hatua za kujiimarisha ikiwa ni pamoja na kuongeza kasi ya kutekeleza mpango mkakati wa kipindi cha miaka mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango mkakati huo unakusudia kupanua wigo wa uzalishaji wa mazao ya Kijeshi, kuongeza wigo wa shughuli za Shirika kwa kuanzisha viwanda vipya vya kutengeneza baruti na kupanua mradi wa kutengeneza mashine ndogondogo kwa ajili ya kuwawezesha wajasiriamali wadogo wadogo na wa kati kufanya uchakataji na kuongezea thamani ya mazao ya kilimo na misitu. Vilevile Shirika limekusudia kuboresha karakana ya utengenezaji samani na kuiimarisha kampuni tanzu ya Mzinga *Holding Company Limited* kwa kuipatia mtaji na vitendea kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Nyumbu; katika kipindi cha mwaka wa fedha 2016/2017, pamoja na

kutekeleza majukumu yake ya msingi ya utafiti na uhawilishaji wa teknolojia, shirika limechangia kupunguza gharama kwa JWTZ kwa kufanya matengenezo ya zana za kijeshi kwa gharama nafuu ambazo zingepaswa kusafirishwa kwenda nje kwa matengenezo na kuzalisha vipuli vya magari, mitambo na mashine mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Shirika limekuwa likihusika na matayarisho ya zana, mitambo na vitendea kazi kwa vikundi vinavyokwenda katika operesheni za ulinzi wa amani. Aidha, shirika limeshiriki katika zoezi la Kitaifa la utengenezaji wa madawati kwa ajili ya shule za msingi na sekondari za Serikali. Katika hatua nyingine, Shirika limetengeza vitanda 652 kwa ajili ya Maafisa na Askari waliohamia Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika pia lilifanikiwa kufanya ukarabati mdogo wa nyumba za makazi na mitambo ya karakana ya shirika, kununua vifaa vya TEHAMA na kukarabati mfumo wa umeme kiwandani. Vilevile, Shirika limeendelea kutekeleza shughuli zake za kufanya utafiti katika teknolojia ya magari na mitambo ya kijeshi, kuimarisha na kuongeza uwezo wa kuhawilisha teknolojia mbalimbali za utafiti na kukarabati miundombinu ya shirika. Shirika limeandaa mpango wa maendeleo wa miaka kumi wenye lengo la kuliimarisha na kulirejeshea shirika hadhi yake ili liweze kushiriki katika maendeleo ya uchumi wa viwanda nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtandao wa mawasiliano salama Jeshini; Wizara imeendelea kutekeleza Mradi wa Mawasiliano Salama Jeshini ambapo hadi kufikia Machi, 2017 jumla ya minara 132 ilikuwa imesimikwa Tanzania Bara na Visiwani. Mawasiliano kupitia mtandao huo yanapatikana katika maeneo ya Zanzibar, Pwani, Dar es Salaam na baadhi ya maeneo ya Morogoro. Kazi ya kuunganisha maeneo mengine ya nchi ikiwemo Mkoa wa Dodoma kwenye mtandao huo inaendelea. Aidha, uunganishaji wa mawasiliano haya salama katika vikosi vyote Jeshini utakamilishwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kudhibiti uvamizi wa maeneo ya Jeshi, upimaji na ulipaji wa fidia. Katika mwaka wa fedha 2016/2017, Wizara haijaweza kupima na kulipa fidia wananchi kwa maeneo yaliyotwaliwa kwa matumizi ya Jeshi kama ilivyopangwa kutokana na upatikanaji mdogo wa fedha za maendeleo. Aidha, kwa lengo la kudhibiti uvamizi zaidi katika maeneo ya Jeshi Wizara kupitia vikosi, vyuo na shule za Kijeshi, imeendelea kupanda miti na kuweka mabango kuzunguka maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto za utekelezaji wa mpango na bajeti katika mwaka wa fedha 2016/2017. Katika mwaka wa fedha 2 016/2017, Wizara iliidhinishiwa jumla ya sh.248,000,000,000 kwa ajili ya shughuli za maendeleo na hadi kufikia mwezi Machi, 2017 kiasi kilichotolewa ni sh.35,900,000,000 sawa na asilimia 14.5 ya bajeti hiyo. Kutokana na kiwango cha fedha kilichopokelewa, Wizara imeweza kulipa sehemu ya madeni ya kimkataba na kuingiza huduma za maji na umeme katika baadhi ya nyumba 6,064 pamoja na ukarabati wa miundombinu katika baadhi ya kambi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtiririko wa fedha kwa ajili ya matumizi mengineyo katika mwaka wa fedha 2016/2017, umeleta changamoto katika kutekeleza kikamilifu mpango kazi kulipia kwa wakati huduma na mahitaji muhimu kwa Wanajeshi, vijana wanaohudhuria mafunzo ya JKT na Watumishi wa Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango na Mwelekeo wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Mpango na Mwelekeo wa bajeti wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa katika mwaka wa fedha 2017/2018 unakusudia kuimarisha utendaji kazi na kuongeza ufanisi wa Jeshi katika kutekeleza majukumu yake kulingana na dira na dhima ya Wizara, Ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015, mpango wa pili wa Taifa wa maendeleo na maelekezo ya Mheshimiwa Rais wakati wa kuzindua Bunge la 11 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 20 Novemba,

2015. Hivyo, Wizara itaendelea kutekeleza majukumu yake muhimu katika maeneo yafuatayo:-

(i) Kuliongezea uwezo Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania utendaji kivita kwa kulipatia vifaa na zana bora pamoja na kutoa mafunzo stahiki kwa Wanajeshi dhidi ya adui wa ndani na nje;

(ii) Kuimarisha mazingira mazuri yakufanyia kazi, makazi na kuimarisha upatikanaji wa huduma, stahili na mahitaji ya msingi kwa Wanajeshi na Watumishi raia;

(iii) Kuwapatia vijana wa Kitanzania mafunzo ya uzalendo, ukakamavu, umoja wa kitaifa na stadi za kazi, utafiti na uhawilishaji wa teknolojia kwa madhumuni ya kuzalisha bidhaa na huduma kwa ajili ya matumzi ya kijeshi na kiraia; na

(iv) Kuimarisha ushirikiano na nchi nyingine Duniani katika nyanja za Kijeshi na kiulinzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shukrani; kabla sijahitimisha hotuba yangu naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa wale wote walioniwezesha kufanikisha na kutekeleza jukumu la kuongoza Wizara ya Ulinzi na Jeshi la kujenga Taifa. Aidha, napenda kutoa shukrani kwa wale wote waliotoa michango iliyosaidia kufanikisha maandalizi ya makadirio ya matumizi ya fedha ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti naomba kutoa shukrani za pekee kwa wafanyakazi wenzangu wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa nikianzia na Katibu Mkuu Dkt. Frolence Turuka; Naibu Katibu Mkuu Bi. Immaculate Ngwale; Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi ,Jenerali Venance Mabeyo; Mnadhimu Mkuu Luteni Jenerali James Mwakibolwa; Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa, Meja Jenerali Michael Lisamuyo; Wakuu wa Kamandi, Wakuu wa Mashirika, Maafisa, Askari na Watumishi wa Umma. Aidha, naishukuru Kamati ya Wizara iliyoandaa hotuba hii kwa ushirikiano walionipatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naomba niwashukuru wapigakura wangu wa Jimbo la Kwahani, kwa ushirikiano wao walionipa katika mwaka wa 2016/2017. Ni matumaini yangu kuwa tutaendelea kushirikiana zaidi kwa manufaa ya Jimbo letu na Taifa kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Serikali naomba pia kutoa shukrani zangu za dhati kwa Serikali za nchi mbalimbali, Mashirika na Wahisani kwa ushirikiano wao na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Wahisani hao ni pamoja na Jamhuri ya Watu wa China, Ujerumani, Canada, Marekani, Ufaransa, India na Uturuki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, tunazishukuru nchi rafiki kwa ushirikiano wao katika shughuli zetu mbalimbali za kiulinzi. Nchi hizo ni pamoja na Afrika Kusini, Bangladesh, DRC, Ghana, Falme za Kiarabu, Indonesia, Misri, Nigeria, Uingereza, Urusi na nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika. Nchi rafiki na wahisani wamekuwa wakishirikiana na Jeshi katika mafunzo, mazoezi ya Kijeshi, na kuimarisha miundombinu ya mawasiliano, makazi na tiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makadirio ya mapato na matumizi ya bajeti ya mwaka 2017/2018. Makadirio ya mapato. Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na taasisi zake haina chanzo cha uhakika cha mapato kinachoweza kuingia kwa kiasi kikubwa katika ukusanyaji wa maduhuli ikizingatiwa majukumu ya msingi ya Wizara hii. Chanzo kikuu cha mapato ni makusanyo ya mauzo yanayotokana na nyaraka za zabuni, suala ambalo kwa sasa linashughulikiwa pia na Wakala wa Serikali wa Ununuzi na Ugavi *(GPSA)* kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2017/2018, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa inakadiria kukusanya jumla ya sh.69,706,000 katika mchanganuo ufuatao:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 38 – NGOME -

Sh.15,601,000/= Fungu 39 JKT Sh.54,003,000/= na Fungu 57 Wizara Sh.102,000/=. Matumizi ya kawaida na maendeleo, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa inaomba kuidhinishiwa jumla ya Sh.1,725,517,816,225 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na matumizi ya maendeleo ili iweze kutekeleza majukumu yake katika mwaka wa fedha wa 2017/2018. Kati ya fedha hizo Sh.1,506,517,816,925 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Sh.219,000,000,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo. Mchanganuo kwa kila Fungu ni ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 38 - Ngome Matumizi ya Kawaida ni Sh.1,205,244,289,563; Matumizi ya Maendeleo Sh.8,000,000,000, jumla Sh. 1,213,244,289,563. Fungu 39 - JKT, matumizi ya kawaida Sh.283,362,530,783; matumizi ya maendeleo ni shilingi 6,000,000,000; jumla ni Sh.289,362,530,783. Fungu 57 - Wizara; Matumizi ya Kawaida ni sh.17,910,996,579; Matumizi ya maendeleo Sh.205,000,000,000. Jumla Sh. 222,910,996,579.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.*(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Hoja imeungwa mkono.

**HOTUBA YA WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA MHESHIMIWA DKT. HUSSEIN ALI MWINYI (MB) AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2017/2018 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**UTANGULIZI**

**1.** ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea, kujadili na

kupitisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2017/18.

**2.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwanza napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, kwa kuniwezesha kuwasilisha hotuba yangu ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2017/18 mbele ya Bunge lako Tukufu. Pili, namshukuru kwa dhati Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu, **Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli,** kwa kuniamini kuendelea kuiongoza Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Kwa namna ya pekee nachukua fursa hii kuungana na watanzania kwa ujumla kumpongeza Mhe. Rais kwa kuchaguliwa kwake kwa kishindo kuwa Mwenyekiti wa Tano wa Chama cha Mapinduzi kufuatia Uchaguzi wa Viongozi wa Chama uliofanyika tarehe 23 Julai, 2016 mjini Dodoma. Watanzania wana matumaini makubwa na safu ya uongozi wa Chama chini ya Mwenyekiti wake ambaye pia ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu. Vilevile, napenda kuwashukuru Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania **Mhe. Samia Suluhu Hassan** na Waziri Mkuu, **Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb)** kwa miongozo na maelekezo wanayonipatia katika kutekeleza majukumu ya Wizara yangu.

**3.** ***Mheshimiwa Spika,*** ahadi yangu kwa Mhe. Rais, kwenu Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wenzangu ni kuwa, nitaendelea kutekeleza majukumu niliyokabidhiwa kwa uadilifu na uaminifu mkubwa. Uongozi wa Awamu ya Tano chini ya Mhe. Rais na wasaidizi wake wakuu katika kipindi cha takriban mwaka mmoja na nusu tangu uingie madarakani umekuwa ni mfano wa kuigwa na umeweka historia ya kipekee nchini kwa kuendelea kutekeleza kwa kasi na ufanisi mkubwa ahadi zilizomo kwenye Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2015.

**4.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba nitumie fursa hii pia kumpongeza Jenerali Venance Salvatory Mabeyo kwa kuteuliwa kuwa Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi. Aidha,

nimpongeze Luteni Jenerali James Aloyce Mwakibolwa kwa kuteuliwa kuwa Mnadhimu Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi. Kipekee, napenda kumshukuru Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi Mstaafu Jenerali Davis Adolf Mwamunyange kwa utumishi wake uliotukuka na kwa namna tulivyoshirikiana katika kuliongoza Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania kwa mafanikio makubwa.

**5.** ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kukupongeza wewe, Spika wa Bunge hili Mhe. Job Yustino Ndugai (Mb), Naibu Spika Mhe. Dkt. Tulia Ackson (Mb) pamoja na Wenyeviti wa Bunge kwa kuendesha vizuri shughuli za Bunge. Namuomba Mwenyezi Mungu azidi kuwapa maarifa, hekima, busara na nguvu za kuendelea kuongoza Bunge hili katika kutekeleza majukumu yake mazito na nyeti.

**6.** ***Mheshimiwa Spika***, vile vile, napenda kutumia nafasi hii kuwashukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama Mhe. Balozi Adadi Rajabu (Mb), Makamu Mwenyekiti Mhe. Kanali Mstaafu Ally Khamis Masoud (Mb) na Wajumbe wote wa Kamati hii Tukufu kwa kuendelea kunipa ushirikiano mkubwa katika kuiongoza Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Kamati hii imetupatia ushauri mzuri wakati wa kuchambua mapendekezo ya makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara yangu kwa mwaka 2017/18. Maoni na mapendekezo yao yametusaidia sana katika kuandaa mpango bajeti hii.

**7.** ***Mheshimiwa Spika***, nachukua fursa hii kuwapongeza Waheshimiwa wafuatao: Alhaji Abdallah Majura Bulembo (Mb.), Prof. Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi (Mb.), Anne Killango Malecela (Mb.), Salma Rashidi Kikwete (Mb.), Dkt. Mch. Getrude Lwakatare (Mb.) na Catherine Ruge (Mb) kwa kuteuliwa kuwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri la Muungano wa Tanzania na Mhe. Juma Ali Juma (Mb.) kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Dimani. Aidha, nampongeza Prof. Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi (Mb.) kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Katiba na Sheria.

**8.** ***Mheshimiwa Spika***, nitumie fursa hii kutoa salamu za

pole kwako Mhe. Spika, Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote kwa kuondokewa na mpendwa wetu Mhe. Samweli John Sitta Mbunge Mstaafu wa Jimbo la Urambo Mashariki na Spika wa Bunge la Tisa la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pia, natoa pole kwako Mhe. Spika kufuatia kifo cha Mhe. Hafidh Ally Tahir aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Dimani, Zanzibar kilichotokea tarehe 11 Novemba, 2016 na Mhe. Dkt. Elly Marko Macha aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum kilichotokea tarehe 31 Machi, 2017.

**9.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninaungana na wenzangu wote waliotangulia kuwapa pole wale waliopatwa na majanga, pamoja na kufiwa na ndugu, jamaa na wapendwa wao katika matukio mbalimbali yaliyotokea nchini yakiwemo tetemeko la Ardhi lililotokea Kagera tarehe 10 Septemba, 2016 na ajali mbalimbali za vyombo vya usafiri yakiwemo mabasi ya abiria. Kwa namna ya pekee natumia fursa hii kuwapa pole wazazi, walimu na watanzania wote kutokana na vifo vya wanafunzi 32, walimu 2 na dereva wa Shule ya Msingi Lucky Vincent ya mjini Arusha vilivyotokana na ajali ya basi iliyotokea tarehe 06 Mei, 2017 katika eneo la Rhotia Wilayani Karatu. Naomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi na kuwajalia majeruhi wote kupona haraka na kurejea katika masomo yao.

**10.** ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya maelezo hayo ya utangulizi, napenda sasa kuchukua fursa hii kuwasilisha hotuba yangu ambayo kiujumla imejikita katika maeneo makuu yafuatayo: Malengo na majukumu ya Wizara; Hali ya Usalama na Mipaka katika mwaka 2016/17; Utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya mwaka 2016/17 na Mpango na Makadirio ya Bajeti kwa mwaka 2017/18.

## MALENGO NA MAJUKUMU YA WIZARA

**11.** ***Mheshimiwa Spika,*** kama ilivyo katika **Dira** ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Wizara imeendelea kuwa Taasisi iliyotukuka ya kulinda na kudumisha amani na usalama

wa Taifa letu. Vivyo hivyo, **Dhima** ya Wizara ni kuendelea kulinda Jamhuri ya Muungano wa Tanzania dhidi ya adui wa aina yoyote kutoka ndani au nje ya nchi na kuhakikisha kuwa mamlaka na maslahi ya nchi yetu yanakuwa salama.

**12.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kufanikisha Dhima yake, malengo ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa yameendelea kuwa kama ifuatavyo:

i. Kuwa na Jeshi dogo na mahiri la Ulinzi wa Nchi lenye weledi, zana bora, vifaa vya kisasa na mawasiliano salama;

ii. Kuendelea kuwajengea vijana wa kitanzania moyo wa uzalendo, ukakamavu, maadili mema, utaifa na kuwafundisha stadi za kazi;

iii. Kuendeleza utafiti na kujenga uwezo katika teknolojia za kijeshi;

iv. Kuimarisha Jeshi la Akiba;

v. Kusaidia Mamlaka za Kiraia katika kukabiliana na athari za majanga na matukio yanayoweza kuhatarisha maisha, amani na utulivu nchini; na

vi. Kudumisha amani na usalama kwa kushirikiana na nchi nyingine duniani.

**13.** ***Mheshimiwa Spika***, ili kufikia malengo yaliyoainishwa, Wizara itaendelea kusimamia utekelezaji wa majukumu yafuatayo:

i. Kuandikisha wanajeshi wenye sifa stahiki kwa lengo la kuwa na Jeshi dogo na mahiri kwa ajili ya Ulinzi wa Taifa na kuwapatia mafunzo na mazoezi ya kinadharia na kivitendo;

ii. Kuwapatia wanajeshi makazi, zana, vifaa na

vitendea kazi bora na vya kisasa pamoja na kusimamia matumizi na matunzo yake;

iii. Kuendesha mafunzo na mazoezi ya Mgambo;

iv. Kuboresha mitaala ya mafunzo ya JKT kwa vijana ili kuwaandaa kuwa wakakamavu, wenye nidhamu na kuwajengea moyo wa uzalendo na mshikamano wa kitaifa na kutekeleza shughuli za kujitegemea;

v. Kuendeleza utafiti na uhawilishaji wa teknolojia za kijeshi kupitia Mashirika ya Mzinga na Nyumbu;

vi. Kuwezesha Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Kujenga Taifa (SUMAJKT) kuwa na tija na faida itakayochangia katika uendeshaji wa shughuli za Jeshi la Kujenga Taifa;

vii. Kushirikiana na Mamlaka za Kiraia katika kukabiliana na majanga na dharura za kitaifa pale inapohitajika; na

viii. Kuimarisha ushirikiano na nchi nyingine katika nyanja za kijeshi na kiulinzi kupitia Jumuiya za Kimataifa, Kikanda na ushirikiano na nchi moja moja.

## UTEKELEZAJI WA MAONI NA USHAURI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA

**14.** ***Mheshimiwa Spika,*** wakati Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ilipokaa na kujadili Makadirio ya Mapato, Mpango na Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa fedha 2016/17 ilitoa maoni, ushauri na maelekezo kadhaa kwa Wizara hii yaliyolenga kuboresha utendaji na utekelezaji wa majukumu yake. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa maoni, ushauri na maelekezo yaliyotolewa yamefanyiwa kazi na hoja mbalimbali zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge wakati wa mjadala huo pia zimezingatiwa katika mpango na bajeti ya mwaka wa fedha 2017/18 ninayowasilisha leo hapa Bungeni.

## HALI YA ULINZI NA USALAMA WA MIPAKA YA NCHI

**15.** ***Mheshimiwa Spika,*** hali ya Ulinzi na Usalama wa mipaka ya nchi yetu kwa ujumla ni shwari. Hata hivyo, kumekuwa na changamoto ya kutotengamaa kwa hali ya usalama kwenye baadhi ya nchi za Ukanda wa Afrika Mashariki, Maziwa Makuu na Pembe ya Afrika ikiwa ni pamoja na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Burundi, Somalia na Sudan Kusini. Aidha, uwepo wa hali ya matishio ya ugaidi wa kimataifa umevilazimu vyombo vya Ulinzi na Usalama kwa kushirikiana na nchi jirani na raia wake kuendelea kuwa katika hali ya tahadhari na umakini ili endapo kutajitokeza dalili yoyote inayotishia usalama, hatua stahiki ziweze kuchukuliwa haraka iwezekanavyo.

**16.** ***Mheshimiwa Spika,*** hali ya mipaka ya nchi yetu yenye jumla ya urefu wa kilomita 5,390 ambayo inahusisha eneo la nchi kavu na eneo la maji imeendelea kuwa shwari. Vyombo vyetu vya Ulinzi na Usalama kwa kushirikiana na wananchi vimeendeleza jitihada za kuimarisha usalama wa mipaka hiyo hatua ambayo imechangia kudhibiti na kupunguza matukio na vitendo vyenye kutishia usalama kama vile, ugaidi, biashara ya dawa za kulevya, usafirishaji haramu wa binadamu, uhamiaji haramu na ujambazi. Hali ya mipaka yetu katika kipindi kinachopitiwa imekuwa kama ifuatavyo:

*Mpaka wa Mashariki*

**17.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mpaka huu ambao una urefu wa kilomita 1,413 nchi yetu inapakana na Bahari ya Hindi na pia nchi za Kenya, Visiwa vya Ushelisheli, Komoro na Msumbiji. Kwa ujumla hali ya usalama katika mpaka huu imeendelea kuwa shwari kutokana na kudhibitiwa kwa vitendo vya uharamia ambapo kumeambatana na kuongezeka kwa doria katika Bahari ya Hindi.

*Mpaka wa Kaskazini*

**18.** ***Mheshimiwa Spika***, kwenye eneo la mpaka huu Tanzania imepakana na nchi za Kenya na Uganda. Hali ya

usalama katika mpaka huu wenye urefu wa kilomita 1,221 kwa ujumla ilikuwa shwari licha ya tatizo la uingiaji wa wahamiaji haramu kutoka nchi za Ethiopia, Eritrea na Somalia ambao hujipenyeza kuingia nchini wakiwa safarini kuelekea maeneo ya Kusini mwa Afrika

*Mpaka wa Magharibi*

**19.** ***Mheshimiwa Spika,*** mpaka huu wenye urefu wa kilomita 1,220 ambako Tanzania imepakana na nchi za Burundi, Rwanda na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) pamoja na kuwa shwari kwa ujumla umekuwa pia na changamoto kadhaa. Mojawapo ya changamoto hizo ni kutokukamilika kwa mazungumzo ya upatanishi ya pande zinazosigana nchini Burundi hali inayosababisha hali ya kiusalama kutotengamaa. Aidha, uwepo wa vikundi vya waasi vyenye silaha vinavyoendesha harakati za kimapigano dhidi ya Majeshi ya DRC na Majeshi ya Umoja wa Mataifa (MONUSCO) ambako kunasababisha ongezeko la wakimbizi hali ambayo inahatarisha usalama kwenye eneo la mpaka huo.

*Mpaka wa Kusini*

**20.** ***Mheshimiwa Spika***, kwenye mpaka wa Kusini ambao una urefu wa kilomita 1,536 Tanzania inapakana na nchi za Msumbiji, Malawi na Zambia. Pamoja na hatua zinazoendelea za usuluhishi wa mgogoro wa mpaka uliopo baina ya Tanzania na Malawi, kwa ujumla hali ya mpaka huu imeendelea kuwa shwari na wananchi wanaendelea na shughuli zao kama kawaida.

## UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA MWAKA 2016/17

**21.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2016/17 Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ilikadiria kukusanya mapato ya jumla ya **shilingi 68,406,000.00** kupitia mafungu yake matatu ya 38-NGOME, 39-JKT na 57-Wizara. Kufikia mwezi Aprili, 2017 mafungu hayo yalifanikiwa kukusanya mapato ya jumla ya **shilingi 43,516,561.80** sawa na **asilimia 63.6** ya

makadirio. Chanzo kikuu cha makusanyo hayo ni mauzo ya nyaraka za zabuni ambayo yameendelea kupungua kwa kuwa utangazaji wa zabuni kwa sasa unafanywa pia na Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini (GPSA).

**22.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2016/17, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa iliidhinishiwa na Bunge lako Tukufu jumla ya **shilingi 1,736,578,102,510.00** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo kwa mafungu yake Matatu. Kati ya fedha hizo, bajeti ya kawaida inayojumuisha mishahara na matumizi mengineyo ni **shilingi 1,488,578,102,510.00** na bajeti kwa ajili ya shughuli za maendeleo ni **shilingi 248,000,000,000.00.** Mchanganuo wa bajeti kwa kila fungu umeoneshwa katika Jedwali Na. 1

**Jedwali Na. 1:** Mchanganuo wa Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2016/17

| Fungu | Matumizi | | |
|---|---|---|---|
| | **Kawaida** | **Maendeleo** | **Jumla** |
| NGOME | 1,187,543,710,510 | 10,000,000,000 | 1,197,543,710,510 |
| JKT | 282,034,214,000 | 8,000,000,000 | 290,034,214,000 |
| Wizara | 19,000,178,000 | 230,000,000,000 | 249,000,178,000 |
| **Jumla** | **1,488,578,102,510** | **248,000,000,000** | **1,736,578,102,510** |

**23.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia mwezi Aprili, 2017 Wizara ilikuwa imepokea jumla ya **shilingi 1,199,292,622,613.00** sawa na **asilimia 69.1** ya bajeti yake yote. Kati ya fedha hizo **shilingi 1,163,392,622,613.00** sawa na asilimia 78.2 ya bajeti iliyoidhinishwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida zilipokelewa. Fedha hizo zimetumika kutekeleza majukumu na mipango ya kazi, kulipia mishahara na posho mbalimbali muhimu ikiwa ni pamoja na kugharamia huduma mbalimbali zikiwemo stahili za Wanajeshi na Watumishi wa Umma, uendeshaji wa Ofisi na kulipa madeni ya Wazabuni.

**24.** ***Mheshimiwa Spika***, kwa upande wa matumizi ya maendeleo, fedha zilizopokelewa ni shilingi **35,900,000,000.00**

sawa na **asilimia 14.5** ya fedha zote zilizoidhinishwa kwa ajili ya matumizi hayo. Fedha hizo zimetumika kulipia madeni ya kimikataba, ujenzi wa miundombinu ya maji safi na maji taka vikosini, kuingiza huduma ya maji na umeme katika baadhi ya nyumba 6,064 zilizojengwa kwa makazi ya Wanajeshi na uingizaji umeme katika minara ya mawasiliano iliyosimikwa katika mikoa ya Morogoro na Dodoma, kuendeleza ukarabati wa maghala ya silaha na milipuko na ukarabati wa kambi mpya tano za Milundikwa na Luwa (Rukwa), Itaka (Songwe), Mpwapwa (Dodoma) na Makuyuni (Arusha). Mchanganuo wa fedha zilizopokewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo hadi mwezi Aprili, 2017 umeoneshwa katika **Kiambatisho Na. 1**

**25.** ***Mheshimiwa Spika*,** kwa kuangalia mchanganuo wa fedha zilizopokelewa hadi kufikia mwezi Aprili, 2017, mwenendo wa upatikanaji wa fedha kwa ajili ya matumizi ya kawaida kwa mafungu yote matatu ya Wizara hususan fedha za mishahara na chakula kwa wanajeshi katika kipindi hicho ulikuwa ni wa kuridhisha. Fedha kwa ajili ya mishahara na marupurupu zilipokelewa kulingana na makisio ya bajeti. Kwa upande wa fedha za shughuli za maendeleo, fedha zilizopokelewa hazikuweza kukidhi mahitaji na hivyo kuathiri utekelezaji wa shughuli za maendeleo ikiwa ni pamoja na ulipaji wa madeni ya kimikataba.

## MAFANIKIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2016/17

### Matumizi ya Shughuli za Kawaida

**26.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2016/17, Wizara imefanikiwa kulipia mahitaji na huduma muhimu kwa maafisa, askari, vijana wa Jeshi la Kujenga Taifa na watumishi wa umma. Aidha, kwa kutumia fedha hizi majukumu mbalimbali ya kiulinzi yaliyotekelezwa ni pamoja na: kufanya mafunzo na mazoezi ya kijeshi, mafunzo ya Mgambo, ushirikiano wa kiulinzi na kijeshi na nchi nyingine,

ushirikiano na Jumuiya za Kikanda na Kimataifa, ushirikiano wa Jeshi na Mamlaka za Kiraia na Mafunzo ya JKT.

*Mafunzo na Mazoezi ya Kijeshi*

**27.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2016/17 Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania, limeendelea kutoa mafunzo na mazoezi kwa wanajeshi wake ili kujiimarisha kiulinzi. Jeshi letu lilifanikiwa kufanya mazoezi mbalimbali ya kimataifa na ya ndani yafuatayo: **"Ex - Eastern Accord"** lililofanyika Tanzania kuanzia tarehe 10 – 22 Julai, 2016 chini ya **USARAF**, "**Ex - Amphibious Landing"** lililofanyika Bagamoyo kuanzia tarehe 19 Agosti, 2016 hadi tarehe 5 Septemba, 2016 ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya sherehe za miaka 52 ya JWTZ, **"Ex - Ushirikiano Imara"** lililofanyika Mombasa nchini Kenya kuanzia tarehe 17 - 19 Novemba, 2016. Aidha, Jeshi liliendelea kutoa mafunzo kwa Maafisa na Askari kwenye vyuo, shule na vituo mbalimbali vya mafunzo kwa wanajeshi katika ngazi mbalimbali ndani na nje ya nchi. Mazoezi na mafunzo haya yalilenga kuwajengea wanajeshi wetu uwezo, weledi na umahiri wa kiutendaji.

*Mafunzo ya Mgambo*

**28.** ***Mheshimiwa Spika,*** mafunzo ya Mgambo kwa wananchi yameendelea kutolewa na Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania. Katika kipindi cha mwaka 2016/17 JWTZ kwa kushirikiana na vyombo vya Usalama limeendesha mafunzo katika ngazi mbalimbali ambapo jumla ya wananchi 13,997 walifuzu. Hili ni ongezeko la wahitimu 7,241 sawa na asilimia 51.7 ikilinganishwa na wananchi 6,756 waliopata mafunzo hayo mwaka 2015/16. Naendelea kutoa wito kwa Viongozi wa ngazi mbalimbali kuhamasisha wananchi kushiriki katika mafunzo ya Mgambo. Kwa maagizo ya Mhe. Rais, jumla ya askari Mgambo 48 walioshiriki katika **"Ex - Onesha Uwezo wa Medani"** lililofanyika katika Mkoa wa Arusha na **"Ex - Amphibious Landing**" lililofanyika katika Mikoa ya Dar es Salaam na Pwani waliandikishwa katika Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania.

*Huduma za Afya na Tiba*

**29.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi husika, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imeendelea kutoa huduma za matibabu kwa maafisa, askari, watumishi wa umma, familia zao na wananchi kwa ujumla. Huduma hizo zimekuwa zikitolewa katika hospitali na vituo vya tiba vya Jeshi hapa nchini. Katika kipindi hicho jumla ya wananchi 217,887 walipata matibabu katika zahanati, vituo vya afya na hospitali za Jeshi. Aidha, Wizara imeendelea na maboresho ya huduma za matibabu kwa Wanajeshi na familia zao, ambapo mchakato wa kuanzisha Mfuko wa Bima ya Afya kwa ajili ya Wanajeshi ulioanza mwaka wa fedha 2015/16 unaendelea kufanyiwa kazi. Hati Maalum (instrument) ya mapendekezo ya uanzishwaji wa Mfuko huo na mabadiliko ya kanuni namba 26 na 27 ya Juzuu ya Kwanza (I) Utawala vimeandaliwa ili viweze kuwasilishwa kwa Mhe. Rais na Amiri Jeshi Mkuu kwa ajili ya kuridhiwa.

*Ushirikiano wa Kiulinzi na Kijeshi na Nchi Nyingine*

**30.** ***Mheshimiwa Spika*,** ushirikiano kati ya nchi yetu na nchi nyingine katika nyanja za kijeshi ni suala muhimu katika mustakabali wa ulinzi na usalama. Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania limeendelea kuwa na ushirikiano mzuri na majeshi ya nchi nyingine hususan katika eneo linalohusu nafasi za mafunzo. Katika mwaka fedha 2016/17 Maafisa na Askari zaidi ya 350 wamekwenda kusoma kozi mbalimbali katika nchi rafiki zikiwemo Afrika Kusini, Burundi**,** Canada, China, Falme za Kiarabu, India, Kenya, Marekani, Misri, Morocco, Rwanda, Uganda, Uingereza, Ujerumani, Urusi na Zambia. Aidha, maafisa kutoka katika baadhi ya nchi hizi wapo hapa nchini katika vyuo vyetu vya kijeshi kwa mafunzo. Vyuo hivyo ni Chuo cha Maafisa Monduli, Chuo cha Ukamanda na Unadhimu (CSC) Arusha na Chuo cha Ulinzi wa Taifa (NDC) Dar es Salaam.

*Ushirikiano na Jumuiya za Kikanda na Kimataifa*

**31.** ***Mheshimiwa Spika*,** Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania, limeendelea kushiriki katika operesheni za ulinzi wa amani chini ya Umoja wa Nchi za Afrika (African Union) na

Umoja wa Mataifa. Nchi yetu imeendelea kuwa na vikosi vyake Darfur nchini Sudan maeneo ya Khor-Abeche; Shangli Tobayi na Menawash chini ya UNAMID. Aidha, Jeshi letu limeendelea kuwepo Mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) kama sehemu ya MONUSCO "Force Intervention Brigade" (FIB). Pia, Kombania mbili za Polisi Jeshi zipo nchini Lebanon kwa majukumu kama hayo. Vikosi na maafisa wa JWTZ waliopo kwenye Operesheni za Ulinzi wa Amani katika maeneo hayo wote wanaendelea vizuri na utekelezaji wa majukumu yao. Vilevile, katika kudumisha mahusiano na kuzuia matishio ya utekaji wa meli katika Bahari ya Hindi, tumeendelea kushirikiana na nchi mbalimbali zikiwemo, nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika, Afrika Kusini, Australia, Bangladesh, China, Hispania, India, Iran, Italia, Pakistan, Sierra Leone, Ufaransa, The Netherlands, Uingereza na Urusi.

*Ushirikiano wa Jeshi na Mamlaka za Kiraia*

**32.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kudhihirisha utayari wa Jeshi letu kushikiri katika shughuli mbalimbali za kiraia na utoaji wa huduma na misaada wakati wowote inapohitajika, katika mwaka wa fedha 2016/17, Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania limeshiriki katika kutoa misaada kwenye maafa ya tetemeko la ardhi lililotokea Mkoani Kagera. Misaada hiyo imehusisha kurejesha miundombinu iliyoharibika, ujenzi wa majengo ya Taasisi za Serikali pamoja na kusaidia wananchi. Aidha, Wizara ilichangia shilingi 76,125,000.00 kwa waathirika wa tetemeko hilo. Nachukua fursa hii kuzipongeza Mamlaka za Kiraia na Taasisi zote kwa kutoa ushirikiano mzuri kwa Jeshi wakati wa kutekeleza majukumu hayo.

**33.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kukabiliana na vitendo vya kihalifu, Wizara kupitia JWTZ, imeendelea kushirikiana na Vyombo vingine vya Usalama na mataifa mengine katika kupambana na matishio ya kiusalama yakiwemo ugaidi, uharamia na biashara haramu ya dawa za kulevya. Aidha, JWTZ limeshiriki katika Operesheni Amboni 2 Mkoani Tanga iliyoanza mwezi Mei, 2016 na kufungwa rasmi mwezi Desemba 2016 ambapo wahalifu hao walidhibitiwa.

**34.** ***Mheshimiwa Spika*,** Wizara imekuwa mstari wa mbele katika kutekeleza agizo la Mhe. Rais la kutatua tatizo la uhaba wa madawati katika shule za Serikali za msingi na sekondari. Aidha, kupitia Taasisi na Mashirika yake Wizara ilipewa jukumu la kutengeneza madawati 60,000. Kazi hiyo ilifanyika kwa ufanisi na weledi mkubwa. Katika zoezi hilo, JKT ilichangia madawati ya ziada 5,005. Wizara kupitia JWTZ imesimamia ujenzi wa Shule ya Sekondari Ihumwa iliyopo Dodoma na inaendelea kusimamia ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Ihungo iliyopo Kagera iliyoathirika na tetemeko la ardhi mwaka 2016.

*Mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa kwa Vijana*

**35.** ***Mheshimiwa Spika,*** mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa yameendelea kutolewa kwa vijana wa kujitolea na wale wa Mujibu wa Sheria kwa lengo la kujenga uzalendo, ukakamavu, maadili mema, utaifa pamoja na kutoa stadi za kazi. Katika mwaka 2016/17, Jeshi la Kujenga Taifa limefanikiwa kuendesha mafunzo kwa vijana 14,748 wa mujibu wa sheria (Compulsory National Service Training), ambapo kati yao wavulana ni 10,863 na wasichana 3,885 waliohitimu Kidato cha Sita mwaka 2016. Idadi hiyo ni sawa na asilimia 73.7 ya lengo la kuchukua vijana 20,000. Pia, JKT limefanikiwa kuchukua vijana wapya wa kujitolea 9,848 kwa ajili ya mafunzo ambapo kati yao, wavulana ni 7,154 na wasichana ni 2,694. Idadi hiyo ni sawa na asilimia 98.5 ya lengo la kuchukua vijana 10,000.

**36.** ***Mheshimiwa Spika,*** wakati wa kuandikisha vijana wa kujitolea kwa ajili ya kujiunga na mafunzo hayo, hutakiwa kujaza na kusaini fomu maalum ya mkataba yenye masharti kwamba kijana awe tayari kurudi nyumbani mara amalizapo mkataba wake. Pamoja na dhamira ya Serikali ya kutoa ajira kwa vijana wanaohitimu mafunzo katika Jeshi la Kujenga Taifa, sio vijana wote wanaohitimu mafunzo hayo wanaweza kupata ajira katika vyombo vya ulinzi, usalama au Taasisi zake. Hivyo, napenda kutoa rai kwa vijana wanaopata mafunzo ya JKT wazingatie maarifa na ujuzi wanaoupata hususan wa stadi za kazi ili waweze kujiajiri na kuweza kujitegemea na hata kuajiri wengine.

**37.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara, kupitia JKT imeendelea kutoa mchango katika kuwapatia vijana wa Kitanzania fursa mbalimbali za ajira kwa kujiajiri wenyewe au kuajiriwa katika Vyombo vya Ulinzi na Usalama, Taasisi za Umma na Kampuni Binafsi. Katika kutekeleza agizo la Mhe. Rais na Amiri Jeshi Mkuu kwa Vyombo vya Ulinzi na Usalama la kuajiri vijana waliohitimu mafunzo ya JKT, jumla ya vijana 732 wa Operesheni Miaka 50 ya Muungano na vijana idadi 6,072 wa Operesheni Kikwete wamenufaika na utaratibu huo katika mwaka wa fedha 2016/17. Aidha, vijana 46 walioshiriki Zoezi la Miaka 52 ya JWTZ waliandikishwa katika Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania.

**38.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuboresha mafunzo ya ujasiriamali na kuwajengea uwezo vijana wanaohitimu mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa, Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kwa kushirikiana na JKT, liliendesha mafunzo ya ujasiriamali na uendeshaji biashara kwa wakufunzi wa vijana wa JKT 134 kwa lengo la kuwafundisha vijana wa kujitolea ili waweze kupata stadi zitakazowawezesha kujitegemea na kujiajiri wenyewe pindi wamalizapo Mkataba. Mafunzo hayo yaliendeshwa na wataalam wanaotambuliwa na Shirika la Kazi Duniani (ILO) katika Vituo vya **831KJ** –Mgulani, **834KJ** –Makutopora na **841KJ** –Mafinga. Kwa kupitia Bunge lako Tukufu, napenda kutoa wito kwa vijana hao kujiunga katika vikundi ili Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi waweze kuwaunganisha katika mabenki na taasisi nyingine za kifedha kwa lengo la kupata mikopo yenye masharti nafuu.

*Mapambano dhidi ya UKIMWI*

**39.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kusimamia kikamilifu mapambano dhidi ya maambukizi ya Virusi vya UKIMWI (VVU) kwa Maafisa, Askari, Vijana, watumishi wa umma na familia zao. Mapambano dhidi ya maambukizi ya Virusi vya UKIMWI yanaendelea kwenye Wizara na Taasisi zake. Baadhi ya mikakati ya mapambano hayo ni pamoja na kutoa elimu kwa wahusika wote kupitia mpango wa Elimu Rika kwa vikundi ili kujadili kwa undani namna ya kujikinga na

maambukizi ya UKIMWI na kupitia mpango wa Tohara kwa vijana wa kiume kwenye kambi za JKT. Mkakati mwingine ni upimaji wa hiari wa VVU kwa maafisa, askari, vijana na watumishi wa Umma na utoaji wa dawa za kufubaisha VVU na lishe kwa wale waliokwishaathirika.

*Utawala Bora*

**40.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imeendelea kutekeleza dhana ya Utawala Bora katika maeneo ya kazi kwa kushirikisha watumishi wake na wadau wengine wa Wizara. Wizara imeendelea kuwaelimisha na kuwakumbusha mara kwa mara Maafisa, Askari na Watumishi wa Umma kuhusu kuzingatia sheria na maadili ya utendaji kazi, uzalendo na kutokujihusisha kwa namna yoyote katika kutoa au kupokea rushwa. Aidha, vikao mbalimbali kwenye vikosi vya JWTZ kuanzia ngazi ya patuni hadi kikosi hufanyika. Pia, viongozi wamekuwa wakifanya ziara mbalimbali vikosini ambapo masuala mbalimbali ya kisera na kistratejia hutolewa ufafanuzi. Wizara imeendelea kushirikisha wadau wa ndani na nje ya Wizara katika kuboresha huduma kwa wananchi na wadau wote kwa ujumla.

*Utunzaji wa Mazingira*

**41.** **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa mazingira, Wizara kupitia Jeshi imeendelea kushirikiana na jamii kutekeleza Sera ya Utunzaji na Uhifadhi wa Mazingira kwa kuhakikisha maeneo yake yanapandwa miti pamoja na kuchukua tahadhari ya moto. Katika mwaka wa fedha 2016/17 jumla ya miti 270,980 imepandwa kwenye vikosi mbalimbali.

**Matumizi ya Shughuli za Maendeleo**

**42.** ***Mheshimiwa Spika,*** fedha zilizopokelewa hadi mwezi Machi katika mwaka wa fedha 2016/17 kwa mafungu yote matatu, ilikuwa sawa na takriban asilimia 14.5 ya bajeti iliyoidhinishwa. Wizara imeweza kutekeleza miradi ifuatayo:

kukamilisha mradi wa ujenzi wa nyumba 6,064 awamu ya kwanza kwa ajili ya makazi ya wanajeshi, kulipia sehemu ya madeni ya kimikataba; kukarabati majengo pamoja na kuboresha mazingira ya kufanyia kazi na makazi katika kambi na vikosi vya JKT; ukarabati wa zana za ulinzi wa anga, ujenzi wa Bwalo la Maafisa katika Shule ya Kijeshi ya Ulinzi wa Anga Tanga; kuweka umeme katika baadhi ya minara ya Mawasiliano Salama Jeshini katika mikoa ya Morogoro na Dodoma. Aidha, kupitia ushirikiano baina ya Tanzania na China ujenzi wa uwanja wa ndege vita Ngerengere umekamilika na kituo cha mafunzo maalum ya kijeshi Mapinga, Bagamoyo ili kukabiliana na matishio mapya ya kiusalama kinaendelea kujengwa.

*Ujenzi wa nyumba, maghala na miundombinu mbalimbali*

**43.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutekeleza mradi wa ujenzi wa nyumba 6,064 ambapo katika mwaka wa fedha 2016/17 huduma za maji na umeme katika nyumba hizo zimepelekwa na hivyo kuwezesha kuanza kutumika kwa nyumba hizo katika kambi zilizopo mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Kagera, Kaskazini Pemba, Kigoma, Morogoro, Pwani na Tanga. Juhudi za kupata fedha za kukamilisha ujenzi wa nyumba 3,936 ili kufikia lengo la ujenzi wa nyumba 10,000 katika kambi zilizobaki zinaendelea. Vile vile, Wizara inaendelea na ujenzi wa maghala ya kuhifadhia milipuko, ambapo maghala 12 yamejengwa Makambako (Njombe) na maghala 6 yamejengwa Dunga (Zanzibar). Aidha, katika kipindi hicho, upanuzi wa uwanja wa ndege vita Ngerengere ulikamilika na kuzinduliwa rasmi na Rais na Amiri Jeshi Mkuu Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli tarehe 06 Machi, 2017. Mradi wa ujenzi wa kituo maalum cha mafunzo (Comprehensive Training Centre) nao unaendelea vizuri na hadi sasa ujenzi umefikia asilimia 30.

*Ununuzi wa Zana na Vifaa vya Kijeshi*

**44.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika juhudi za kuliongezea uwezo wa kiutendaji na kuimarisha mazingira ya kufanyia

kazi, Serikali imeendelea kulipatia Jeshi zana na vifaa mbalimbali. Katika mwaka wa fedha 2016/17, Jeshi limepokea zana na vifaa mbalimbali kwa ajili ya ulinzi wa nchi kavu, anga na majini. Kupatikana kwa zana na vifaa hivyo kumeongeza uwezo wa Jeshi kutekeleza majukumu yake ya msingi ya kiulinzi. Mpango wa ununuzi wa zana na vifaa vya kisasa na bora pamoja na mafunzo ya namna ya kutumia na kutunza zana na vifaa hivyo utakuwa endelevu.

*Shirika la Uzalishaji Mali la JKT (SUMAJKT)*

**45.** ***Mheshimiwa Spika***, SUMAJKT limeendelea kutekeleza shughuli zake katika misingi ya kibiashara kupitia Kampuni Tanzu, Idara na miradi yake ifuatayo: Kampuni ya Ulinzi (SUMAJKT Guard Ltd); Kampuni ya Ujenzi (National Service Construction Department); Kampuni ya Ubia; Idara ya Kilimo, Uvuvi na Mifugo; Idara ya Viwanda na mradi wa matrekta.

**46.** ***Mheshimiwa Spika,*** SUMAJKT kupitia kampuni yake ya Ulinzi SUMAJKT Guard Ltd, inaendesha shughuli za ulinzi katika Ofisi za Serikali, Mashirika ya Umma na sekta binafsi zikiwemo Benki na Migodi. Kwa mwaka 2016/17 imefanikiwa kuongeza huduma za ulinzi kwa wafuatao: Wakala wa Serikali Mtandao (eGA); Air Tanzania Corporation Limited (ATCL); Julius Nyerere International Airport (JNIA); Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA); Local Authority Pension Fund (LAPF); Wakala wa Ndege za Serikali (TGFA); Medical Stores Department (MSD); Tanzania Insurance Regulatory Authority (TIRA); Wakala wa Nishati Vijijini (Rural Energy Agency); TANROADS; Procurement and Supplies Profession Technician Board (PSPTB); Tanzania Forests Services (TFS); Bank of Africa (BOA); BOT-Dodoma; FINCA; DCB Bank; Dar es Salaam Maritine Institute na KUDU Resources LTD.

**47.** ***Mheshimiwa Spika,*** Kampuni imetoa mchango kwa Serikali kwa kupunguza tatizo la ajira nchini kwa kuajiri vijana 4,150 mwaka 2016/17 ikilinganishwa na vijana 2,777 mwaka 2015/16. SUMAJKT Guard Ltd pia limeboresha mfumo wa ulinzi kwa kutumia teknolojia ya kisasa (CCTV systems). Katika mwaka wa fedha 2017/18, Kampuni imekusudia kuimarisha

shughuli zake kwa kununua vitendea kazi vipya kama vile; vifaa vya kupambana na moto na uokoaji (Fire fighting and rescue equipment), vifaa vya kudhibiti vurugu (anti riot equipment), vifaa vya kuhakikisha usalama katika usafirishaji fedha (cash in transit equipment) na gari la kusafirishia wagonjwa (Ambulance) ili kuongeza tija kwa shirika kwa ujumla.

**48.** ***Mheshimiwa Spika***, mradi wa matreka mpaka sasa umeshasambaza matrekta 2,222 yenye thamani ya shilingi 87,878,744,388.00. Matrekta hayo yaliuzwa kwa mkopo na fedha taslimu. Mpaka kufika Machi, 2017 jumla ya shilingi 46,513,791,226.72 zilikuwa zimekusanywa sawa na asilimia 52.9. SUMAJKT imekuwa ikitumia vyombo vya habari kutoa matangazo kwa umma ya kuwataka wakopaji kulipa madeni yao ili mradi huu uwe endelevu. Hadi kufikia mwezi Machi, 2017 matrekta mapya 80 na majembe 120 yameshawasili kwa ajili ya kuwauzia wananchi.

**49.** ***Mheshimiwa Spika***, SUMAJKT, kupitia Kampuni ya Ujenzi (NSCD), inatekeleza miradi mbalimbali ya ujenzi wa majengo na barabara kama ifuatavyo: ujenzi wa Ofisi za Chama cha Walimu Tanzania (CWT) katika mikoa 8 ya Tanzania, ujenzi wa bandari kavu Vigwaza yenye hekta 125, na ujenzi wa miundombinu ya Kiwanda cha Sukari Mkulazi Morogoro. Kampuni hiyo imeshiriki katika ujenzi wa uzio katika mabweni ya wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ambayo yalizinduliwa na Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 15 Aprili, 2017.

**50.** ***Mheshimiwa Spika***, Idara ya Kilimo, Ufugaji na Uvuvi ya Shirika inashughulika na uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara, mbegu bora, ufugaji na uvuvi. Katika mwaka wa fedha 2016/17 Shirika limelima mazao ya chakula na biashara ekari 4,787 na jumla ya mifugo 7,982 kati yake ng'ombe ni 1,471, mbuzi 302, kuku 5,885, kondoo 240 na nguruwe 174. Aidha, Shirika lina boti tatu za uvuvi moja ya tani 5 iko 836 KJ Mbweni JKT (Dar es Salaam) na boti mbili ziko 822 KJ Rwamkoma (Mara). Katika mwaka wa fedha 2017/18, Shirika limepanga kujielekeza kwenye kilimo cha

umwagiliaji (Irrigation System) katika vikosi vya JKT ili kuongeza uzalishaji na kukabiliana na tatizo la mabadiliko ya tabia nchi. Kupitia shughuli za kilimo cha mboga mboga, SUMAJKT limeweza kuchangia kiasi cha shilingi 500 kwa siku kwa kila kijana anayehudhuria mafunzo ya JKT.

**51.** ***Mheshimiwa Spika,*** Shirika kupitia kampuni yake Tanzu ya SUMA JKT Seed Co. Ltd limeendelea na uzalishaji wa mbegu bora za mazao mbalimbali. Mbegu hizo huuzwa kwa kampuni mbalimbali zinazojishughulisha na uuzaji wa mbegu. Hata hivyo, kampuni hii imekuwa ikikabiliwa na changamoto ya kutolipwa kwa wakati kutoka kwa washitiri wake. Hadi kufikia Mei, 2017 kampuni ilikuwa inadai jumla ya shilingi 494,131,226.00. Kwa kupitia Bunge lako Tukufu, natoa rai kwa kampuni zinazodaiwa kulipa madeni yao mapema iwezekanavyo ili kuliwezesha SUMA JKT Seed Co. Ltd kufikia malengo yake na kuendelea kuzalisha mbegu bora kwa faida ya Taifa letu.

**52.** ***Mheshimiwa Spika***, katika masuala ya viwanda, SUMAJKT imeimarisha viwanda vyake vya ushonaji (Ruvu na Mgulani), utengenezaji wa samani (Changómbe Furniture Factory) na mradi wa ubia wa kokoto (SUMAJKT - ANIT ASFALT CO. LTD). Aidha, Shirika lipo katika mchakato wa kuanzisha viwanda vifuatavyo: Kiwanda cha Maji ya Kunywa ya Chupa; Kiwanda cha Mess tin; Masufuria na bidhaa nyigine za Aluminium; Kiwanda cha Utengenezaji Bidhaa za Ngozi; Kiwanda cha Usindikaji Minofu ya Samaki na Kiwanda cha Kusindika Minofu ya Nyama.

**53.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuongeza ufanisi wa utendaji wake wa kazi, SUMA JKT imeendelea kuhuisha muundo wake. Hii ni pamoja na kutenganisha shughuli za vikosi vya Jeshi la Kujenga Taifa na zile za SUMAJKT pamoja nan a kwamba zinaweza kuwa katika sehemu moja. Aidha, ili kuongeza ufanisi na tija, mikataba ya utendaji imewekwa baina ya Mkurugenzi Mtendaji na Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa.

*Shirika la Mzinga*

**54.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2016/17 Shirika la Mzinga limeendelea na utekelezaji wa majukumu yake ya msingi ya kufanya utafiti wa kuwezesha uzalishaji wa mazao ya kijeshi kwa kutumia malighafi zinazopatikana hapa nchini na kufanya matengenezo na ukarabati wa zana za kijeshi. Pamoja na changamoto ya upatikanaji wa fedha za maendeleo, Shirika limeendelea kupanua uzalishaji wa mazao ya kijeshi kwa gharama nafuu ikilinganishwa na kuagiza bidhaa hizo kutoka nje ya nchi.

**55.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kutekeleza azma ya Serikali ya kuwa na uchumi wa viwanda, na pia kukabiliana na changamoto za upatikaji wa malighafi za kistratejia na mtaji, Shirika limeendelea kuchukua hatua za kujiimarisha ikiwa ni pamoja na kuongeza kasi ya kutekeleza Mpango Mkakati wa Kipindi cha Miaka Mitano (2016/17 – 2020/21). Mpango Mkakati huo unakusudia kupanua wigo wa uzalishaji wa mazao ya kijeshi, kuongeza wigo wa shughuli za Shirika kwa kuanzisha viwanda vipya vya kutengeneza baruti na kupanua mradi wa kutengeneza mashine ndogo ndogo kwa ajili ya kuwawezesha wajasiriamali (wadogo na wa kati) kufanya uchakataji na kuongezea thamani ya mazao ya kilimo na misitu. Vile vile, Shirika limekusudia kuboresha karakana ya utengenezaji samani na kuiimarisha Kampuni Tanzu ya Mzinga Holding Co. Ltd kwa kuipatia mtaji na vitendea kazi.

*Shirika la Nyumbu*

**56.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka wa fedha 2016/17, pamoja na kutekeleza majukumu yake ya msingi ya utafiti na uhawilishaji wa teknolojia, Shirika limechangia kupunguza gharama kwa JWTZ kwa kufanya matengenezo ya zana za kijeshi kwa gharama nafuu ambazo zingepaswa kusafirishwa kwenda nje kwa matengenezo na kuzalisha vipuli vya magari, mitambo na mashine mbalimbali. Pia, Shirika limekuwa likihusika na matayarisho ya zana,

mitambo na vitendea kazi kwa vikundi vinavyokwenda katika operesheni za ulinzi wa amani. Aidha, Shirika limeshiriki katika zoezi la kitaifa la utengenezaji wa madawati kwa ajili ya shule za msingi na sekondari za Serikali. Katika hatua nyingine, Shirika limetengeza vitanda 652 kwa ajili ya maafisa na askari waliohamia Dodoma.

**57.** ***Mheshimiwa Spika,*** Shirika pia lilifanikiwa kufanya ukarabati mdogo wa nyumba za makazi na mitambo ya karakana ya Shirika; kununua vifaa vya TEHAMA na kukarabati mfumo wa umeme kiwandani. Vile vile, Shirika limeendelea kutekeleza shughuli zake za kufanya utafiti katika teknolojia ya magari na mitambo ya kijeshi, kuimarisha na kuongeza uwezo wa kuhawilisha teknolojia mbalimbali za utafiti na kukarabati miundombinu ya Shirika.

**58.** ***Mheshimiwa Spika,*** Shirika limeandaa Mpango wa Maendeleo wa Miaka Kumi (Ten Years Development Plan 2017/18 – 2026/27) wenye lengo la kuliimarisha na kulirejeshea Shirika hadhi yake ili liweze kushiriki katika maendeleo ya uchumi wa viwanda nchini. Rasimu ya kwanza ya mpango huo imeandaliwa na kuwasilishwa kwa wadau mbalimbali ili kupata maoni na ushauri ili hatimaye kuweza kuwasilishwa kwenye ngazi za maamuzi.

*Mtandao wa Mawasiliano Salama Jeshini*

**59.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutekeleza Mradi wa Mawasiliano Salama Jeshini (Independent Mobile Secured Communication Network) ambapo hadi kufikia Machi, 2017 jumla ya minara 132 ilikuwa imesimikwa Tanzania Bara na Visiwani. Mawasiliano kupitia mtandao huo yanapatikana katika maeneo ya Zanzibar, Pwani, Dar es Salaam na baadhi ya maeneo ya Morogoro. Kazi ya kuunganisha maeneo mengine ya nchi ikiwemo Mkoa wa Dodoma kwenye mtandao huo inaendelea. Aidha, uunganishaji wa mawasiliano haya salama katika vikosi vyote Jeshini utakamilishwa mwaka wa fedha 2017/18.

*Kudhibiti Uvamizi wa Maeneo ya Jeshi, Upimaji na Ulipaji Fidia*

**60.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2016/17, Wizara haijaweza kupima na kulipa fidia wananchi kwa maeneo yaliyotwaliwa kwa matumizi ya Jeshi kama ilivyopangwa kutokana na upatikanaji mdogo wa fedha za maendeleo. Aidha, kwa lengo la kudhibiti uvamizi zaidi katika maeneo ya Jeshi, Wizara kupitia vikosi, vyuo na shule za kijeshi, imeendelea kupanda miti na kuweka mabango kuzunguka maeneo hayo.

## CHANGAMOTO ZA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KATIKA MWAKA WA FEDHA 2016/17

**61.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2016/17 Wizara iliidhinishiwa jumla ya **shilingi 248,000,000,000.00,** kwa ajili ya shughuli za maendeleo na hadi kufikia mwezi Machi, 2017 kiasi kilichotolewa ni **shilingi 35,900,000,000.00** sawa na **asilimia 14.5** ya bajeti hiyo. Kutokana na kiwango cha fedha kilichopokelewa, Wizara imeweza kulipa sehemu ya madeni ya kimkataba, na kuingiza huduma za maji na umeme katika baadhi ya nyumba 6,064 pamoja na ukarabati wa miundombinu katika baadhi ya kambi.

**62.** ***Mheshimiwa Spika,*** mtiririko wa fedha kwa ajili ya matumizi mengineyo katika mwaka wa fedha 2016/17, umeleta changamoto katika kutekeleza kikamilifu mpango kazi, kulipia kwa wakati huduma na mahitaji muhimu kwa wanajeshi, vijana wanaohudhuria mafunzo ya JKT na watumishi wa Umma.

## MPANGO NA MWELEKEO WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/18

**63.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mpango na Mwelekeo wa Bajeti wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa katika mwaka 2017/18 unakusudia kuimarisha utendaji kazi na kuongeza ufanisi wa Jeshi katika kutekeleza majukumu yake kulingana na Dira na Dhima ya Wizara, Ilani ya Uchaguzi ya Chama

cha Mapinduzi ya mwaka 2015, Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo na Maelekezo ya Mhe. Rais wakati wa kuzindua Bunge la 11 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 20 Novemba, 2015. Hivyo, Wizara itaendelea kutekeleza majukumu yake muhimu katika maeneo yafuatayo:

i. Kuliongezea uwezo Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania utendaji kivita kwa kulipatia vifaa na zana bora pamoja na kutoa mafunzo stahiki kwa wanajeshi dhidi ya adui wa ndani na nje;

ii. Kuimarisha mazingira mazuri ya kufanyia kazi, makazi na kuimarisha upatikanaji wa huduma, stahili na mahitaji ya msingi kwa wanajeshi na watumishi raia;

iii. Kuwapatia vijana wa Kitanzania mafunzo ya uzalendo, ukakamavu, umoja wa kitaifa na stadi za kazi;

iv. Utafiti na uhawilishaji wa teknolojia kwa madhumuni ya kuzalisha bidhaa na huduma kwa ajili ya matumzi ya kijeshi na kiraia na

v. Kuimarisha ushirikiano na nchi nyingine duniani katika nyanja za kijeshi na kiulinzi.

## SHUKRANI

**64.** ***Mheshimiwa Spika,*** kabla sijahitimisha Hotuba yangu naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa wale wote walioniwezesha kufanikisha na kutekeleza jukumu la kuongoza Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Aidha, napenda kutoa shukrani kwa wale wote waliotoa michango iliyosaidia kufanikisha maandalizi ya makadirio ya matumizi ya fedha ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka 2017/18.

**65.** **Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa shukrani za pekee kwa wafanyakazi wenzangu wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa nikianzia na Katibu Mkuu Dkt. Florens M. Turuka, Naibu Katibu Mkuu Bi. Immaculate P. Ngwale, Mkuu wa

Majeshi ya Ulinzi Jenerali Venance S. Mabeyo, Mnadhimu Mkuu Luteni Jenerali James A. Mwakibolwa, Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa Meja Jenerali Michael J. Isamuhyo, Wakuu wa Kamandi, Wakuu wa Mashirika, Maafisa, Askari na Watumishi wa Umma. Aidha, naishukuru Kamati ya Wizara iliyoandaa hotuba hii kwa ushirikiano walionipatia.

**66.** ***Mheshimiwa Spika,*** vile vile naomba niwashukuru wapiga kura wangu wa Jimbo la Kwahani kwa ushirikiano wao walionipa katika mwaka 2016/17. Ni matumaini yangu kuwa tutaendelea kushirikiana zaidi kwa manufaa ya Jimbo letu na Taifa kwa ujumla.

**67.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa niaba ya Serikali naomba pia kutoa shukrani zangu kwa Serikali za nchi mbalimbali, Mashirika na Wahisani kwa ushirikiano wao na Wizara ya Ulinzi na JKT. Wahisani hao ni pamoja na Jamhuri ya Watu wa China, Ujerumani, Canada, Marekani, Ufaransa, India na Uturuki. Aidha, tunazishukuru nchi rafiki kwa ushirikiano wao katika shughuli zetu mbalimbali za kiulinzi. Nchi hizo ni pamoja na Afrika Kusini, Bangladesh, DRC, Ghana, Falme za Kiarabu, Indonesia, Misri, Nigeria, Uingereza, Urusi na nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika. Nchi rafiki na wahisani wamekuwa wakishirikiana na Jeshi katika mafunzo, mazoezi ya kijeshi, na kuimarisha miundombinu ya mawasiliano, makazi na tiba.

## MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA BAJETI YA MWAKA 2017/18

*Makadirio ya Mapato*

**68.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na Taasisi zake haina chanzo cha uhakika cha mapato kinachoweza kuchangia kwa kiasi kikubwa katika ukusanyaji wa maduhuli ikizingatiwa majukumu ya msingi ya Wizara hii. Chanzo kikuu cha mapato ni makusanyo ya mauzo yanayotokana na nyaraka za zabuni suala ambalo kwa sasa linashughulikiwa pia na Wakala wa Serikali wa Ununuzi na Ugavi (GPSA) kwa kiasi kikubwa.

**69.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/18 Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa inakadiria kukusanya jumla ya **shilingi 69,706,000.00** katika mchanganuo ufuatao:

| | |
|---|---|
| Fungu 38 – NGOME | **shilingi 15,601,000.00** |
| Fungu 39 – JKT | **shilingi 54,003,000.00** |
| Fungu 57 – Wizara | **shilingi 102,000.00** |

*Matumizi ya Kawaida na Maendeleo*

**70.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa inaomba kuidhinishiwa jumla ya **shilingi 1,725,517,816,925.00** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na matumizi ya maendeleo ili iweze kutekeleza majukumu yake katika mwaka 2017/18. Kati ya fedha hizo **shilingi 1,506,517,816,925.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **shilingi 219,000,000,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo. Mchanganuo kwa kila Fungu ni ufuatao:

**Fungu 38 – NGOME**

| | | |
|---|---|---|
| Matumizi ya Kawaida | **shilingi** | **1,205,244,289,563.00** |
| Matumizi ya Maendeleo | **shilingi** | **8,000,000,000.00** |
| **Jumla** | **shilingi** | **1,213,244,289,563.00** |

**Fungu 39 – JKT**

| | | |
|---|---|---|
| Matumizi ya Kawaida | **shilingi** | **283,362,530,783.00** |
| Matumizi ya Maendeleo | **shilingi** | **6,000,000,000.00** |
| **Jumla** | **shilingi** | **289,362,530,783.00** |

**Fungu 57 – Wizara**

| | | |
|---|---|---|
| Matumizi ya Kawaida | **shilingi** | **17,910,996,579.00** |
| Matumizi ya Maendeleo | **shilingi** | **205,000,000,000.00** |
| **Jumla** | **shilingi** | **222,910,996,579.00** |

## 2.0 MWISHO

**71.** ***Mheshimiwa Spika,*** Naomba kutoa Hoja.

**MWENYEKITI:** Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama.

**MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB – MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza kusoma taarifa yangu ningependa kuwapongeza kwa dhati kabisa Majenerali ambao wamepandishwa Vyeo na Mheshimiwa Rais kwa wakati huu. Tunampongeza sana Jenerali Venance Mabeyo kuwa Mkuu wa Majeshi, tunampongeza pia Luteni Jenerali James Mwakibolwa kuwa Mnadhimu Mkuu wa Jeshi na tunampongeza Meja Jenerali Michael Isamuyo kuwa Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa fedha 2016/2017, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kifungu cha Sita 6(3) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ni jukumu la Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama. Aidha, Kifungu cha 7(1)cha Nyongeza hiyo kimeainisha kuwa Kamati za Kudumu za Kisekta, pamoja na mambo mengine, zina jukumu la kushughulikia Bajeti za Wizara zinazosimamia. Kwa utaratibu wa kibajeti, Wizara hii inahusisha Mafungu matatu (3): Fungu 38- Ngome, Fungu 39- Jeshi la Kujenga Taifa na Fungu 57- Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo ya awali, sasa naomba kubainisha mpangilio wa Taarifa ninayoiwasilisha kwa kutaja mambo makuu manne. Mambo hayo ni:-

(i) Matokeo ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo;

(ii) Mapitio ya taarifa ya utekelezaji wa mpango wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2016/2017;

(iii) Uchambuzi wa makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2017/2018; na

(iv) Maoni na ushauri wa Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya Kifungu cha 98(1), Kamati ilitembelea na kukagua miradi ya maendeleo iliyo chini ya Wizara tatu inazozisimamia ikiwemo Wizara hii, kuanzia tarehe 22 hadi 24 Machi, 2017. Tulitembelea Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ambayo ilikuwa na Miradi kumi na tatu (13) ya Maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2016/2017, Kamati ilitembelea na kukagua mradi mmoja tu chini ya Wizara hii kutokana na ufinyu wa muda uliotengwa kwa ajili ya kutembelea na kukagua utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa na Wizara tatu zinazosimamiwa na Kamati hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi uliokaguliwa ni Mradi namba 6103 uliojulikana kama '*Defence Scheme*' na kutekelezwa chini ya Kifungu namba 2002 – '*Military Research and Development'* chini ya Fungu 57. Matokeo ya Ukaguzi huo yanadhihirisha mambo makuu mawili ambayo ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, upatikanaji wa fedha kwa kiasi kidogo. Upatikanaji wa fedha kwa kiasi kidogo ikilinganishwa na Bajeti iliyoidhinishwa ni jambo lililobainika katika utekelezaji wa mradi huu. Kwa Mwaka wa Fedha unaoisha, jumla ya bilioni 151.1 zilitengwa kwa kuidhinishwa na Bunge lako kwa ajili ya mradi huu. Hata hivyo, Kamati ilielezwa kuwa hadi kufikia mwezi Machi, 2017 ikiwa ni robo ya tatu ya mwaka wa fedha, Wizara ilikuwa imepokea kiasi cha shilingi bilioni 30 tu ambazo ni sawa na asilimia 20 tu ya fedha zilizotengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri kuwa asilimia 80 ya bajeti iliyotengwa kwa ajili ya mradi huu haikuwa imepokelewa kutoka Hazina jambo ambalo limeathiri ratiba ya utekelezaji kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili ni kutoanzishwa kwa maabara za utafiti. Vilevile katika ziara hiyo Kamati ilibaini kuwa Shirika la Nyumbu limeshindwa kuanzisha maabara hizo licha ya kuwa utafiti ni shughuli zake za msingi. Hali hii imetokana na kutopatikana kwa fedha za kutekeleza shughuli hiyo kwa kipindi cha miaka saba mfululizo. Shirika la Nyumbu halikupelekewa fedha zozote kwa ajili ya maendeleo tangu mwaka 1996 hadi 2003. Athari ya changamoto hiyo, ni upungufu na uchakavu wa miundombinu ya kiteknolojia na kushindikana kuanzishwa kwa maabara za utafiti katika Shirika hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni ya jumla kuhusu utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2016/2017; Kutokana na matokeo ya ziara ya ukaguzi wa mradi uliotekelezwa chini ya Fungu 57, Kamati inatoa maoni kwamba mwenendo wa upatikanaji wa fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo ni jambo linalohitaji kuboreshwa zaidi. Kwa kuwa, utekelezaji wa miradi ya maendeleo yenye tija kwa Taifa ni jambo muhimu ni vema Serikali ikaweka uzito unaostahili dhidi ya miradi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Serikali imeendelea kuimarisha ulinzi wa Taifa letu, ni vema miradi yote inayohusu sekta ya ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa iendelee kupewa kipaumbele kibajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa mpango wa bajeti na uzingatiaji wa maoni ya Kamati kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Uchambuzi wa Kamati katika mapitio ya utekelezaji wa mpango wa Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2016/2017, ulijielekeza katika makusanyo ya mapato ikilinganishwa na lengo la makusanyo pamoja na upatikanaji wa fedha za matumizi kwa ajili ya shughuli zilizopangwa kutekelezwa, hususan fedha za

matumizi mengineyo *(OC)* na fedha za miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, Kamati ilizingatia taarifa mbalimbali zilizowasilishwa mbele ya Kamati kwa kipindi cha Oktoba, 2016 na Januari 2017 na mahojiano yaliyochangia upatikanaji wa taarifa muhimu na za ziada wakati wa vikao vya Kamati. Naomba kuwasilisha uchambuzi huo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka wa fedha 2016/2017, Wizara ilikadiria kukusanya mapato ya jumla ya sh.68,406,000.00 kutokana na mauzo ya nyaraka za zabuni. Kamati ilijulishwa kuwa hadi mwezi Machi, 2017, Wizara ilifanikiwa kukusanya jumla ya sh.30,169,863.80 sawa na asilimia 44.1 ya lengo. Uchambuzi wa Kamati umebainisha mchanganuo wa makusanyo kama inavyoonekana katika Jedwali Namba Moja (1).

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchanganuo huo Kamati imebaini yafuatayo:-

(i) Makusanyo katika Fungu 38 – Ngome, yalikusudiwa kuchangia katika lengo la Wizara kwa asilimia 22.8 lakini taarifa ya makusanyo ilionesha kuwa Fungu 38 limechangia kwa asilimia 45.1 ya kiasi kilichokusanywa.

(ii) Makusanyo ya Fungu 39 –JKT, yalikusudiwa kuchangia katika lengo la Wizara kwa asilimia 76, lakini hali halisi imeonesha kuwa makusanyo ya JKT yamekuwa ni asimia 54.9 ya makusanyo ya kiasi kilichokusanywa.

(iii) Makusanyo ya Fungu 57 – Wizara, yalikusudiwa kuchangia katika lengo la makusanyo kwa asilimia 1.2, lakini taarifa ya Wizara imeonesha kuwa hakuna kiasi kilichokusanywa kwenye Fungu hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ulinganisho huo wa malengo ya makusanyo kwa kila Fungu ikilinganishwa na kiasi kilichokusanywa na kila Fungu, ulisababisha Kamati kuchambua zaidi ili kupata sababu za mwenendo huo wa

ufikiaji malengo. Kubwa lililobainika ni kuwa chanzo kikuu cha mapato kwa mafungu yote ya Wizara hii ni mauzo ya nyaraka za zabuni jambo linalosababisha makusanyo kuwa chini na yasiyo ya uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upatikanaji wa fedha kutoka Hazina; Pamoja na Bunge lako Tukufu kuendelea kusisitiza kila mwaka kuhusu umuhimu wa Serikali kutoa fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya matumizi ya Serikali, upatikanaji wa fedha hizo umeendelea kuwa changamoto kwa Wizara nyingi. Kwa kuzingatia hilo, Kamati ilitaka kujiridhisha kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa kufanya ulinganisho wa fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya matumizi yote ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2016/2017 na kiasi kilichopatikana hadi kufikia mwezi Machi, 2017. Uchambuzi huo ulibainisha yafuatayo:-

(i) Hadi kufikia mwezi Machi, 2017, Wizara ilikuwa imepokea asilimia 69.6 ya bajeti ya matumizi ya kawaida iliyoidhinishwa na asilimia 14.5 ya bajeti ya maendeleo.

(ii) Kiasi kilichopokelewa na Wizara kwa ajili ya miradi ya maendeleo ni pungufu kwa asilimia 10.25 ikilinganishwa na Sh.40,000,000,000/= zilizotolewa kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

(iii) Pesa kwa ajili ya bajeti ya matumizi ya uendeshaji *(OC)* ilipokelewa kwa asilimia 69.6 ikiwa ni ongezeko la 6%, ikilinganishwa na fedha za Matumizi ya Uendeshaji zilizotolewa katika kipindi cha 2015/2016.

(iv) Kati ya Sh.35,900,000,000 zilizopokelewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendelo, asilimia 94 ya fedha hizo ni kwa ajili ya Fungu 57- Wizara, asilimia sita tu kwa ajili ya Fungu 38 na Fungu 39 ikiwa ni asilimia tatu ya fedha hizo kwa kila Fungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na uchambuzi huo, Kamati ina maoni kuwa mwenendo huu wa upatikanaji

wa fedha za maendeleo kwa Fungu 38 -Ngome na Fungu 39-Jeshi la Kujenga Taifa, siyo mzuri na unaathiri ratiba na mpango wa utekelezaji wa miradi muhimu ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipopitia mpango na makadirio ya Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka 2016/2017, ilitoa ushauri katika maeneo kumi na nne (14) yanayohusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii. Naomba kulijulisha Bunge hili kuwa ushauri kuhusiana na baadhi ya maeneo umezingatiwa kikamilifu na unaendelea kuzingatiwa na ushauri mwingine haujazingatiwa kabisa kama inavyoonekana katika Kiambatisho Namba Moja (1).

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano wa ushauri uliozingatiwa kikamilifu ni kuhusu kurasimishwa kisheria kwa maeneo yote yaliyotolewa na Mamlaka za Mikoa kwa ajili ya matumizi ya Jeshi. Taarifa ya Utekelezaji imeonesha kuwa ushauri huu umeanza kutekelezwa kwa kurasimishwa maeneo ya Jeshi Mkoani Singida, Korutambe - Tarime Mkoani Mara, yaliyotolewa na Mamlaka ya Mikoa hiyo kwa ajili ya matumizi ya Jeshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano wa pili ni utekelezaji wa ushauri kuhusu kulipa madeni yote ya Wizara yaliyohakikiwa. Naomba kutoa taarifa kuwa Serikali imejiwekea utaratibu wa kutenga fedha kila mwaka kwa ajili ya kulipa madeni hayo kwa awamu. Kamati ilijulishwa kuwa kwa mwaka wa fedha 2016/2017, jumla ya Sh.151,146,888,000.00 zilitengwa kwa ajili ya kulipa madeni ya kimikataba. Hata hivyo, Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi aliijulisha Kamati kuwa hadi kufikia mwezi Machi, 2017 ni shilingi bilioni 30 tu zilikuwa zimetolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano huu wa ushauri ambao haukuzingatiwa kikamilifu ni kuhusu Serikali kutoa shilingi bilioni 35 kwa ajili ya kulipa fidia kwa maeneo yaliyochukuliwa na Jeshi. Sababu zilizotolewa ni ufinyu wa bajeti na kutokutolewa kwa fedha iliyoidhinishwa. Taarifa ya Wizara inaonesha kuwa katika Mwaka wa Fedha 2016/2017,

Wizara iliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 27 kwa ajili ya kupima na kulipa fidia wananchi ambao maeneo yao yalitwaliwa kwa matumizi ya Jeshi. Hadi kufikia mwezi Machi, 2017 fedha hizo zilikuwa hazijatolewa kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia madaraka ya Bunge yaliyoainishwa katika Ibara ya 63(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Kamati inaendelea kusisitiza kuwa ushauri ambao haujazingatiwa unapaswa kufanyiwa kazi na kuwa sehemu ya ratiba ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa mpango na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Ili kujiridhisha na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hii, Kamati ilirejea Hati Idhini ya Mgawanyo wa Majukumu ya Wizara za Serikali, Toleo la tarehe 22 Aprili, 2016 na kuoanisha na malengo ya Bajeti ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Kamati ilibaini kuwa katika kutekeleza majukumu ya msingi manne yaliyoainishwa katika Hati Idhini, Wizara inalenga kuimarisha utendaji kazi na ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yake kulingana na Dira na Dhima kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo hili limepangwa kufikiwa kwa kutekeleza majukumu saba ikiwemo kuendeza utafiti na teknolojia kwa madhumuni ya kuzalisha bidhaa na huduma kwa ajili ya matumizi muhimu pamoja na kupima ardhi inayotumika kwa shughuli za Jeshi na kulipa fidia katika maeneo yaliyotwaliwa kwa ajili ya matumizi ya kijeshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi umeonesha kuwa majukumu yaliyopangwa yatawezesha ufikiaji wa lengo kwa ufanisi endapo tu Serikali itazingatia mpango na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara kwa kutoa fedha zitakazoidhinishwa na Bunge kwa ukamilifu na kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uchambuzi wa

Makadirio ya Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mafungu yote matatu inategemea kukusanya mapato ya jumla ya Sh.69,706,000.00. Mchanganuo wa lengo hilo la makusanyo unaonekana katika Jedwali Namba Mbili (2) la Taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uchambuzi huo, Kamati imebaini yafuatayo:-

(i) Lengo la makusanyo kwa Mafungu yote ya Wizara limeongezeka kwa asilimia 1.9 ikilinganishwa na lengo la makusanyo kwa mwaka wa fedha unaoisha.

(ii) Mwaka wa fedha 2016/2017, lengo lilifikiwa kwa asilimia 44.1 hadi robo ya tatu ya mwaka wa fedha, lengo la makusanyo kwa Mwaka 2017/2018 limeongezeka kidogo badala ya kupungua.

(iii) Fungu 38 – Ngome linategemewa kwa kiasi cha asilimia 22.38 na mwaka 2016/2017 linategemewa kuwa asilimia 22.8.

(iv) Fungu 39 – JKT linategemewa kuwa katika makusanyo kwa kiasi cha 77.47% kwa mwaka 2016/2017 linategemewa kuwa asilimia 76.

(v) Fungu 57 linategemewa kuwa na makusanyo kwa kiasi cha asilimia 0.015 wakati mwaka 2016/2017 linategemewa kuwa na asilimia 1.2.

(vi) Makadirio ya mapato kwa Fungu 57 yamekuwa yakipungua kila mwaka na makusanyo yake yameendelea kuwa siyo ya kuridhisha. Kwa mfano, mwaka 2015/2016, Wizara (Fungu 57) ilikusanya Sh.100,000.00 sawa na asilimia 0.9 tu kati ya Sh.11,002,000.00 zilizokadiriwa kukusanywa. Kwa kuoanisha na mwenendo wa upatikanaji wa fedha kwa Mwaka 2016/2017, inawezekana kabisa hadi kufikia mwezi Machi, 2018, Wizara hii ikawa imekusanya kiasi cha Sh.30,740,346.00.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maelezo hayo, ni maoni ya Kamati kuwa lengo la ukusanyaji linapaswa kuzingatia mambo mengi ili kuwa na uhalisia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa makadirio ya matumizi. Maelezo ya Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi kwenye Kamati yalionesha kuwa katika mwaka wa fedha 2017/2018, Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa inayoombwa kwa mafungu yote matatu ni Sh.1,725,517,816,925.00. Kati ya fedha hizo, Sh.1,506,517,816,925.00 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Sh.219,000,000,000.00 ni kwa ajili ya kugharamia miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2017/2018 imepungua kwa Sh.11,012,596,075 ikilinganishwa na bajeti ya mwaka wa fedha 2016/2017. Hata hivyo, tofauti hiyo ni pungufu kwa asilimia 0.6.

Pili; Wakati bajeti kuu ya Mwaka wa Fedha 2017/2018, kwa mujibu wa maelezo yaliyotolewa na Waziri wa Fedha tarehe 28 Machi, 2017, imeongezeka kwa asilimia 6.64 bajeti ya Wizara hii imepungua kwa asilimia 0.6.

Tatu; Asilimia 12.7 ya bajeti ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2017/2018 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo na asilimia 87.3 ya bajeti hii ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

Nne; Wakati asilimia 38 ya bajeti kuu kwa mwaka 2017/2018 ni kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo, asilimia 12.7 ya bajeti ya Wizara hii ni kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo.

Tano; Wakati mwaka 2016/2017 asilimia 3.2 ya bajeti ya Wizara hii ilikuwa ni kwa ajili ya uendeshaji, mwaka wa 2017/2018 asilimia tatu ya bajeti ya Wizara hii ni kwa ajili kugharamia uendeshaji wa shughuli za Wizara.

Sita; Wakati jukumu la msingi la Wizara hii kwa mujibu

wa Hati Idhini ni kusimamia Sera zinazohusiana na Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, hakuna kasma zilizotengwa maalum kwa ajili ya utayarishaji na ukamilishaji wa Sera ya Ulinzi, Marekebisho ya Sheria ya Ulinzi wa Taifa wala Marekebisho ya Sheria ya Jeshi la Kujenga Taifa; na

Saba; Licha ya azma ya Serikali ya kuongeza vijana wanaokwenda mafunzo ya JKT kwa mujibu wa sheria, Kasma zinazohusika na mafunzo hayo kwa Fungu 39 hazijaongezewa fedha ikilinganishwa na mwaka 2017. Fungu 39 – JKT, limetengewa Sh.26,100,000,000 kwa mwaka wa fedha wa 2016/2017 na mwaka 2017/2018 limeombewa Sh.12,500,000,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo hayo yametokana na uchambuzi wa Kamati baada ya kupitia randama za Mafungu matatu ya Wizara hii na kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya Kifungu cha 98(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Naliomba Bunge lako Tukufu kupokea maelezo hayo yatakayosaidia majadiliano kuhusu hoja iliyowasilishwa na Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa mapema hii leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na ushauri wa Kamati; kwa kuzingatia taarifa ya utekelezaji wa maoni ya Kamati kwa mwaka wa fedha 2016/2017, sambamba na majadiliano ya kina kuhusu makadirio ya mapato, mipango na bajeti ya Wizara ya Ulinzi na JKT kwa mwaka 2017/2018, ikilinganishwa na Dhima ya Wizara ya kulinda uhuru, maslahi na mipaka ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Kamati inatoa ushauri kwa kila Fungu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu Namba 38 - Ngome ambalo linahusika na mambo ya msingi kwa uwepo wa nchi yetu na kwa kuwa kasma za matumizi muhimu zipo katika Fungu hili, Kamati inashauri kama ifuatavyo:-

Moja, kwa kuwa mpaka kufikia mwezi Machi, 2017 Serikali ilitoa asilimia 14.5 tu ya fedha zote za maendeleo zilizoidhinishwa na Bunge, jambo lililoathiri utekelezaji wa

miradi ya maendeleo, Fungu 38 - Ngome lipatiwe fedha zote zilizopaswa kutolewa kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Pili, Serikali itafute uwezekano wa kutoa shilingi bilioni 27 zilizotengwa kwa mwaka wa fedha 2016/2017 kwa ajili ya kulipia fidia kwa maeneo yaliyochukuliwa na Jeshi kabla ya tarehe 30 Juni, 2017 ili kuwezesha wananchi ambao maeneo yao yametwaliwa, kulipwa fidia. *(Makofi)*

Tatu, Serikali ione umuhimu wa kuliwezesha Jeshi kumiliki ardhi kisheria kwa kufanya tathmini na upimaji wa maeneo ya zamani na maeneo mapya yaliyotwaliwa na Jeshi na kuyapatia Hatimiliki. Umuhimu huu utaonekana endapo Serikali itatoa Sh.27,700,000,000.00 zilizotengwa katika mwaka wa fedha 2016/2017 kwa ajili ya kutekeleza shughuli hiyo, lakini hadi hadi kufikia Machi, 2017 hakukuwa na fedha zozote zilizokuwa zimetolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 39 - JKT. Kwanza; Serikali ikamilishe mchakato wa kufanya marekebisho katika Sheria ya Jeshi la Kujenga Taifa, Sura Namba193 *The National Service Act*, *Cap*. 193 ili iweze kuendana na wakati, mifumo ya utawala na mahitaji ya sasa ya kisheria katika Sekta ya Ulinzi.

Pili; Kamati inaendelea kuishauri Serikali ione umuhimu wa suala la fidia kwa vijana wanaopata mafunzo ya JKT kutekelezwa chini ya Sheria ya JKT ya mwaka 1964 ili kuondoa changamoto zilizopo kwenye malipo ya fidia kwa vijana hao.

Tatu; Fungu 39 liwezeshwe kibajeti ili kumudu mahitaji ya kuwezesha vijana wengi zaidi kujiunga na Jeshi la Kujenga Taifa.

Nne; Serikali itoe kipaumbele kwa vijana waliopitia mafunzo ya JKT wakati wa kuajiri vijana kwa ajili ya shughuli za ulinzi katika shirika la SUMA JKT.

Tano; Serikali ilipe madeni ya Shirika la SUMA *Guard* ili liendelee kujiendesha kwa ufanisi. Aidha, Serikali ione

umuhimu wa kuweka utaratibu kwa Taasisi za Serikali wa kutumia huduma za ulinzi za SUMA *Guard* badala ya kuajiri makampuni binafsi.

Sita; Serikali itoe fedha zote zilizotengwa katika mwaka wa fedha 2016/2017, kwa ajili ya ujenzi wa ukarabati wa miundombinu katika makambi mapya kwa ajili ya mafunzo na makazi ya vijana wanaotakiwa kujiunga kwa mujibu wa sheria. Aidha, kwa kuwa bajeti ya maendeleo ya Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 imepunguzwa ikilinganishwa na bajeti hiyo kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Kamati inaishauri Serikali kuongeza bajeti hiyo ili Jeshi la Kujenga Taifa liweze kuchukua vijana wengi wanaohitimu kidato cha sita na kuwapatia mafunzo ya JKT kama sheria inavyotaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Hazina ione umuhimu wa kuongeza kasi ya kulipa madeni yote ya Wizara yaliyohakikiwa yenye jumla ya Sh.212,375,287,250 ili kuzuia mgogoro unaoweza kutokea kati ya Wizara na wazabuni waliotoa huduma mbalimbali. Hadi kufikia mwezi Februari zilikuwa zimetolewa Sh.31,628,607,462.47 zilikuwa zimetolewa na Hazina sawa na asilimia 18.8 tu ya madeni yote.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itoe shilingi 10,500,000,000 kwa ajili ya kulipa madeni ya kimikataba kabla ya mwaka wa fedha 2016/2017 kwisha. Hii itaepusha ongezeko la deni linalotokana na ongezeko la riba.

Tatu, Ili kutatua tatizo la uchakavu na upungufu wa miundombinu kwa mashirika ya Nyumbu na Mzinga kwa lengo la kuwezesha ufanisi zaidi katika shughuli ya utafiti na uhawilishaji wa teknolojia pamoja na uzalishaji wa bidhaa kwa matumizi muhimu, Serikali itenge bajeti ya kutosha kwa ajili ya ukarabati wa ujenzi huo.

Nne, Shirika la Nyumbu kimsingi lipo chini ya Wizara ya Ulinzi na JKT na kwa wakati huo huo linamilikiwa kisheria na Msajili wa Hazina. Serikali iangalie uwezekano wa kulifanya

Shirika hilo kumilikiwa kisheria na kuwajibika chini ya Mamlaka moja ili kuondoa mkanganyiko uliopo.

Tano, katika kutekeleza majukumu ya msingi ya Wizara hii, Sera ya Ulinzi na Usalama *(The National Defence Policy)* ni jambo la msingi. Serikali ikamilishe mchakato wa kuandaa Sera hiyo muhimu kwa Taifa.

Mwisho, Serikali ikamilishe mchakato wa kufanya marekebisho katika Sheria ya Ulinzi wa Taifa, Sura 198 *(The National Defence Act, Cap. 192)* ili iweze kuendana na wakati, mifumo ya utawala na mahitaji ya sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi hii kwa ajili ya kuwasilisha taarifa hii. Napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ambao maoni yao, ushauri wao na ushirikiano wao, umewezesha kukamilisha kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati hii napenda kutumia fursa hii kumshukuru Waziri wa Ulinzi na JKT, Mhe. Dkt. Hussein Mwinyi kwa ushirikiano wake mzuri katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu ya Kikanuni ya Kamati. Waziri huyu ni mfano kila Kamati ilipokuwa inakwenda Waziri anakuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, namshukuru Katibu Mkuu Ndugu Florence Turuka, Mkuu wa Majeshi Jenerali Venance Mabeyo, Mnadhimu Mkuu wa Jeshi Luteni Jenerali James Mwakibolwa, Mkuu wa JKT Meja Jenerali Michael Isamuyo pamoja na Watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, tunapenda kumshukuru Katibu wa Bunge Dkt. Thomas Kashilillah kwa kuratibu vema shughuli za Kamati za Bunge. Aidha, nawashukuru Mkurugenzi wa Kamati Ndugu Athumani Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Bi. Angelina Sanga na Makatibu wa Kamati hii Ndugu Ramadhan Abdallah na Bi. Grace Bidya

wakisaidiwa na Bi. Rehema Kimbe kwa kuratibu vema, shughuli za Kamati na kuhakikisha Taarifa hii inakamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Ulinzi na JKT kwa mwaka wa fedha 2017/2018 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017; PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**3.0 UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa Kifungu cha 6 (3) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ni jukumu la Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama. Aidha, Kifungu cha 7 (1) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge kimeainisha kuwa

Kamati za Kudumu za Kisekta, pamoja na mambo mengine, zina jukumu la kushughulikia Bajeti ya Wizara inazozisimamia. Kwa utaratibu wa kibajeti, Wizara hii inahusisha Mafungu matatu (3): Fungu 38- Ngome, Fungu 39- Jeshi la Kujenga Taifa na Fungu 57- Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

**Mheshimiwa Spika**, Baada ya Maelezo hayo ya awali, sasa naomba kubainisha mpangilio wa Taarifa ninayoiwasilisha kwa kutaja mambo makuu manne (4) katika Taarifa hii. Mambo hayo ni:-

(i) Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo;
(ii) Mapitio ya Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017;
(iii) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018; na
(iv) Maoni na Ushauri wa Kamati.

## 4.0 MATOKEO YA UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA KWA MWAKA 2016/2017

### 4.1 Maelezo kuhusu Miradi ya Maendeleo iliyokaguliwa

**Mheshimiwa Spika**, Kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 98 (1), Kamati ilitembelea na kukagua miradi ya maendeleo iliyo chini ya Wizara tatu inazozisimamia ikiwemo Wizara hii, kuanzia tarehe 22 hadi 24 Machi, 2017. Pamoja na kuwa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ilikuwa na Miradi kumi na tatu (13) ya Maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2016/2017, Kamati ilitembelea na kukagua mradi mmoja tu chini ya Wizara hii kutokana na ufinyu wa muda uliotengwa kwa ajili ya kutembelea na kukagua utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa na Wizara tatu zinazosimamiwa na Kamati hii.

Mradi uliokaguliwa ni Mradi namba 6103 uliojulikana kama '*Defence Scheme*' na kutekelezwa chini ya Kifungu namba 2002 – '*Military Research and Development'* cha Fungu 57.

## 4.2 Matokeo ya Ukaguzi wa Mradi Namba 6103

**Mheshimiwa Spika**, Matokeo ya ukaguzi wa Mradi huu yanadhihirisha mambo makuu mawili ambayo ni:-

### 4.2.1 Upatikanaji wa fedha kwa kiasi kidogo

**Mheshimiwa Spika**, Upatikanaji wa fedha kwa kiasi kidogo ikilinganishwa na Bajeti iliyoidhinishwa ni jambo lililobainika katika utekelezaji wa Mradi huu. Kwa Mwaka wa Fedha unaoisha, jumla ya **Shilingi Bilioni 151.1** zilitengwa na kuidhinishwa na Bunge lako tukufu kwa ajili ya Mradi huu. Hata hivyo, Kamati ilielezwa kuwa hadi kufikia Mwezi Machi, 2017 ikiwa ni robo ya tatu ya Mwaka wa Fedha, Wizara ilikuwa imepokea kiasi cha **Shilingi Bilioni 30** sawa na **asilimia 20** tu ya fedha zilizotengwa. Ni dhahiri kuwa asilimia 80 ya bajeti iliyotengwa kwa ajili ya Mradi huu haikuwa imepokelewa kutoka Hazina jambo ambalo limeathiri ratiba ya utekelezaji kwa kiwango kikubwa.

### 4.2.2 Kutoanzishwa kwa maabara za Utafiti

**Mheshimiwa Spika**, Vilevile, katika ziara hiyo Kamati ilibaini kuwa Shirika la Nyumbu limeshindwa kuanzisha maabara hizo licha ya kuwa utafiti ni shughuli zake za msingi. Hali hii imetokana na kutopatikana kwa fedha za kutekeleza shughuli hiyo kwa kipindi cha miaka 7 mfululizo. Shirika la Nyumbu halikupelekewa fedha zozote kwa ajili ya maendeleo tangu mwaka 1996 hadi 2003. Athari ya changamoto hiyo, ni upungufu na uchakavu wa miundombinu ya kiteknolojia na kushindikana kuanzishwa kwa maabara za Utafiti katika Shirika hili.

## 4.3 Maoni ya Jumla kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017

**Mheshimiwa Spika,** Kutokana na matokeo ya ziara ya ukaguzi wa mradi unaotekelezwa chini ya Fungu 57, Kamati inatoa maoni kwamba mwenendo wa upatikanaji wa fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo ni jambo linalohitaji

kuboreshwa zaidi. Kwa kuwa utekelezaji wa miradi ya Maendeleo yenye tija kwa taifa ni jambo muhimu, ni vema Serikali ikaweka uzito unaostahili kwa miradi hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** Vilevile, kwa kuwa Serikali imeendelea kuimarisha ulinzi wa taifa letu, ni vema miradi yote inayohusu sekta ya ulinzi na jeshi la kujenga Taifa iendelee kupewa kipaumbele kibajeti.

## 5.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA BAJETI NA UZINGATIAJI WA MAONI YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017

### 5.1 Uchambuzi wa Mapitio ya utekelezaji wa mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Kamati katika Mapitio ya utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2016/ 2017, ulijielekeza katika makusanyo ya mapato ikilinganishwa na lengo la makusanyo pamoja na upatikanaji wa fedha za matumizi kwa ajili ya shughuli zilizopangwa kutekelezwa, hususan fedha za matumizi mengineyo (OC) na fedha za miradi ya maendeleo. Vilevile, Kamati ilizingatia taarifa mbalimbali zilizowasilishwa mbele ya Kamati kwa kipindi cha Oktoba, 2016 na Januari 2017, na mahojiano yaliyochangia upatikanaji wa taarifa muhimu na za ziada wakati wa vikao vya Kamati. Naomba kuwasilisha uchambuzi huo kama ifuatavyo:-

### 5.2 Uchambuzi wa Taarifa kuhusu ukusanyaji wa mapato

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2016/2017, Wizara ilikadiria kukusanya mapato ya jumla ya Shilingi **68,406,000.00** kutokana na mauzo ya nyaraka za zabuni. Kamati ilijulishwa kuwa hadi mwezi Machi, 2017, Wizara ilifanikiwa kukusanya jumla ya Shilingi **30,169,863.80** sawa na asilimia 44.1 ya lengo. Uchambuzi wa Kamati umebainisha Mchanganuo wa makusanyo kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 01.

| FUNGU | MAKADIRIO | % YA JUMLA YA LENGO | MAKUSANYO | % YA JUMLA YA MAKUSANYO |
|---|---|---|---|---|
| 38 - Ngome | 15,601,000.00 | 22.8 | 13,613,561.00 | 45.1 |
| 39 - JKT | 52,003,000.00 | 76.0 | 16,556,302.80 | 54.9 |
| 57 - Wizara | 802,000.00 | 1.2 | 0 | 0.0 |
| **JUMLA** | **68,406,000.00** | **100.0** | **30,169,863.80** | **100.0** |

**Mheshimiwa Spika**, Katika mchanganuo huo, Kamati imebaini yafuatayo:-

(i) Makusanyo katika Fungu 38 – Ngome yalikusudiwa kuchangia katika lengo la Wizara kwa asilimia 22.8 lakini Taarifa ya Makusanyo ilionesha kuwa Fungu 38 limechangia kwa asilimia 45.1 ya kiasi kilichokusanywa.

(ii) Makusanyo ya Fungu 39 –JKT yalikusudiwa kuchangia katika lengo la Wizara kwa asilimia 76.0, lakini hali halisi imeonesha kuwa makusanyo ya JKT yamekuwa ni asimia 54.9 ya makusanyo ya kiasi kilichokusanywa.

(iii) Makusanyo ya Fungu 57 – Wizara, yalikusudiwa kuchangia katika lengo la makusanyo kwa asilimia 1.2, lakini taarifa ya Wizara imeonesha kuwa hakuna kiasi kilichokusanywa kwenye Fungu hili.

**Mheshimiwa Spika,** ulinganisho huo wa malengo ya makusanyo kwa kila fungu ikilinganishwa na kiasi kilichokusanywa na kila fungu, ulisababisha Kamati kuchambua zaidi ili kupata sababu za mwenendo huo wa ufikiaji malengo. Kubwa lililobainika ni kuwa chanzo kikuu cha Mapato kwa mafungu yote ya wizara hii ni mauzo ya nyaraka za zabuni jambo linalosababisha makusanyo kuwa chini na yasiyo ya uhakika.

## 5.3 Upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina

**Mheshimiwa Spika,** Pamoja na Bunge lako Tukufu kuendelea kusisitiza kila mwaka kuhusu umuhimu wa Serikali kutoa fedha

zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya matumizi ya Serikali, upatikanaji wa fedha hizo umeendelea kuwa changamoto kwa Wizara nyingi.

Kwa kuzingatia hilo, Kamati ilitaka kujiridhisha kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa kufanya ulinganisho wa fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya matumizi yote ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2016/ 2017 na kiasi kilichopatikana hadi kufikia mwezi Machi, 2017. Uchambuzi huo ulibainisha yafuatayo:-

(i) Hadi kufikia Mwezi Machi, 2017 Wizara ilikuwa imepokea asilimia 69.6 ya bajeti ya matumizi ya kawaida iliyoidhinishwa na asilimia 14.5 ya Bajeti ya Maendeleo.

(ii) Kiasi kilichopokelewa na Wizara kwa ajili ya miradi ya maendeleo ni pungufu kwa asilimia 10.25 ikilinganishwa na **shilingi 40,000,000,000/=** zilizotolewa katika Mwaka wa Fedha 2015/2016.

(iii) Pesa kwa ajili ya Bajeti ya Matumizi ya Uendeshaji (OC) ilipokelewa kwa asilimia 69.6 ikiwa ni ongezeko la asilimia 6 ikilinganishwa na fedha za Matumizi ya Uendeshaji zilizotolewa katika kipindi cha 2015/2016.

(iv) Kati ya Shilingi 35,900,000,000 zilizopokelewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendelo, asilimia 94 ya fedha hizo ni kwa ajili ya Fungu 57- Wizara, na asilimia 6 tu kwa ajili ya Fungu 38 na Fungu 39 ikiwa ni asilimia 3 ya fedha hizo kwa kila Fungu.

**Mheshimiwa Spika**, Kutokana na uchambuzi huo, Kamati ina maoni kuwa mwenendo huu wa upatikanaji wa fedha za maendeleo kwa Fungu 38-Ngome na Fungu 39-Jeshi la Kujenga Taifa, si mzuri na unaathiri ratiba na mpango wa utekelezaji wa miradi muhimu ya maendeleo.

## 5.4 Mapitio ya utekelezaji wa ushauri wa Kamati

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipopitia Mpango na Makadirio ya Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa

Mwaka 2016/2017, ilitoa ushauri katika maeneo kumi na nne (14) yanayohusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii. Naomba kulijulisha Bunge hili kuwa ushauri kuhusiana na baadhi ya maeneo umezingatiwa kikamilifu au unaendelea kuzingatiwa na ushauri mwingine haujazingatiwa kabisa kama inavyoonekana katika Kiambatisho Namba 1.

**Mheshimiwa Spika**, Mfano wa ushauri uliozingatiwa kikamilifu ni kuhusu kurasimishwa kisheria kwa maeneo yote yanayotolewa na Mamlaka za Mikoa kwa ajili ya matumizi ya Jeshi. Taarifa ya Utekelezaji imeonesha kuwa ushauri huu umeanza kutekelezwa kwa kurasimishwa maeneo ya jeshi mkoani Singida na Korutambe- Tarime mkoani Mara yaliyotolewa na Mamlaka za Mikoa hiyo kwa ajili ya matumizi ya Jeshi.

Mfano wa pili ni utekelezaji wa ushauri kuhusu kulipa madeni yote ya Wizara yaliyohakikiwa. Naomba kutoa taarifa kuwa Serikali imejiwekea utaratibu wa kutenga fedha kila mwaka kwa ajili ya kuyalipa madeni hayo kwa awamu. Kamati ilijulishwa kuwa kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017, jumla ya shilingi **151,146,888,000.00** zilitengwa kwa ajili ya kulipa madeni ya kimikataba. Hata hivyo, Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi aliijulisha Kamati kuwa hadi kufikia mwezi Machi, 2017 shilingi **bilioni 30** zilikuwa zimetolewa.

**Mheshimiwa Spika**, Mfano wa Ushauri ambao haukuzingatiwa kikamilifu ni kuhusu Serikali kutoa shilingi **bilioni 35** kwa ajili ya kulipa fidia kwa maeneo yaliyochukuliwa na Jeshi. Sababu zilizotolewa ni ufinyu wa bajeti na kutokutolewa kwa fedha iliyoidhinishwa. Taarifa ya Wizara ilionesha kuwa katika Mwaka wa Fedha 2016/2017 Wizara iliidhinishiwa jumla ya shilingi **bilioni 27** kwa ajili ya kupima na kulipa fidia wananchi ambao maeneo yao yalitwaliwa kwa matumizi ya Jeshi. Hadi kufikia mwezi Machi, 2017 fedha hizo zilikuwa hazijatolewa kabisa.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia madaraka ya Bunge yaliyoainishwa katika Ibara ya 63 (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Kamati inaendelea

kusisitiza kuwa ushauri ambao haujazingatiwa unapaswa kufanyiwa kazi na kuwa sehemu ya ratiba ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

## 6.0 UCHAMBUZI WA MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

### 6.1 Mpango wa Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2017/ 2018

**Mheshimiwa Spika,** ili kujiridhisha na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii, Kamati ilirejea Hati Idhini ya Mgawanyo wa Majukumu ya Wizara za Serikali, Toleo la tarehe 22 Aprili, 2016 na kuoanisha na malengo ya Bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018. Kamati ilibaini kuwa katika kutekeleza majukumu ya msingi manne yaliyoainishwa katika Hati Idhini, Wizara inalenga kuimarisha utendaji kazi na ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yake kulingana na Dira na Dhima kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

Lengo hili limepangwa kufikiwa kwa kutekeleza majukumu saba ikiwemo kuendeza utafiti na teknolojia kwa madhumuni ya kuzalisha bidhaa na huduma kwa ajili ya matumizi muhimu pamoja na kupima ardhi inayotumika kwa shughuli za Jeshi na kulipa fidia katika maeneo yaliyotwaliwa kwa ajili ya matumizi ya kijeshi.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi umeonyesha kuwa majukumu yaliyopangwa yatawezesha ufikiaji wa lengo kwa ufanisi endapo tu Serikali itazingatia mpango na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara kwa kutoa fedha zitakazoidhinishwa na Bunge kwa ukamilifu na kwa wakati.

### 6.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018

**Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mafungu yote matatu inategemea kukusanya mapato ya jumla ya **shilingi 69,706,000.00**. Mchanganuo wa lengo hilo la makusanyo unaonekana katika Jedwali Na. 2 la Taarifa hii.

**Jedwali Na. 02 : Mchanganuo wa mapato**

| Fungu | Makadirio | | Asilimia ya lengo la Wizara |
|---|---|---|---|
| 38 - Ngome | Shilingi | 15,601,000.00 | 22.38 |
| 39 - JKT | Shilingi | 54,003,000.00 | 77.47 |
| 57 - Wizara | Shilingi | 102,000.00 | 0.15 |
| **JUMLA** | Shilingi | **69,706,000.00** | **100.00** |

**Chanzo: Taarifa ya Wizara**

Kwa uchambuzi huo, Kamati imebaini yafuatayo:-

(i) Lengo la makusanyo kwa mafungu yote ya Wizara limeongezeka kwa asilimia 1.9 ikilinganishwa na lengo la makusanyo kwa Mwaka wa Fedha unaoisha.

(ii) Wakati Mwaka 2016/2017 lengo lilifikiwa kwa asilimia 44.1 hadi robo ya tatu ya Mwaka wa Fedha, lengo la makusanyo kwa Mwaka 2017/2018 limeongezeka kidogo badala ya kupungua.

(iii) Fungu 38 – Ngome linategemewa kwa kiasi cha asilimia 22.38 na Mwaka 2016/2017 lilitegemewa kwa asilimia 22.8.

(iv) Fungu 39 – JKT linategemewa katika makusanyo kwa kiasi cha asilimia 77.47 na Mwaka 20116/ 2017 lilitegemewa kwa asilimia 76.

(v) Fungu 57 linategemewa kwa makusanyo kwa kiasi cha asilimia 0.15 wakati Mwaka 2016/2017 lilitegemewa kwa asilimia 1.2

(vi) Makadirio ya mapato kwa Fungu 57 yamekuwa yakipungua kila mwaka na makusanyo yake yameendelea kuwa si ya kuridhisha. Kwa mfano, kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016, Wizara (Fungu 57) ilikusanya **shilingi 100,000.00** sawa na asilimia 0.9 tu kati ya **shilingi 11,002,000.00** zilizokadiriwa kukusanywa.

(vii) Kwa kuoanisha na mwenendo wa ukusanyaji

wa fedha kwa Mwaka 2016/2017, inawezekana kabisa hadi kufikia mwezi Machi, 2018 Wizara hii ikawa imekusanya kiasi cha shilingi **30,740,346.00**.

**Mheshimiwa Spika**, kwa maelezo hayo, ni maoni ya Kamati kuwa lengo la ukusanyaji linapaswa kuzingatia mambo mengi ili kuwa na uhalisia.

### 6.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi

**Mheshimiwa Spika**, Maelezo ya Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi kwenye Kamati yalionesha kuwa katika Mwaka wa Fedha 2017/2018, Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa inayoombwa kwa mafungu yote matatu ni shilingi **1,725,517,816,925.00.** Kati ya Fedha hizo, shilingi **1,506,517,816,925.00** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi **219,000,000,000.00** kugharamia miradi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, ili kukidhi mantiki ya Masharti ya Kanuni ya 98 (2) ya Kanuni za Bunge, Kamati ilifanya uchambuzi wa makadirio hayo kwa kupitia kasma(Items), vifungu (Subvotes) na Mafungu (Votes) zote ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa na kutekelezwa kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Naomba kubainisha yafuatayo:-

i) Bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 imepungua kwa **shilingi 11,012,596,075** ikilinganishwa na bajeti ya Mwaka wa Fedha 2016/2017. Hata hivyo tofauti hiyo ni pungufu kwa kiwango cha asilimia 0.6.

ii) Wakati bajeti kuu kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 kwa mujibu wa maelezo yaliyotolewa na Waziri wa fedha tarehe 28 Machi, 2017, imeongezeka kwa asilimia 6.64 Bajeti ya Wizara hii imepungua kwa asilimia 0.6.

iii) Asimia 12.7 ya bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo na asilimia 87.3 ya bajeti ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

iv) Wakati asilimia 38 ya bajeti kuu kwa Mwaka

2017/2018 ni kwa ajili ya kugharamia miradi ya Maendeleo, asilimia 12.7 ya bajeti ya Wizara hii ni kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo.

v) Wakati Mwaka 2016/2017 asilimia 3.2 ya bajeti ya Wizara hii ilikuwa ni kwa ajili ya uendeshaji (OC), Mwaka 2017/2018 asilimia 3 ya bajeti ya wizara hii ni kwa ajili kugharamia uendeshaji wa shughuli za Wizara (OC).

vi) Wakati jukumu la msingi la Wizara hii kwa mujibu wa Hati idhini ni kusimamia Sera zinazohusiana na ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, hakuna kasma zilizotengwa maalumu kwa ajili ya utayarishaji na ukamilishaji wa Sera ya Ulinzi, Marekebisho ya Sheria ya Ulinzi wa Taifa wala Marekebisho ya Sheria ya Jeshi la Kujenga Taifa.

vii) Licha ya azma ya Serikali ya kuongeza vijana wanaokwenda mafunzo ya JKT kwa mujibu wa sheria, Kasma zinazohusika na mafunzo hayo katika Fungu 39 hazijaongezewa fedha ikilinganishwa na mwaka 2016/2017. Fungu 39 – JKT, lilitengewa **shilingi bilioni 20,100,000,000** kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017, na Mwaka 2017/2018 linaombewa **shilingi bilioni 12,500,000,000**.

**Mheshimiwa Spika**, maelezo hayo yametokana na uchambuzi wa Kamati baada ya kupitia randama za Mafungu matatu ya Wizara hii na kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 98 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Niliombe Bunge lako tukufu kupokea maelezo hayo yatakayosaidia majadiliano kuhusu hoja iliyowasilishwa na Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa mapema leo hii.

## 7.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia taarifa ya utekelezaji wa maoni ya Kamati kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 sambamba na majadiliano ya kina kuhusu Makadirio ya Mapato, Mipango na Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na JKT kwa mwaka 2017/2018 ikilinganishwa na Dhima ya Wizara ya

kulinda uhuru, maslahi na mipaka ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Kamati inatoa ushauri kwa kila fungu.

### 7.1 Fungu 38 - Ngome

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa Fungu 38 Ngome, linahusika na mambo ya msingi kwa uwepo wa nchi yetu, na kwa kuwa kasma za matumizi muhimu zipo katika fungu hili, Kamati inashauri kama ifuatavyo:-

i) Kwa kuwa mpaka kufikia mwezi Machi, 2017 Serikali ilitoa asilimia 14.5 tu ya fedha zote za maendeleo zilizoidhinishwa na Bunge jambo linaloathiri utekelezaji wa miradi ya maendeleo, Fungu 38 Ngome lipatiwe fedha zote zilizopaswa kutolewa kwa Mwaka wa Fedha 206/2017.

ii) Serikali itafute uwezekano wa kutoa shilingi **bilioni 27** zilizotengwa katika Mwaka wa Fedha 2016/2017 kwa ajili ya kulipa fidia kwa maeneo yaliyochukuliwa na Jeshi kabla ya tarehe 30 Juni, 2017 ili kuwezesha wananchi ambao maeneo yao yametwaliwa, kulipwa fidia.

iii) Serikali ione umuhimu wa kuliwezesha Jeshi kumiliki ardhi kisheria kwa kufanya tathmini na upimaji wa maeneo ya zamani na maeneo mapya yaliyotwaliwa na Jeshi na kuyapatia hati miliki. Umuhimu huu utaonekana endapo Serikali itatoa **shilingi 27,700,000,000.00** zilizotengwa katika Mwaka wa Fedha 2016/2017 kwa ajili ya kutekeleza shughuli hiyo. Hadi kufikia mwezi Machi, 2017 hakukuwa na fedha zozote zilizokuwa zimetolewa.

### 7.2 Fungu 39 JKT

i) Serikali ikamilishe mchakato wa kufanya marekebisho katika *Sheria ya Jeshi la Kujenga Taifa,* Sura 193 (*The National Service Act*, Cap. 193) ili iweze kuendana na wakati, mifumo ya utawala na mahitaji ya sasa ya kisheria katika sekta ya Ulinzi.

ii) Kamati inaendelea kuishauri Serikali ione

umuhimu wa suala la fidia kwa vijana wanaopata mafunzo ya JKT kutekelezwa chini ya Sheria ya JKT ya Mwaka 1964 ili kuondoa changamoto zilizopo kwenye malipo ya fidia kwa vijana hao.

iii) Fungu 39 liwezeshwe kibajeti ili kumudu mahitaji ya kuwezesha vijana wengi zaidi kujiunga na Jeshi la Kujenga Taifa.

iv) Serikali itoe kipaumbele kwa vijana waliopitia mafunzo ya JKT wakati wa kuajiri vijana kwa ajili ya shughuli za ulinzi katika shirika la SUMA JKT.

v) Serikali ilipe madeni ya shirika la SUMA GUARD ili liendelee kujiendesha kwa ufanisi. Aidha, Serikali ione umuhimu wa kuweka utaratibu kwa Taasisi za Serikali wa kutumia huduma za ulinzi za SUMA GUARD badala ya kuajiri makampuni binafsi.

vi) Serikali itoe fedha zote zilizotengwa katika Mwaka 2016/2017 kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu katika makambi mapya kwa ajili ya mafunzo na makazi ya vijana wanaotakiwa kujiunga kwa mujibu wa Sheria. Aidha, kwa kuwa bajeti ya maendeleo ya Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 imepunguzwa ikilinganishwa na bajeti hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017, Kamati inaishauri Serikali kuongeza bajeti hiyo ili Jeshi la Kujenga Taifa liweze kuchukua vijana wengi wanaohitimu kidato cha sita na kuwapatia mafunzo ya JKT kama Sheria inavyotaka.

## 7.3 Fungu 57 – Wizara

i) Serikali kupitia Hazina ione umuhimu wa kuongeza kasi ya kulipa madeni yote ya Wizara yaliyohakikiwa yenye jumla ya **shilingi 212,375,287,250.69** ili kuzuia mgogoro unaoweza kutokea kati ya Wizara na wazabuni/wakandarasi waliotoa huduma mbalimbali. Hadi kufikia mwezi Februari, 2017, **shilingi 31,628,607,462.47** zilikuwa zimetolewa na Hazina sawa na asilimia 14.8 tu ya madeni yote yaliyohakikiwa.

ii) Serikali itoe **shilingi 10,500,000,000** kwa ajili ya kulipa madeni ya kimikataba kabla ya Mwaka wa Fedha 2016/2017 kuisha. Hii itaepusha ongezeko la deni litokanalo na ongezeko la riba.

iii) Ili kutatua tatizo la uchakavu na upungufu wa miundombinu kwa mashirika ya Nyumbu na Mzinga kwa lengo la kuwezesha ufanisi zaidi katika shughuli za utafiti na uhawilishaji wa teknolojia pamoja na uzalishaji wa bidhaa kwa matumizi muhimu, Serikali itenge bajeti ya kutosha kwa ajili ya ukarabati na ujenzi wa miundombinu kwa mashirika hayo.

iv) Shirika la Nyumbu kimsingi lipo chini ya Wizara ya Ulinzi na JKT na wakati huo huo linamilikiwa kisheria na Msajili wa Hazina. Serikali iangalie uwezekano wa kulifanya Shirika hilo kumilikiwa kisheria na kuwajibika chini ya Mamlaka moja ili kuondoa mkanganyiko uliopo.

v) Katika kutekeleza Majukumu ya msingi ya Wizara hii, Sera ya Ulinzi wa Taifa (*The National Defence Policy*) ni jambo la msingi. Serikali ikamilishe mchakato wa kuandaa Sera hiyo muhimu kwa Taifa.

vi) Serikali ikamilishe mchakato wa kufanya marekebisho katika Sheria ya Ulinzi wa Taifa, Sura 192 (*The National Defence Act, Cap. 192*) ili iweze kuendana na wakati, mifumo ya utawala na mahitaji ya sasa ya kisheria katika sekta ya Ulinzi.

## 8.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi kwa ajili ya kuwasilisha Taarifa hii. Napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha kukamilika kwa taarifa hii. Naomba niwatambue kwa majina kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Balozi Adadi Mohamed Rajabu, Mb, **Mwenyekiti**
2. Mhe. Kanal (Mst) Masoud Ali Khamis, Mb, **M/Mwenyekiti**
3. Mhe. Capt. George Huruma Mkuchika, Mb
4. Mhe. Salma Rashid Kikwete, Mb
5. Mhe. Mussa Hassan Mussa, Mb
6. Mhe. Prosper J. Mbena, Mb
7. Mhe. Mhe. Victor Kilasile Mwambalasa, Mb
8. Mhe. Mch. Peter Simon Msigwa, Mb
9. Mhe. Cecilia Daniel Paresso, Mb
10. Mhe. Alphaxad Kangi Lugola, Mb
11. Mhe. Shamsi Vuai Nahodha, Mb
12. Mhe. Cosato David Chumi, Mb
13. Mhe. Jumanne Kibera Kishimba, Mb
14. Mhe. Bonnah Kaluwa, Mb
15. Mhe. Juliana Daniel Shonza, Mb
16. Mhe. Kiswaga Boniventura Destery, Mb
17. Mhe. Rose Cyprian Tweve, Mb
18. Mhe. Joel Mwaka Makanyaga, Mb
19. Mhe. Haji Khatib Kai, Mb
20. Mhe. Lucy Simon Magereli, Mb
21. Mhe. Masoud Abdalla Salim, Mb
22. Mhe. Sophia Hebron Mwakagenda, Mb
23. Mhe. Lazaro S. Nyalandu, Mb
24. Mhe. Stephene J. Masele, Mb
25. Mhe. Machano Othman Said, Mb
26. Mhe. Hasna Sudi Katunda Mwilima, Mb
27. Mhe. Khamisi Yahya Machano, Mb
28. Mhe. Yahya Omari Masare, Mb

**Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati napenda kutumia fursa hii kumshukuru Waziri wa Ulinzi na JKT Mhe. Dkt. Hussein Mwinyi (Mb) kwa ushirikiano wake mzuri katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu ya kikanuni ya Kamati. Aidha, namshukuru Katibu Mkuu Ndugu Florens Turuka pamoja na watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano wao.

**Mheshimiwa Spika,** mwisho napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Dkt. Thomas Kashililah kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na Bunge. Aidha, nawashukuru Mkurugenzi wa Idara

ya Kamati za Bunge Ndg. Athumani Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Bi. Angelina Sanga na Makatibu wa Kamati hii Ndg. Ramadhan Abdallah na Bi. Grace Bidya wakisaidiwa na Bi. Rehema Kimbe kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na kuhakikisha Taarifa hii inakamilika kwa wakati**.**

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na JKT kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

Balozi Adadi Mohamed Rajabu**, Mb**
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA**
16 Mei, 2017

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, maelezo ya Spika kuhusu taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani Bungeni kwa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la kujenga Taifa, naomba mnisikilize vizuri.

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamwita Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, ili awasilishwe taarifa yake naomba nitoe maelezo machahe.

Mheshimiwa Spika amesoma taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani Bungeni kuhusu Wizara ya Ulinzi na Jeshi la kujenga Taifa juu ya makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2017/2018 iliyowasilishwa mezani asubuhi ya leo na ameelekeza baadhi ya aya ziondolewe.

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Spika alikwishatoa maamuzi *(rulling)* hapa Bungeni na akatoa waraka rasmi kwa Wanadhimu Wakuu wa Kambi zote

Bungeni kwamba maudhui ya hotuba zote zinazowasilishwa hapa Bungeni hayatakiwi kupingana na masharti ya Kanuni ya 64(1) ya Kanuni za Bunge, Toleo la Januari, 2006; na kwamba hotuba yoyote au sehemu ya hotua yoyote itakayoonekana kuwa kwa ujumla wake inakinzana na masharti ya kanuni hiyo haitakubalika wala kusomwa Bungeni. *(Makofi)*

Hivyo, aya ya tatu katika ukurasa wa pili na aya ya tatu katika ukurasa wa kumi wa taarifa ya Msemaji wa Upinzani, aya hizo zimeondolea. Kwa mantiki hiyo nakala za taarifa mlizogawiwa Waheshimiwa Wabunge nakala ambazo Msemaji Mkuu wa Upinzani ataisoma hapa Bungeni na ambayo ndiyo itaingia katika Taarifa Rasmi za Bunge haitakuwa na aya hizo.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani naomba uzingatie sababu tunazungumzia Wizara nyeti na kuna mambo yameoneka na yana ni *classified information* hayatakiwi kuanikwa katika Bunge hili katika hadhara hii kwa kipindi hiki. Kwa hiyo *rulling* ya Kiti ni hiyo, nakuomba uyachukulie hivyo, kama utakuwa na mambo yoyote muhimu kwa Taifa hili yawasilishe katika sehemu zinazohusika siyo katika mjadala ambao maadui wa nchi hii wanaweza wakachukua *advantage* ya mambo hayo.

Mheshimiwa Msemaji wa Kambi ya Upinzani, karibu. *(Makofi)*

**MHE. MWITA C. WAITARA (K.n.y. MHE. JUMA HAMAD OMAR - MSEMAJI MKUU WA UPINZANI WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitazingatia kisu cha ngaliba kimepitia baadhi ya maeneo kwa hiyo sitayasoma. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Juma Hamad Omar Mbunge, naomba kuwasilisha maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka

2016/2017 pamoja na makadirio ya mapato na matumizi ya fedha ya Wizara hiyo, kwa mwaka wa fedha 2017/2018

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijawasilisha maoni hayo, napenda kuchukua fursa hii, kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia sote uhai na kutuwezesha kushiriki katika Mkutano huu wa Bunge, kujadili Bajeti ya Serikali tukiwa salama. Aidha, napenda kutumia fursa hii kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, kulipongeza Jeshi la Wananchi wa Tanzania kwa jinsi walivyojitoa kwa moyo wa uzalendo kabisa, kusaidia kuratibu zoezi la kuaga miili ya wanafunzi 32, Walimu wawili na Dereva mmoja wa shule ya *Lucky Vincent* waliofariki kwa ajali ya gari huko Karatu – Arusha. Sambamba na hilo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatoa salamu za rambirambi kwa wote walioguswa na msiba huo mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa sina fadhila, kama sitawashukuru kwa dhati ya moyo wangu, wapiga kura wangu wa Jimbo la Ukonga, kwa imani na ushirikiano mkubwa wanaonipa, katika utekelezaji wa majukumu yangu ya Kibunge. Naendelea kuwaahidi utumishi uliotukuka na kamwe sitawaangusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee napenda kuishukuru familia yangu, kwa kunifariji na kunitia moyo katika kutekeleza majukumu yangu, lakini zaidi sana kwa kunivumilia, hasa pale ninapokuwa mbali nao, kutokana na shughuli zangu za Kibunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu inayofuata ngaliba amepitia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia nimshukuru Kiongozi wa Kambi wa Kambi ya Upinzani Rasmi Bungeni Mheshimiwa Freeman Aikael Mbowe Mwenyekiti wa CHADEMA Taifa na Mbunge wa Jimbo la Hai, kwa kuwa na imani na mimi na kuniteua kuwa Naibu Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda wa kufanya kazi katika Taasisi za Serikali ni masaa nane kuanzia saa moja na nusu asubuhi hadi saa tisa na nusu alasiri. Ikiwa mtumishi yeyote ataendelea kufanya kazi baada ya saa tisa na nusu alasiri kwa sababu yoyote ile, atahesabika kwamba amefanya kazi katika muda wa ziada wa kazi na atastahili kulipwa posho ya masaa ya ziada ya kazi yaani *overtime allowance*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kawaida Wanajeshi walikuwa wanafanya kazi hadi saa tisa na nusu alasiri na kurejea nyumbani au kambini, lakini kimsingi Wanajeshi wapo kazini masaa yote, kwa kuwa kukitokea dharura yoyote, huwa wanaitwa na kushughulikia dharura iliyojitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni, kwa hali ambayo siyo ya kawaida, Wanajeshi wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania wamepewa amri ya kuwepo kazini hadi saa kumi na mbili jioni bila kuelezwa sababu ya kufanya hivyo. Kutokana na hali hiyo, Wanajeshi wamepokea taarifa hiyo kwa taharuki kubwa na kwa mtazamo hasi, jambo ambalo siyo afya kwa utendaji katika Jeshi letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la msingi hapa ni kwamba, dhamira ya kuongeza muda wa kazi ni nini? Je, kuna tangazo la hali ya hatari nchini ambapo sasa inabidi Wanajeshi wafanye kazi ya ziada? Je, kuna *mission* yoyote waliyopewa ikafeli, kwa hiyo sasa wanapewa adhabu kwa kufanya kazi ya ziada?(Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikumbukwe kwamba Jeshi letu limesifiwa kote duniani kuwa ni Jeshi lenye weledi na nidhamu ya hali ya juu, hata Waziri hapa amewapongeza kwa hilo. Kama Jeshi hilo lina weledi mkubwa na nidhamu ya hali ya juu, hata kusifiwa katika medani za Kimataifa, kumetokea nini cha ajabu hadi wafanyishwe kazi kwa masaa yote hayo? Au weledi wao na nidhamu yao imeshuka? Kwa hiyo, wako katika prorogramu maalum ya kuongeza weledi na nidhamu? Kama hivyo, ndivyo, programu hiyo itadumu kwa muda gani.(Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vema Serikali ikaweka bayana dhamira na lengo la kuongeza muda wa kazi Jeshini hadi kufikia saa 12 jioni, ili Wanajeshi wafanye kazi kwa moyo mkunjufu. Bila kufanya hivyo, watakuwa na dukuduku na kibaya zaidi ni kwamba, wataweza kuwa na mgomo baridi kutokana na kutoridhika na uamuzi huo na hivyo kuathiri ufanisi na tija ya Jeshi zima.

*Mheshimiwa Mwenyekiti, athari za kuongeza muda wa kufanya kazi kwa Wanajeshi ni nyingi na zinamgusa Mwanajeshi mmoja mmoja na Taifa zima kwa ujumla. Athari mojawapo kubwa ni kuhatarisha ulinzi na usalama nchini. Katika mazingira ya Dar es Salaam, mathalani, ambako kuna shida ya usafiri, hali ya ulinzi na usalama kuanzia saa 12 jioni hadi saa nne usiku wakati Wanajeshi wanapokuwa wanarudi nyumbani, inakuwa ngumu sana Polisi wanapata shida kufanya doria kwa kuwa wanakuwa na Wanajeshi wengi, kwa hiyo itawawia vigumu wakati mwingine kutambua nani Mwanajeshi nani siyo Mwanajeshi katika mazingira hayo.*

*Mheshimiwa Mwenyekiti, athari nyingine kubwa ya kuongeza muda wa kufanya kazi ni kudorora kwa mahusiano ya kifamilia miongoni mwa Wanajeshi. Tukichulia tena mfano wa changamoto ya usafiri Dar es Salaam, ili Mwanajeshi aweze kufika kazini saa moja asubuhi ni lazima awe ameondoka nyumbani kwake angalau saa kumi au saa kumi na moja alfajiri. Muda huo watoto wake bado wamelala.*

*Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa changamoto hiyo ya usafiri, atarudi nyumbani saa nne mpaka saa tano usiku anakuta watoto wameshalala. Kwa mwendelezo huo, kuna siku watoto hao wanaweza kumwita Baba Mjomba au Mama wakamwita Shangazi kwa kuwa hawajui kama kweli hao ndiyo wazazi wao halisi...* ***[Maneno haya sio sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]***

**MHE. KAPT. (MST) GEORGE H. MKUCHIKA:** Mwongozo wa Mwenyekiti

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara....

**MHE. MWITA C. WAITARA (K.n.y MSEMAJI MKUU WA UPINZANI WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA):** Mheshimiwa Mwenyekiti naomba niendelee...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara hebu subiri, kaa katika kiti chako.

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. KAPT. (MST) GEORGE H. MKUCHIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nataka ku-*declare interest* kwamba mimi ni Mwanajeshi Mstaafu. Naomba huo mwongozo wako kwamba, katika kazi za Jeshi tunaapa kulinda nchi muda wa saa 24 usiku na mchana. Katika kazi za Jeshi tunatii amri ya mkubwa wako bila kuuliza maswali. Katika kazi za Jeshi Kamanda anaruhusiwa kutoa amri atakayoona ina manufaa kwa nchi. *(Makofi)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Kuhusu utaratibu.

**MHE. KAPT. (MST) GEORGE H. MKUCHIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo aliyotoa Kamandi ya kuongeza muda wa kufanya kazi hapaswi kuhojiwa na mtu yeyote. Kwa hiyo, naomba mwongozo wako, naomba tu upande wa pili muwe na nidhamu, mkae. Naomba mkae na Mheshimiwa Mbunge yule amewasha kipaza sauti, Mheshimiwa amewasha...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mkuchika unazungumza na Kiti unazungumza na Wabunge? Zungumza na Kiti .

**MHE. KAPT. (MST) GEORGE H. MKUCHIKA:** Sijamaliza kuomba mwongozo.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge subirini, Kwanza Mheshimiwa Halima Mdee kaa chini, tabia ya kusimama bila kuitwa ni kosa la Kibunge, kama una hoja muache azungumze hoja yake, simama nawe utapewa nafasi.

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** No no no! bado mnabisha? jengo limezungukwa na pingu leo hili. Subirini, kaa chini. Mheshimiwa Mkuchika.

**MHE. CAPT. (MST) GEORGE H. MKUCHIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo...

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliendelea kuongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hamuwezi kukiongoza Kiti, Kiti kinawaongoza ninyi kama unaona unapoteza muda toka nje, ukakae nje ama nenda kantini. Ndio maana yake! Kwa sababu mnakosa nidhamu, mnataka kuingilia shughuli za Kiti. Unasikitika kitu gani Mheshimiwa Rukia.

**MHE. CAPT. (MST) GEORGE H. MKUCHIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo ninaouomba ni kwanba...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mkuchika subiri kaa kwanza..

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliendelea kuongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kama kuna mtu anasimama kuomba mwongozo kwenye Wizara hii nyeti, ziko taratibu za kuuliza, kama ni Mwongozo au kama ni Taarifa. Mheshimiwa Mkuchika kama unatoa taarifa au unatoa mwongozo toa sasa nikusikilize na isiwe ni mjadala. Haya nayasema mimi siyo ninyi, msubiri amalize.

**MHE. CAPT. (MST) GEORGE H. MKUCHIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo ninaouomba kutoka kwako ni kwamba Kamanda ametoa amri kwa jinsi ilivyoona inafaa. Je, Bunge hili lina majukumu ya kumpangia Kamanda lini atoe amri na lini asitoe.*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, haya Mheshimiwa Paresso, hapa anasimama *Chief Whip,* wewe Halima kaa. (*Kicheko*)

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Kiti chako kisiyumbe, kwa sababu...

**MWENYEKITI:** Kwanza ukishasema Kiti kinayumba tutayumba mimi na wewe hapa, ukisema Kiti kinayumba nitayumba na wewe. Wewe sema hoja yako. *(Kicheko)*

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ni kwamba, kwa mujibu wa Kanuni na Taratibu zetu na kwa mujibu wa uendeshaji wa Bunge, Msemaji wa Kambi ya Upinzani au hata Waziri akiwa anasoma pale huwa hakuna Taarifa wala Mwongozo. Mwongozo na Taarifa unakuja baada ya uwasilishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tayari Ofisi yako imeshapitia, ikaondoa, ikakata baadhi ya maneno kwa nini bado baadhi ya Wabunge akiwepo Mheshimiwa Mkuchika anaingilia. Kwa hiyo, tunaomba Kiti chako kiruhusu isomwe, kama Mbunge yeyote ana hoja zaidi ya hapo ataieleza baadae wakati wa uchangiaji. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sawa. Waheshimiwa Wabunge, Taarifa hii ameshapitia Mheshimiwa Spika, lakini haizuii Mbunge yeyote mwingine akiona kuna kasoro ndani ya Taarifa na pili, hatuzungumzii taarifa za Wizara ya Maji wala Wizara ya Umeme humu ndani. Mheshimiwa haya maneno yana *allegation* nzito sana. Unaweza ukaulizwa uthibitishe umezitoa wapi, Bunge linaweza likasema tunaomba uthibitisho wa hizi tuhuma. Kwa hiyo, ninachokuomba Mheshimiwa Waitara...

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, msicheze na *impatience* yangu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Waitara, kuna vitu humu ndani vinaweza

vikakubana mwenyewe. Kuna maneno ambayo unayatumia yanaweza yakakubana mwenyewe, utashindwa kabisa kuyathibitisha haya maneno unayosema. Siyo mazuri kwako. Nilitoa *ruling* mwanzo kama kuna vitu ambavyo unaviona vinaathiri (vina changamoto) yako maeneo ambayo unaweza ukazipeleka hizi taarifa zikashughulikiwa. Kuna maneno ambayo unaweza ukayabeba, ukayaokota mitaani, yatakuathiri mwenyewe ndani ya Bunge.

Mheshimiwa Mbunge, kwa hiyo, nakuomba, maeneo yote haya yaliyosemwa hapa ya watu kuchelewa nyumbani yote nayatoa kwenye *Hansard.* Endelea na taarifa yako.

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MHE. MWITA C. WAITARA (K.n.y. MHE. JUMA HAMAD OMAR - MSEMAJI MKUU WA UPINZANI WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba muda wangu ulindwe. Haya ambayo hampendi kuyasikia ndiyo hoja na malalamiko ya Wanajeshi huko waliko. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Wewe endelea.

**MHE. MWITA C. WAITARA (K.n.y. MHE. JUMA HAMAD OMAR - MSEMAJI MKUU WA UPINZANI WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA)::** Mheshimiwa Mwenyekiti, athari nyingine ni ya kiuchumi. Wanajeshi wanapokuwa wakitoka kazini saa tisa na nusu alasiri walikuwa na muda wa kufanya shughuli za kijasiriamali ili kupunguza ukali wa maisha kutokana na posho zao kuwa ni kidogo. Kwa mabadiliko haya ya muda wa kufanya kazi, hakuna muda tena kufanya kazi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maelezo yote hapo juu, itoshe kusema Serikali itoe maelezo ya sababu za kuongeza muda wa kufanya kazi Jeshini ili kuwe na ufahamu wa pamoja baina ya Serikali na Jeshi na hivyo kuondoa manung'uniko miongoni mwa Wanajeshi na hatimaye kuongeza ufanisi Jeshini. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inaitaka Serikali kulieleza Bunge hili, iwapo

imewalipa Wanajeshi posho ya masaa ya ziada ya kazi *(overtime allowance)* tangu walipoanza kutekeleza amri ya kufanya kazi hadi saa 12 jioni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kusitishwa kwa utoaji wa fedha za likizo kwa Wanajeshi. Likizo ni stahiki ya kisheria ya mtumishi yoyote iwe ni katika Sekta ya Umma au Sekta Binafsi. Msingi wa likizo ni kumpatia mtumishi muda wa kupumzika, kubadili mazingira ya kazi na hivyo ku-*refresh* akili na hatimaye kurudi kazini akiwa na ari na nguvu mpya ya kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo likizo zenye malipo na ambazo hazina malipo. Yapo malalamiko miongoni mwa Wanajeshi kwamba malipo ya fedha za likizo, kwa likizo zenye malipo yamesitishwa kimya kimya bila Wanajeshi kupewa taarifa ya kinachoendelea. Kwa mujibu wa taarifa kutoka kwa baadhi ya Wanajeshi ni kwamba, mara tu walipoanza kuulizia fedha zao za likizo walitishwa na *Chief of Staff* kuwa ni marufuku kuulizia na kuzungumzia popote kuhusu fedha hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kulieleza Bunge hili, kama haitaki Wanajeshi watoe malalamiko yao kwa ngazi husika ndani ya Jeshi wanataka wakatoe malalamiko yao wapi? Kitendo cha kuwatisha Wanajeshi, kwa kuwapiga marufuku kuyazungumzia maslahi yao halali, tena ndani ya mamlaka za ndani ya Jeshi, ni cha kulaaniwa na anayefanya hivyo achukuliwe hatua, kwani anachochea hasira miongoni mwa Wanajeshi, jambo ambalo linaweza kupelekea uasi ndani ya Jeshi na kuhatarisha amani na usalama wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kuitahadharisha Serikali kuwa, vikosi vya waasi kama vile Boko Haram, Al-Shaabab na M23 vilianza kutokana madai madogo madogo ndani vya vikosi vyao vya Jeshi ambayo hayakuthaminiwa wala kushughulikiwa. Hadi ninapozungumza hapa, kwa mujibu wa taarifa ya *DW* na *BBC* ya jana asubuhi ni kwamba, Jeshi la *Ivory Coast* limeasi

kutokana na madai ya malipo ya fedha ambayo Serikali ya *Ivory Coast* haikufanyia kazi mapema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kushughulikia madai na mahitaji mengine ya msingi yanayowahusu Wanajeshi kwa wakati, kwa kuwa yanapoanza kusikika nje yanashusha hadhi ya Jeshi letu. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, haikupaswa kujua madai hayo, lakini imeyajua kwa kuwa, hayapewi uzito unaostahili na wala hayashughulikiwi na Wanajeshi hawaruhusiwi kuandamana, hivyo lazima watafute sehemu ya kupumulia na ni kupitia Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhana ya kubana matumizi Serikalini inavyoathiri misingi ya kuanzishwa kwa Jeshi la Ulinzi. Kutokana na azma ya Serikali ya Awamu ya Tano kubana matumizi ya Serikali, tayari Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama ameanza kutekeleza azma hiyo, kwa kuwaagiza Wakuu wa Vikosi kumuunga Rais mkono kubana matumizi ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, akiwa katika ziara ya kutembela vikosi mbalimbali baada ya kuapishwa kushika wadhifa huo, Mkuu wa Majeshi alinukuliwa akiwaagiza Wakuu wa Vikosi kuanza kubuni miradi ya uzalishaji mali ili waweze kujiendesha kwa matumizi madogo madogo kama vile vifaa vya ofisi yaani *stationaries.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, agizo hilo la kufanya shughuli za uzalishaji mali linakiuka msingi mkuu wa uanzishwaji wa wa Jeshi la Wananchi, Jeshi la Ulinzi ambalo ni ulinzi na usalama wa mipaka ya nchi yetu. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatambua kwamba kipo kitengo cha uzalishaji mali katika Jeshi la Kujenga Taifa yaani SUMA JKT, na kinafanya kazi nzuri. Jambo la msingi ni kuiwezesha SUMA JKT ili izalishe kwa wingi na kuchangia gharama hizo siyo kulifanya Jeshi zima kuwa la uzalishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, manunuzi ya vifaa mbalimbali Jeshini. Ninapozungumzia vifaa Jeshini nadhani naeleweka,

vifaa Jeshini siyo vifaa vya kawaida, ni vifaa ambavyo ni *sensitive* na kwa maana hiyo, manunuzi yake pamoja na utunzaji wake, lazima ufanywe kwa makini na weledi wa hali ya juu ili kuepuka madhara yanayoweza kutokea kutokana na *mismanagement.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo taarifa kwamba Maafisa wa ngazi za juu waliopo kwenye Bodi ya Manunuzi ndiyo wanaojipa nafasi ya kwenda nje kununua vifaa hivyo na kuwaacha Maafisa wenye utaaalam na vifaa hivyo. Matokeo yake ni kwamba vinanunuliwa vifaa vinavyogharimu mabilioni ya fedha, ambavyo ama vimepita muda wake wa matumizi au havifai kutumiwa katika mazingira yetu na hivyo kuisababishia hasara Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu inayofuata kisu cha Ngariba kimepitia. Kwa hiyo nitaparuka kwa heshima ya Kiti chako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inatokana na Bodi ya Manunuzi kutofuata taratibu za manunuzi na sababu kubwa ya kutokufanya hivyo, ni tamaa ya kifedha na imebainika kwamba wanajipangia kwenda kufanya manunuzi hayo ili wapate posho ya safari na maslahi mengine. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali *with a serious note* kwamba isifanye mzaha kwenye eneo hili la manunuzi ya vifaa, kwani licha ya eneo hilo kutumia fedha nyingi pengine kuliko maeneo hayo yote.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

**MHE. MWITA C. WAITARA (K.n.y. MHE. JUMA HAMAD OMAR - MSEMAJI MKUU WA UPINZANI WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nafasi ya Mkuu wa wa Majeshi katika kujenga Jeshi imara lenye nidhamu, utii na mshikamano.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Subirini, kaeni.

**MHE. MWITA C. WAITARA (K.n.y. MHE. JUMA HAMAD OMAR - MSEMAJI MKUU WA UPINZANI WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mkuu wa Majeshi Mstaafu Jenerali Davis Mwamunyange akimkabidhi Mkuu mpya wa Majeshi alimwambia kwamba amelitoa Jeshi kwenye tope na kulifikisha sehemu nzuri na kwamba, Mkuu huyu wa sasa alifikishe kwenye lami.

**MHE. KAPT. (MST) GEORGE H. MKUCHIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo wa Spika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara subiri. Mheshimiwa Mkuchika, Mheshimiwa Gulamali kaa chini.

**MHE. KAPT. (MST) GEORGE H. MKUCHIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimesoma hiyo *paragraph* yote namba sita. Nataka kusema yafuatayo kabla sijaomba mwongozo wako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza *CDF* Mkuu wa Majeshi anateuliwa na Rais kwa jinsi anavyoona inafaa. *CDF* tuliyenae kabla hajateuliwa alikuwa *number two,* kwa hiyo amepandishwa kutoka *number two* kuwa namba moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ninalotaka kusema ni Sheria ya *National Defence Act* ya Mwaka 1966 inasema ni marufuku mtu kusema mambo ya Jeshi kama siyo Msemaji wa Jeshi. Nataka kurudia tena... (Makofi)

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mkuchika Endelea.

**MHE. KAPT. (MST) GEORGE H. MKUCHIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Watakomaa lini hawa?

**MWENYEKITI:** Zima hiyo *microphone* pembeni yako hapo.

**MHE. KAPT. (MST) GEORGE H. MKUCHIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Ulinzi ya Mwaka 1966 inasema: Marufuku mtu ambaye si Msemaji wa Jeshi kusema mambo ya Jeshi. Hata Wanajeshi wenyewe, hata awe Meja Jenerali, hata awe nani, marufuku kuongea masuala ya Jeshi kwa vyombo vya habari, kwa umma kama si Msemaji wa Jeshi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *paragraph* hii yote inazungumza mwenendo wa Jeshi na utendaji kazi wa *CDF.* Kwa hiyo, najua ningeliweza watoe kwa sababu siyo Wanajeshi. Ningeweza kuomba waeleze maneno hayo wameyatoa wapi, watapata matatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo ninaouomba au ushauri, *paragraph* yote ya sita inazungumza mwenendo wa Jeshi ifutwe katika kitabu hiki na usiruhusu kusomwa. Naomba Mwongozo wako. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Paresso unataka kusema nini?

*(Hapa Mbunge fulani aliongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa usiingilie kazi ya Kiti. *(Makofi)*

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Mwongozo wako kwa sababu hizo hoja anazosema Mheshimiwa Mkuchika, nadhani ni fursa ya Waziri baadae kuja kujibu kama kuna hoja ambazo zimekuwa *raised* na Kambi ya Upinzani. Ndiyo utaratibu wa uendeshaji bora wa Bunge humu ndani umekuwa ukitumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sana Kiti chako kizingatie haya.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa nimepitia ukurasa wa 11 *paragraph* ya sita. Ni kweli anachosema Mheshimiwa Mkuchika haya mambo hayatakiwi yawe *public, this is classified information.* Kwenye masuala ya kujibu, kuna

mambo mengi ya Jeshi hayazungumzwi humu wala pesa zao hazitoki humu *including* utendaji huu ambao ameuandika Mheshimiwa Waitara kama haukuonekana mwanzo mimi nauona. Kwa mamlaka ya Kiti, *paragraph* hii ya sita, ukurasa wa 11 yote nayatoa, na wewe usiyasome. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waitara kwa hiyo, anza ukurasa wa 12. Twende.

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika.

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, kaeni chini wote.

**MHE. MWITA C. WAITARA (K.n.y. MHE. JUMA HAMAD OMAR - MSEMAJI MKUU WA UPINZANI WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Hii ni shida ya kupokea taarifa vipande vipande, lakini ujumbe umefika. Hatujadili utendaji wa *CDF* tunazungumza mambo yakafanyiwe kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuelewa lakini ujumbe umefika, naenda sasa ukurasa wa 13 namba saba; huduma ya nishati ya umeme...

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Mwacheni asome, mngetaka si mngekuja msome ninyi hapa mbele?

**MHE. MWITA C. WAITARA (K.n.y. MHE. JUMA HAMAD OMAR - MSEMAJI MKUU WA UPINZANI WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Taarifa kama ilivyowasilishwa iingie kwenye *Hansard* yote pamoja na marekebisho yake...

**MWENYEKITI:** Msipige kelele hapa siyo sokoni wala *canteen* hapa. *No, no!* kutokuwa na nidhamu, kwa mujibu wa Kanuni *keep quiet.*

**MBUNGE FULANI:** Acha ubabe.

**MWENYEKITI:** Ndiyo maana yake.

**MHE. MWITA C. WAITARA (K.n.y. MHE. JUMA HAMAD OMAR - MSEMAJI MKUU WA UPINZANI WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma ya nishati ya umeme katika Kambi za Jeshi. Ni jambo linalofahamika kwamba, Taasisi za Umma hulipia gharama za huduma mbalimbali kama vile huduma za maji na umeme, kupitia bajeti ya matumizi mengineyo *(OC)* inayotolewa na Hazina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, Taasisi nyingi za Umma yakiwemo Majeshi yetu yamekuwa yakishindwa kulipia huduma hizo kutokana na bajeti ndogo ya matumizi mengineyo na mbaya zaidi fedha za *OC* hazitolewi kwa ukamilifu wake na hata hizo kidogo zinazotolewa huchelewa. *(Makofi)*

*Mheshimiwa Mwenyekiti, dawa ya kuondokana na udaiwa sugu kwa Taasisi za Umma yakiwemo Majeshi ni Serikali kutoa fedha za matumizi mengineyo kwa utoshelevu na kwa wakati na siyo Serikali kuyaamuru makampuni au mashirika yanayotoa huduma kukata huduma hizo kwa Taasisi za Umma kwa kutumia neno 'KATA'. (Makofi/Kicheko)*

*Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatafsiri kitendo cha Mkuu wa Nchi kuiamuru TANESCO kukata umeme kwenye kambi za Jeshi kuwa ni kuhatarisha usalama wa nchi. Jeshi ni taasisi nyeti katika usalama wa nchi, na kwa maana hiyo, Serikali inatakiwa kuhakikisha kuwa, huduma zote zikiwemo maji, umeme, afya na kadhalika zinapatikana kwa utoshelevu ili Jeshi liweze kuendelea kufanya kazi zake za kulinda usalama wa nchi yetu dhidi ya adui yeyote. Ikiwa Jeshi limeshindwa kulipia huduma*

*hizo, basi Serikali ndiyo inayotakiwa kuwajibika kwa kutotoa fedha za kutosha za OC kulipia gharama hizo....* ***[Maneno haya siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]***

Mheshimiwa Mwenyekiti, usalama wa mipaka ya nchi. Kumekuwa na mvutano kuhusu mpaka wa Malawi na Tazania hususan katika Ziwa Nyasa. Hata hivyo, Serikali kwa nyakati tofauti imekuwa ikisema kwamba mgogoro huo unashughulikiwa kwa ajili ya kuupatia ufumbuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya Serikali kusema kuwa, kuna dalili njema ya maafikiano kuhusu mgogoro huo, kuna viashiria kwamba majirani zetu wa Malawi hawaafikiani na usuluhishi wowote utakaowafanya wasimiliki Ziwa lote la Nyasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Mtandano wa *extractives* ni kwamba Serikali ya Malawi imeweka msimamo kwamba haitakubaliana na usuluhishi wowote ambao utaipa Tanzania sehemu ya Ziwa Nyasa. Jambo hili linathibitishwa na Kauli ya aliyekuwa Katibu Mkuu Kiongozi wa Serikali ya Malawi, Ndugu George Mkondiwa kwamba; *"Malawi will never, and has never, at any time, acquiesced to Tanzania's unwarranted and unjustified territorial claims,"*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kauli kama hiyo, kutoka kwa Kiongozi mkubwa katika Serikali ya Malawi, huku mazungumzo ya usuluhishi yakiendelea, kwa vyovyote vile ni kauli nzito na Tanzania haipaswi kuipuuza. Kwa sababu hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kujua mazungumzo yaliyokuwa yakiendelea kuhusu usuluhishi wa mgogoro wa mpaka katika ya Tanzania na Malawi yamefikia wapi, na ni nini hatma ya mgogoro huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kueleza hali ya usalama wa mipaka ya Tanzania kwa ujumla wake, ambayo kwa siku za nyuma iligundulika kuwa *beacons* za mipaka hiyo zilikuwa

zimeng'olewa na pia raia kutoka nchi jirani walikuwa wanaingia nchini mwetu kwa njia za panya kutokana na mipaka yetu kupenyeka kirahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafasi ya Jeshi katika kupambana na matukio ya kigaidi nchini.'

**MHE. KAPT. (MST) GEORGE H. MKUCHIKA:** Kuhusu Utaratibu.

**MHE. MWITA C. WAITARA (K.n.y. MHE. JUMA HAMAD OMAR - MSEMAJI MKUU WA UPINZANI WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA):** Sawa Jecha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mkuchika.

## KUHUSU UTARATIBU

**MHE. KAPT. (MST). GEORGE H. MKUCHIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama kwa mujibu wa Kifungu Namba 64 majadiliano yetu Bungeni, ambacho kinasema: Mbunge hatatumia jina la Rais kwa dhihaka katika mjadala kwa madhumuni ya kutaka kulishawishi Bunge kuamua jambo lolote kwa namna fulani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukurasa wa 14 Msemaji wa Kambi ya Upinzani anasema Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatafsiri kitendo cha Mkuu wa nchi kuamuru *TANESCO* kukata umeme kwenye Kambi za Jeshi kuwa ni kuhatarisha usalama wa nchi. Mkuu wa Nchi hapa anatuhumiwa kwa kuhatarisha usalama wa nchi. Ninavyofahamu agizo la Mheshimiwa Rais amesema watu wote ambao wametumia umeme hawajalipa, walipe. Hajaamrisha kukata...

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MHE. KAPT. (MST). GEORGE H. MKUCHIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kwa maoni yangu...

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Subiri kwanza, subiri, Mheshimiwa Mkuchika endelea.

**MHE. KAPT. (MST). GEORGE H. MKUCHIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maoni yangu maneno haya yanazungumzia mwenendo wa Rais ambaye tumekatazwa kuzungumza hapa ndani.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima kabisa kwanza nimpe Taarifa baba yangu pale naona ameamua kupata dakika tatu, nne za kuchangia na kupoteza muda wetu wa Bunge...

**MWENYEKITI:** Kaa chini huna Taarifa.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu Mheshimiwa Rais alisikika akisema kabisa na akataja Jeshi kwamba likatiwe umeme.

**MWENYEKITI:** Kaa chini.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Kwa hiyo, asipotoshe na asitupotezee muda wa Bunge.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nataka tumalize kwa usalama hapa.

**MHE. UPENDO F. PENEZA:** Kuhusu Utaratibu.

**MWENYEKITI:** Kaa chini, Upendo kaa chini. Naomba tumalize kwa usalama. Yapo maneno ambayo kwa kweli kwa mujibu wa Kanuni zetu hayaruhusiwi na ninyi mnayafanya si sababu hamjui. Unaposema inatafsiriwa kitendo cha Mkuu wa Nchi kuiamuru *TANESCO...* Hawakuambiwa waende kwenye vyombo vya ulinzi...

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Ilikwenda yote kwa ujumla. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waitara utaendelea na Taarifa yako na baadhi ya haya maneno natoa kwenye *Hansard.* Endelea Mheshimiwa Waitara.

**MHE. UPENDO F. PENEZA:** Kuhusu Utaratibu…

**MWENYEKITI:** Kaa chini.

**MHE. UPENDO F. PENEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Kuhusu Utaratibu…

**MWENYEKITI:** Nazungumza na *Chief Whip* wenu tu basi. Kaa chini.

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MHE. MWITA C. WAITARA (K.n.y. MHE. JUMA HAMAD OMAR - MSEMAJI MKUU WA UPINZANI WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba muda wangu ulindwe.

**MWENYEKITI:** Utalindwa, endelea.

**MHE. MWITA C. WAITARA (K.n.y. MHE. JUMA HAMAD OMAR - MSEMAJI MKUU WA UPINZANI WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, wazingatie tu, cha muhimu hapa ni umeme urudishwe Jeshini, usikatwe, basi! Kelele zote zitakwisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uteuzi wa Wanajeshi katika nafasi za kisiasa. Katika hotuba yake mwaka jana, Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni alizungumzia athari za kuwateua Wanajeshi katika nafasi za kisiasa. Alionesha jinsi ambavyo Mwanajeshi anayeteuliwa kuwa Mkuu wa Wilaya au Mkuu wa Mkoa anavyounganishwa na Chama Tawala, kwa kutakiwa kuwa Mjumbe wa Kamati ya Siasa ya Chama katika Wilaya au Mkoa husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuunganishwa huku na Chama, kumewekwa bayana na Katiba ya CCM ya mwaka 1977, katika Ibara ya 80(1)(c) inayowataja Wakuu wa Wilaya kuwa Wajumbe wa Kamati ya Siasa ya CCM katika Wilaya husika na Ibara ya 94(1)(c) inayowataja Wakuu wa Mikoa kuwa Wajumbe wa Kamati ya Siasa ya CCM katika Mikoa husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitendo cha Katiba ya CCM kuwatambua Wakuu wa Wilaya na Mikoa kama Wajumbe wa Kamati ya Siasa ya Wilaya au Mkoa husika, kinadhihirisha kwamba, Wakuu hao ni wanachama wa chama cha siasa, na kwa maana hiyo ni wanasiasa. Kwa hiyo, Mwanajeshi anayeteuliwa kuwa Mkuu wa Wilaya au Mkoa *automatically* anakuwa mwanachama wa Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maelezo yake, alinukuu Ibara ya 147(3) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayosema kwamba:

*"Itakuwa ni marufuku kwa Mwanajeshi yeyote kujiunga na chama chochote cha siasa, isipokuwa tu kama atakuwa na haki ya kupiga kura iliyotajwa katika Ibara ya Tano (5) ya Katiba hii."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Ibara ndogo ya (4) inasema kwamba:

*"Kwa madhumuni ya Ibara hii Mwanajeshi maana yake ni Askari aliyeajiriwa kwa masharti ya muda au ya kudumu katika Jeshi la Ulinzi, Jeshi la Polisi, Jeshi la Magereza au Jeshi la Kujenga Taifa."*

Uteuzi huu wa Wanajeshi kushika nafasi za kisiasa umetanuliwa wigo wake, ambapo sasa Wanajeshi wanaanza kuteuliwa na Chama Tawala kuwa Viongozi wa Chama. Uteuzi wa Kanali Ngemela Eslom Lubinga kuwa Katibu wa *NEC* ya Chama cha Mapinduzi Siasa na Uhusiano wa Kimataifa ni uthibitisho kwamba Jeshi linaingizwa kwenye siasa kidogo kidogo *(Politicization of the army). (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, athari za jambo hili ni kwamba Jeshi litaanza kupoteza ile sifa yake ya kuwa Jeshi la Wananchi na badala yake litaanza kufanya kazi kwa *bias* – kwa kupokea amri na maagizo ya Chama Tawala. Athari kubwa zaidi ni kwamba, utawala wa kiraia *(Civil Governance)* utapoteza maana yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatafsiri kitendo cha kuendelea kuwateua Wanajeshi kushika nafasi za kisiasa hata baada ya kutahadharishwa ni mwendelezo wa vitendo vya Serikali hii ya Awamu ya Tano vya kupuuza Katiba ya nchi yetu, jambo ambalo halina afya sana katika utawala bora. Kwa sababu hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutoa maelezo mbele ya Bunge hili, ni kwa nini haiheshimu katazo la Ibara ya 147(3) na (4) ya Katiba kuhusu Wanajeshi kujihusisha na kazi za siasa?

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Kuhusu taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lukuvi. Mheshimiwa Waitara, hebu subiri kwanza kwani hunisikii, basi kakae.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampa taarifa Kada wetu wa zamani, huyu alikuwa Katibu wa Vijana wa Umoja wa Vijana CCM. Nadhani ameisoma vibaya Katiba yetu. Mwanajeshi anapoteuliwa kuwa Mkuu wa Wilaya, Mkuu wa Mkoa hapewi kadi ya CCM, Mheshimiwa Mbunge unapoitwa Diwani kuingia kwenye *Council,* uligombea Udiwani? Nasema ni kama Mheshimiwa Diwani anapoingia kwenye Kikao cha *Council* lakini bado anaitwa Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huyu Mkuu wa Wilaya na Mkuu wa Mkoa anaingia kwa sababu ya utaratibu wa kikatiba. Chama Tawala ndicho kinachoisimamia Serikali. Kwa vyovyote vile, Chama chochote kinachotawala lazima kinakuwa na utaratibu wa watendaji waliowekwa kwenye

madaraka kwenda kutoa taarifa za utekelezaji wa Ilani. Sio kwa maana ya wanachama. Ndiyo maana na ninyi mnaingia kwenye *Council* unawekwa kwenye Kamati zile za Madiwani mkijua ninyi ni Wabunge. Kwa hiyo, tusipotoshe hapa kwamba wanapewa kadi, hawapewi kadi na CCM, mtu yoyote mwenye uthibitisho huo atuletee hapa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI**: Ahsante wameshakuelewa, Mheshimiwa *Chief Whip* wa Upinzani

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakuomba kwa heshima kubwa sana, hizi hoja zinaweza kujibiwa baadaye wakati fursa ya uchangiaji ikisha fikia tunaomba hotuba yetu isomwe imalizwe, hoja hizo zijibiwe baadaye.

**MWENYEKITI**: Kaa chini nimeshakuelewa, Mheshimiwa Waitara endelea na taarifa unaipokea hiyo?

**MHE. MWITA C. WAITARA (K.n.y. MHE. JUMA HAMAD OMAR - MSEMAJI MKUU WA UPINZANI WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya ndugu yangu kada wa Chama cha Mapinduzi na Waziri wa Nchi, siipokei kwa sababu ya uwongo inapotesha ukweli.

**MWENYEKITI:** Endelea na taarifa yako.

**MHE. MWITA C. WAITARA (K.n.y. MHE. JUMA HAMAD OMAR - MSEMAJI MKUU WA UPINZANI WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naomba niendelee, hawa ni Wajumbe wa Kamati za Siasa wa Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba hilo Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa maelezo ni kwa nini Wanajeshi wanaoteuliwa kushika nafasi za kisiasa wanaendelea kuvaa *uniform* za Kijeshi wakati ilitakiwa wastaafu kwanza Jeshi ili sasa wawe Watumishi wa Umma?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu posho ya chakula *(ration allowance)*. Mheshimiwa Mkuchika vipi hajasimama! *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa miaka mingi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imekuwa mstari wa mbele kutetea maslahi ya Wanajeshi wetu ikiwemo posho ya chakula *(ration allowance)*. Msingi wa kutetea maslahi ya Wanajeshi ni kuwapatia Wanajeshi wetu lishe bora na kuwafanya wawe na nguvu ya kuhimili mazoezi na kazi mbalimbali za kiaskari wanazofanya. Aidha, lengo lingine ni kuwafanya wawe na utulivu wa ndani ili waweze kufanya kazi yao ya kulinda usalama wa nchi yetu wakiwa hawana mawazo ya kwamba watakula nini pamoja na familia zao na ndugu wanaowategemea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu uliopo ni kwamba, posho hii ya chakula hutolewa moja kwa moja kwa Askari kila mwezi. Askari anayepokea posho hii huwa na uhuru wa kuitumia au kutokuitumia pamoja na familia yake. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inazo taarifa kwamba kuna mkakati wa kubadili mfumo wa utoaji wa posho hiyo kwa Wanajeshi. Utaratibu mpya unaotaka kuanza kutumika ni kwamba Wanajeshi hawatapewa tena posho badala yake itapelekwa Kantini na wataanza kula chakula kama wanafunzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi Bungeni inaitaka Serikali kuufuta utaratibu huo na kuendelea kutoa posho ya chakula moja kwa moja kwa Wanajeshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema mwanzo taarifa yangu yote iingizwe kwenye *Hansard* kama itashindwa kumalizika ndani ya muda uliopangwa baada ya shughuli nyingi za kusumbuasumbua katika hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushirikiano wa Jeshi na Mataifa mengine. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatambua Jeshi la Wananchi wa Tanzania linashiriki katika operesheni za Kijeshi katika mataifa mengine kupitia katika

Mpango wa kulinda amani wa Umoja wa Afrika na ule wa Umoja wa Mataifa. Pamoja na kwamba ushiriki huu unaliongezea Jeshi letu uzoefu wa kufanya kazi katika mazingira tofauti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutafakari upya faida hususan za kiuchumi na kiteknolojia ambazo kama Taifa tunanufaika nazo kwa Jeshi letu kushiriki katika operesheni hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inapendekeza hivi kwa sababu kama Taifa tusipojipanga kimkakati zaidi, tutaishia kupokea miili ya Wanajeshi wetu waliokufa katika operesheni hizo huku Taifa likibaki bila manufaa yoyote. Kwa sababu hiyo, tunapendekeza kwamba kuwe na malengo mahsusi na ya kimkakati Jeshi letu linapokwenda kushiriki operesheni katika Mataifa mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikakati hiyo iwe ni pamoja na kufanya utafiti wa masuala ya kiuchumi na kiteknolojia yaani kwa maneno mengine wafanye ujasusi wa kiuchumi *(economic espionage)* ili baada ya operesheni hizo kuwe na faida ya kidola itakayopatikana na siyo tu maslahi ya kifedha, wanayopata Wanajeshi baada ya kushiriki operesheni hizo.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Kujenga Taifa na Uzalishaji wa Chakula; ni aibu kwa Taifa hili kuwa na matukio ya ukosefu wa chakula na njaa huku kukiwa na Jeshi la Kujenga Taifa. Miaka iliyopita tulipendekeza kuwa pamoja na mambo mengine, Jeshi hili lipimwe kwa uzalishaji ambao litakuwa limefanya. Tulieleza kwamba dhima ya Jeshi la Kujenga Taifa ni kwamba pamoja na mambo mengine, lina wajibu wa kuwafunza vijana wetu kufanya kazi za uzalishaji mali kwa ajili ya kujenga uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imekuwa ikishauri miaka nenda, miaka rudi kwamba Serikali itumie nguvukazi iliyopo kwenye Jeshi la Kujenga Taifa katika kujenga uchumi wa kweli nchini na hasa kipindi hiki cha uchumi wa viwanda Jeshi la Kujenga Taifa ndilo lilitakiwa litoe dira ya namna ya kuwa na uchumi wa viwanda.

Tulishauri kwamba Serikali itenge mashamba makubwa ili vijana hawa wawapo mafunzoni, wafanye mafunzo kwa vitendo ya kilimo ili nchi iweze kujitegemea kwa chakula.

Mheshimwa Mwenyekiti, aidha, tuliishauri Serikali iwaagize Wakuu wa makambi ya JKT kutengeneza programu maalum za uzalishaji mali katika sekta mbalimbali kama vile kilimo, viwanda, ufundi, uvuvi na kadhalika kila mwaka. Tulipendekeza pia kwamba, Waziri mwenye dhamana awe anatoa taarifa ya kazi zilizofanywa na uzalishaji uliofanywa na JKT na mapato maalum (maduhuli) yaliyopatikana kutokana na eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.Kumeanza kutokea mazoea mabaya ya utekelezaji duni wa bajeti ya maendeleo katika Wizara hii jambo ambalo linatia wasiwasi kama kweli Serikali ina nia ya dhati ya kupandisha ubora na ufanisi wa Majeshi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka huu, fedha ya kutekeleza miradi ya maendeleo liyoidhinishwa na Bunge katika Fungu 38 - Ngome ilikuwa ni shilingi bilioni 10, hadi Machi 2017 ilikuwa imetolewa shilingi bilioni moja tu sawa na asilimia 10 ya fedha iliyokuwa imeidhinishwa.

Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kulieleza Bunge hili, hiyo bilioni moja iliyotolewa, ndiyo itaweza kununua zana za kisasa zinazoendana na teknolojia ya sasa, kutoa mafunzo ya Kijeshi ya kisasa na kupandisha ubora na ufanisi wa Jeshi la Wananchi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Fungu 39 - JKT, fedha ya maendeleo iliyoidhinishwa ilikuwa ni shilingi bilioni nane, fedha iliyopatika mpaka sasa ni shilingi bilioni moja tu, sawa na asilimia 12.5 ya fedha iliyokuwa imepitishwa na Bunge hili. Hii ina maana kwamba bajeti ya maendeleo katika Fungu hili haijatekelezwa kwa asilimia 87.5.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inahoji JKT itawezaji kutekeleza miradi yake ya maendeleo kwa madhumuni ya kujenga Taifa ikiwa mwenendo wa utekelezaji wa bajeti uko namna hii? Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutoa maelezo ni kwa nini JKT imekusanya maduhuli kidogo asilimia 31.8 tu wakati ina miradi mingi ya uzalishaji mali chini ya SUMA JKT?

Mheshimiwa Mwenyekiti, halikadhalika kwa upande wa Wizara, fedha iliyokuwa imeidhinishwa na Bunge ilikuwa shilingi bilioni 230, lakini hadi kufikia Machi, 2017 shilingi bilioni 33.9 tu sawa na asilimia 14.7 ilikuwa imetolewa. Tafsiri nyepesi ya utekelezaji huu duni wa bajeti ya maendeleo, unairudisha nyuma Wizara na unapunguza ufanisi, ubora na tija ya Majeshi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka Serikali, kwa kadri ile ambayo inalisifu Jeshi letu kuwa ni imara, lenye weledi na ufanisi mkubwa, basi sifa hizo zionekane katika kutenga fedha na kupeleka fedha yote kutekeleza miradi ya maendeleo katika eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika randama yay a Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa Fungu 57 kuna baadhi ya vitengo havikutengewa fedha kabisa tena fedha za mishahara. Kwa mfano, *Subvote* 1005 – *Procurement Management,* ukurasa wa 18 hakuna fedha yoyote iliyotengwa kwa ajili ya mshahara; *Subvote* 2003 – *Building Consulting Unit*, ukurasa 36 haikutengewa fedha za mshahara kabisa na *Subvote* 2004 – *Estate Management and Development Unit* ukurasa 39 hakuna fedha ya mshahara. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inaitaka Serikali kulieleza Bunge hili ni kwa nini vitengo hivyo havijatengewa fedha za mishahara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho, naomba nimalizie hotuba yangu kwa kulipongeza Jeshi la Wananchi wa Tanzania kwa umahiri mkubwa, kwa jinsi linavyoendesha operesheni zake mbalimbali, lakini zaidi jinsi linavyojishughulisha na masuala ya kijamii kunapotokea

maafa na majanga mbalimbali. Hata hivyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ingependa kujua Jeshi limesaidia vipi kutoa msaada kwa wananchi waliokumbwa na mafuriko kipindi hiki cha masika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni matamanio ya kila raia wa Tanzania kuona Jeshi letu likiendelea kupanda viwango vya ubora na ufanisi na hivyo kuwa na tija. Hata hivyo, ili viwango vipande, lazima mambo kadhaa yashughuliwe kikamilifu. Kwanza, Serikali ihakikishe kwamba, bajeti inayoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya Majeshi yetu inatolewa kwa wakati na kwa ukamilifu wake. Pili, Serikali ihakikishe kwamba, maslahi na stahiki zote za Wanajeshi zinatolewa kwa wakati na kwa ukamilifu wake ili kuondoa manung'uniko miongoni mwa Wanajeshi na hivyo kuwangezea morali ya kufanya kazi kwa moyo.

**MWENYEKITI**: Ahsante. Nimekuongezea dakika nne zimeshakwisha. Kwa hiyo nenda kaketi, upumzike, usubiri majibu.

**HOTUBA YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA MHE. JUMA HAMAD OMAR AKIWASILISHA MAONI YA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KUHUSU BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA FEDHA 2017/2018 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**1. UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Juma Hamad Omar (Mb), naomba kuwasilisha maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka 2016/17 pamoja na makadirio ya mapato na matumizi ya fedha ya wizara hiyo, kwa mwaka wa fedha 2017/18.

**Mheshimiwa Spika,** kabla sijawasilisha moani hayo, napenda kuchukua fursa hii, kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutujalia sote uhai na kutuwezesha kushiriki katika Mkutano

huu wa Bunge, kujadili Bajeti ya Serikali tukiwa salama. Aidha, napenda kutumia fursa hii kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, kulipongeza Jeshi la Wananchi wa Tanzani kwa jinsi walivyojitoa kwa moyo wa uzalendo kabisa, kusaidia kuratibu zoezi la kuaga miili ya wanafunzi 32, walimu wawili na dereva mmoja wa shule ya Lucky Vincent waliofariki kwa ajali ya gari huko Karatu – Arusha. Sambamba na hilo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatoa salamu za rambi rambi kwa wote walioguswa na msiba huo mkubwa.

**Mheshimiwa Spika,** nitakuwa sina fadhila, kama sitawashukuru kwa dhati ya moyo wangu, wapiga kura wangu wa Jimbo la Ukonga, kwa imani na ushirikiano mkubwa wanaonipa, katika utekelezaji wa majukumu yangu ya kibunge. Ninaendelea kuwaahidi utumishi uliotukuka, na kamwe sitawaangusha.

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee napenda kuishukuru familia yangu, kwa kunifariji na kunitia moyo katika kutekeleza majukumu yangu, lakini zaidi sana kwa kunivumilia, hasa pale ninapokuwa mbali nao, kutokana na shughuli zangu za kibunge.

**[MANENO YAMEONDOLEWA KWA MAELEKEZO YA SPIKA]**

**Mheshimiwa Spika,** nimeona nilisemee hilo, kwa kuwa matukio kama hayo, aghalabu yanahatarisha usalama wa nchi yetu, na yanatoa taswira mbaya kwa mataifa mengine, kwamba, Tanzania pengine si mahali salama tena pa kuishi! Ni rai yangu na rai ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwamba, Serikali ifanye uchunguzi wa matukio hayo, na kuleta taarifa ya uchunguzi huo hapa Bungeni, ili kurejesha imani ya wananchi kwa Serikali yao, ambayo kwa sasa inapungua kwa kasi, kutokana na Serikali kutoonekana ikichukua hatua za haraka, za kupambana na uhalifu huu dhidi ya raia wake. Na hii inatokana na ukweli kwamba, jukumu la msingi la Serikali yoyote duniani ni kuwahakikishia wananchi wake ulinzi na usalama.

## 2. SAA ZA KUFANYA KAZI JESHINI

**Mheshimiwa Spika,** muda wa kufanya kazi katika taasisi za Serikali ni saa nane (8) – yani kuanzia saa moja na nusu asubuhi hadi saa tisa na nusu alasiri. Ikiwa mtumishi yeyote ataendelea kufanya kazi baada ya saa tisa na nusu alasiri kwa sababu yoyote ile, atahesabika kwamba amefanya kazi katika muda wa ziada wa kazi, na atastahili kulipwa posho ya masaa ya ziada ya kazi (overtime allowance).

**Mheshimiwa Spika,** kwa kawaida wanajeshi walikuwa wanafanya kazi hadi saa tisa na nusu alasiri na kurejea nyumbani au kambini, lakini kimsingi wanajeshi wapo kazini masaa yote, kwa kuwa kukitokea dharura yoyote, huwa wanaitwa na kushughulikia dharura iliyojitokeza.

**Mheshimiwa Spika,** hivi karibuni, kwa hali ambayo si ya kawaida, wanajeshi wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania wamepewa amri ya kuwepo kazini hadi saa kumi na mbili jioni bila kuelezwa sababu ya kufanya hivyo. Kutokana na hali hiyo, Wanajeshi wamepokea taarifa hiyo kwa taharuki kubwa na kwa mtazamo hasi, jambo ambalo sio afya kwa utendaji kazi jeshini. Swali la msingi hapa ni kwamba; dhamira ya kuongeza muda wa kazi ni nini? Je, kuna tangazo la hali ya hatari nchini, ambapo sasa inabidi wanajeshi wafanye kazi ya ziada? Na je, kuna mission yoyote waliyopewa ikafeli, kwa hiyo sasa wanapewa adhabu kwa kufanya kazi ya ziada?

**Mheshimiwa Spika,** ikumbukwe kwamba Jeshi letu limesifiwa kote duniani kuwa ni Jeshi lenye weledi na nidhamu ya hali ya juu, na hata waziri hapa amewapongeza kwa hilo. Kama Jeshi letu lina weledi mkubwa na nidhamu ya hali ya juu hata kusifiwa katika medani za kimataifa, kumetokea nini cha ajabu hadi wafanyishwe kazi kwa masaa yote hayo? Au weledi wao na nidhamu yao imeshuka, kwa hiyo wako katika prorogramu maalum ya kuongeza weledi na nidhamu? Kama hivyo, ndivyo, program hiyo itadumu kwa muda gani?

**Mheshimiwa Spika,** ni vema Serikali ikaweka bayana dhamira

au lengo la kuongeza muda wa kazi jeshini hadi kufikia saa kumi na mbili jioni, ili wanajeshi wafanye kazi kwa moyo mkunjufu. Bila kufanya hivyo, watakuwa na dukuduku, na kibaya zaidi ni kwamba, wanaweza kuwa na mgomo baridi kutokana na kutoridhika na uamuzi huo, na hivyo kuathiri ufanisi na tija ya Jeshi zima.

**Mheshimiwa Spika,** athari za kuongeza muda wa kufanya kazi kwa Wanajeshi ni nyingi, na zinamgusa Mwanajeshi mmoja mmoja na Taifa zima kwa jumla. Athari mojawapo kubwa ni kuhatarisha ulinzi na usalama nchini. Katika mazingira ya Dar es Salaam, mathalani, ambako kuna shida ya usafiri, hali ya ulinzi na usalama kuanzia saa 12 jioni hadi saa nne usiku wakati Wanajeshi wanarudi nyumbani, inakuwa ngumu sana. Polisi wanapata shida kufanya doria kwa kuwa kunakuwa na Wanajeshi wengi kwa hiyo inawawia vigumu wakati mwingine kutambua nani mwanajeshi na nani jambazi. Kuna uwezekano mkubwa kwa majambazi kutumia mwanya huo wakavaa kombati za Jeshi na kufanya uhalifu na itakuwa vigumu kuwabaini kutokana na uwepo wa Wanajeshi wengi mitaani muda huo waliovalia sare zao wakirudi majumbani kutoka kazini.

**Mheshimiwa Spika,** athari nyingine kubwa ya kuongeza muda wa kufanya kazi ni kudorora kwa mahusiano ya kifamilia miongoni mwa wanajeshi. Tukichulia tena mfano wa changamoto ya usafiri Dar es Salaam, ili mwanajeshi aweze kufika kazini saa moja asubuhi ni lazima awe ameondoka nyumbani angalau saa kumi na moja alfajiri. Muda huo watoto wake bado wamelala. Kwa changamoto hiyo hiyo ya usafiri, atarudi nyumbani saa nne mpaka saa tano usiku. Anakuta watoto wamewameshalala. Kwa mwendelezo huo, kuna siku watoto hao wanaweza wakamwita baba mjomba au mama wakamwita shangazi kwa kuwa hawajui kama kweli hao ndio wazazi halisi, kwa kuwa hawawaoni.

**Mheshimiwa Spika,** athari nyingine ni ya kiuchumi. Wanajeshi walipokuwa wakitoka kazini saa tisa na nusu alasiri walikuwa na muda wa kufanya shughuli za kijasiriamali ili kupunguza

ukali wa maisha kutokana na posho zao kuwa ni kidogo. Kwa mabadiliko haya ya muda wa kufanya kazi, hakuna muda tena wa kusimamia miradi ya kiuchumi, na matokeo yake hali za kiuchumi za wanajeshi tayari zimeshaanza kuwa mbaya. Kama Serikali haioni umuhimu wa miradi hii, katika kuwapunguzia wanajeshi ukali wa maisha, basi wawapatie wanajeshi mahitaji yao yote kwa asilimia mia moja ili waachane na miradi hiyo na kutumikia hadi saa 12 jioni.

**Mheshimiwa Spika,** athari ya mwisho lakini si kwa umuhimu, ni hatari ya kupungua kwa uwezo wa kuzaa na kupata watoto miongoni mwa wanajeshi kutokana na uchovu mwingi unaosababishwa na muda mrefu wa kazi. Na hii ndiyo athari mbaya kuliko zote.

**Mheshimiwa Spika,** utakumbuka kwamba maandiko matakatifu yanasema kwamba, waana wa Israeli walipokuwa utumwani Misri, Farao aliwafanyisha kazi nyingi ili wasizaane na kuongezeka kwa kuwa walikuwa wanaonekana kuwa tishio kwa wamisri kutokana na wingi wao na uhodari wao katika kufanya kazi. Hivyo ni dhahiri kwamba mtu akichoka sana kwa kazi, ile kazi nyingine mbayo ni amri ya Mwenyezi Mungu pia, ya kuzaa na kuijaza dunia, inakuwa ni ngumu zaidi kwa kuwa inahitaji nguvu nyingi.

**Mheshimiwa Spika,** kwa maelezo yote hayo, itoshe tu Serikali itoe maelezo ya sababu za kuongeza muda wa kufanya kazi jeshini ili kuwe na ufahamu wa pamoja baina ya Serikali na Jeshi na hivyo kuondoa manung'uniko miongoni mwa wanajeshi na hatimaye kuongeza ufanisi jeshini. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inaitaka Serikali kulieleza Bunge hili, iwapo imewalipa wanajeshi posho ya masaa ya ziada ya kazi (overtime allowance) tangu walipoanza kutekeleza amri ya kufanya kazi hadi saa 12 jioni.

## 3. KUSITISHWA KWA UTOAJI WA FEDHA ZA LIKIZO KWA WANAJESHI

**Mheshimiwa Spika,** likizo ni stahili ya kisheria ya mtumishi yoyote iwe ni katika sekta ya umma au sekta binafsi. Msingi

wa likizo ni kumpatia mtumishi muda wa kupumzika, kubadili mazingira ya kazi na hivyo ***ku-refresh*** akili na hatimaye kurudi kazini akiwa na ari na nguvu mpya ya kufanya kazi.

**Mheshimiwa Spika,** zipo likizo zenye malipo na likizo ambazo hazina malipo kutegemeana na aina ya kada na taratibu walizojiwekea. Utaratibu uliopo kwa upande wa Jeshi ni kwamba, wanajeshi wanatakiwa kulipwa fedha ya likizo kila baada ya miaka mitatu, ingawa wanaenda likizo kila mwaka. Hii ina maana kwamba miaka miwili wanakwenda likizo bila malipo na mwaka unaofuata wanakwenda likizo yenye malipo.

**Mheshimiwa Spika,** yako malalamiko miongoni mwa wanajeshi kwamba; malipo ya fedha za likizo, kwa likizo zenye malipo yamesitishwa kimyakimya bila wanajeshi kupewa taarifa ya kinachoendelea. Kwa mujibu wa taarifa kutoka kwa baadhi ya wanajeshi ni kwamba, mara tu walipoanza kuulizia fedha zao za likizo walitishwa na *Chief of Staff* kuwa ni marufuku kuulizia au kuzungumzia popote kuhusu fedha hizo.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kulieleza Bunge hili, kama haitaki wanajeshi watoe malalamiko yao kwa ngazi husika ndani ya Jeshi wanataka wakatoe wapi malalamiko yao? Kitendo cha kuwatisha Wanajeshi,kwa kuwapiga marufuku wasizungumzie maslahi yao halali, tena ndani ya mamlaka za ndani ya Jeshi, ni cha kulaaniwa na anayefanya hivyo achukuliwe hatua, kwani anachochea hasira miongoni mwa wanajeshi, jambo ambalo linaweza kupelekea uasi ndani ya jeshi na kuhatarisha amani na usalama wanchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kuitahadharisha Serikali kuwa, vikosi vya waasi kama vile Bhoko Haram, Alshaabab na M23 vilianza kutokana madai madogo madogo ndani vya vikosi vyao vya Jeshi ambayo hayakuthaminiwa wala kushughulikiwa. Hadi ninapozungumza hapa, kwa mujibu wa taarifa ya *DW* na *BBC* ya jana asubuhi ni kwamba, Jeshi la Ivory Coast limeasi

kutokana na madai ya malipo ya fedha ambayo Serikali ya Ivory Coast haikuyafanyia kazi mapema.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kushughulikia madai na mahitaji mengine ya msingi yanayowahusu wanajeshi kwa wakati, kwa kuwa yanapoanza kusikika nje yanashusha hadhi ya jeshi letu. Kambi Rasmi ya Upinzani mathalani, haikupaswa kujua madai hayo, lakini imeyajuwa kwa kuwa, hayapewi uzito unaostahili na wala hayashughulikiwi, na wanajeshi hawaruhusiwi kuandamana, hivyo lazima watafute sehemu ya kupumulia.

## 4. DHANA YA KUBANA MATUMIZI SERIKALINI INAVYOATHIRI MISINGI YA KUANZISHWA KWA JESHI LA ULINZI

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na azma ya Serikali ya awamu ya tano kubana matumizi ya Serikali, tayari Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama ameanza kutekeleza azma hiyo, kwa kuwaagiza wakuu wa vikosi kumuunga Rais mkono kubana matumizi ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** akiwa katika ziara ya kutembela vikosi mbalimbali baada ya kuapishwa kushika wadhfa huo, Mkuu wa Majeshi alinukuliwa akiwaagiza wakuu wa vikosi kuanza kubuni miradi ya uzalishaji ili waweze kujiendesha kwa matumizi madogomadogo kama vile vifaa vya ofisi (stationeries).

**Mheshimiwa Spika,** agizo hilo la kufanya shughuli za uzalishaji mali linakiuka msingi mkuu wa uanzishwaji wa wa Jeshi la Ulinzi ambao ni ulinzi na usalama wa mipaka ya nchi yetu. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatambua kwamba kipo kitengo cha uzalishaji katika Jeshi la Kujenga Taifa (SUMA JKT), na kinafanya kazi nzuri. Jambo la msingi ni kuiwezesha (SUMA JKT) ili izalishe kwa wingi na na kuchangia gharama hizo na sio kulifanya Jeshi zima kuwa la uzalishaji.

## 5. MANUNUZI YA VIFAA MBALIMBALI JESHINI

**Mheshimiwa Spika,** ninapozungumzia vifaa jeshini nadhani

naeleweka, vifaa jeshini siyo vifaa vya kawaida, ni vifaa ambavyo ni '*sensitive*', na kwa maana hiyo, manunuzi yake pamoja na utunzaji wake, lazima ufanywe kwa makini na weledi wa hali ya juu ili kuepuka madhara yanayoweza kutokea kutokana na '*mismanagement*'.

**Mheshimiwa Spika,** zipo taarifa kwamba maafisa wa ngazi za juu waliopo kwenye bodi ya manunuzi ndio wanojipa nafasi ya kwenda nje kununua vifaa hivyo na kuwaacha maafisa wenye utaaalam na vifaa hivyo. Matokeo yake ni kwamba vinanunuliwa vifaa vinavyogharimu mabilioni ya fedha, ambavyo ama vimepita muda wake wa matumizi, au havifai kutumiwa katika mazingira yetu na hivyo kuisababishia hasara Serikali.

**[MANENO YAMEONDOLEWA KWA MAELEKEZO YA SPIKA]**

**Mheshimiwa Spika,** hii inatokana na bodi ya manunuzi kutofuata taratibu za manunuzi, na sababu kubwa ya kutokufanya hivyo, ni tamaa ya fedha. Imebainika kwamba wanajipangia kwenda kufanya manunuzi hayo, ili wapate posho ya safari, na maslahi mengine. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali '*with a serious note*' kwamba; isifanye mzaha kwenye eneo hili la manunuzi ya vifaa, kwani licha ya eneo hilo kutumia fedha nyingi, pengine kuliko maeneo yote, lakini madhara yanayoweza kutokea kutokana na kununua vifaa vibovu, au vilivyopitwa na wakati ni makubwa zaidi. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaishauri Serikali, kuitazama upya bodi hiyo ya manunuzi – kwa maana ya uhakiki wa taaluma zao ili kujiridhisha kama bado ina uwezo na weledi wa kufanya kazi hiyo.

## 6. NAFASI YA MKUU WA MAJESHI KATIKA KUJENGA JESHI IMARA LENYE NIDHAMU, UTII NA MSHIKAMANO

**Mheshimiwa Spika,** wakati Mkuu wa Majeshi Mstaafu Generali Davis Mwamnyange anamkabidhi Mkuu mpya wa Majeshi alimwambia kwamba amelitoa jeshi kwenye tope na kulifikisha sehemu nzuri na kwamba, mkuu huyu wa sasa alifikishe kwenye lami.

**Mheshimiwa Spika,** bila shaka maneno hayo ya Mkuu wa Majeshi Mstaafu yanaashiria kwamba alijali sana maslahi ya wanajeshi wake, na kwa maana hiyo, nidhamu ilikuwa juu, jeshi lilikuwa na mshikamano wa hali ya juu, utii wa hali ya juu na zaidi ya yote walimpenda Mkuu wao wa Majeshi. Jeshi linapokuwa na nidhamu ya hali juu, utii na mshikamano hakuna shaka jeshi hilo linakuwa imara pia.

**Mheshimiwa Spika,** yapo malalamiko miongoni mwa wanajeshi kwamba mara tu baada ya Mkuu mpya wa Majeshi kuanza kazi, kuna mabadiliko mengi yametokea ambayo yanawaathiri wanajeshi na familia zao moja kwa moja. Miongoni mwa mabadiliko hayo ni kama vile kuongeza muda wa kufanya kazi bila kutoa sababu yoyote, nafasi za wanajeshi kujiendeleza kielimu (elimu za kiraia) ambazo zilikuwepo kipindi cha nyuma sasa zimefutwa; wanajeshi wanaokwenda kwenye kozi za kijeshi hawapewi ration allowance ingawa fedha hiyo iliidhinishwa na bunge. Aidha, wakati uliopita wanajeshi walihimizwa kumiliki vyombo binafsi vya usafiri ili kuwasaidia kurahishisha shughuli zao nyingine, lakini sasa inasemekana vyombo hivyo vya kiraia ni uchafu kwenye mazingira ya jeshi na kwa maana hiyo havitakiwi.

**Mheshimiwa Spika,** siku za nyuma bidhaa katika maduka ya bei nafuu jeshini (duty free shops) zilikuwa na ruzuku ya Serikali na hivyo wanajeshi walikuwa wanapata bidhaa hizo vikiwemo vinywaji, kwa bei nafuu. Sasa hivi maduka hayo yameondolewa kwa ahdi kwamba wanajeshi wangepewa shilingi laki tatu ili kuweza kujinunulia bidhaa kwa bei za uraiani. Hii shilingi laki tatu imetolewa mara moja tu, na haina maelezo kama itakuwa inatolewa kila mwezi au kila baada ya miezi sita au vinginevyo. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inataka Serikali kulieleza bunge hili, hiyo shilingi laki tatu itakuwa inatolewa kila baada ya muda gani?

**Mheshimiwa Spika,** malalamiko mengine ni pamoja na kutopandishwa vyeo hata kwa wale waliokidhi vigezo vya kukaa kazini kwa miaka minne, na wenye sifa stahiki za kupandishwa vyeo. Aidha, nauli kwa safari za kikazi

hazitolewi. Askari akipangiwa safari inabidi ajitafutie nauli, na nauli hiyo hairudishwi. Inasemekana jambo hili linawaumiza sana askari wa vyeo vya chini ila wakubwa wakisafiri wanapewa nauli mara moja. Yapo pia malalamiko kwamba wanajeshi waliohamishiwa Dodoma hawajalipwa fedha zao za uhamisho, na wanaishi kwa taabu.

**Mheshimiwa Spika,** mambo haya yote, kwa tafsiri nyepesi, ni kwamba, hayatalipeleka jeshi kwenye lami, bali yanalirudisha kule kwenye tope ambapo lilikuwa limeshatoka huko. Kutokana na hali hii, kuna viashiria vingi vya manung'niko na hali ya kutoridhika miongoni mwa wanajeshi, jambo ambalo linaweza kusababisha kupungua kwa utii au imani (loyalty) kwa uongozi.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inaishauri Serikali tena kwa msisitizo mkubwa kuhakikisha kwamba suala la mahusiano mazuri miongoni mwa wanajeshi na hususan uongozi na wanajeshi wengine linafanyiwa kazi haraka iwezekanavyo ili kuwe na jeshi moja lenye upendo na mshikamano. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Seirikali kutatua kero zote zinazolalamikiwa na wanajeshi ili wafanye kazi kwa ari zaidi.

## 7. HUDUMA YA NISHATI YA UMEME KATIKA MAKAMBI YA JESHI

**Mheshimiwa Spika,** ni jambo linalofahamika kwamba, taasisi za umma hulipia gharama za huduma mbalimbali kama vile huduma za maji na umeme, kupitia bajeti ya matumizi mengineyo (OC) inayotolewa na hazina. Hata hivyo, taasisi nyingi za umma yakiwemo majeshi yetu zimekuwa zikishindwa kulipia huduma hizo kutokana na bajeti ndogo ya matumizi mengineyo na mbaya zaidi fedha za OC hazitolewi kwa ukamilifu wake na hata hizo kidogo zinazotolewa, hazitolewi kwa wakati. Kutokana na hali hiyo, taasisi nyingi za umma zimekuwa wadaiwa sugu wa shirika la umeme (TANESCO), na makampuni au mashirika mbalimbali yanayotoa huduma za maji.

**Mheshimiwa Spika,** dawa ya kuondokana na udaiwa sugu kwa taasisi za umma yakiwemo majeshi ni Serikali kutoa fedha za matumizi mengineyo kwa utoshelevu na kwa wakati na sio Serikali kuyaamuru makampuni au mashirika yanayotoa huduma kukata huduma hizo kwa taasisi za umma.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatafsiri kitendo cha Mkuu wa Nchi kuiamuru TANESCO kukata umeme kwenye makambi ya Jeshi kuwa ni kuhatarisha usalama wa nchi. Jeshi ni taasisi nyeti katika usalama wa nchi, na kwa maana hiyo, Serikali inatakiwa kuhakikisha kuwa, huduma zote zikiwemo maji, umeme, afya n.k zinapatikana kwa utoshelevu ili Jeshi liweze kuendelea kufanya kazi zake za kulinda usalama wa nchi yetu dhidi ya adui yoyote. Ikiwa jeshi limeshindwa kulipia huduma hizo, basi Serikali ndiyo inayotakiwa kuwajibika kwa kutotoa fedha za kutosha za OC kulipia gharama hizo.

## 8. USALAMA WA MIPAKA YA NCHI

**Mheshimiwa Spika,** kumekuwa na mvutano kuhusu mpaka wa Malawi na Tazania hususan katika Ziwa Nyasa. Hata hivyo, Serikali kwa nyakati tofauti imekuwa ikisema kwamba mgogoro huo unashughulikiwa kwa ajili ya kuupatia ufumbuzi.

**Mheshimiwa Spika,** licha ya Serikali kusema kuwa, kuna dalili njema ya maafikiano kuhusu mgogoro huo, kuna viashiria kwamba majirani zetu wa Malawi hawaafikiani na usuluhishi wowote utakaowafanya wasimiliki ziwa lote la Nyasa.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Mtandano wa '*extractives*' ni kwamba Serikali ya Malawi imeweka msimamo kwamba haitakubaliana na usuluhishi wowote ambao utaipa Tanzania sehemu ya Ziwa Nyasa. Na jambo hili linathibitishwa na Kauli ya aliyekuwa Katibu Mkuu Kiongozi wa Serikali ya Malawi, Bwana George Mkondiwa kwamba; ***"Malawi will never, and has never, at any time, acquiesced to Tanzania's unwarranted and unjustified territorial claims,"***

**Mheshimiwa Spika,** kauli kama hiyo, kutoka kwa kiongozi mkubwa katika Serikali ya Malawi, huku mazungumzo ya usuluhishi yakiendelea, kwa vyovyote vile ni kauli nzito na Tanzania haipaswi kuipuuza. Kwa sababu hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kujua mazungumzo yaliyokuwa yakiendelea kuhusu usuluhishi wa mgogoro wa mpaka katika ya Tanzania na Malawi yemefikia wapi, na ni nini hatima ya mgogoro huo. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kueleza hali ya usalama wa Mipaka ya Tanzania kwa ujumla wake, ambayo kwa siku za nyuma iligundulika kuwa beacons za mipaka hiyo zilikuwa zimeng'olewa na pia raia kutoka nchi jirani walikuwa wanaingia nchini mwetu kwa njia za panya kutokana na mipaka yetu kupenyeka kirahisi.

## 9. NAFASI YA JESHI KATIKA KUPAMBANA NA MATUKIO YA KIGAIDI NCHINI.

**Mheshimiwa Spika,** siku za hivi karibuni kumekuwa na matukio ya kigaidi ya kuvamiwa kwa vituo vya Polisi na watu wasiojulikana na kupora silaha, kuwauwa askari Polisi na kuporwa silaha, pamoja na wananchi kuuawa na hususan viongozi wa Serikali za Mitaa katika Wilaya ya Rufiji mkoani Pwani.

**Mheshimwa Spika,** matukio haya yanaashiria kwamba watu wanaoyafanya ni watu wenye mafunzo ya kijeshi na mbinu za kivita ndio maana wameweza kutekeleza uhalifu huo bila kukamatwa na bila kujulikana kwa majina yao, na hata walikoelekea.

**Mheshimiwa Spika,** kuna kila dalili kwamba Polisi wamezidiwa mbinu na nguvu ya kukabiliana na magaidi hao. Kwa sababu hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inashauri na kupendekeza Jeshi la Ulinzi liingilie kati na hususan kitengo cha upelelezi wa kijeshi (Millitary Intelligence) ili kutoa msaada wa ki-pelelezi na hatimaye kuwabaini na kuwashughulikia wahalifu hao.

## 10. UTEUZI WA WANAJESHI KATIKA NAFASI ZA KISIASA

**Mheshimiwa Spika,** katika hotuba yake mwaka jana, Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni alizungumzia athari za kuwateua wanajeshi katika nafasi za kisiasa. allionyesha jinsi ambavyo mwanajeshi anayeteuliwa kuwa Mkuu wa Wilaya au Mkuu wa Mkoa anavyounganishwa na chama tawala, kwa kutakiwa kuwa mjumbe wa Kamati ya siasa ya chama katika Wilaya au Mkoa husika. Kuunganishwa huku na chama, kumewekwa bayana na Katiba ya CCM ya mwaka 1977, katika ibara ya 80(1) (c) inayowataja Wakuu wa Wilaya kuwa wajumbe wa Kamati ya Siasa ya CCM katika Wilaya husika, na Ibara ya 94(1) (c) inayowataja Wakuu wa Mikoa kuwa wajumbe wa Kamati ya Siasa ya CCM katika mikoa husika.

**Mheshimiwa Spika**, kitendo cha katiba ya CCM kuwatambua Wakuu wa Wilaya na Mikoa kama wajumbe wa Kamati ya Siasa ya Wilaya au Mkoa husika, kunadhihirisha kwamba, wakuu hao ni wanachama wa chama cha siasa, na kwa maana hiyo ni wanasiasa. Kwa hiyo, Mwanajeshi anayeteuliwa kuwa Mkuu wa Wilaya au Mkoa *automatically* anakuwa mwanachama wa CCM.

**Mheshimiwa Spika,** katika maelezo yake, alinukuu Ibara ya 147 (3) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayosema kwamba, *"Itakuwa ni marufuku kwa mwanajeshi yeyote kujiunga na chama chohote cha siasa, isipokuwa tu kama atakuwa na haki ya kupiga kura iliyotajwa katika ibara ya 5 ya Katiba hii".* Aidha, Ibara ndogo ya (4) inasema kwamba; *Kwa madhumuni ya ibara hii, "mwanajeshi" maana yake ni askari aliyeajiriwa kwa masharti ya muda au ya kudumu katika Jeshi la Ulinzi, Jeshi la Polisi, Jeshi la Magereza au Jeshi la Kujenga Taifa*.

**Mheshimiwa Spika,** uteuzi huu wa wanajeshi kushika nafasi za kisiasa umetanuliwa wigo wake, ambapo sasa wanajeshi wanaanza kuteuliwa na chama tawala kuwa viongozi wa chama. Uteuzi wa Kanali Ngemela Eslom Lubinga kuwa Katibu wa NEC ya CCM - Siasa na Uhusiano wa Kimataifa,

ni uthibitisho kwamba Jeshi linaingizwa kwenye siasa kidogokidogo (Politicization of the army)

**Mheshimiwa Spika,** athari za jambo hili ni kwamba jeshi litaanza kupoteza ile sifa yake ya kuwa Jeshi la Wananchi na badala yake litaanza kufanya kazi kwa *bias* – k*wa* kupokea amri na maagizo ya chama tawala. Athari kubwa zaidi ni kwamba, utawala wa kiraia (civil governance) utapoteza maana yake.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatafsiri kitendo cha kuendelea kuwateua wanajeshi kushika nafasi za kisiasa hata baada ya kutahadharishwa, ni mwendelezo wa vitendo vya Serikali hii ya awamu ya tano, vya kupuuza Katiba ya nchi yetu, jambo ambalo halina afya sana katika utawala bora. Kwa sababu hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutoa maelezo mbele ya Bunge hili, ni kwa nini haiheshimu katazo la ibara ya 147(3) na (4) ya Katiba kuhusu wanajeshi kujihusisha na kazi za siasa?

**Mheshimiwa Spika,** sambamba hilo, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa maelezo ni kwanini wanajeshi wanaoteuliwa kushika nafasi za kisiasa wanaendelea kuvaa uniform za kijeshi wakati ilitakiwa wastaafu kwanza jeshi ili sasa wawe watumishi wa umma?

## 11. POSHO YA CHAKULA KWA WANAJESHI (RATION ALLOWANCE)

**Mheshimiwa Spika,** kwa miaka mingi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imekuwa mstari wa mbele kutetea maslahi ya wanajeshi wetu ikiwemo posho ya chakula (ration allowance). Msingi wa kutetea maslahi ya wanajeshi ni kuwapatia wanajeshi wetu lishe bora na kuwafanya wawe na nguvu ya kuhimili mazoezi na kazi mbalimbali za kiaskari wanazofanya. Aidha, lengo jingine ni kuwafanya wawe na utulivu wa ndani ili waweze kufanya kazi yao ya kulinda usalama wa nchi yetu wakiwa hawana mawazo ya kwamba watakula nini pamoja na familia zao.

**Mheshimiwa Spika,** utaratibu uliopo ni kwamba, posho hii ya chakula hutolewa moja kwa moja kwa akari kila mwezi. Askari anayepokea posho hii huwa na uhuru nayo wa kuitumia kwa namna yoyote ile ikiwa ni pamoja na kuitumia na familia yake.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inazo taarifa kwamba kuna mkakati wa kubadili mfumo wa utoaji wa posho hiyo kwa wanajeshi. Utaratibu mpya unaotaka kuanza kutumika ni kwamba wanajeshi hawatapewa tena posho hii moja kwa moja kwenye akaunti zao za benki, isipokuwa ataitwa mzabuni wa kuwapatia wanajeshi chakula, na ile posho ya chakula atapewa mzabuni.

**Mheshimiwa Spika,** tafsiri ya utaratibu huo ni kwamba sasa wanajeshi wanalazimishwa kula chakula kwa mzabuni na wasipofanya hivyo, posho hiyo itakuwa haiwahusu. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaona kwamba huo ni udhalilishaji wa hali ya juu kwa wanajeshi wetu. Wanajeshi ni watu wazima wanajua ni saa ngapi wale chakula na kwa kiasi gani hivyo lazima tuwaheshimu, na tusiwachukulie kama watoto wa shule ya msingi. Ikumbukwe pia kwamba posho hii inavyolipwa kwa mwanajeshi moja kwa moja anakula pia na familia yake. Kumlazimisha mwanajeshi ale kazini peke yake ni kuikosesha familia yake riziki ya chakula pia. Huu ni ubinafsi na uchoyo wa hali ya juu kabisa unatoka kufanywa na Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali kuufuta utaratibu huo, na kuendelea kutoa posho ya chakula moja kwa moja kwa wanajeshi.

## 12. USHIRIKIANO WA KIJESHI NA MATAIFA MENGINE

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatambua Jeshi la Wananchi wa Tanzania linashiriki katika operesheni za kijeshi katika mataifa mengine kupitia katika Mpango wa kulinda amani wa Umoja wa Afrika na ule wa Umoja wa Mataifa.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na kwamba ushiriki huo unaliongezea jeshi letu uzoefu wa kufanya kazi katika mazingira tofauti tofauti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutafakari upya faida hususan za ki-uchumi na ki-teknolojia ambazo kama taifa tunanufaika nazo kwa Jeshi letu kushiriki katika operesheni hizo.

**Mheshimiwa Spika,** nasema hivi kwa kuwa sera ya uchumi ya nchi yetu kwa sasa inasisitiza mapinduzi ya viwanda ambapo ili tufanikiwe, ni lazima tuwe na mkakati maalum wa uvumbuzi na ugunduzi wa sayansi na teknolojia ambayo kwa kiasi kikubwa inapatikana katika nchi zilizoendelea.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilieleza katika hotuba yake mwaka jana kwamba, nchi ambazo zimeendelea tayari kama vile Marekani na Uingereza hazipeleki majeshi yao kupigana vita au kulinda amani katika nchi nyingine kama hakuna maslahi yoyote na hasa ya ki-uchumi kwa mataifa yao. Na ndio maana sera zao za mambo ya nje ziko bayana kwamba ni maslahi ya nchi zao kwanza ndio mambo mengine yafuate.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inapendekeza hivi kwa sababu kama taifa tusipojipanga kimkakati zaidi, tutaishia kupokea miili ya wanajeshi wetu waliokufa katika operesheni hizo huku taifa likibaki bila manufaa yoyote. Kwa sababu hiyo, tunapendekeza kwamba kuwe na malengo mahsusi na ya kimkakati Jeshi letu linapokwenda kushiriki operesheni katika mataifa mengine. Mikakati hiyo iwe ni pamoja na kufanya utafiti wa masuala ya kiuchumi na kiteknolojia – yaani kwa maneno mengine wafanye ujasusi wa kiuchumi (economic espionage) ili baada ya operesheni hizo kuwe na faida ya kidola itakayopatikana na sio tu maslahi ya kifedha wanajeshi wanayopata kwa kushiriki operesheni hizo.

## 13. JESHI LA KUJENGA TAIFA NA UZALISHAJI WA CHAKULA.

**Mheshimiwa Spika,** ni aibu kwa taifa hili kuwa na matukio ya ukosefu wa chakula na njaa huku kukiwa na Jeshi la

Kujenga Taifa. Miaka iliyopita tulipendekeza kuwa pamoja na mambo mengine, jeshi hili lipimwe kwa uzalishaji ambao litakuwa limefanya . Tulieleza kwamba; dhima ya Jeshi la Kujenga taifa ni kwamba pamoja na mambo mengine, lina wajibu wa kuwafunza vijana wetu kufanya kazi za uzalishaji mali kwa ajili ya kujenga uchumi wa Taifa letu.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imekuwa ikishauri miaka nenda miaka rudi kwamba; Serikali itumie nguvu kazi iliyopo kwenye Jeshi la Kujenga Taifa katika kujenga uchumi wa kweli nchini, na hasa kipindi hiki cha uchumi wa viwanda Jeshi la Kujenga Taifa ndio lilitakiwa litoe dira ya namna ya kuwa a uchumi wa viwanda. Tulishauri kwamba Serikali itenge mashamba makubwa ili vijana hawa wawapo mafunzoni, wafanye mafunzo kwa vitendo ya kilimo ili nchi iweze kujitegemea kwa chakula. Aidha, tuliishauri Serikali iwaagize wakuu wa makambi ya JKT kutengeneza programu maalum za uzalishaji mali katika sekta mbalimbali kama vile kilimo, viwanda, ufundi, uvuvi nk kila mwaka. Tulipendekeza pia kwamba, Waziri mwenye dhamana awe anatoa taarifa ya uzalishaji uliofanywa na JKT na mapato (maduhuli) yaliyopatikana kutokana na uzalishaji huo katika kila Bunge la bajeti.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kutoa ushauri huo kwa siku nyingi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kupewa mrejesho wa utekelezaji wa ushauri huo. Serikali ilieleze Bunge, JKT imekeleza miradi mingapi ya uzalishaji na imeingiza fedha kiasi gani kutokana na uzalishaji huo, na ina mpango wa kuteleza miradi mingapi kwa mwaka wa fedha 2017/18.

## 14. UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA KWA MWAKA WA FEDHA 2016/17

**Mheshimiwa Spika,** kumeanza kutokea mazoea mabaya ya utekelezaji duni wa bajeti ya maendeleo katika wizara hii jambo ambalo linatia wasiwasi kama kweli serikali ina nia ya dhati ya kupandisha ubora na ufanisi wa majeshi yetu.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa taarifa ya utekelezaji wa

bajeti ya wizara hii, fedha ya kutekeleza miradi ya maendeleo liyoidhinishwa na bunge katika fungu 38 (Ngome) ilikuwa ni **shilingi bilioni 10,** lakini hadi machi 2017 ilikuwa imetolewa **shilingi bilioni 1 tu** sawa na **asilimia 10** ya fedha iliyokuwa imeidhiniswa. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kulieleza Bunge hili, hiyo bilioni moja iliyotolewa, ndiyo itaweza kununua zana za kisasa zinazoendana na teknolojia ya sasa, na kutoa mafunzo ya kijeshi ya kisasa na kupandisha ubora na ufanisi wa jeshi kwa kiwango tunachokusudia?

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa fungu 39 (JKT), fedha ya maendeleo iliyoidhinishwa na Bunge ilkuwa ni **shilingi bilioni 8,** lakini hadi machi, 2017 ilikuwa imetolewa **shilingi bilioni moja tu,** sawa na **asilimia 12.5** ya fedha iliyoidhinishwa na bunge. Hii ina maana kwamba bajeti ya maendeleo katika fungu hili haijatekelezwa kwa asilimia **87.5**. Kambi Rasmi ya Upinzani inahoji, JKT itawezaji kutekeleza miradi yake ya maendeleo kwa madhumuni ya kujenga taifa ikiwa mwenendo wa utekelezaji wa bajeti uko namna hii? Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutoa maelezo ni kwani nini JKT imekusanya maduhuli kidogo (asilimia 31.8 tu) wakati ina miradi mingi ya uzalishaji chini ya SUMA JKIT?

**Mheshimiwa Spika,** halikadhalika kwa upande wa wizara, fedha iliyokuw imeidhinishwa na bunge ilikuwa **shilingi bilioni 230,** lakini hadi kufikia machi, 2017 **shilingi bilioni 33.9** tu sawa na asilimia 14.7 ilikuwa imetolewa.

**Mheshimiwa Spika,** tafsiri nyepesi ya utekelezaji huu duni wa bajeti ya maendeleo, unairudisha nyuma wizara na unapunguza ufanisi, ubora na tija ya majeshi yetu. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka Serikali, kwa kadri ile ile ambayo inalisifu jeshi letu kuwa ni imara, lenye weledi na ufanisi mkubwa, basi sifa hizo zionekane kwenye utekelezaji wa bajeti ya maendeleo ya majeshi hayo. Vinginevyo itakuwa tunajifurahisha tu kwa maneno kumbe hali halisi ni mbaya.

**Mheshimiwa Spika,** katika randama yay a wizara ya Ulinzi

na Jeshi la Kujenga Taifa (Fungu 57) kuna baadhi ya vitengo havikutengewa fedha kabisha tena fedha za mishahara. Kwa mfano Subvote 1005 – Procurement Management, uk. 18 hakuna fedha yoyote iliyotengwa kwa ajili ya mshahara; Subvote 2003 – Building Consulting Unit, uk. 36 haikutengewa fedha za mshahara na Subvote 2004 – Estate Management and Development Unit uk.39 hakuna fedha ya mshahara. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inaitaka Serikali kulieleza Bunge hili, ni kwa nini vitengo hivyo havijatengewa fedha za mishahara kwa muwa wa fedha 2017/18 au vitengo hivyo havina watendaji?

## 15. HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** naomba nimalizie hotuba yangu kwa kulipongeza Jeshi la Wananchi wa Tanzania kwa umahiri wake; kwa jinsi linavyoendesha operesheni zake; lakini zaidi sana kwa jinsi linavyojishughulisha na masuala ya kijamii kunapotokea maafa na majanga mbalimbali. Hata hivyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ingependa kujua Jeshi limesaidia vipi kutoa msaada kwa wananchi waliokumbwa na mafuriko kipindi hiki cha masika.

**Mheshimiwa Spika,** ni matamanio ya kila raia wa Tanzania kuona Jeshi letu likiendelea kupanda viwango vya ubora na ufanisi na hivyo kuwa na tija. Hata hivyo ili viwango vipande, lazima mambo kadhaa yashughuliwe kikamilifu. Kwanza, Serikali ihakikishe kwamba, bajeti inayoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya majeshi yetu inatolewa kwa wakati na kwa ukamilifu wake. Pili, Serikali ihakikishe kwamba, maslahi na stahiki zote za wanajeshi zinatolewa kwa wakati na kwa ukamilifu wake ili kuondoa manung'niko miongoni mwa wanajeshi na hivyo kuwangezea morali ya kufanya kazi kwa moyo. Tatu, Serikali ihakikishe kwamba kuna mahusiano mazuri kati ya uongozi wa Jeshi na maafisa wengine wa Jeshi ili kuwa na Jeshi imara lenye mshikamano, utii na nidhamu ya hali ya juu.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaamini kwamba, mambo hayo yakifanyiwa kazi kwa dhati, Jeshi letu litaendelea kupanda viwango vya ubora na hivyo

kuendelea kushikilia nafasi yake katika medani za kimataifa kwamba, ni miongoni mwa majeshi yenye weledi na nidhamu ya hali ya juu duniani.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha.

Mwita Mwikwabe Waitara (Mb)
**Kny. MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KATIKA WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA**

16 Mei, 2017

**MHE. UPENDO F. PENEZA:** Mwongozo wa Spika.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kuna tangazo dogo hapa, nawatangazia kuwa Kampuni ya simu *TTCL* ipo hapa katika viwanja vya Bunge kuanzia tarehe 15 hadi 19, wanatoa huduma mbalimbali za mawasiliano, tafadhali mnaombwa kwenda kuonana nao.

Waheshimiwa Wabunge, mnatangaziwa pia mchukue nyaraka zenu kwenye visanduku vya kuhifadhi nyaraka ili Bunge lipate nafasi ya kuweka nyaraka zingine. Kwa hiyo, mnakuja humu ndani, mnazozana nyaraka hamzisomi ziko kwenye *pigeon hole.*

Tangazo kwa Waheshimiwa Wabunge wote wa Imani ya Kikristo, Waheshimiwa Wabunge wote wanatangaziwa kuhudhuria Ibada katika eneo la *Chapel* yetu ya Pius Msekwa ghorofa ya pili. Aidha, tutakuwa na Mtumishi Laizer katika Ibada hiyo na kwaya ya Jerusalem kutoka Kanisa la Anglikana Kisasa. Waheshimiwa Wabunge wote wanakaribishwa.

Waheshimiwa Wabunge, tunaanza mjadala.

**MHE. UPENDO F. PENEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo wa Spika.

**MWENYEKITI:** Pendo unasemaje?

**MHE. UPENDO F. PENEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti nasimama na Kanuni 68(7).

**MWENYEKITI**: Wewe hata usisome sema tu.

**MHE. UPENDO F. PENEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa. Wakati Mheshimiwa Waitara akisoma hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, kuna eneo la ukurasa Na. 12 ambalo lilifutwa kwa kutokana na mwongozo alioomba Mheshimiwa Mkuchika, lakini maelezo ambayo yanatokana na ukurasa Na. 12 yapo katika Ukurasa Na. 19 katika sehemu ya posho ya chakula ya Wanajeshi kwa maana ya *ration allowance.* Ukiangalia katika ukurasa huo wa 12 hakuna kitu ambacho kipo *classified* kama ambavyo inaelezwa zaidi ya kuelezea maslahi na huduma bora kwa ajili ya Wanajeshi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuomba Mwongozo wako, kama ukurasa na 19 aya 11 imekubalika kwa nini sehemu hiyo ya ukurasa Na. 12 imeondolewa wakati inaongelea manufaa hayo ya Wanajeshi. Ahsante.

**MWENYEKITI**: Ahsante. Nimeshakuelewa kaa chini. Viwango vya *level* za *classified information.* Kaa kwanza unasimama! Tafsiri ya *classified Information* wewe huwezi kujua, kaa chini.

**MWENYEKITI**: Waheshimiwa tunaanza Fakharia, Shomar Hamis, Jasson Rweikwiza na Mheshimiwa Masoud Salim atafuata.

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza sina budi kumshukuru Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kazi nzuri mnayoifanya humu ndani ya Bunge, kwa uweledi mliokuwa nao na kazi nzuri iliyotukuka, lazima mpongezwe.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina budi kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na Watendaji wake kwa kazi aliyotuletea hapa ametufahamisha, tumeelewa, lakini wenzetu wa upande wa pili walikuja na kashfa hawakuja na maelezo ya kuujulisha umma. Kwa mfano, mtu anazungumza Jeshini wanafanya kazi saa moja na nusu....

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa Fakharia subiri, mnasemaje

**MHE. CECILIA D. PARESSO**: Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Msemaji anayesema ama afute maneno yake, asitoe kashfa kwa upande wa pili kwa hicho anachokiongea kwamba hatujaja na *point,* tumekuja tu na mambo yasiyo ya msingi kwa kweli kama ana hoja ajibu hizo.

**MWENYEKITI:** Kaa chini ahsante nimekuelewa.

Waheshimiwa Wabunge, hoja za Upinzani zitajibiwa na Serikali. Jielekezeni kwenye hoja za msingi za masuala ya Wizara ya Ulinzi, hakuna sababu ya kusimama kusema huyu kasema hiki, huyu kasema hiki. Tupo kwenye Bunge, Wapinzani wana wajibu wa Kikatiba kusema ambayo wanataka kuyasema na wameyasema yaliyoruhusiwa yatajibiwa na Serikali, mamlaka ambayo ipo *competent* na ina majibu sahihi ya kuwajibu.

Kwa hiyo, nakuomba Mheshimiwa Fakharia endelea na mjadala wako kwenye hoja za msingi. Kuna matatizo mengi Zanzibar yazungumzie hayo, acha mambo mengine ambayo Serikali itafanya kazi ya kujibu. *(Makofi)*

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, lakini habari ndiyo hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili suala nilitaka kulizungumza kwa sababu tayari Wanajeshi walikuwa wanagombanishwa na Serikali yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina budi kumpongeza

Mheshimiwa Waziri kwa sababu Zanzibar iko kwenye hali ya amani na utulivu, kuanzia uchaguzi uliofanywa wa marudio walikuwepo Wanajeshi wakaweza kuiweka hali ya salama na utulivu na hadi leo hali hiyo inaendelea ya usalama na utulivu, tunashukuru. Sina budi kuzungumza...

**TAARIFA**

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba nimpe taarifa mzungumzaji Mama yangu anayeongea siyo kazi ya Jeshi la Wananchi kusimamia uchaguzi, hiyo ni kazi Jeshi la Polisi. Kwa hiyo, kama anataka kuwashtaki kwamba walifanya uchaguzi wa Zanzibar atuambie vizuri, kazi ya Polisi ndiyo ya kusimamia Mambo ya Ndani.

**MWENYEKITI:** Ahsante umeshaeleweka. Mheshimiwa Fakharia.

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Taarifa yake siipokei kwa sababu ilikuwa ishara tayari walishaonesha upande wa pili na walioweza kutuliza ni Jeshi waliofanya kazi na tukaenda kwa amani na utulivu. Polisi walikuwepo wakifanya shughuli zao na wao walikuwa wakiangalia amani na utulivu wa nchi yetu na hadi hii leo tunaendelea kuwa na amani na utulivu katika nchi yetu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Fakharia hebu kaa kwanza.

Waheshimiwa Wabunge, nataka tumalize hii bajeti ni ya siku moja tu, tunamaliza leo jioni. Hizi *interruption* ambazo naziona zinataka ku-*delay* mpango wa bajeti hii sitokubali na maneno ya Wabunge mnaochangia humu ndani, Mbunge yeyote atakayeenda kinyume na taratibu wa chama chochote humu ndani, nitamdhibiti.

Waheshimiwa Wabunge, hivyo sitaki taarifa, sitaki mwongozo, nitasikiliza watu wawili tu, *Chief Whip* wa Upinzani na wa Serikali basi. Mheshimiwa Fhakharia endelea.

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nilindie muda wangu. Naomba kuzungumzia habari ya viwango vidogo vya pensheni wanavyolipwa askari wastaafu wa zamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila siku tunavyokwenda hali ya maisha inapanda na siku zinavyokwenda mishahara inapanda, lakini wale wastaafu wa zamani kiwango kinakuwa kiko kile kile, ambapo hakiongezeki. Sasa ningemwomba Mheshimiwa Waziri awe anaangalia, baada ya muda na wale askari wastaafu wa zamani viangaliwe viwango vyao. Kama kuna Koplo/Sajenti/Luteni Kanali wa sasa kastaafu basi na wale kiwango kile kile kwa mwaka ule waweze kuwapa wasiwaachie kile kiwango duni ambacho wanacho na kinaweza kuwapa maradhi, labda akapata sukari, *pressure* matumizi yake yatakuwa madogo wakati matumizi yako juu na yamepanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja na suala lingine la JKT. JKT Mheshimiwa Waziri kaizungumza katika ukurasa wa 26 na amezungumza vizuri, tunakupongeza. Lakini ningekuomba Mheshimiwa Waziri idadi ya vijana wa Zanzibar wanaokwenda JKT utuongezee. Kwa sababu umesema kule wanapata elimu ya ukakamavu, elimu ya kujiajiri na elimu ya kuajiri wenzi wao. Sasa ukituongezea idadi ya vijana wetu wakaenda kule wakarejea tena kufanya kazi hiyo ya kwenda kujiajiri, wakawa wakakamavu watapata ajira nyingi za ukakamavu, watapata kujiajiri wao na wenzi wao. Naomba Mheshimiwa Waziri ulipokee ili uweze kutusaidia kwa upande wa Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumzia eneo la mambo ya kuingiliana baina ya majeshi na raia mitaani. Kuna maeneo kimazingira ni magumu, kuna maeneo ambayo wanayo jeshi lakini maeneo yale yalikuwa ya raia hapo wakati wa mabibi na mababu zetu, lakini jeshi sasa hivi imehodhi. Watu wa pale ilikuwa inabidi walipwe kwa kutoa viwanja vyao lakini huwa hawalipwi hivyo kunakuwa na mvutano baina ya raia na Jeshi. Sasa liangalie hili na kwa upande

wenyewe tuangalie, kama upande wa Unguja Ukuu, Kisakasaka matatizo hayo yapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna mengine, wanajeshi wanawalipa raia, lakini baada ya kuwalipa raia hawaondoki sehemu ile na ninyi mnakuwa hamna uthibiti wa kuyazuia yale maeneo yenu; sasa kunakuwa mvutano mwingine mpya. Utayakuta haya kama kule Dunga, Mgeni Haji, sasa na hayo myaangalie. Kama mtu mmeshamlipa aondoke, kama hamjawalipa na wamekubali kuondoka itabadi muwalipe ili kuweka amani na utulivu uliokuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ya Jeshi lazima mfanye utafiti kwa sababu hivi sasa maeneo ya Jeshi yameshaingiliana na ya raia. Bila kufanya utafiti mkaweza kujua sehemu zenu ziko wapi na za raia ziko wapi hapo mwisho kutazuka mtafaruku baina ya Jeshi na raia. Mimi ninajua Ninyi Wanajeshi ni wasikivu, walinzi na pia mnawapenda raia wenu. Sasa naomba Mheshimiwa Waziri na hili mliangalie ili kuondoa mtafaruku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache naunga mkono hoja, sina matatizo. *(Makofi)*

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika Wizara hii, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ulinzi na Usalama, JKT na wasaidizi wake wote na Wakuu wa Majeshi kwa kazi nzuri wanayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Rais Magufuli kwa kazi nzuri sana ya kuendelea kuiweka nchi yetu katika hali ya usalama na amani. Unaposikia amani inakuwepo si kazi rahisi, ni kazi ya Mheshimiwa Magufuli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaenda kwenye mchango wangu, na leo nitaongelea mikataba ya kimataifa; kwanza niweke vizuri Taarifa ya Kambi Rasmi ya Upinzani ambayo imepotosha mambo mengi. Moja ya eneo ambalo imepotosha wanashauri kwamba jeshi litumike kufanya *economic espionage;* hii si kazi ya jeshi, *economic espionage* si kazi ya jeshi, tuwaachie wanaohusika na hiyo wafanye si wanajeshi. Lakini maeneo mengine ambako wamepotosha yako mengi...

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA:** ...wanazungumzia kuhusu Al-Shabab na Boko Haram.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa nimeshasema taarifa sasa hivi nimezizuia napokea za watu wawili tu *Chief Whip* wa *Opposition* na *Chief Whip* wa Serikali, *period.*

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA:** ...bahati mbaya hawajui hata historia ya Somalia wala ya Nigeria. Al-Shabaab ni kikundi cha kikabila kiko Somalia, ni watu wa kabila fulani huwa wanapingana na kabila lingine wamejiandaa na silaha zao ndiyo wanafanya mambo ya Al- Shabaab.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Boko Haram vilevile ina ukabila, ina *element* za ukabila kule Nigeria, lakini pia ni kutokana na matatizo ya kiuchumi, wanajiona kwamba wametengwa, wako *marginalized* ndiyo maana wameunda kikundi cha Boko Haram wanashambulia wananchi wengine wenzao wa Nigeria si mambo waliyoyasema wao ambao ni upotoshaji mtupu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamezungumzia suala la Malawi, kwamba Malawi imesema haitakubali usuluhishi, wameyapata wapi? Usuluhishi huu bado, unafanywa na

Kamati Maalum inaongozwa na Mheshimiwa Joaquim Chissano, Rais Mstaafu wa Msumbiji na usuluhishi haujatolewa. Sasa kusema Malawi wamekataa wamekataa wapi na lini? Kwa hiyo, hili wao ndio wachonganishi, wanachonganisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamezungumzia wakuu wa mikoa, wakuu wa wilaya kuingia kwenye Kamati za Siasa za CCM, huu ni uchonganishi na upotoshaji. Tumewahi kuwa na Wakuu wa Mikoa ambao si wana-CCM, tuna mifano hai. Mkuu wa Mkoa wa Geita hakuwa mwana-CCM, alikuwa haingii kwenye Kamati ya Siasa. Tulikuwa na Mkuu wa Mkoa wa Kigoma hakuwa mwana-CCM alikuwa haingii kwenye Kamati ya Siasa ya Mkoa, labda kama anaitwa kutoa taarifa maalum kwa sababu CCM ndicho Chama Tawala, kina majukumu ya kusimamia Ilani ya Uchaguzi. Hata wewe Waitara leo ukiwa Mkuu wa Wilaya ukaitwa kwenye Kamati ya Siasa utakwenda tu, huna ujanja kwa sababu CCM ndiyo inayoendesha Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona niyaweke sawa haya ili kuondoa upotoshaji.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa. Wewe umesema kwamba tutajibiwa na Serikali yule ni Waziri? Haiwezekani hii ni *double standard* hii. Hii ni *double standard.*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, Mheshimiwa Rweikiza endelea.

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la usalama na ulinzi. Nimesema namshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuweka nchi yetu katika hali ya usalama, lakini nishauri kidogo, usalama upo lakini lazima tuzidi kuuimarisha na kuulinda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasikia hivi karibuni kuna mashambulizi pale Mikoa ya Pwani, hasa Mkoa wa Pwani wenyewe, Rufiji, Kibiti watu wanauawa, jana au juzi kauawa

Katibu wa CCM mmoja na wengine, lakini miaka miwili iliyopita tulisikia mauaji ya watu kule Tanga na mengine yalitokea pale Mwanza ya watu wengi na inaaminika kwamba haya mauaji yalifanywa na Al-Shabaab.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hii inayofanywa kule Pwani hatujui lakini inawezekana ikawa ni Al-Shabaab wanakuja wanaingia kwenye maeneo yetu, wanaleta madhara ambayo ni kuua watu. Sasa kuna taarifa kwamba Al-Shabaab wanaanza kufanya ushirikiano na Boko Haram, na kuna taarifa kwamba haya makundi mawili ya kigaidi wanajaribu kutafuta silaha za sumu *(biological weapons),* ambazo wazitumie kwenye mapambano yao na raia wasiokuwa na hatia huko Somalia, Nigeria na kwingineko. Tunasikia wanavyofanya Kenya wanaua watu huko shuleni, wanaua wanafunzi vyuo vikuu, wanafanya maangamizi sehemu mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama watapata silaha za sumu kama wanavyojitahidi kufanya, itakuwa ni hatari kubwa sana hata kwetu. Kama kweli waliingia wakafanya mauaji pale Tanga miaka miwili iliyopita, halafu wakiwa na silaha za sumu tutakuwa katika hali ngumu sana ya kiusalama. Tanzania na Somalia haziko mbali sana, kati yetu kuna Kenya tu kama kilometa 400 kutoka Somalia mpaka Tanga pale kwa kwenye Maji; kwa hiyo kuna haja ya kuimarisha ulinzi katika maeneo haya.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mkataba...

**MWENYEKITI:** Ahsante, muda wako umekwisha.

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, dakika kumi zimeisha?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Masoud Abdalla Salim.

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru nimepokea taarifa kwa Mheshimiwa Fakharia Shomar akisema kwamba uchaguzi wa Zanzibar ulitawaliwa na Jeshi la Wananchi la Tanzania, hongera sana Mheshimiwa Fakharia tumepokea taarifa na sisi upande wa pili tujiandae zaidi kwa kushinda kura si kwa njia nyingine yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rweikiza nikwambie tu kwamba Jeshi la Marekani wakati wa amani linafanya shughuli za uchumi, watu waliotembea sana shughuli hizo wanajua na majeshi mengi duniani wakati amani yanafanya shughuli za uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukarasa saba Mheshimiwa Waziri anasema dhima kubwa ni kuwa na jeshi dogo na mahiri la ulinzi wa nchi lenye weledi. Hatuwezi kuwa na jeshi dogo, mahiri na lenye weledi ikiwa bajeti ya maendeleo yenye shilingi bilioni kumi unatoa shilingi bilioni moja, hakuna kitu. Hatuwezi kuwa na jeshi lenye weledi na mahiri ikiwa bajeti ya maendeleo ya JKT shilingi bilioni nane unatoa shilingi bilioni moja, hakuna kitu, hapo hakuna weledi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatutaki kuona sisi umeme unakatwa kwenye Kambi za Jeshi la Wananchi wa Tanzania, hatutaki. Hatutaki kuona kabisa wanajeshi wanafanya kazi pamoja na mkataba wao kula kiapo ndani ya masaa 24 lakini kwamba baada ya saa tisa na nusu *ration allowance* yao nayo inaondoka, hatutaki. Tunataka kuona *ration allowance* ya wanajeshi wetu inapandishwa si kwamba *ration allowance* inaondolewa kiaina aina hatutaki. Hiyo ilikuwa ni chombeza ya kwanza mambo hasa yanakuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna malalamiko ya muda mrefu sana juu ya fidia kwa wananchi ambao maeneo yao yamechukuliwa na Serikali kwa ajili ya Jeshi la Wananchi. Maeneo haya ambayo wanajeshi wana shughuli zao jumla yake ni maeneo 262, kati ya maeneo haya ambayo yamepimwa ni maeneo 17 tu. Kwa kweli hii ni njia ya dhuluma, wananchi wamenyanganywa, wananchi wamedhulumiwa na mpaka leo Jeshi la Wananchi katika maeneo 262 maeneo 17 waliyoyapima na kuthamini hakuna fidia na mengine hayajapimwa kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu mwaka 1966, 1970 mpaka leo miaka 50, wananchi wengine wameshakufa wameacha watoto wao wanadai, wala hawajui waende wapi, mmechukua maeneo yao mbalimbali, mbona mambo mnayotaka kufanya mnayafanya? Mbona hawa hamuwapi fedha zao? Hamtoi fidia zao? Kuna mambo mengine ambayo mnayafanya na fedha zinapatikana, kwa nini hamtoi fidia kwa hawa na tatizo ni nini? Nakuomba Mheshimiwa Waziri utuambie utakapokuja hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 57 - Wizara, katika mwaka 2016/2017 ulikuwa na shilingi bilioni 27.7 ni kasma 2004, zilitengwa hizi fedha hakuna shilingi iliyotoka! Wananchi wasemee wapi sasa? Wananchi wanadhulumiwa na wananyonywa hawana mdomo wa kusema, mdomo wao ni sisi, lakini Serikali inasema inatafuta fedha, fedha ikipatikana, mbona fedha za kuhamia Dodoma mlizipata, zilikuwa kwenye bajeti? Fedha za kuhamia Dodoma mlizipata wapi na hazikuwa kwenye bajeti? Kwa nini hawa fedha zao hamuwapi? Kuna wazee wamekufa wameacha watoto wao nao wamekufa, shida kweli Tanzania jamani! Twende wapi sasa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ndiyo mambo ya msingi ya kuwasemea wananchi wetu na kuwaonea huruma, kwamba Serikali inasema inawapenda wananchi wake, inawathamini wananchi wake lakini wapi! Miaka 50 fedha zao hamuwapi mnawatesa kwa njaa, tutafika kweli? Hatufiki, shida kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendelee, ni miaka kadhaa tumesema, tunajifunzaje baada ya mlipuko wa mabomu kule Mbagala na Gongo la Mboto? Baada ya hapo wakasema wanajenga maghala fedha mimi ni mmoja wa walioidhinisha, maghala yamekuwa magofu hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabilioni ya fedha yamepotea, maghala hayaendelezwi yako vilevile. Mungu asijaalie kutokea, likitokea la kutokea nani ataulaumiwa? Maghala mengi ambayo tumetoa fedha yakianzwa hayamalizwi. Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi utakapokuja naomba hili uliseme ni kwa nini mpaka sasa maghala haya bado hayajamalizwa na fedha hizo zimetumika zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Sera ya Ulinzi wa Taifa, umesema sana kwenye kitabu chako hiki. Mambo ya Sera bado hujakaa vizuri. Tangu mwaka 1966 mpaka leo sera ni ya zamani. Unataka jeshi la weledi lakini sera ndiyo itakayopelekea sheria, Sheria ya Ulinzi ni ya zamani. Kwa hiyo hili nalo ni tatizo kubwa. Mheshimiwa Waziri sasa utuambie hii sera lini itaweza kukamilika? Tatizo wewe unalijua zaidi, tena sana, tu kwamba utuambie hii sera ya ulinzi wa Taifa ni lini itakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pengine ningesema jambo linguine, wanajeshi wanakwenda kulinda amani Darfur, DRC na Lebanon wengine wameshaletwa tumeshawazika. Sawa ni kazi zao na wajibu wao lakini mbona familia zao hamzitunzi? Mnawapa fedha za muda wa miezi minne wale vizuka mpaka leo lakini watoto wao hawasomi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa inakuwa ni tatizo kubwa, kwamba tumeshaletewa hapa sisi wale maiti tumeshazika lakini watoto hawasomi, familia zimekuwa masikini imekuwa kama wale wanajeshi wastaafu au wengine ambao walikwenda kwenye vita. Tunawapeleka Lebanon, Darfur na kwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri utuambie mpango mkakati wa ziada kuona kwamba watu hawa hasa wajane wanapatiwa fedha zinazostahili.

**MWENYEKITI:** Endelea bado dakika moja.

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** *Yes?*

**MWENYEKITI:** Malizia dakika moja.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hayo basi ningeomba kusema kwamba sambamba na hilo Mheshimiwa Waziri utakapokuja utuambie wastaafu walio kuanzia ngazi ya *private* hadi *Brigadier General* kwa nini hamrekebishi maslahi yao, tatizo ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ngazi nyingine wanalipwa vizuri wengine hawa mnawadhulumu na wewe ulisha ahidi mwaka wa jana kwamba kuanzia *Private* hadi *Brigadier General,* wastaafu hawa wa Jeshi hasa wale wa zamani basi mafao yako katika machakato na mkasema kwamba yako katika hatua ya mwisho ni hatua ipi, mbona mnachelewa sana na hakuna kitu? Naomba Mheshimiwa Waziri na hili uliseme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo machache, nashukuru lakini muda wangu naona kama mmenibia.

**MWENYEKITI:** Ahsante.

Waheshimiwa jioni tutaanza na Rhoda Kunchela dakika tano, Sophia Mwakagenda dakika tano, Mheshimiwa Saada Mkuya dakika na Martha dakika tano. Nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja jioni.

*(Saa 6.57 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Tukae.

Niliwataja asubuhi wachangiaji wetu wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Rhoda Kunchela dakika tano na Mheshimiwa Sophia dakika tano.

**MHE. RHODA E. KUNCHELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nilitaka nichangie machache kuhusiana na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Kwanza nataka niunge hoja asilimia 100 hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani kutokana na hotuba hii kuonesha mwelekeo wa namna gani Wizara inaweza kutatua kero ambazo zinalikabili Jeshi letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia suala la usalama wa nchi kama wapinzani lakini pia kama Watanzania ambao tuna haki ya kuzungumza na kuikosoa Serikali hatuna maana mbaya, tunathamini kabisa michango ya Jeshi, tunaelewa kabisa kazi ambazo zinafanywa na Jeshi letu, kwa hiyo, si kwamba tunapinga kila kitu. Tunachotaka ni kuikosoa Serikali katika yale mapungufu ambayo tunaona kabisa kupitia Jeshi hili basi linaweza likafanya marekebisho katika baadhi ya sehemu ili tukaenda sawa na wananchi wakawa na amani hiyo ambayo mnaisema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nataka nizungumzie kidogo kuhusiana na migogoro ya ardhi kati ya wananchi na Jeshi. Kumekuwa na changamoto kubwa kwenye maeneo mengi ya Jeshi ambayo sasa wananchi wamekuwa wanayalalamikia, kwamba Jeshi limeingilia kwenye makazi ya watu, lakini unakuta tena Jeshi hilo hilo linasema wananachi wamevamia maeneo ya Jeshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunaiomba Serikali na Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha aeleze ni mkakati gani ambao sasa Wizara au Serikali hii imepanga ili kutatua migogoro hii ya ardhi ambayo imesababishwa na Jeshi, aidha, wananchi kuvamia maeneo ya Jeshi au Jeshi kuvamia maeneo ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nilitaka niseme kidogo, katika Mkoa wangu wa Katavi kuna kata ya Misunkumilo pamoja na Kata ya Mpanda Hoteli. Katika maeneo haya kuna wananchi wako pale wamejenga wana miaka zaidi ya 60 mpaka leo. Vilevile kuna viwanda pale na pia kuna wananchi wana mashamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii wamezuiliwa kuendelea kufanya shughuli za kiuchumi kwenye maeneo yale, wameshindwa kulima, wananchi wanakufa na njaa katika kata zile. Eneo lile lina mgogoro lakini Serikali mpaka sasa haijawahi kusema ni lini sasa mgogoro huu utakwisha ili hawa wananchi sasa waache kupigwa, waache kunyanyaswa na Serikali ambayo mnasema ni Serikali ya amani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la malipo ya wanajeshi. Hivi tunavyoongea kuna wanajeshi zaidi ya 250 ambao wamehamishwa kutoka Makao Makuu kuja Dodoma hapa katika Mji wa Dodoma, hawajalipwa na wengine wako humu ndani. Serikali ina mkakati gani wa kuwalipa hawa wanajeshi? Mmewahamisha, mmewaleta hapa watu wameacha familia zao. Tunaomba sasa katika bajeti hii itengwe fedha kwa ajili ya kuwalipa hawa wanajeshi, wanateseka na familia zao zinateseka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niongelee pia suala la mwisho linalohusu utawala bora. Tunathamini kabisa kazi zinazofanywa na Jeshi, lakini tunaomba hawa wanajeshi bajeti hii sasa ilenge maana ya kuwajengea nyumba ili watoke katika makazi ya watu, maana imekuwa ni kero; wananchi wanakuwa wanaogopa, lakini na Jeshi nalo zile kambi zake zinashindwa kufanya yale majukumu kama Jeshi kwenye maeneo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na migogoro mingi. Ni kweli, wanajeshi wana haki kabisa endapo mwananchi anakuwa amekosea, lakini kero nyingine inapokuja kuna makosa madogo madogo, unakuta mwananchi amemuudhi huyu mwanajeshi basi hicho kipigo

atakachokipata, wengine ni vilema. Ukiangalia katika fukwe zetu unakuta mwanajeshi anamlazimisha mwananchi kula samaki mbichi, leo hii tumefikia hapa! Wananchi wetu wanateseka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaliomba Jeshi, ni kweli wananchi wanakosea, sasa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Sophia Mwakagenda

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na mimi nichukue nafasi hii kuweza kuchangia katika Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, binafsi ninayo maswali kwa Waziri atakapokuja hapa kuhitimisha. Tunataka tujue, Jeshi lina madeni makubwa sana linayodaiwa na watu waliohudumia Jeshi. Sasa sifahamu ni lini Serikali itaweka pesa tunazozipitisha hapa Bungeni na kuhakikisha fedha hizo zinakwenda kwenye Wizara hii kuweza kutimiza majukumu yao? Leo hii mnajinasibu kwamba mnahitaji Jeshi lisiaibike, lakini wakati huo huo shilingi bilioni 200 lakini mnatoa chini ya asilimia 14. Sielewi mnaongea nini na mnafanya nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, tunafahamu Kiwanda cha Nyumbu ni sehemu ambayo Tanzania yetu ingweza kujivunia, wanatengeneza magari, lakini ukifika pale utashangaa sana mashine ni toka Nyerere yupo, alipokuwa akitegemea mkonge na sasa tuna dhahabu. Mnasema Tanzania ya viwanda, kwa nini tusiwekeze kwenye jeshi pale upande wa nyumbu tukaona hiyo dhamira ya viwanda ikitekelezwa kwa kutumia jeshi lile? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda pale vifaa havifanyi kazi, mashine ni mbovu, lakini pesa bado ni ndogo. Ndugu zangu mimi ninaomba tuache siasa katika mambo ambayo ni ya msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati huohuo wanajeshi hawa, amezungumza aliyepita, unawezaje kuhamisha wanajeshi ukawaleta, ni kweli wao wanatii, wakati wa kuhama unaambiwa uondoke asubuhi unaondoka, lakini ni lazima tufikirie hawa watu wana familia zao! Mheshimiwa Waziri utakapokuja kutujibu, utuambie ni lini wanalipwa, kwa sababu si kweli kwamba tunasubiri bajeti hii; kama pesa ni za bajeti iliyopita lazima utuambie wanalipwa lini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapinga UKIMWI kama Taifa, leo mwanaume mwanajeshi yuko Dodoma, familia yake iko Dar es Salaam, hajui anarudije kwa sababu kazi zao zinaenda kwa *order,* usipompatia hela unataka nini? Mke wake kule atatafuta mtu, atatafuta mbadala na yeye huku atatafuta mbadala. Kwa hiyo, ninaomba walipwe sawa sawa na stahiki yao wanayotaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jeshini kulikuwa kuna maduka ambayo yana punguzo la bei, lakini tunaambiwa kwamba yale maduka yamefungwa. Wanajeshi hawa hawana muda wa kufanya biashara, wanahitaji kupata *incentives,* kumuwekea duka lenye bei nafuu ni kumtia moyo wa utendaji kazi. Sasa sijajua hizo bajeti na jinsi ya kufunga mikanda kama kunafika hadi kwenye Jeshi, tukifika hapo nchi inaangamia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kauli zinasemwa na Waheshimiwa Wabunge wengine, sitaki kuwataja umekataza, tunapozungumzia haki sisi sio Wazambia, sisi ni Watanzania, ni wazawa, tunazungumzia mustakabali wa Taifa hili bila kupendelea. Si sawa kutuona sisi ni magaidi tunapozungumzia na kusema tunawachonganisha wanajeshi na wananchi, kwani wanajeshi hawajui kama wao wanakosa haki zao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna haki ya kuzungumza pasipo kupendelea; na msijifiche kwenye kichaka cha kwamba sisi ni wapinzani, tunayo haki, tunalipwa mshahara sawa na ninyi na lazima tulalamike na lazima msimamie haki na muifanye kazi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Wananchi linajitahidi sana kutetea Taifa letu, lakini ijapokuwa hii inahusika na miundombinu pia, kwenye mipaka yetu madaraja ni mabovu. Leo hii tukipata shida kama nchi mimi nakwambia hivyo vifaru ambavyo wanavyo kwa kupitisha hawana. Sasa hapa Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi uonane na Waziri wa Miundombinu uone ni jinsi gani utaweka mipakani madaraja. Kule kwetu Kyela madaraja ni mabovu, Malawi wameonesha chokochoko kuja kwetu, je, wakifanya kweli, tunapita wapi? Ninaomba unapokuja kuhitimisha ujaribu kuliweka hili wazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna vijana wanafanya kazi ya ulinzi kwenye SUMA JKT, mishahara wanayopata ni midogo. Sote tunajua kuna makampuni ya ulinzi yanalipa hadi shilingi 500,000 wafanyakazi wao, vijana hawa wanapata chini ya shilingi 200,000, mimi nafikiri si sawa. Ninaomba Mheshimiwa Waziri kwa bajeti inayokuja ufikirie jinsi gani vijana wale wataongezewa mshahara. Na ninaomba pia na ninashauri kama ikiwezekana makampuni binafsi mengine yapunguzwe, ili tuongeze idadi ya vijana kwenye JKT na kuchukua *tender,* ikiwezekana zote kwenye Serikali, lakini pia hata makampuni binafsi tulazimishe wachukue SUMA JKT. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Wananchi pamoja...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Saada dakika tano, Mheshimiwa Mattar dakika tano.

**MHE. SAADA SALUM MKUYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mimi pia nachukua fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kazi kubwa ambayo anaifanya.

Nadhani hatuna budi vile ile kulipongeza Jeshi letu la Wananchi wa Tanzania, hususan kwa upande wetu wa Zanzibar nadhani limejitahidi sana kurejesha *discipline* ambayo ilikuwa imeanza kutetereka, kwa hivyo tunalipongeza sana Jeshi letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja atueleze, kuna hospitali abazo zinaendeshwa na Jeshi. Ni Hospitali za Kijeshi ambazo wananchi wamekuwa na *confidence* nazo kwa kiasi kikubwa. Mwananchi ukimwambia aende katika hospitali ya kawaida na Hospitali ya Jeshi anakwenda katika Hospitali ya Jeshi kutokana na *confidence* kubwa aliyokuwanayo juu ya utendaji wa wanajeshi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hospitali hizi ziko katika hali mbaya sana, dawa hakuna, hakuna vifaa, lakini hata wale madaktari ambao si wanajeshi ambao wanapangiwa katika vituo vile wanakuwa hawakai kutokana na mazingira duni ambayo yapo katika vituo vile. Sasa tunaomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha atuambie ni mkakati gani hasa umewekwa kuhakikisha kwamba hivi vituo ambavyo vinatoa huduma kwa wananchi vinaimarishwa ili viwe na ufanisi zaidi kwa watendaji lakini vilevile kwa vifaa na dawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inafika hadi kwa mwezi vituo kama vile vinapata *OC* ya shilingi 100,000, haviwezi kuendesheka kwa namna kama ile. Jimboni kwangu kipo kituo cha namna hiyo, inafika hadi hata *panadol* ya kuwapa wale wananchi wanaowatibu hawana. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri nadhani hili lichukuliwe *special consideration* na utuambie mkakati ambao unatarajia kufanya katika bajeti hii ya mwaka 2017/2018. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumzia kuhusiana na wanajeshi wastaafu. Wanajeshi wetu wastaafu Mheshimiwa Waziri wanahangaika sana kufuata mafao yao. *Once* wanapostaafu tu ile *connection* baina yao na yule aliyekuwa mwajiri wao inakatika. Kwa hiyo, anapostaafu huyu

mwanajeshi, na hii ni kwa sababu ya *experience* ninayo, anakuwa hana msaada wowote zaidi ya kuanza kuhangaika kwenda kurudi, kwenda Hazina kudai mafao yao. Pengine wale ambao walikuwa wakihangaika katika kudai mafao yao kwa muda mrefu huenda taarifa zao zimepotea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kule jimboni kwangu kuna mwanajeshi amestaafu muda mrefu, ni mtu mzima, amenipa namba yake ya *file* nimekwenda Hazina, namba ya *file* ndio, lakini jina silo kabisa. Hii inaashiria kwamba, wale wanajeshi wetu wakistaafu inakuwa ile *connection* hata zile taarifa zao zinakuwa hazipo, zinapotea, hakuna mtu wa kuwafuatilia. Kwa hiyo, tunaomba sana Mheshimiwa Waziri hawa wanajeshi wetu kuwe kuna mkakati maalum wa kutunza taarifa zao wakati ambapo wapo kwenye ajira, lakini wanapostaafu lazima kuwe kuna usaidizi kutoka katika taasisi zao walizokuwa ili wasiende kule kupata taabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa ni watu ambao wamefanya kazi nzuri kwa Taifa hili, ni watu ambao wameweza kulinda mali pamoja na roho za raia kwa kipindi kirefu na katika wakati mgumu. Haiwi vyema na haiwi busara kuona kwamba wakistaafu ndiyo sasa waanze wao wenyewe kuhangaika, waende Hazina, wapande ngazi warudi; na mara nyingine, hususan familia zile zinazoathirika. Wakati mwingine mwanajeshi anakuwa amefariki na familia ile kuanza kufuatilia mafao ya marehemu inakuwa ni kazi kubwa sana, wanakuwa hawapati usaidizi wowote kutoka katika jeshi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu, kama walivyosema wengi kwamba sasa hivi kumekuwa kuna mchanganyiko baina ya makazi ya raia na Kambi zetu za Jeshi. Tunapata taabu sana sisi ambao tuna majimbo na tukiwa tunataka kukarabati miundombinu ambayo raia wao wenyewe pia wanatumia, lakini zimepita katika maeneo ya Jeshi, tunapata tabu sana. Sasa Mheshimiwa Waziri tunaomba hili nalo liangaliwe vizuri, jinsi gani sasa kama tukitaka kukarabati

miundombinu katika sehemu ambazo Kambi za Jeshi zinapita lakini na raia wanatumia, tunafanya nini? Kwa sababu hii imekuwa ni changamoto kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la mwisho ni kuhusiana na mafunzo haya ya JKT. Upande wetu kule Zanzibar hizi nafasi zinakuja...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mattar.

**MHE. SAADA SALUM MKUYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. MATTAR ALI SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia katika Wizara ya Ulinzi. Kwanza nimpongeze Waziri wa Ulinzi, kaka yangu Mheshimiwa Hussein Mwinyi kwa kazi nzuri ambayo anaifanya katika kuliendesha Jeshi hili, nikupongeze sana kaka yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nigusie suala la...

**MWENYEKITI:** Ajiandae Mheshimiwa Khadija Aboud!

**MHE. MATTAR ALI SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Naam!

**MWENYEKITI:** Endelea, endelea!

**MHE. MATTAR ALI SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mimi nigusie katika uchukuaji wa vijana kwenda JKT. Kwa upande wa Zanzibar uchukuaji wa vijana kwenda JKT tulikuwa tukilipigia kelele sana, nafikiri hata Bunge lililopita nimelizungumzia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wetu wa Zanzibar bado uchukuaji wa vijana hawa ni kidogo sana.

Kwa hiyo nimuombe sana Mheshimiwa Waziri, aweze kutusaidia kwa hili, aliangalie kwa macho mapana ili kuhakikisha vijana wetu kutoka Zanzibar wanaongezeka katika kuchukuliwa, na hasa kuangalia kwa sasa kama kauli yake juzi alivyoisema kwa makini kuwa vikosi vyote vya ulinzi, hata Jeshi la Polisi, basi watakuwa wanachukua vijana hawa kutoka ndani ya JKT.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimuombe sana Mheshimiwa Waziri aweze kutuongezea kwa upande wa Zanzibar kuchukua vijana hawa wa kwenda JKT angalau tufike vijana 600 kutoka vijana 300 ambao wapo sasa hivi. Nimuombe sana Mheshimiwa Waziri kwa hili aliangalie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Mheshimiwa Waziri nikuombe sana, nilikuwa nikilizungumza sana Zanzibar tuna Kikosi chetu cha JKU ambacho kinafanana sana na Kikosi hiki cha JKT, nikuombe sana Mheshimiwa Waziri katika mipango yako na mazungumzo yako vijana hawa wa JKT ukitaka kuwachukua kwa kutoka upande wa Zanzibar ni bora sana kuchukua eneo hili la JKU kwa sababu unapata vijana ambao wanakuwa wameshapata mafunzo mazuri, vijana ambao wana mwelekeo mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nikuombe sana Mheshimiwa Waziri uweze kulifikiria hili. Mheshimiwa Waziri hili hata bajeti iliyopita mimi nililizungumzia sana kuhakikisha kama vijana unapotaka kuchukua basi uelekee katika kikosi hiki cha JKU kwa sababu, hiki kikosi tayari kuna vijana wameshaandaliwa kwa muda mrefu, vijana wazuri ambao wana haki ya kupelekwa katika JKT na kupata ajira ya jeshi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, nigusie upandishaji wa vyeo vyeo vya juu kwa askari kutoka Zanzibar. Ni jambo la kushangaza sana kwamba hata hawa askari wetu kutoka Zanzibar bado upandishaji wao wa vyeo vya juu umekuwa hafifu sana katika jeshi hili. Kwa hiyo, nimuombe sana Mheshimiwa Waziri aweze kuliangalia hili kwa makini,

hata akija akatoa maelezo yake hapo atueleze kuna askari wa vyeo vya juu wangapi kutika Zanzibar, kwa sababu tuangalie katika uwiano mzuri, ili tuweze kufika pazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu nigusie ile *pension* ya askari wastaafu wa zamani. Hili ni jambo kubwa sana Mheshimiwa Waziri, hawa wazee wanapostaafu huko wanalalamika sana. Kuna Sajenti aliyestaafu, sasa hivi pensheni yake analipwa takriban zaidi ya shilingi 600,000, lakini jambo la kushangaza sana yule yule Sajenti wa zamani ambaye ameondoka katika hili Jeshi hata nusu yake hafiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sana hawa ni wazee wetu ambao wamefanyakazi kwa nguvu zao katika Jeshi hili lakini hatimaye basi malipo yao ni madogo sana.Wanapata taabu na wanaadhirika sana. Nimuombe Mheshimiwa Waziri aweze kuliangalia kwa makini suala hili ili kuhakikisha kwamba hawa wazee wetu wanapandishwa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Mattar, Mheshimiwa Khadija Aboud, ajiandaye Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso

**MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Awali ya yote kwanza naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza na Kambi ambazo zimezungukwa na maeneo ya raia. Naomba Serikali ilishughulikie suala hili kwa haraka kwa sababu tayari kuna baadhi ya maeneo ya kambi ukipita nje yanayofanyika ndani ya Kambi ya Jeshi yote raia wanayaona. Mfano Kambi ya Mwanyanya inahitaji ukarabati wa kujengewa ukuta. Pia naomba Serikali sasa ilipe fidia lakini pia izungumze na Serikali kupata maeneo mengine kwa ajili ya Jeshi, maeneo yawe ni

ya Serikali yasiyohitaji watu kulipwa fidia ili kuweka akiba kwa hapo baadaye kwa ujenzi wa Kambi na matumizi mengine ya Jeshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ajira za JKT, nashauri pia isiwe kwenye vikosi vya Jeshi tu lakini pia hata ajira za taasisi nyingine za Serikali na Serikali kwa ujumla iwafikirie vijana wetu hawa wanatoka katika Jeshi la Kujenga Taifa ili wapewe kipaumbele kwa sababu vijana hawa tayari wameshafunzwa uzalendo, ujasiri pamoja na maandili ya kuitumikia nchi na Taifa kwa jumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nalipongeza Jeshi letu kwa kukabiliana na vitendo mbalimbali viovu vinavyofanyika katika mipaka yetu ndani na nje ya Tanzania ikiwemo kudhibiti mambo ya uharamia na mambo mengine yote yanayojitokeza yanayoashiria mambo ya kigaidi na mengineyo. Nalipongeza sana Jeshi letu kwa kazi nzuri linayoifanya katika kusaidia mambo mbalimbali yakiwemo majanga na maafa yanayotokea ndani ya nchi, wamekuwa mstari wa mbele sana kutoa msaada wa hali na mali na nguvu zao zote katika kuhakikisha wananchi wanaishi kwa amani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe pongezi za dhati kabisa kwa Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Tanzania, Waziri wa Ulinzi, Mkuu wa Majeshi, Kamanda wetu wa Majeshi na Majeshi yote nchini Tanzania kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kulinda nchi yetu, mipaka yetu na raia kwa ujumla. Kama ilivyotokea kuashiria kwa uvunjifu wa amani uliotokea Zanzibar wakaenda pale kwa ajili ya kulinda amani ya nchi na hawakwenda kushiriki uchaguzi wamekwenda kusimamia amani ya nchi na wameifanya kwa uzalendo mkubwa na nchi sasa iko shwari nchi iko salama, mipaka ya nchi yetu iko salama, tunawashukuru wanajeshi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachokiomba mahitaji yao ya msingi tuwasaidie, yakiwemo marupurupu na mambo mengine ya kupandishwa vyeo na madaraja ili waweze kufanya kazi zao kwa weledi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ninaloliomba, mwenzangu alichangia kuhusu vituo hivi vya afya, ni kweli vituo vya afya na Hospitali za Jeshi zinatoa msaada mkubwa sana kwa raia. Naomba ziongezewe vifaa na ziongezewe watalaam na kuwapatia mafunzo zaidi ikiwemo kuwapatia mafunzo wanajeshi wetu ili kukabiliana na hatari zinazojitokeza za kimataifa za uharamia na ugaidi. Naomba mafunzo hayo yaendelee kutolewa zaidi kwa wanajeshi wetu na hasa vijana wadogo ambao ni nguvu kazi kubwa ya Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho niongezee tu kwa kusema kwamba Jeshi letu ni imara, Jeshi letu linafanya kazi nzuri, na ninakipongeza kwa dhati kikosi kile ya Makomandoo wa Jeshi. Mheshimiwa Waziri kikosi kile ukione kwa jicho lingine zaidi la huruma kwa sababu ndicho kikosi ambacho tunakitegemea yatakapotokea majanga na maafa makubwa ndani ya nchi yetu, lakini Mwenyenzi Mungu naomba yasitokee hayo, nchi yetu iendelee kuishi tuishi kwa amani na salama, mipaka yetu iwekwe salama, na nchi yetu iwekwe salama**.** *(Makofi)*

Mheshimwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante*. (Makofi)*

**MWENYEKITI:** ahsante, Mheshimiwa Kakoso jiandae Mheshimiwa Maryam Msabaha

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwenye Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Awali ya yote nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa sana anayoifanya pamoja na Waziri husika wa Ulinzi na Usalama pamoja na wanajeshi kwa ujumla. Niwapongeze kwa kazi nzuri wanayoifanya ya uzalendo kwa nchi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nizungumzie sana suala la ulinzi na usalama hasa kwenye mipaka yetu. Mheshimiwa Waziri alipokuwa anawasilisha amezungumzia mpaka mrefu wa Mashariki. Mimi niiombe tu Wizara hii

ielekeze nguvu sana kwenye mpaka wa Mashariki hasa kwenye maeneo ya Mkoa wa Pwani, Lindi na Mtwara ili kuhakikisha mipaka hii inaimarishwa vizuri. Maeneo haya kwa sasa yameanza kuwa na dalili za ugaidi. Ni dalili ambayo Jeshi la ulinzi ni vema likajipanga vizuri kudhibiti yale yanayojitokeza ili kuokoa Watanzania wenzetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo ningependa kuzungumzia ni mpaka wa Magharibi, kwa maana ya Ziwa Tanganyika. Niipongeze sana Serikali kwa kutuletea kituo cha Jeshi la Ulinzi kwenye eneo la jimbo langu pale Kata ya Ikola. Kituo hiki ni kituo muhimu na kimesaidia vitu vingi sana hasa mali za raia ambao kipindi cha nyuma walianza kuwa na wasiwasi mkubwa baada ya Waasi wa Kongo wale waliokuwa wakizidiwa wanakimbilia nchini kwetu na kufanya uhalifu kiasi kwamba wananchi wa mwambao wa Ziwa waliishi bila amani lakini baada ya kuweka kile kituo, ukweli kimewasaidia sana wananchi na amani ipo ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu kwa Serikali hasa kupitia Wizara hii, tunaomba kile kituo mkiangalie kwa makini sana vitendea kazi ambavyo wanafifanyia shughuli pale havitoshelezi. Wanajeshi ambao wako pale hawana gari zuri la kufanyia kazi, hawana boti za doria ambazo kimsingi ni vitendea kazi vinavyohitajika ili viweze kusaidia usalama wa nchi yetu. Mimi nilikuwa naomba eneo hili liangaliwe sana, sambamba na kuwawekea umeme kwenye kituo chao ambacho wanafanyia kazi. Hata hivyo, bado wanajeshi wanaofanyakazi kwenye maeneo haya ni wazalendo kweli kweli; hata zahanati hawana. Mimi nilikuwa naomba Wizara iangalie umuhimu wa kuweka angalau kituo kidogo pale ambacho kitasaidia afya za wanajeshi kwenye maeneo yale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kuishukuru sana Serikali kupitia SUMA JKT ambao tumewapa maeneo makubwa sana kwenye Wilaya ya Mpanda kwa ajili ya uwekezaji. Kuwapa nafasi ya kutengeneza mazingira ya uwekezaji kwenye Wilaya yetu kutasaidia sana kutoa elimu kwa wananchi hasa wa Mkoa wa Katavi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inapojipanga kuwekeza kupitia SUMA JKT, niombe yale maeneo ambayo watakuwa wamepewa wafanye kazi ya kuwasaidia wananchi wanaozunguka miradi ile ya maendeleo kwenye eneo hilo. Hii ni sambamba na kuwashirikisha, kuwapa elimu hasa kwenye suala zima la kilimo,ufugaji pamoja na kusaidia pembejeo kama watakuwa wanazo kwenye maeneo yale ili Jeshi liwe na dhamana ya kutengeneza mazingira ya kwao na kusaidia wananchi ambao kimsingi Halmashauri imetoa eneo bure bila kutoza gharama ya aina yoyote. Ninaomba sana katika hili Serikali kupitia JKT lisaidie kwenye maeneo hayo.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe sana Serikali, JKT wamepewa maeneo yale ni pamoja na kuomba msaada wa kusaidia suala zima la uhifadhi mazingira. Eneo hilo ni miongoni mwa maeneo ambayo yamekuwa na uvamizi wa mazingira ambayo wananchi wanaingia kwenye misitu; sasa tunaamini ujio wa SUMA JKT utasaidia pamoja na kutatua tatizo lile la uharibifu wa mazingira ambayo kila mara unakuwa inajitokeza kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hali ya usalama, tuna misitu mikubwa sana ambayo ni pamoja na Msitu wa Tongwe Mashariki, Msitu wa Tongwe Magharibi. Kimsingi eneo hili linahitaji msaada sana ambao tutahitaji SUMA JKT watakapokuwa wanafanya shughuli zao za uzalishaji watusaidie na hali ya kutunza usalama kwenye maeneo yale na ikizingatiwa maeneo ambayo tayari tulikuwa ni maeneo yaliyokuwa na wakimbizi, kwa sasa hivi ni maeneo ambayo tayari wamekuwa Watanzania wapya. Hata hivyo wapo wachache ambao wanafikiria mazingira bado ni yale yale. Kwa hiyo, tutaiomba Serikali idhibiti wale wachache wenye malengo mabaya tofauti na Serikali ili waweze kutusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho niombe sana ushirikiano na Serikali kwa ujumla, kwamba tunaomba sasa nafasi za kazi zitakapotoka wananchi wa maeneo yale wapewe kipaumbele ili waajiriwe na Jeshi la Kujenga Taifa

kwa sababu ni nafasi pekee ambayo tumeipata itakayowasaidia Watanzania wote kwa ujumla na Mkoa wa Katavi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Maryam Msabaha.

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa hii ili nichangie kwenye Wizara ya Ulinzi na Usalama. Kabla ya yote nimshukuru Mwenyenzi Mungu kwa kunipa uhai na pumzi, nimesimama tena katika Bunge lako hili, ni shukrani ya pekee nairudisha kwa Mwenyenzi Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nimpe pole kaka yangu Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi kwa kutotendewa haki katika Wizara yake kwa sababu tumekuwa tukipitisha bajeti hewa, kwa sababu Wizara haitendewi haki. Hii Wizara ni Wizara nyeti, na Wizara hii mnategemea miujiza gani na hawa mnasema wasiseme, lakini wataandamana kwenye mioyo yao. Niiombe Serikali ihakikishe Wizara hii inatendewa haki kama wizara nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe Serikali iangalie Wizara ya Ulinzi pamoja na Jeshi la Kujenga Taifa. Hili si Jeshi tu la kutuma wakati wa uchaguzi bali niseme Jeshi hili lipo kwa ajili ya kulinda mipaka ya nchi na kwamba halipo kwa ajili ya kulinda uchaguzi. Niwapongezea pia kwa weledi wao mzuri wa kulinda mipaka ya Nchi ambayo iko salama mpaka sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la kukata nishati ya umeme katika Kambi za Jeshi. Mimi nashangaa sana, kwa nini Serikali isipeleke pesa kwa wakati? Kama Wizara ilikuwa inatengewa pesa kwa wakati fedha zinazotengwa hapa zinapitishwa zinapelekwa kama zilivyo pia deni hili la nishati ya umeme lingepunguzwa, lakini nasijaabu mnasema mnakata umeme mkikata umeme jueni Jeshini kuna kazi nyeti

kazi nyingine haziwezi kutajwa zile kazi zitafanyika vipi au mnategemea miujiza gani? Hawa wanajeshi wawashe tochi? Kuna sehemu nyingine hawawezi kuwasha tochi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima wawe na umeme masaa ishirini na nne, lazima umeme uwake Jeshini, hakuna kusema hapa kazi Jeshini kazini umeme ni lazima uwake, Mheshimiwa Rais akate umeme sehemu zote, lakini si Jeshini. Kuna vitu nyeti vya ndani ya Serikali viko Jeshini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna kufunga luku, luku mtawafungia vipi wanajeshi jamani? Tangu enzi ya Nyerere mbona akujafungwa luku hiyo luku inatoka wapi? Angalieni mkipeleka pesa haya masuala yote yataondoka, na kama kuna pesa za kurudishwa kwenye nishati zitarudishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine mnasema wanajeshi wanaripoti kazini kuanzia saa 12 asubuhi anakaa mpaka jioni. Kwa mfano, anatoka Kibaha na kurudi Dar es Salaam, labda Mbagala au wapi, sasa huyu mmemfanya yeye *robbot?* Toeni stahiki ambazo zinapaswa kwa wanajeshi. Leo mnahamisha wanajeshi mnawapeleka vituo vingine vya kazi lakini huku nyuma wanaacha familia, mnategemea nini? kuna matukio mbalimbali yametokea wanajeshi kuua wake zao; hawawaui kwa makusudi ni hasira huko alikokwenda pesa hajapewa huku mke wake labla kafanya michepuko, ninyi ndio mnasababisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naomba fedha itolewe kwa wanaopata uhamisho wapewe stahiki zao waende na familia zao hakuna kutengeneza mambo mengine vifo kwa wanawake visivyokuwa na sababu na kutengeneza UKIMWI usiokuwa na sababu. Kwa hiyo, naombeni chonde chonde muangalie kwa makini, isiwe leo tunapitisha shiingi bilioni kumi na moja lakini hata shilingi bilioni moja hampeleki mnategemea nini? Yale magwanda nayo yanahitajika yafuliwe, viatu vinataka vibrashiwe *(be brushed)* kama mlivyosema kwamba huko barabarani *traffic* wakikamata nao wanataka ya *brush* na hawa pia wanataka *brush*.

Mheshimiwa Mwenyekiti tuangalie hospitali; hizi hospitali, kwa mfano Lugalo. Hospitali ya Lugalo imekuwa ni hospitali hata viongozi wengi wa kitaifa wakifa wanapelekwa kule. Lakini tuangalie changamoto zilizopo katika hospitali ya Lugalo. Naomba Serikali iziangalie hospitali hizi kwa jicho la makini, na bajeti inayopagwa tuhakikishe ina madaktari wanajeshi wanapata stahiki zao wanapata mafunzo, wanapata masomo, wapewe kila kinachopaswa kwa sababu hospitali hizi hazihudumii wanajeshi tu, zinahudumia na raia wa kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Zanzibar unakujua na Migombani unakujua. Hospitali ile ya Jeshi ya Migombani ni ya siku nyingi kituo kile ni cha siku nyingi na kipo sehemu nyeti sana wewe mwenyewe inaijua iko karibu na Ikulu ya Migombani, lakini kituo kile kimekuwa kinapokea watu wengi mpaka majeruhi, kituo kile ni cha tangu enzi ya ukoloni. Angalieni namna gani ya kuboresha kituo kile ili kiende na sayansi na tecknolojia. Tusikae tu kituo kile ni kidogo na kiko barabarani kubwa, sehemu yenyewe ni nyeti, lakini kituo hakiko katika ubora wowote. Kwa hiyo, hilo pia naomba lifanyiwe kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kuhusu mipaka ya Jeshi umeangalia migogoro nakushukuru, migogoro ya Zanzibar mingi umeishughulikia, lakini bado kuna migogoro umebaki wakati wa kwenda kulenga shabaha mwangalie na kule wakishalenga shabaha na vile vitu ambavyo vinavyobaki kule viondoshwe ili visiwadhuru...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Matiko dakika tano.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuweza kunipatia nami fursa kuchangia bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Wizara ambayo ni muhimu sana kwa ulinzi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa masikitiko makubwa kwamba tunakaa hapa tunapitisha bajeti ambazo hazina uhalisia na hatimaye utekelezaji wake unakuwa ni wa kusuasua. Waziri wakati anawasilisha bajeti yake hapa ameainisha bayana kwamba fedha za maendeleo ambazo zilikuwa ni shilingi bilioni 248 zimetolewa asilimia 14.5 tu ambazo ni sawa na shilingi bilioni 35.9

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii kuna wazabuni wengi sana wanaidai Serikali ambao wametoa huduma kwenye Jeshi letu la JKT pamoja na Jeshi la Wananchi wa Tanzania. Hawa wazabuni wamekopa fedha kwenye benki, wanafilisiwa na wengine wanafariki kwa sababu ya *pressure.* Nilikuwa naomba Serikali tunapokuja hapa tunatenga hizi bajeti hasa za maendeleo ziwe na uhalisia ili ziweze kwenda kukidhi mahitaji kwa muda wa mwaka nzima kama tunavyokuwa tumepanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine napenda kuzungumzia fedha ambazo zinatolewa kwa ajili ya kupima, kuthamini na kulipa fidia kwa yale maeneo ambayo Jeshi imeyatoa kwa wananchi, tena wakati mwingine bila kufuata Sheria za Ardhi. Katika hili nitajikita zaidi katika eneo ambalo Jeshi la Wananchi wa Tanzania wamejitwalia kule Tarime katika kata ya Nyamisangura na kata ya Nkende ambapo kwa kweli kila mwaka ninakuwa ninasimama hapa naelezea, na Mheshimiwa Waziri amekuwa akiniambia kwamba wanakuja kumaliza kuwalipa fidia. Mwaka jana tulitenga shilingi bilioni 27.7 Mheshimiwa Waziri ameeleza hapa na wote tunaona kwamba haikutolewa hata shilingi 1,000 kwenda kufanya hii kazi; shilingi bilioni 27.7 hata shilingi 1,000 haijatolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nilikuwa nashauri, kwa sababu wanajeshi kwa mfano kwa Tarime kile kosi kilipewa eneo kubwa sana Kata ya Nyandoto; tunaomba waondoke kwa sababu mmeshindwa kulipa kwa miaka yote hii kuanzia mwaka 2008, tunaomba hawa wanajeshi warudi kwenye maeneo yao kule Nyandoto eneo ni kubwa sana ni pori kubwa kuliko kuja kuchangamana na wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi yao iko kule Nyandoto ya kikosi cha 28KJ warudi kule, wakakae kule ili waweze kulinda vizuri dhidi ya mipaka ya Nchi yetu kwa upande wa Kenya. Huku kwenye kata ya Nyamisangura na Nkende wanachangamana sana na wananchi na mmeshindwa kulipa. Kwa hiyo naomba leo Mheshimiwa Waziri uniambie *either* mnatulipa kwa kipindi cha bajeti ya mwaka huu au mwende mkawaombe wale wanajeshi waondoke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanachokifanya sasa hivi kwanza wanakodisha yale maeneo kwa raia yaani wamepoka maeneo ya wananchi halafu wanakodisha kwa kufanya biashara, zaidi ni maslahi ya watu binafsi kule. Naomba uje na wewe mwenyewe Tarime ukae na wataalam wako tulimalize suala hili. Mimi binafsi kama mwakilishi inaniuma sana ninapoona wananchi wanakaa kwa miaka mingi bila kufanya shughuli za maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine, wale ndugu zetu wanajeshi ambao wanakwenda kusoma nje ya nchi mnachelewesha kuwapelekea fedha za kijimu, wanakuwa wanateseka sana. Kwa hiyo, naomba kabisa wakati mnapanga bajeti muweze kuzingatia mjue kwamba mnapeleka wanajeshi wangapi kusoma nje ya nchi muwapelekee fedha za kujikimu ili wamalize mafunzo yao wakiwa na utulivu wa akili na kurudi Tanzania kuweza kulinda nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale wanajeshi ambao unakuta wanatumwa kwenda kulinda amani kwenye nchi zingine; Kambi za Tanzania za wale wanajeshi wetu wanaokwenda kukaa kule ni mbovu, hazina hadhi ukilinganisha na kambi za nchi zingine ambazo wameenda kulinda amani kwenye sehemu husika.

Tunaomba wakati mnawatuma wanajeshi wetu kwenda kulinda amani huko basi na wenyewe muwape hadhi, wawe na makambi mazuri kama wale wengine

ambao wametoka nchi zingine. Ukienda ukiangalia kambi za wanajeshi kule zinatia fedheha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mwisho nimalizie kwenye *top up allowance.* Wanajeshi mara ya mwisho wamelipwa hizi *top up allowance* ni mwaka wa jana mwezi wa tatu. Sasa hivi ni zaidi ya mwaka hamuwalipi hizi stahiki zao. Tunarudi pale pale, tunapopanga bajeti zetu tupange bajeti yenye uhalisia, tujue kwamba katika Wizara hii tuna mahitaji haya na haya. Tuweze kutimiza yale mahitaji ambayo ni ya muhimu, kwa mfano hii *top up allowance* ni hitajio ambalo mtu anapokuwa anafanya kazi anajua kabisa anatakiwa alipwe. Sasa inapita mwaka bila kuwalipa; na ndiyo maana hotuba ya kambi rasmi ya Upinzania imejikita zaidi kuelezea matatizo na maslahi ya wanajeshi wetu.

Kwa hiyo, naomba kipekee kabisa; Hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imeelezea kwa kina sana, dakika tano ni chache kuchambua, naomba Mheshimiwa Waziri uifanyie kazi yale yote ambayo yamebainishwa kwenye Hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni yafanyiwe kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ni kuhusu wanajeshi wetu wastaafu na wale ambao unakuta wameaga dunia. Ni dhahiri na mimi mwenyewe nina ndugu ambao wengine waliaga dunia na wengine ni wastaafu wanakuwa wanaangahika sana kupata mafao yao; naomba muwatendee haki. Hawa ndugu unakuta wametumikia nchi hii kwa uaminifu zaidi, lakini ikija kwenye mafao inakuwa wanatendewa ndivyo sivyo, nashukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Elibariki Kingu, ajiandae Mheshimiwa Deo Ngalawa. Kama Kingu hayupo Mheshimiwa Deo Ngalawa, Ajiandae Mheshimiwa Vedastus Manyinyi.

**MHE. DEOGRATIAS F. NGALAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa ya kusimama kwenye Bunge lako Tukufu kwa ajili ya kuchangia mjadala wa Wizara

ya Ulinzi na Usalama. Kwanza nilipongeze Jeshi letu kwa kazi ambazo linazifanya, kwa kweli ni kazi zilizotukuka na zinastahili kupewa pongezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nijikite moja kwa moja katika suala la ulinzi na usalama. Mimi natoka Ludewa ambako Ziwa Nyasa lipo na kama kwenye hotuba ya Kambi ya Upinzani kwenye ukurasa wao wa 14 na 15 walizungumzia juu ya mgogoro wa Ziwa Nyasa. Labda tu nipende kuweka vizuri taarifa yao kwamba Ziwa Nyasa limezungukwa na nchi tatu; limezungukwa na Tanzania, Malawi na Msumbiji. Kwa hiyo, katika hali ya kawaida Malawi hawezi ku-*demand* eneo la Msumbiji, analo-*demand* ni eneo la Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ulinzi na usalama eneo lile ni pana hasa eneo la upande wa Ludewa. Eneo la upande wa Ludewa bado ninaendelea kusisitiza kwamba lina urefu wa kilometa zisizopungua 250 *around the shore of the lake,* lakini kiusalama na kiulinzi bado limewekwa nyuma. *(Makofi) (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ukijaribu kuangalia eneo lote hilo lenye urefu huo mkubwa bado hakuna vyombo vyetu vya ulinzi na usalama ambavyo vipo huko. Napenda kuchukua tu fursa hii kuliomba jeshi, kuiomba wizara na kumuomba Mheshimiwa Waziri kwamba kuna haja ya kuweka mkakati wa makusudi kwa ajili ya kuimarisha ulinzi na usalama wa eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nazungumza hivyo? Nazungumza hivyo kwa sababu eneo lile halina mawasiliano ya simu; eneo hilo halina miundombinu ya barabara kwa urefu wote huo niliokua nimeuzungumza. Kwa hiyo basi, ifike mahali sasa kwa sababu ya haya mambo yanayoendelea hapa sasa hivi inakuwa ni ngumu sana *incase* ikitokea kitu chochote wananchi kuripoti, *incase* kuchukua kitu chochote, wananchi hata kukimbia basi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imekuwa ikizungumzwa kwamba hapa pana mgogoro na ilifika mahali kipindi kile

yanachimbwa mafuta, unakuta ndege ya Malawi inakuja Tanzania na wananchi hawana *facilitation* yoyote ya kusema kwamba wanaweza wakaripoti. Kwa hiyo, ina maana kuwa kama litatokea janga lolote uwezekano ni mkubwa sana kwenda hayo maeneo na ukakuta kwamba mambo yameshaharibika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, napende tu kuisihi Wizara ikiwezekana sasa na kama itakuwa imeruhusu basi kuwepo na vyombo vya kiulinzi ambavyo vina-*patrol,* angalau kuwepo hata na *marine boats* ambazo zitakuwa zinazungukia kule kwa ajili ya kuimarisha usalama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo naweza kulizungumzia ni juu ya Uwanja wa Ndege Sagalu, uwanja ule ni wa Jeshi lakini kwa mara ya mwisho inaweza kuwa ni miaka 30 iliyopita, ule uwanja umeshakuwa ni pori. Sasa kwa sababu kuna ujio wa makaa ya mawe Mchuchuma na chuma cha Liganga naamini kabisa *facility* ya uwanja ni muhimu. Labda twende kuliuliza Jeshi kwamba *incase* kama utakuwa hauna matumizi kwa sasa, turudishieni Halmashauri ili tuweze kuandaa mazingira ya kufanya kazi nyingine yoyote ya kimaendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kwa kusema hivyo basi naamini; tuna kambi moja ya Jeshi pale Manda ambayo ipo mpakani kabisa mwa Mto Ruhuhu. Sasa ukiangalia lile eneo lote mpaka unakuja unaigusa Kyela hakuna chombo chochote cha ulinzi, hakuna mawasiliano ya simu na hakuna mawasiliano ya miundombinu ya barabara. Kwa hiyo, nichukue tu nafasi hii kuishauri Serikali kwamba ipeleke vyombo vya usalama kule angalau basi hata wananchi wafarijike *incase* kama kitatokea kitu chochote waweze ku-*accommodate.* *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine ambacho ningependa kukizungumzia hapa ni juu ya dhana ya viwanda...

**MWENYEKITI:** Endelea.

**MHE. DEOGRATIAS F. NGALAWA:** ... ni juu ya dhana ya viwanda kwa Jeshi. Ifike mahali sasa Jeshi letu lijiendeshe kisayansi, kwa sababu ninaamini kwamba Jeshi letu lina *multi professionals,* lina madaktari na ma-*engineer.* Kwa hiyo nalo lipange mpango mkakati na ifike mahali jeshi lenyewe kama Jeshi lijitegemee na lisiwe inategemea ruzuku tu peke yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi ninaamini kabisa jeshi lina uwezo wa kujiendesha kisasa kama ilivyoanza ule Mradi wa Nyumbu bado unaweza likaanzisha miradi mingine yoyote ambayo inaweza ikaliingizia kipato japo kwamba litaendelea kupata ruzuku kutoka Serikalini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache mimi niishie hapo, ila napenda tu kwa dhati ya moyo wangu, eneo lile la Ziwa Nyasa sasa hivi lipewe kipaumbele kwani wananchi wameamua kulima barabara wenyewe. Kwa hiyo, tunaiomba Wizara ya Ulinzi maeneo ambayo ni magumu basi tutakapoomba baruti watuletee, na maeneo ambayo yana madaraja ikiwezekana basi tupate hayo madaraja. Kuna baadhi ya maeneo Jeshi huko nyuma lilishaweka madaraja; sasa bahati nzuri maeneo yale imeshapita barabara yale madaraja yanakuwa sasa hivi ni kama hayana kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tungeomba sisi tutakapokuwa tunaomba yale madaraja basi tuletewe kwa ajili ya kufanya *facilitation* ya wananachi wetu kule ili paweze kupitika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Manyinyi ajiandae Mheshimiwa Dau Mbaraka.

**MHE. VEDASTUS M. MANYINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia kidogo katika hii hotuba ya bajeti ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika kwamba wote tunajua kazi kubwa ya ulinzi inayofanywa na Jeshi letu, ni kazi nzuri na niseme tu kwamba hasa kwetu sisi ambao wakati mwingine tumekuwa watembezi tembezi kidogo katika nchi za wenzetu, ukija Tanzania ndiyo unaweza kujua kwamba kweli Jeshi letu linafanya kazi nzuri kwasababu ukilala una uhakika wa kuamka kesho yake. Kwa hiyo baada ya kuwapongeza kwa hiyo kazi nzuri lakini kuna baadhi ya mambo ambayo tunapaswa tuendelee kuwasaidia na ambayo yatahakikisha kwamba kazi zao zinakwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja; Jeshi letu bado lina matatizo makubwa ambayo ni pamoja na madeni. Tunaamini kwamba wanashindwa kufanya mipango yao mizuri kutokana na madeni na kwa maana ya ukwasi wa fedha. Kwa mfano kati ya miradi mizuri waliyonayo ni pamoja na kile kiwanda cha kutengeenza magari kile cha Nyumbu, ni kiwanda ambacho tulitakiwa tuone matokeo yake ya haraka, lakini naamini kwamba kinasua sua hii yote si kwa sababu nyingine lakini ni kwa sababu ya ufinyu wa bajeti. Kwa hiyo, ningeomba Serikali iangalie uwezekano wa kuwasaidia ili waweze kufanya kazi zao vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua kwamba Jeshi wanayo madeni, kwa maana ya wale wazabuni. Kwa hiyo, napo kuna tatizo kubwa kwa sababu fedha wanazopata hazikidhi mahitaji yao, kwa hiyo, Serikali inahitaji kuangalia namna ya kuendelea kuwasaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tu niseme kwamba katika miradi waliyonayo, kwa mfano hawa wenzetu wa JKT; JKT kwangu mimi ninavyofahamu leo tukiamua kuitumia vizuri inaweza ikaleta *impact* kubwa hasa kwa vijana wetu. Nadhani Waheshimiwa Wabunge wenzangu watakubaliana na mimi kwamba kila linapotoka tangazo kwamba sasa kuna nafasi za kwenda JKT katika kila Wilaya unakuta wapo vijana zaidi ya 1,000 wanajipanga pale msululu kwa ajili ya kuomba waende JKT. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na wote tunakubaliana kwamba katika nchi hii kama kuna tatizo kubwa tulilonalo ni tatizo la ajira kwa vijana. Sasa basi JKT kwanza wanafundisha maadili, lakini wanaendelea kufundisha vijana kuipenda nchi yao. Kwa hiyo, katika yale mafunzo wanayofundisha ambayo ni pamoja na mafunzo ya kufanya kazi ambayo ni ya ujuzi ni imani yangu kwamba kama Serikali itaweka nguvu kubwa kwa JKT basi kwa kiasi kikubwa itapunguza tatizo la ajira kwa hawa vijana wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni imani yangu kwamba kwa yale mafunzo ambayo vijana wangekuwa wanayapata pale mfano unazungumzia mafunzo ya kilimo. Ingekuwa ni rahisi zaidi vijana wakafika pale wakapata mafunzo ya uvuvi na mafunzo mbalimbali, sasa wakitoka hapo ni rahisi zaidi wakasaidiwa kidogo na wakaenda kuanza maisha yao kuliko hivi ambavyo tunavyowaacha vijana wanahangaika mtaani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ninaamini kwamba JKT ni mahali pekee ambapo panaweza pakaleta *impact* kubwa. Unaona tunafikia mahali tunakuwa na upungufu wa chakula, lakini tunayo mabonde mazuri, na mengine; labda niseme tu moja, kwa mfano ukiangalia pale kwenye Wilaya ya Musoma walipewa eneo kubwa lakini hawakupewa uwezo; kwa hiyo, mwisho wa yote wameendelea tu kuliangalia lile eneo mpaka mwisho. Kwa hiyo, tunadhani kwamba hayo ni baadhi ya mambo ambayo Serikali ikiwasaidia basi wataweza kufanya mambo mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja karibu na mwisho; kwa bahati nzuri hili tulishalizungumza na Mheshimiwa Waziri; ni suala la fidia kwa ajili ya wale wananchi walioombwa waondoke kwenye eneo ambalo Jeshi imelichukua, eneo la Makoko. Hili ni suala ambalo tumehangaika nalo sasa zaidi ya miaka 15. Tangu mwaka 2005 tumekuwa tukilizungumzia lakini hadi leo. Jeshi walishakubali kwamba wanalipa fidia, kwa maana ya Serikali, lakini hadi leo kila leo wale wananchi wameshindwa kuyaendeleza maeneo yale, lakini vile vile

wameshindwa kuhamia mahali pengine kwa sababu bado hawajalipwa fidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mwisho, nadhani ni wiki tatu zilizopita wale wananchi walituma wawakilishi wao, bahati nzuri baada ya kuona nimezidiwa niliwapeleka moja kwa moja tukakaa na Mheshimiwa Waziri na akahaidi kwamba kwenye bajeti hii tutawalipa fidia. Sasa Mheshimiwa Waziri naomba *commitment* yako utakaposimama kuzungumza uwahakikishie hawa wananchi ili wakae wakijua, kama ulivyoniambia siku ile, wawe na uhakika kwamba kama kweli watapata hizi fedha zao. Maana sasa ukiangalia ni muda mrefu na hata kati ya hao wenye hizo familia wengine walishafariki, sasa familia zao nazo zipo pale zile nyumba zinaelekea kuanguka lakini wameshindwa waende wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni imani yangu kwamba baada ya kupata hayo majibu mazuri kwa mwaka huu tunaweza kumaliza hilo tatizo la wananchi ambalo limewasumbua kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo na mimi naungana na wenzangu kusema naipongeza Serikali yangu kwa kazi nzuri ambayo inaifanya, na ninaendelea kusema tupo pamoja na ni jukumu letu sisi kuendelea kuisaidia ili waendelee kutekeleza majukumu hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Dau dakika tano, ajiandae Mheshimiwa Mwantumu Dau.

**MHE. MBARAKA K. DAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa fursa hii. Nianze kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa mtoa hoja, Waziri Dkt. Hussein Mwinyi kwa kutuletea hotuba nzuri sana yenye kuleta matumaini kwa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi natokea Kisiwa cha Mafia ambacho kipo mpakani kabisa na Comoro kule. Takribani miezi miwili, mitatu iliyopita tulipata bahati ya kutembelewa na aliyekuwa Mkuu wa Majeshi Jenerali Mwamunyange, katika juhudi za kuhakikisha kwamba wanafungua kikosi pale cha Jeshi katika Kisiwa cha Mafia ili kuhakikisha kwamba suala la ulinzi na usalama linaimarika pale kisiwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni jambo jema sana na sisi watu wa Mafia tumelipokea kwa mikono miwili. Lakini kuna mambo mawili hapa ni vizuri niyaweke kwa *attention* ya Mheshimiwa Waziri ayaangalie yaweze kutusaidia ili hili jambo liwe jema zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza; *site* ambayo wameichagua pale sisi na wenzetu pale Wilayani tumeiona kwamba sio *site* nzuri kwa sababu ni katikati ya Mji wa Kilindoni pale. Lakini kuna *site* ambayo iko maeneo ya Jimbo takribani kilometa 30 kutoka Mjini Kilindoni pale; tulikuwa tunapendelea na tungefurahi sana kama jeshi lingekwenda kule ili kukataa hizi *crush* na wananchi kwa sababu kule kidogo kumejitenga na watu wapo wachache. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini angalizo la pili tungependa pia Kikosi cha Maji kiwepo pale kwa sababu sisi tunapakana na bahari kuu na kule kuna maharamia wale wa Kisomali na pia kuna meli za uvuvi ambazo zinakuja kuvua kule bila ya kibali cha mamlaka husika. Kwa hiyo, tungependa sana kije kikosi cha maji pale ili waweze ku-*patrol* ile bahari na kuhakikisha kwamba hakuna aina yoyote ya uvuvi wa kuvamia wa meli kubwa zinazokuja kuvua pale Kisiwani Mafia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo ningependa nijielekeze sasa kwenye suala la vijana wanaoingia kwenye JKT. Mimi kwa ufahamu wangu kila wilaya imetengewa sehemu yake ya vijana watakaokwenda JKT kila mwaka, lakini kwa bahati mbaya na masikitiko

makubwa sana Mheshimiwa Waziri, inapofika Wilaya ya Mafia wale washauri wa mgambo sijui wanatoka wapi, sijui wapo chini yenu au wako chini ya nani, Mshauri wa Mgambo wa Mafia siku zote lazima ataandikisha vijana kutoka nje ya Mafia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri, hili tunaomba sana mwaka huu lisijirudie, na kama litajirudia basi kuna hatari ya kuvunjika kwa amani katika Kisiwa cha Mafia, kwa sababu vijana wenye *qualification* wapo, lakini Mshauri wa Mgambo analazimisha kuwaleta vijana kutoka nje ya Mafia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanapowachukua wale huku nyuma tunaanza kuulizwa na wazazi, vijana wamemaliza shule za kata hizi, *form four* wanakosa nafasi, kwa nini nafasi hizi wanakwenda kuzichukua watu wanaotoka nje ya Mafia? Serikali imefanya hivi kwa makusudi kwa sababu ya kuleta uwiano ili Jeshi letu liwe na uwakilishi mzuri, kwamba kijana kutoka kila wilaya ya Tanzania anakuwepo katika Jeshi. Sasa zinapokuja nafasi zetu sisi mshauri wako wa mgambo Mheshimiwa Waziri anatuletea watu kutoka nje ya Mafia, inatukera. kwa hiyo kwa mwaka huu sasa tunasisitiza, hili jambo lisijirudie, kama ni kuvumilia tumevumilia kwa miaka ya nyuma huko inatosha sasa, *enough is enough. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti,...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa mchango wako mzuri. Mheshimiwa Mwantumu Dau, ajiandae Mheshimiwa Kingu na wewe kwa dakika tano. *(Makofi)*

**MHE. MBARAKA K. DAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. MWATUMU DAU HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kuwa na hali ya uzima na afya. Nishukuru

ukumbi huu leo wote tuliopo hapa pia tupo wazima wa afya mpaka hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi naomba kuchangia Hotuba hii ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nachangia kuhusu JKT hasa kwa vijana na kule kwetu Zanzibar. Kule Zanzibar kuna vijana wetu ambao wanakwenda JKT na wanakuwa wazuri tu wakirudi kule wameiva, lakini wakifika kule wanakuwa hawana ajira rasmi za kujiajiri, wanahangaika isipokuwa ajira zao ziwe mikononi mwao. Vijana hawa wanakuwa wanatupigia kelele sana sisi wazazi au kama hivi sasa mimi ni Mheshimiwa, lakini huko nyuma nakumbuka sisi Wabunge waliopita walikuwa wanapata hizi ajira kama kwa mtoto wake au mtoto wa ndugu yake lakini ajira walikuwa wanapata kwa mtu mmoja mmoja, kwa hiyo zoezi hili limeondoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi naomba hili zoezi lirudi tena sisi Wabunge tuwe mfano wa kupata kwa kila mtoto kama mmoja mmoja au katika jamii tulizonazo wapate ajira hizi za Jeshi ili na wao wajiajiri na wajisikie. Na wanakuwa na hamu sana ya kwenda Jeshini, lakini ajira kama tunavyozungumza ni ngumu. Hili lirudi na lizingatiwe sana ili wale vijana wawe na imani na Nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niwapongeze Jeshi kwa kazi zao wanazozifanya na hasa jana tu, wakati mimi nakuja huku Bungeni nipo maeneo ya Mlandizi, ilitokea ajali mbaya kati ya basi la Tanga na *coaster* inayotokea Morogoro, walisaidia roho za binadamu pale... *(Makofi)*

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

## TAARIFA

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mzungumzaji anayezungumza anasema kwamba zamani watoto au jamaa za Wabunge walikuwa wanapewa ajira Jeshini, hii haijatokea hata kidogo. Wanapewa ajira Jeshini kutokana na uwezo wao, bila upendeleo, hakuna kitu kama hicho wala haitatokea wala haijatokea. Anapewa ajira Jeshini kutokana na uwezo wake, si mtoto wa Mbunge wala mtoto wa *DC* wala mtoto wa Rais. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dau, taarifa hiyo unaipokea?

**MHE. MWATUMU DAU HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hiyo siikubali kwa sababu mimi sikusema kwamba huyo Mbunge ndiye anayetoa hiyo ajira hapo.

**MWENYEKITI:** Endelea.

**MHE. MWATUM DAU HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nieleweke.

**MWENYEKITI:** Endelea na mchango wako.

**MHE. MWATUMU DAU HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, umesikia, mimi naomba kwamba sisi Wabunge hivi sasa tunaomba kwamba zikitokea hizi ajira za Jeshi basi kama kuna uwezekano tuzipate ili tuwasaidie wale vijana na wale watoto wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea na hotuba yangu hii…

**MBUNGE FULANI:** Majimboni!

**MHE. MWATUMU DAU HAJI: …**majimboni, hata ikiwa majimboni ikiwa kwa jamii lakini tunaomba kwamba tupatiwe na sisi hizi ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi jana limeokoa roho za binadamu pale Mlandizi kati ya basi la Tanga na basi la

*coaster* linalotokea Morogoro, ana-*overtake* basi la Tanga kwa bahati yule amejitahidi kulivusha lakini hakufanikiwa likaenda uso kwa uso dereva katoka miguu hana. Kwa hiyo, pale watu walishindwa kumtoa kila mmoja na imani yake basi walitokea vijana wetu hawa wa Jeshi na wakaenda pale wakaokoa roho zile wakawakwamua na palepale ikatokea gari wakapelekwa hospitali. Mimi ninawashukuru sana na ninawapongeza sana kwa kitendo kile walichokifanya jana. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Dau, bado Waheshimiwa Wabunge wako hapa unaweza ukawafuata ukawaambia vilevile kuwashukuru. Mheshimiwa Kingu, dakika tano.

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kutoa mchango wangu mdogo kwa ajili ya bajeti hii ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa kwa dhati ya moyo wangu nianze kwa kuipongeza Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi kwa kazi kubwa inayofanywa na vyombo vyetu vya ulinzi na usalama hasa Jeshi la Wananchi wa Tanzania na waswahili wanasema ukiona vinaelea ujue vimeundwa, nidhamu kubwa inayooneshwa na Jeshi la Wananchi wa Tanzania ni kielelezo cha utekelezaji bora wa sera za Chama cha Mapinduzi katika kipindi chote toka Taifa limepata uhuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, si siri, Jeshi la Wananchi wa Tanzania ni miongoni mwa majeshi duniani yenye nidhamu ya hali ya juu. Taifa letu la Tanzania tumepata sifa kitaifa na kimataifa, tumeshiriki operesheni mbalimbali duniani na Jeshi letu; ninataka nijivunie hata makamanda mliopo humu kwenye ukumbi; tunasema ya kwamba Chama cha Mapinduzi kinatakiwa kipongezwe kwa kuwa katika kipindi

cha takribani miaka 50 ya Uhuru Jeshi letu limekuwa na nidhamu... *(Makofi)*

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** ...na dunia yote imetutambua kwa kazi kubwa inayofanywa na wapiganaji wetu.

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Alberto.

**T A A R I F A**

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Napenda kumpa taarifa msemaji kwaba si sahihi kulihusisha Jeshi na chama cha siasa, Jeshi lipo kwa ajili ya nchi, halipo kwa ajili ya chama na ndiyo maana tunasema zamani kabisa Jeshi limetolewa katika chama. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kingu, endelea.

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli wa Chama cha Mapinduzi chini ya nidhamu ya Jeshi la Wananchi Tanzania huwezi ku-*exclude* kwa sababu utendaji na utekelezaji wa sera zote toka tumepata uhuru nchi hii imekuwa ikitawaliwa na Chama cha Mapinduzi, unawezaje ukakitenga Chama cha Mapinduzi, unawezaje ukaitenga CCM na mafanikio makubwa yanayopatikana kutokana na nidhamu ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ngoja niwaambie Waheshimiwa Wabunge, nidhamu ya Jeshi letu na ndiyo maana hata leo mchana wakati kuna hoja zimetolewa juu ya vijana wa Jeshi la Polisi wamepigapiga risasi pale juu kidogo jana kwa sababu ya tukio lilikuwa limetokea kwa Mheshimiwa Malima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *let me tell you one thing,* tunapozungumzia nidhamu ya vyombo vya dola, unajua kuna mataifa mimi nimejaribu kutembeatembea kidogo duniani, kuna mahali haya mambo tunayoyaona Tanzania sisi tunayapuuza lakini nataka niwaambieni hawa wapiganaji wa Tanzania kama ni Bunge tukiamua leo tukasema kwamba kwa nidhamu wanayoionesha mimi natoa rai kabisa Waheshimiwa Wabunge kwa bajeti zinazokuja naomba Jeshi la Wananchi wa Tanzania tulipe kipaumbele cha kwanza kwa sababu wapiganaji hawa wameonesha nidhamu ya hali ya juu na Taifa letu limepata sifa kitaifa na kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende katika sekta nzima ya suala la JKT.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hizo *interruption* uzipuuze ili niweze kuendelea na mchango wangu kwa sababu nina muda mfupi.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, JKT kama moja ya sehemu ya kuzalisha ajira, ninaomba nitoe ushauri kwa Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi. JKT, ninatoa ushauri, kwa sababu JKT ina-*recruit* vijana wengi wanakwenda kupata mafunzo, naiomba Serikali tutenge fedha za kutosha, vijana wanapokwenda JKT wakafanya *training* ya kijeshi, wakamaliza kwa kipindi cha miezi sita wapelekwe na watafutiwe mashamba makubwa wafanye uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii italisaidia Taifa kupata chakula lakini pia vijana hawa kwa kipindi hicho watakuwa wanapata ajira *in phase,* wamemaliza walichozalisha kinakuwa mali yao wanaondoka wanaingia wengine, hivi

ndivyo wanavyofanya mataifa makubwa kama China na mataifa mengine duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ninatoa ushauri, wastaafu wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania sasa hivi kuna chama chao kinaitwa MUWAWATA, huu ni umoja wa wastaafu wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania, kwa maslahi ya usalama wa nchi si sahihi sana umoja huu kuwa nje ya mfumo wa usimamizi wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania. Hatari hii inaweza ikajitokeza wakaingiliwa na kuanza kulishwa sumu na kusababisha uasi kwenye nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kwa Serikali ya Chama cha Mapinduzi, MUWAWATA waendelee kuwa na uratibu chini ya Serikali kupitia Jeshi la Wananchi kwa sababu hawa ni wapiganaji wa akiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina takwimu, miaka michache ya nyuma MUWAWATA ulikopeshwa bajaji na wakalipishwa hela nyingi na vikundi vya wafanyabiashara, *this is very dangerous* kwa *security* ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa ushauri, kaka yangu Kamanda Mabeyo najua uko hapa, kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Mwinyi, najua uko hapa kipenzi cha Watanzania, ninaomba upeleke hii *proposal* mkahakikishe kwamba MUWAWATA inakuwa chini ya usimamizi wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kuunga mkono hoja ya Wizara ya Ulinzi

na Jeshi la Kujenga Taifa kuhusiana na makadirio ya matumizi ya fedha ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dunia inashuhudia mabadiliko makubwa katika mifumo ya maisha na mazingira ya kiusalama yasiyotabirika. Katika mazingira haya, ulinzi wa mipaka ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na uhuru wa nchi yetu ni jambo la kufa na kupona linalopaswa kupewa umuhimu mkubwa na wa kipekee sasa kuliko wakati mwingine wowote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika zama hizi za mabadiliko makubwa ya teknolojia na changamoto za ushindani katika ukuzaji uchumi wa viwanda, kama nchi usalama wetu na uhuru wetu unategemea sana uwepo wa jeshi imara la kisasa lenye weledi, vifaa vya kisasa, uzalendo na nidhamu ya hali ya juu. Hivyo basi ni wajibu wetu kama Taifa kuhakikisha inakuwepo bajeti ya kutosha itakayoliwezesha jeshi letu kukabiliana kikamilifu na changamoto za sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Mkinga inapakana na nchi jirani ya Kenya. Katika jitihada za kuimarisha ulinzi Halmashauri ya ilitenga fedha za kujenga daraja ili kuwezesha ulinzi na ukaguzi wa mpaka wetu. Hii ni kutokana na ukweli kuwa kabla ya uwepo wa daraja hilo, ukaguzi wa mpaka wetu ilibidi ufanyike kwa kupitia Kenya. Kazi ya kujenga daraja hilo ilikabidhiwa kwa JWTZ. Natoa pongezi kwa JWTZ kwa kukamilisha kazi ya kujenga daraja hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kuiomba Serikali iongeze nguvu katika ulinzi wa mipaka yetu kwa kuweka miundombinu muhimu kama barabara na madaraja yanayokidhi viwango na mahitaji ya kijeshi katika maeneo yote ya Wilaya za mipakani.

Aidha, fedha na jukumu la kujenga miundombinu muhimu katika maeneo haya ya kimkakati, kiulinzi na kiusalama lisiachwe mikononi mwa Halmashauri bali liwe jukumu la moja kwa moja la JWTZ.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata ya Mwakijembe ni miongoni mwa kata 22 za Wilaya ya Mkinga. Kata hii ipo katika mpaka wetu na nchi ya Kenya na kwa miongo kadhaa wananchi hawa wamefanya kazi kubwa ya kuwa walinzi wa mpaka wetu. Naipongeza sana Serikali kwa uamuzi wake wa kuimarisha ulinzi katika Kata ya Mwakijembe kwenye mpaka wetu na nchi ya Kenya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, wakati naipongeza Serikali kwa hatua hii, utekelezaji wake umekuwa na dosari na hivyo kuitia doa Serikali. Doa hili linatokana na JWTZ kutwaa mashamba ya wananchi bila kutoa fidia stahiki kwa wananchi. Inasikitisha kuwa Jeshi lilitumia mabavu kuwapora wananchi ardhi yao tena kwa kufyeka mazao yaliyokuwa mashambani. Hali hii imeleta manung'uniko na wananchi wanaona wamedhulumiwa na Serikali yao wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kihistoria eneo hili limekuwa mali ya wananchi kwa miongo na vizazi kadhaa. Hata pale Halmashauri ilipoamua kuanzisha skimu ya umwagiliaji, iliamua kuyajumuisha maeneo haya ya wananchi kwenye skimu lakini ikahakikisha umiliki wa maeneo hayo unaendelea kuwa mikononi mwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba sana Serikali ifanye tathmini ya haraka kwa ardhi ya wananchi iliyotwaliwa ili wananchi hawa waweze kulipwa fidia stahiki. Wananchi ambao mashamba yao yametwaliwa ili kuwekwa kambi/ makazi ya jeshi ni Ndugu Benard Kinyili (ekari moja); Ndugu Ngoma Joseph (ekari moja na nusu); Ndugu Hamisi Joseph (ekari moja na nusu); Ndugu Mlewa Malonza (ekari mbili) na Ndugu Mwanza Kiziku (ekari mbili).

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja nikiamini kuwa malalamiko ya wananchi wa Mkinga yatapatiwa ufumbuzi wa haraka.

**MHE. MGENI JADI KADIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia afya njema na kuniwezesha kuchangia hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanajeshi wanaostaafu wanahangaika, hawapati stahili zao mapema, wanapata taabu sana. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali iwaangalie kwa jicho la huruma. Hawa ni watumishi wetu kama watumishi wengine mpaka wengine wanafariki bila kupata haki zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu huduma ya umeme katika Kambi ya Jeshi, Jeshi ni taasisi kubwa leo kukatiwa umeme itakuwa hawajatendewa haki. Wanajeshi ndio wanatulinda sisi ndani ya nchi yetu na mipaka ya nchi yetu ni lazima tuwape heshima. Tunalipongeza Jeshi letu kwa kazi kubwa. Kwa hiyo, wanastahili kulipwa maslahi makubwa na marupurupu wapewe pamoja na kupandishwa vyeo ili waweze kuitumikia nchi yetu kwa weledi mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Vitongoji Ali Haji Camp* waboreshewe nyumba zao, ni za zamani na nyingi ni mbovu na nyumba zilizoko Matangatuani Pemba nazo ziboreshwe. Kambi na Wanajeshi iliyoko Matangatuani ina wanajeshi walio imara na wanafanya kazi kwa weledi mkubwa.

Nashauri wanapopata uhamisho wapewe fedha za kutosha ili watoto wao wasipate shida na matatizo ya kuendesha maisha yao. Pia nataka kujua ni kwa nini wanajeshi wanapopata uhamisho wasichukue familia zao ili kuwapunguzia matatizo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. RIZIKI S. MNGWALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie kwa kutoa masikitiko yangu katika maeneo mawili tu. Moja ni suala la kutumia vibaya Jeshi letu la Ulinzi (JWTZ). Si sahihi hata kidogo kwa jeshi letu kutumiwa kuvuruga shughuli za kidemokrasia nchini hasa chaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ni mbaya na ya kutisha Zanzibar. Binafsi nilipata fursa ya kuwa Zanzibar wakati wa uchaguzi mdogo wa marudio Jimbo la Dimani. Nilishuhudia malori ya JWTZ yaliyobeba "mazombi" watu waliovalia sare za jeshi na soksi usoni (wakijificha) walioshikilia silaha juu yakienda na kurudi barabara ya Fumba. Kwa hakika nilishtushwa sana na tukio hili na kwa heshima kubwa namwomba Mheshimiwa Waziri akomeshe vitisho hivi na matumizi mabaya ya jeshi letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili linalonisikitisha ni Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) kushindwa kujitegemea kiuchumi na kulisaidia Taifa. Hili ni jeshi lenye makambi karibu nchi nzima na nguvu kazi ya kutosha ya vijana wetu wanaokwenda huko karibuni muda wote. Jeshi lina mashamba makubwa, miradi ya mifugo, ujenzi na kadhalika. Ni vipi Jeshi hili lishindwe kuendesha kilimo cha kisasa na chenye tija? Waziri kwa kweli alifanyie kazi suala hili ipasavyo. Kwa wataalam wa fani mbalimbali waliojaa JKT ni aibu kubwa kuwa na jeshi la aina hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine dogo ninalopenda kuchangia kwa leo ni kuomba Bunge kuipa Wizara hii hadhi yake stahiki yaani kuwa Wizara ya Muungano. Kwa hadhi hii Wizara hii inastahiki kupewa muda wa kutosha kwa Wabunge kuchangia kwa nafasi badala ya kupangiwa siku moja tu ambayo inaanza kwa kipindi cha maswali na majibu. Nililisema Mkutano wa Bunge la Bajeti ya mwaka uliopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni Bunge la Jamhuri ya Muungano na siyo la Tanzania Bara. Imekuwa ni tabia/ mazoea ya Bunge hili kutumia muda mwingi (mpaka siku tatu) kujadili masuala ya Tanzania Bara tu (Kilimo, TAMISEMI, Afya na kadhalika) badala ya masuala ya Muungano (Ulinzi, Mambo ya Nje, Ofisi ya Makamu wa Rais na kadhalika).

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho naomba Waziri mhusika aipitie vizuri hotuba ya Kambi ya Upinzani, kwa uadilifu na bila hiyana kwa maslahi mapana/ya jumla ya nchi

yetu na maslahi mahsusi ya walinzi wetu (wanajeshi) wa majeshi yote mawili –JWTZ na JKT.

Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru na naunga mkono hotuba ya Kambi ya Upinzani na kumtakia kila la kheri Waziri wa Ulinzi kwa jukumu nyeti na muhimu alilopewa na nchi yetu.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, washauri wa mgambo hawatendi haki katika kuchukua vijana wanaojiunga na JKT na wengi wao wanatuhumiwa kuchukua rushwa kwa kuwapa vijana nje ya eneo la Wilaya husika. Jambo hili linachafua jeshi letu. Hatua ichukuliwe kuchunguza mambo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tunduru Kusini inapakana na Mto Ruvuma na Msumbiji lakini eneo lote la mpaka huu hakuna ulinzi wowote wa jeshi na wala hamna mawasiliano yoyote ya simu jambo ambalo ni hatari kwa nchi. Hata ile barabara ya mpaka ambayo ilikuwepo miaka 1970 na 1980 haipo kabisa, barabara hiyo imekufa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tunduru kulikuwa na Kambi za Jeshi la Wananchi wa Tanzania maeneo yale yamebaki kuwa mapori. Hivyo tunaomba Serikali iyakabidhi maeneo yale kwa Halmashauri ya Wilaya ili yatumike kwa shughuli zingine za wananchi ikiwa ni pamoja na makazi ya wananchi.

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naunga mkono hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Kujenga Taifa ni la Watanzania wote na inapotokea Kambi ya Jeshi inapokuwa katika kata au jimbo au vijiji naona ni fursa na faraja kwa jamii inayopakana na kambi hizo. Hali imekuwa tofauti kwa

mahusiano kati ya Chita JKT ndani ya Jimbo la Mlimba, Wilaya ya Kilombero na Kata ya Mngeta, Kijiji cha Ikule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya wananchi wa Kijiji cha Ikule inasikitisha. Ni kwa miaka mingi wananchi wa kijiji hicho wanaishi na kufanya shughuli zao za kilimo kwa maisha yao yote. Hivi nichangiapo hapa na Waziri anajua wananchi wale wamenyang'anywa maeneo yote ya kilimo. Kibaya zaidi hata mazao yao ya chakula, mahindi, ndizi, mihogo, viazi, miwa, mpunga na kadhalika vyote vilifukiwa na trekta na baadhi ya wanajeshi na kuzuia kabisa kufika huko wakidai ni maeneo ya jeshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ingawa wananchi na viongozi wa Serikali ngazi ya kijiji waliopo na waliopita wanasema na wako tayari kuongea popote kuwa hawajawahi kuidhinisha mashamba yao waliyokuwa wanalima miaka yote kabla hata ya kambi hiyo kuwepo hapo kuwa walikubaliana katika Mkutano wa Kijiji kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi kwamba wameridhia kukabidhi hiyo ardhi kwa jeshi. Hivi niwasilishapo, tokea mwaka 2016 Desemba hadi leo, wananchi na viongozi wa kijiji, kata akiwemo na Diwani wa Kata hiyo wapo mahabusu kwa madai mbalimbali na hawajui hatma yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuundwe Tume huru kwenda kijijini hapo kutafuta ukweli wa masuala mbalimbali yanayoendelea huko, kwani inasemekana katika vurugu za kugombania mashamba, yuko mwanajeshi aliyeuawa. Pia zipo taarifa kwamba wananchi wengi nao wameuawa (habari ambazo hazijathibitishwa) na hali ya kijijini hapo si shwari hata kidogo, kwani wakati wowote wanajeshi huingia kijijini na kukamata na kupekua nyumba, hata wakati wa usiku na kuleta mashaka kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia kusema uwepo wa Kambi ya Chita ni faraja kwetu na uhakika wa kiulinzi kwa raia, isipokuwa manyanyaso ndiyo karaha kwa majirani wa Kijiji cha Ikule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nipate majibu ya Serikali. Ahsante.

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kuchangia kuhusu JWTZ wanaolinda mpaka - Wilaya ya Kakonko. Wapo wanajeshi wanaolinda mipaka ya nchi yetu kufuatia ujio wa wakimbizi Wilayani Kakonko. Wanajeshi hawa husumbua raia wanaotoka Burundi kuja kwenye masoko ya ujirani mwema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nimepata taarifa juu ya JWTZ kupiga Warundi waliokuja soko la Kabare, Kata ya Gwarama. Nashauri askari hawa watekeleze majukumu yao bila kuvunja sheria za nchi, wawe karibu na wananchi ili kujenga mahusiano mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ma-*DC* na *RC* kuvaa sare za jeshi; Wakuu wa Wilaya na Mikoa ambao ni wanajeshi wamekuwa wakivaa mavazi ya kijeshi wanapokuwa wanatekeleza majukumu yao ya Kiserikali ofisini. Jambo hili huwapa hofu sana wananchi ambao hawajazoea kuona Mkuu wa Wilaya/Mkoa akawa ndani ya vazi la kijeshi na hivyo kushindwa kupeleka shida zao kwa wakuu hao. Huu si utawala bora pale ambao mtawala anaogopwa na wale anaowaongoza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mchakato wa vijana kujiunga na JKT; zoezi la kusajili vijana wanaojiunga na mafunzo ya JKT linagubikwa na vitendo vya rushwa sana na hivyo zoezi zima kutokuwa huru kwa raia wote.

Mheshimiwa Mwenyeikiti, Kambi ya JKT Kamembwa bado mipaka yake haijakaa vizuri kwani raia wa Kazilamihunda wanadai eneo lao linavamiwa na jeshi na hivyo kuleta malalamiko mengi. Nashauri ufanyike upimaji rasmi wa kuweka mipaka ukishirikisha viongozi wa Kijiji cha Kazilamihunda na uongozi wa Jeshi (Kambi ya Kanembwa).

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa SUMA JKT ambapo ni jeshi la uzalishaji mali lielekeze miradi yake kufanyika/

kupatikana kila kambi ili JKT zote nchini ziweze kutekeleza majukumu ya mradi huo bila kutegemea toka Dar es Salaam.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Jeshi letu kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba hii naomba nichangie kwa kumuomba Mheshimiwa Waziri maana anajua na kama amesahau nimkumbushe, ni ukweli usiofichika Wilaya ya Kilindi katika Mkoa wa Tanga ni eneo ambalo linanyemelewa na watu wabaya wenye kuhatarisha usalama wa nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo wananchi takribani 50 au pungufu wamekamatwa kwa kujihusisha na vikundi vya ugaidi na kwa kuzingatia jiografia ya Wilaya ile yenye misitu, milima mingi, hivyo kuwa ni sehemu ya kujificha. Nimuombe Mheshimiwa Waziri kwa kushirikiana na viongozi wetu wa Jeshi la Ulinzi kama taratibu zitaruhusu basi tupatiwe Kituo cha Jeshi ambacho kitasaidia kulinda amani ya eneo hili pamoja na Taifa kwa ujumla, tusisubiri mpaka hali mbaya ikatokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeyasema haya nikifahamu kabisa katika Mkoa wa Tanga tuna Kambi ya JKT iliyopo Wilaya ya Handeni lakini pana umbali baina ya Wilaya hizi mbili. Mimi naamini kabisa kuna gharama ya kuanzisha vituo hivi lakini usalama wa eneo hili ndiyo wa muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. OMARY T. MGUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia hoja hii muhimu ya ulinzi wa nchi yetu na mipaka yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kumshukuru Rais, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli na Serikali yake hasa Waziri wa Ulinzi na wataalam

wake kufika katika Jimbo langu la Morogoro Kusini Mashariki katika Wilaya ya Morogoro Vijijini kufuatilia uwanja wa ndege wa Jeshi letu pale Kizuka Ngerengere. Tunasema ahsante sana.

Mheshmiwa Mwenyekiti, pia namshukuru Rais, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufulu kwa maamuzi yake ya kuagiza kutujengea barabara ya lami kutoka Ubena – Zomozi – Kizuka mpaka Ngerengere kupitia uwanja wa Kizuka.

Mheshiwa Mwenyekiti, baada ya shukrani hizo za watu wa Morogoro Kusini Mashariki hususani wananchi wa Tarafa ya Ngerengere na Tarafa ya Mvuha, naomba sasa nitoe ombi langu rasmi kwa Serikali hasa kwa Rais, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa tuna Kambi mbili za Jeshi pale Ngerengere yaani ya Kizuka na Sangasanga na kwa kuwa barabara itakayowekwa lami ni ya Ubena – Zomozi – Kizuka - Ngerengere na kwa kuwa umbali kutoka Kizuka - Ngerengere - Sangasanga siyo mbali na Kambi ya Sangasanga wanatumia barabara ya Mdaula – Sangasanga yenye urefu wa kilometa 10, kwa hiyo basi, naomba barabara hii nayo iwekwe lami kwani watoto hawa wa Sangasanga na Kizuka ni baba na mama mmoja ili wale Sangasanga wasione wametengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali yangu kulipa uzito suala hili na hasa kwa umuhimu wa jeshi letu na hasa kikosi hiki cha Sangasanga kutokana na uzito wa majukumu yake. Naomba barabara ya Mdaula – Sangasanga - Ngerengere kuwekwa lami ili kuunganika na ile ya Ubena - Kizuka - Ngerengere na kurahisisha usafiri kwa jeshi letu na wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia kuhusu hali ya usalama nchini. Kwa sasa hivi unaweza kusema kuna utulivu tu; kwa sababu tumeshuhudia siku za hivi karibuni pamekuwepo na matukio mengi sana ya watu kuuawa bila sababu, kwa mfano askari waliouawa huko Kisarawe kwa kupigwa risasa na watu wasiojulikana, matukio kama haya yametokea Pangani na Mwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali imeshafanya uchunguzi wahusika ni akina nani? Watu hawa wanaweza kuanza taratibu uhalifu huu kwa kuanzia pembezoni mpaka wakafika mjini, tutakuwa tumechelewa, je, Serikali inawaeleza nini Watanzania kuhusu matukio haya yanayotishia usalama wa Watanzania?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Jeshi hili linajishughulisha na kazi za maendeleo kupitia vikosi vyake kama ujenzi wa barabara, mpaka gari wamewahi kuunda, na kwa kupitia Jeshi hili tunaweza kuokoa fedha nyingi sana hata kuwapa *tender* za samani za ofisi za Serikali kama walivyotengeneza madawati, nawapongeza sana. Hata hivyo changamoto kubwa ni utolewaji wa fedha za maendeleo ndiyo unawakwamisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano waliomba shilingi 248,000,000,000/= kwa ajili ya maendeleo lakini wamepata shilingi 35,000,000,000/=, sawa na asilimia 14.5 ya bajeti waliyoomba. Je, kwa ufinyu huu unaotolewa wataweza kutimiza majukumu yao? Hii ni kuwarudisha nyuma, badala ya kuendelea wamebakiwa na kulipa madeni. Tukumbuke Jeshi hili kwa sasa ndilo linalotusaidia kuwajenga vijana wetu kimaadili kwa kwenda jeshini, wale wanaomaliza kidato cha sita. Je mpaka sasa hivi Serikali imeweza kuchukua vijana wangapi kwenda jeshini?

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni Wizara muhimu kwa uhai na mustakbali wa nchi yoyote, bado naafiki Jeshi halisi la JKT kimuundo. Ningependa Jeshi letu liende katika usawa kivifaa, lakini imeonekana Jeshi kwa

sasa halina *powerful public branding* ili kusimama kama taasisi yenye chapa ya Kitaifa. Wananchi hupata *public relations* ya Jeshi *only* wakati wa sherehe tu, na si vinginevyo na hivyo Jeshi hubakia katika *obscurity*. Bila shaka mazoezi ya kijeshi ni moja ya njia hizo kama ile *amphibious* iliyofanywa Bagamoyo. Ningependa Jeshi liji-*brand* pia kwenye kufanya kazi za dhamana mara zinapotokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa kuna dharura za mvua/upepo lakini Jeshi halijitokezi kikamilifu. Kazi hizo hufanywa kwenye matukio ya *big magnitude* tu. JKT inapaswa ipitie upya jukumu lile la kujenga uzalendo ambalo linaonekana limeshindwa hata katika hili, inafaa JKT ijitathmini upya.

**MHE. BALOZI DKT. DIODORUS B. KAMALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Sehemu kubwa ya mpaka kati ya Tanzania na Uganda iko Wilaya ya Misenyi – Kagera. Kama unavyofahamu kuna mambo mengi yanayoendelea katika mpaka huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali iwe karibu zaidi na ifuatilie kila siku yanayoendelea kwenye mpaka huo kwa nia ya kuimarisha ulinzi, ujirani mwema na kuimarisha utangamano. Aidha, suala la ng'ombe wanaoletwa kutoka nchi jirani (Uganda) na kuja kula majani Tanzania inabidi liangaliwe kwa umakini na lidhibitiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo uwe kwamba ardhi ya Tanzania itumiwe na Watanzania tu na kwamba wanaoleta mifugo kutoka nchi jirani wadhibitiwe na watumie ardhi ya nchi zao. Jambo hili la kudhibiti mifugo kutoka nchi jirani litawezekana tu kama wale tunaowapa majukumu ya kulinda mipaka wakizingatia miongozo wanayopewa na kuzingatia maadili ya Tanzania. Aidha, usalama wa Watanzania wanaoishi maeneo ya mipakani na mali zao upewe kipaumbele pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatambua umuhimu wa Wizara hii na kazi kubwa sana na nzuri inayofanyika. Aidha, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa namna anavyoongoza Wizara hii kwa hekima na utulivu mkubwa . Pamoja na pongezi hizi naomba nimpongeze pia Jenerali Venance Salvatory Mabeyo kwa heshima kubwa aliyopewa na Mheshimiwa Rais, kwa kumteua kuwa Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, hongera sana. Kwa imani kubwa aliyonayo Rais wetu kwake ndivyo na sisi Watanzania tuna imani sana na yeye. Tunaamini ataendelea kushirikiana na viongozi wote walio chini yake na walio juu yake ili kuendelea kuwa na utulivu na amani tuliyo nayo nchini pamoja na usalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizi pia niwapongeze wanajeshi wote kwa kazi nzuri ya kulinda mipaka ya nchi yetu, hakika tunawapongeza kwani tunatambua kazi kubwa waliyonayo. Wakati wengine tunaendelea na shughuli zetu wao wakiwa katika shughuli nzito ya kutulinda wakati wengine tukiwa tumelala, wao wakiwa macho kutulinda. Hakika tunawashukuru sana. Tuna imani na Jeshi letu, Mungu awabariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizi naomba nitoe maoni yangu kwa ufupi kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa hapa Tanzania vijana walioko sekondari na hasa wanaohitimu kidato cha nne, mitihani yao huwa inafanyika mwishoni mwa mwezi wa kumi kila mwaka. Hivyo watoto hawa wanaotajarajia kuendelea na masomo ya kidato cha tano husubiri kwa takribani miezi minane na zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo hali hiyo huwa ni kipindi cha mpito mgumu sana kwa wazazi na hata watoto pia kwani mazingira yanaweza kumuathiri mtoto na kujikuta anabadili nia yake ya kuendelea na masomo yake ya kidato cha tano ama wengine kuangukia kwenye tabia za ama kupata mimba au dawa za kulevya au ulevi na tabia nyingine zitakazokwamisha ndoto yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo kutokana na hali hiyo, naomba nishauri kuwa watoto hawa wanaomaliza kidato cha nne, mara baada ya matokeo yao ya mitihani Wizara iandae namna ya kuwachukua watoto hawa kujiunga na JKT kwa miezi kati ya sita na mitatu ili wasipoteze muda bure na pia kutunza uadilifu na nia yao njema ya kuendelea na shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Jeshi la Kujenga Taifa ya mwaka 1964 (na marekebisho yake) kifungu cha 5(2) kinatoa nafasi kwa kijana mwenye umri wa miaka 16 kujiunga na Jeshi hilo; hivyo haitakuwa tatizo kuwachukua wanafunzi hawa. Kwa sheria hiyo Wizara iongee/ishirikiane na Wizara ya Elimu ili kubadili mfumo wa kuwapeleka JKT vijana wanaomaliza kidato cha sita badala yake tunaanza na wanaosubiri kwenda kidato cha tano kwani hawa wana muda wa kutosha sana kuliko wa kidato cha sita wanaosubiri kwenda vyuo vikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu, vijana watakaofaulu kuanzia *division one* hadi *division three* ndio waweze kupata nafasi ya kujiunga na JKT. Pia itaweza kurahisisha kuwapata wanaotaka kujiunga na Majeshi yetu kama Polisi, Magereza, Uhamiaji, Jeshi la Wananchi na kadhalika kuliko utaratibu wa sasa unaotumika kuwasaka mitaani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho najua jambo hili linaweza kuonekana ni gumu sana, lakini ninaona manufaa yake ni makubwa zaidi, kwani tunaokoa Taifa letu na nguvu kazi pamoja na wasomi na tunapata waadilifu zaidi kwani watoto hawasahau.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa naunga mkono hoja asilimia mia moja.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Tabora una Kambi ya muda mrefu ambayo inaitwa *Milambo Barracks.* Kumekuwa na changamoto za uchakavu wa miundombinu ya barabara zinazozunguka kambi hiyo ya muda mrefu. Niombe Serikali iangalie mambo yafuatayo:-

Kwanza, ukarabati wa barabara, pili, ukarabati wa nyumba zao na tatu, ukarabati wa jengo la geti lililoko kabla ya kuingia ndani ya kambi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha niiombe Serikali kupeleka vifaa vya kisasa kwa ajili ya Hospitali ya Jeshi, ipeleke Madaktari Bingwa hususani wa magonjwa ya wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuomba msaada huo kunatokana na kutokuwa na Hospitali ya Manispaa ya Wilaya na hivyo kusababisha watu wengi kwenda Jeshini kupata huduma hiyo. Miundombinu ya maji ikarabatiwe kwani ni michakavu sana.

Vilevile Serikali ilipe madeni ya maji/*TANESCO* ili kusitokee ukataji wa huduma hizo kwenye majeshi kwani kukatiwa huduma hizo ni aibu kubwa. Fedha za matumizi hayo zipelekwe kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Serikali kupeleka fedha zilizoombwa bila kupunguza, pia kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hotuba hii.

**MHE. RISALA S. KABONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi ya kuchangia katika Wizara hii muhimu kwa nchi yetu. Kama ilivyo katika dira ya Taifa ya kulinda na kudumisha amani na usalama wa Taifa letu; pamoja kuendelea kulinda Jamhuri ya Muungano wa Tanzania dhidi ya maadui wa ndani na nje ya nchi yetu; usalama wa mipaka ya nchi, mgogoro wa mpaka wa Ziwa Nyasa kati ya nchi ya Tanzania na Malawi umekuwa wa muda mrefu hivyo kuendelea kuathiri ukuaji wa uchumi kwa nchi yetu hasa kwa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgogoro huo unaendelea kuathiri shughuli za uwekezaji katika eneo la Ziwa Nyasa na hivyo kufanya mdororo wa kiuchumi kwa wananchi na kupoteza mapato katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha aniambie mgogoro huu umefikia wapi ili kuweka mahusiano mazuri kati ya nchi ya Tanzania na Malawi na pia kuinua uchumi wa nchi yetu kupitia fursa zilizopo katika Ziwa Nyasa na mikoa ya Nyanda za Juu Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ajira kwa vijana waliopata mafunzo ya JKT; kumekuwa na changamoto kubwa ya ajira nchini na hii ni pamoja na vijana wanaomaliza mafunzo JKT na kupelekea vijana hawa kujiingiza katika vitendo vya uvunjaji wa amani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka ya nyuma taasisi za Kiserikali, kwa mfano *TANAPA* ilikuwa ikichukua vijana wengi waliomaliza JKT na kuwapatia ajira hali ambayo kwa sasa imepungua na kufanya nidhamu kupungua sana kwa taasisi zinazojihusisha na masuala ya ulinzi na usalama wa maliasili zetu.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kuchangia kuhusu kuyapa uwezo wa kifedha mashirika ya Nyumbu, Mzinga na SUMA JKT. Nikiwa mjumbe wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama nilitembelea Nyumbu na wajumbe wenzangu na kujionea kazi nzuri inayofanywa na shirika hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo Shirika lingeweza kufanya kazi kwa ufanisi zaidi kama lingekuwa huru hasa kwa mujibu wa sheria. Ilivyo sasa shirika hili kwa mujibu wa sheria liko chini ya Msajili wa Hazina hali hii inasababisha si tu mgongano wa kimaagizo, lakini pia utekelezaji wa mipango na maono *(vision)* ya shirika unachelewa kwa sababu ya mlolongo wa kiutawala, kwa mfano kuna nchi zilionesha nia ya kushirikiana na Shirika la Nyumbu tangu mwaka 2007,

hata hivyo uamuzi haukutolewa kwa wakati kutokana na sababu za kisheria na kiutawala na hivyo kupoteza fursa hiyo muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo nashauri Serikali ione uwezekana wa kuleta mabadiliko ya sheria ili Shirika la Nyumbu liwe chini ya Wizara/Jeshi kwa asilimia moja. Ninaamini uchambuzi wa kina ulifanyika, itathibitika kuwa mabadiliko ya sheria yataleta tija kwa Shirika na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sikufanikiwa kutembelea Mzinga kama ilivyokuwa kwa wenzangu, lakini uhalisia ni kuwa kuna fursa za wazi za kiuchumi na kimapato ikiwa Mzinga itawezeshwa, ninaamini kuna soko kubwa nje ya nchi kutokana na bidhaa zitakazozalishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu SUMA JKT, binafsi nimetembelea kila mwaka maonesho na huwa sikosi kutembelea mabanda ya SUMA JKT. Pia nimefanya ziara binafsi ya mafunzo katika Kambi ya Ruvu nikiwa na baadhi ya vijana kutoka Jimboni. Hakika iwe ni katika kilimo,ufugaji, ufundi na kadhalika, SUMA JKT inafanya kazi nzuri mno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ulinzi tumeshauri mara kadhaa kuwa maeneo yote ya Serikali na taasisi za umma ulinzi ufanywe na SUMA JKT, lakini pia Serikali ihakikishe wote wanaodaiwa wanalipa kwa wakati, ikibidi fedha zao za *OC* zikatwe zikalipe deni. SUMA JKT ipewe wigo mpana katika kushiriki suala la kuelekea uchumi wa viwanda hasa viwanda vidogo vidogo. Hili litawezekana tu ikiwa itawezeshwa kifedha kwa namna *(mechanism)* ambayo Serikali itaona inafaa; kwa mfano kuidhamini kwa mikopo ya riba nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mafunzo ya vijana - JKT; katika ukurasa wa tano wa kitabu cha Taarifa ya Kamati imeeleza kuwa ikiwa fedha kiasi cha shilingi bilioni nane zitatolewa JKT itaweza kukarabati makambi na hivyo kuongeza vijana wa kujiunga na JKT. Mpaka tunajadili bajeti

hii ni kiasi kidogo cha shilingi bilioni moja tu kimetolewa. Suala la mafunzo ya JKT kwa vijana wetu ni muhimu sana kwa sababu linaongeza uzalendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo wengi wao wanaingia katika ajira na kujiajiri. Ushauri wangu, katika wakati huu ambapo matumizi ya mitandao yamekuwa yakichangia kumomonyoa maadili ya vijana, mafunzo haya ni muhimu katika kujenga Taifa la kesho linalojitambua. Ninaamini kila kijana anayepitia JKT anajenga ushawishi *(influence)* kwa vijana wengine na wasiopungua 100 katika kijiji au mtaa anaoishi na kwa ushawishi huo wapo vijana waliohamasisha vijana wenzao kujiunga katika vikundi vya kuzalisha mali. Naomba kuwasilisha.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Mkuu wa Majeshi Jenerali Mabeyo na makamanda wote kwa kazi nzuri ya ulinzi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Pamoja na kuunga mkono hoja hii naomba kuchangia maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kurudisha kambi ya JKT ya Mpwapwa. Hata hivyo kambi hiyo ina mapungufu yafuatayo:-

Kwanza ni kuhusu upungufu wa majengo, hivyo nashauri Serikali iwajengee majengo ya kutosha kwa ajili ya makazi yao na ofisi za kufanyia kazi. Pili, vitendea kazi kama vile magari, matrekta kwa ajili ya kilimo kwa kuwa eneo hilo ni zuri kwa kilimo na chakula kinachopatikana watumie wenyewe ili kupunguza gharama ya Serikali kupeleka chakula kambini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, JKT Mpwapwa ianze kuchukua vijana wa kujitolea wa *form four* na *form six* kama makambi mengine ya JKT. Katika JKT Makutupora majengo yafanyiwe ukarabati, vyombo vya usafiri viongozwe kama

vile magari na kadhalika. Posho za askari Wanajeshi wa JKT na JWTZ ziongezwe. Majeshi yote yajengewe makazi badala ya kupanga uraiani, kambi zijengwe za kutosha ili wanajeshi wote wasipange mitaani. Usafiri katika majeshi yote hautoshi hivyo nashauri magari yaongezwe katika kambi zote ikiwemo Kambi ya Ihumwa, Makutupora na Mpwapwa. Posho ya chakula ya wanajeshi wote iongezwe haitoshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia huduma ya maji iboreshwe na barabara zikarabatiwe katika Kambi ya JKT Mpwapwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na matukio kadhaa hapa nchini ya wananchi kuokota mabomu ambayo yalikuwa ardhini tangu wakati wa Vita ya Majimaji na Vita vya Dunia. Mifano ni mingi, lakini kwa Mkoa wa Lindi maeneo ya Mahiwa, Kiwalala na Ndanda yamekuwa yakitokea mara kwa mara .

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Jeshi lifanye utafiti wa kutosha hususan katika maeneo yote ambayo Vita vya Majimaji vilipigana pamoja, Vita vya Kwanza na vya Pili vya Dunia. Wanajeshi wa Ujeremani katika maeneo mengi walizika silaha zao ardhini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafadhali suala hili mlipe uzito unaostahili mfanye utafiti wa kutosha ili kuepusha madhara zaidi. Mifano mizuri ni maeneo ambayo Wajerumani walikuwa na mashamba ya mkonge na baadhi ya sehemu ya ngome zao. Ahsante sana.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema Serikali ikatoa fedha kwa wakati za maendeleo kwa Jeshi letu ili liweze kutekeleza majukumu yake ya kila siku, kwani kwa kuchelewesha, tunarudisha nyuma maendeleo ya Jeshi letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeshangaa kuona maduka yenye gharama nafuu yaliyokuwa yanasaidia familia hizi yamefungwa. Naomba Serikali itoe majibu, ni kwa nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wetu walioajiriwa kwenye Shirika la SUMA JKT hasa kwenye ulinzi wa makampuni, wanalipwa kiasi kidogo cha mshahara kwani hii linaweza kuleta ushawishi mbaya wa vijana wetu na kuweza kuleta madhara kwa makampuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiwanda cha Mzinga ni muhimu kwa Taifa na Jeshi lenyewe, ila hakipati fungu la kutosha kutekeleza majukumu yake na kwa kuwa Serikali hii imetangaza mwaka wa viwanda, inabidi iwekeze sana kwenye kiwanda hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kwamba Serikali ifuatilie hati miliki za makambi yote ya Jeshi ili kuondoa sintofahamu na wananchi wanaovamia makambi hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka ya 2000 Jeshi lilianzisha shule za sekondari nyingi na zilisaidia sana kutoa elimu bora kwa vijana wengi na hata michezo ilifanyika na kutoa wachezaji bora. Hivyo, Serikali iendeleze uwekezaji huu kwani ni muhimu kwa Taifa hili.

**MHE. VEDASTUS M. MANYINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali yangu kwa kazi nzuri sana ya maendeleo ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo tatizo kubwa Musoma Mjini kwani wananchi waliombwa kupisha eneo la Jeshi katika eneo la Makoko na wameendelea kupata ahadi ya kulipwa fidia. Sasa ni zaidi ya miaka kumi hadi leo bado hawajapata chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri anakumbuka wale wananchi walituma mwakilishi wao. Na mimi nilimleta kwake na tukakaa pamoja akaahidi kwamba

katika bajeti hii hao wananchi wa Musoma watalipwa fidia. Naomba kauli yake hapa Bungeni, kwani wamehangaika kwa muda mrefu sana ili suala hilo tulimalize.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naunga mkono hoja ya bajeti ya Wizara hii.

**MHE. CAPT. ABBAS ALI MWINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia katika Wizara hii muhimu kwa Taifa letu ambayo imeendelea kudumisha amani na utulivu kwa Taifa letu pamoja na kulinda Muungano dhidi ya maadui wa ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na ufinyu wa bajeti kumekuwa na upungufu mkubwa wa makazi ya wanajeshi wetu na wale waliobahatika kupata makazi, hayapo katika hali ya kuridhisha. Upungufu huo wa makazi unapelekea baadhi ya wanajeshi kuishi nje ya Kambi za Jeshi, jambo ambalo ni hatari kwa askari wetu. Suala la askari kuchanganyika na raia kunawashushia hadhi yao kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na changamoto kubwa ya ajira kwa vijana wanaomaliza JKT Bara na Visiwani. Nashauri Wizara ya Ulinzi zishirikiane na Wizara nyingine kutoa vipaumbele vya ajira kwa vijana wanaomaliza JKT. Hii itasaidia kwa kiwango kikubwa kurudisha nidhamu ya utumishi wa umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri, atakapokuja kuhitimisha (kufanya majumuisho) ananiambie nafasi za ajira zinazopelekwa kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ziko kwa uwiano gani ukilinganisha na Tanzania Bara?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na uwiano mdogo kati ya wanawake na wanaume kwa maafisa wa ngazi za juu wa uongozi wa JWTZ. Naomba kujua kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, anapokuja kuhitimisha, ni kwa nini hali hii inajitokeza?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, hali ya ulinzi na usalama wa mipaka ya nchi yetu ni shwari kwa mujibu wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri. Napenda kujua mgogoro wa mpaka wa Malawi na Tanzania kupitia Ziwa Nyasa ambao umechukua muda mrefu, ambao unaweza kuleta athari za uwekezaji katika nchi yetu, na hivyo kupelekea hasa Ukanda wa Nyasa kudorora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. Naunga mkono hoja.

**MHE. ASHA MSHIMBA JECHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Naipongeza Wizara kupitia wanajeshi wetu kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuilinda nchi yetu na kubaki katika hali ya utulivu na amani. Hongereni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu vijana wanaojiunga na JKT mara wamalizapo mafunzo ya kujitolea (kujitegemea), baadhi yao huajiriwa na vikosi vyetu vya ulinzi, lakini baadhi hurudi katika maeneo yetu na kuzurura bila kazi maalum ya kufanya. Je, Serikali haioni sasa wakati umefika kwa vijana hawa wanaopitia JKT kuwa na mfuko maalum wa kuwasaidia vijana hawa mara tu wamalizapo mafunzo, kupewa na kuanzisha miradi na kujiajiri wenyewe?

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile wakati wakiwa JKT wapewe mafunzo ya ujasiriamali ili wakitoka wawe tayari kujiajiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii.

**MHE. DESDRIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kuunga mkono hoja iliyoko mbele ya Bunge lako Tukufu. Nampongeza Mheshimiwa Waziri, mchapakazi, mtulivu na mwenye tabia ya pekee kimaadili. Hongera kiongozi, unakubalika ukiitwa mtoto wa Rais Mstaafu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni Serikali ilifuta Shule ya Milundikwa Sekondari kupisha makazi ya Kambi ya

Jeshi JKT. Pamoja na kukubaliana kwa shingo upande, uamuzi huo umetuathiri wananchi wa Kata ya Nkandasi na Jimbo la Nkasi Kusini kutokana na miundombinu mbalimbali ya elimu kutwaliwa pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tuna sekondari changa sana ile ilikuwa inajitosheleza kwa miundombinu mingi ikiwa ni pamoja na maabara, mabweni ya wasichana na wavulana, madarasa na nyumba za walimu pamoja na kisima cha maji.

Pamoja na msaada wa nguvu kazi kwa wanajeshi, tunaomba Wizara hii inisaidie kujenga mabweni na maabara kwa kadri wanavyoweza ili kutuwezesha kukamilisha miundombinu pungufu. Pia Serikali izingatie familia za askari wetu, nao pia watasoma katika shule hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi la pili ni kwamba Jeshi lisitwae eneo lote, yale maeneo ambayo wananchi wanalima wasiwafukuze, wawaachie waendelee kulima kwa yale ambayo yako mbali na Kambi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi la tatu, naomba Wizara isaidie kujenga mnara wa mawasiliano katika Kata moja ya mpakani mwa Congo DRC; Kata ya Kala ili kuimarisha ulinzi wa mpakani na vilevile kuboresha mawasiliano ya simu za mkononi. Hii ni Kata pekee iliyobaki bila mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kazi nzuri sana ya wanajeshi, zipo dosari ndogo ndogo mfano, Wilayani Nkasi imewahi kutokea kama mara mbili wanajeshi kuwapiga wananchi na mara nyingi ni ugomvi wa mapenzi na mara zote raia huumizwa na wakati mwingine kuuawa. Siyo jambo zuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hapa Dodoma imewahi kutokea mahali pengine nchini. Naomba wapewe

somo la maadili, kwani siku zote raia akimwona mwanajeshi huona kama mkombozi wake, huu ndiyo utamaduni wa Kitanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza wanajeshi wote.

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Baada ya kuunga mkono hotuba hiyo, napenda kulipongeza Jeshi letu kwa kazi kubwa linazofanya katika kulinda usalama wa mipaka yetu na kujishughulisha na shughuli mbalimbali za ujenzi wa Taifa letu na kushiriki katika kukabiliana na majanga mbalimbali yanayolikumba Taifa letu kwa nyakati mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kwa Serikali ni kuwa Serikali iongeze bajeti kwa Wizara hii ili kuziwezesha taasisi ndani ya Wizara hii za Nyumbu na Mzinga ili zijikite kikamilifu katika shughuli za utafiti wa kisayansi na ugunduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, historia inaonesha dhahiri kuwa taasisi za ulinzi na usalama hasa Majeshi ya Ulinzi katika nchi mbalimbali duniani zimeshiriki kikamifu katika kuleta mapinduzi ya viwanda na zana za kivita. Mfano, mifumo ya *computer* ilibuniwa na Jeshi la Marekani kabla ya kuingizwa katika shughuli za kiraia. Ugunduzi na ubunifu wa vifaa vya kivita kama vile vifaru, ndege za kivita, meli za kivita, makombora ya masafa mafupi, ya kati na marefu yote ni matokeo ya shughuli za kijeshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine napenda kuishauri kulitumia vema Jeshi la Wananchi katika harakati za uvuvi wa bahari kuu *(deep sea fishing)* ili meli za kivita ambazo zinakaa muda mrefu bila kufanya kazi, zitumike katika kukuza uchumi wa Taifa letu wakati huu amani ikitamalaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naishauri Serikali kulitumia vizuri Jeshi la Kujenga Taifa kwa kulipatia zana za

kisasa za uzalishaji mali, yakiwemo matrekta ili kuzalisha mazao ya chakula na biashara kama vile kahawa, mahindi na mpunga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nashauri JKT iwezeshwe kuwa chimbuko la ufugaji bora wa ng'ombe wa nyama na maziwa. Ni imani yangu kuwa Serikali ikiliwezesha Jeshi letu wakati huu, upo uwezekano mkubwa wa kuwa mchangiaji mkubwa katika shughuli za ukuzaji uchumi kama majeshi ya nchi nyingine yanavyofanya, mfano, Ethiopia hapa Barani Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. LUCIA M. MLOWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali iwalipe maslahi wanajeshi yanayoendana na gharama za maisha, kwani gharama za maisha zimepanda. Naiomba Serikali imalize migogoro ya ardhi kati ya Kambi za Jeshi na wananchi ili wananchi waweze kuishi kwa amani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali ishughulikie mafao ya wanajeshi waliostaafu. Mfano, kuna wanajeshi katika Mkoa wa Njombe ambao wamestaafu, lakini hawajalipwa mafao yao. Naomba kuwasilisha.

**MHE. HALIMA ALI MOHAMMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukurasa 33 aya 46 Mheshimiwa Waziri ameelezea kuhusiana na SUMA JKT kupitia kampuni yake ya *SUMA JKT Guard Ltd.* kuendesha shughuli za ulinzi katika Ofisi za Serikali, Mashirika ya Umma na sekta binafsi zikiwemo Benki na Migodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, walinzi hawa maisha yao ni magumu, posho ni ndogo sana, mishahara hawana na Serikali iliwaahidi itawapatia mishahara kamili kama askari wengine. Nitoe mfano, walinzi wanaoimarisha ulinzi Ofisi ya *TRA* Bandarini, kazi wanayofanya ni nzuri tena katika ofisi nyeti, lakini Serikali haijali kitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali iangalie upya maslahi ya walinzi hawa, iwaboreshee mishahara, iwapatie vitendea kazi pamoja na stahiki nyingine, kwani sehemu ya bandari ni muhimu katika kuingiza mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee kuhusu malipo ya wastaafu wa JWTZ. Hawa ni watumishi ambao walifanya kazi kubwa ya kulinda nchi yetu, kuweka heshima, lakini pia kuimarisha ujirani mwema. Siyo vyema kuwa sasa hivi wao ni ombaomba. Nashauri wapewe stahiki zao kwa kuzingatia thamani ya shilingi ya Kitanzania kwa sasa au mnawasubiri wafe wote? Hilo siyo jambo zuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wako wananchi eneo la Kengeja, Jimbo la Mtambile, Wilaya ya Kusini Pemba ambao ardhi yao imechukuliwa na JWTZ. Hadi hii leo ni kimya, hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa na ni maeneo ambayo wanayategemea kwa kilimo cha chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali uthamini ufanyike kwa haraka. Mheshimiwa Waziri atoe kauli ni lini wananchi hawa watapatiwa haki zao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi ya majeshi ya JWTZ wakati wa uchaguzi kwa mfano, uchaguzi mdogo wa Jimbo la Dimani - Zanzibar ni uthibitisho kuwa na matumizi mabaya ya Jeshi letu, matumizi mabaya ya fedha za walipa kodi, lakini siyo hivyo tu, ni uminyaji wa demokrasia, kwani walikuwa wakipita njiani na silaha. Hii inawatisha wananchi na matokeo yake wapo wananchi wengi tu ambao waliogopa na hawakujitokeza kutimiza haki yao ya kupiga kura. Hii ni aibu kwa nchi inayojigamba kama ina demokrasia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ushauri, Serikali isitumie madaraka vibaya, badala yake wanajeshi wa JWTZ waachiwe wafanye majukumu yao kwa mujibu wa sheria za nchi yetu kwa manufaa ya ustawi wa nchi yetu na wanasiasa wafanye siasa. Kutumia fedha za walipakodi kwa

jambo ambalo halina msingi, ni kuwanyima wananchi kutumia haki yao ya maamuzi na kuwanyima nafasi ya kupata maendeleo. Ahsante sana.

**MHE. MARY D. MURO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali kuimarisha Jeshi la Kujenga Taifa ili liweze kuwa na tija kama miaka ya zamani lilipojenga uchumi badala ya kuwa *consumer* wa Pato la Taifa. Miaka hiyo Mlale ilitoa mahindi mengi, Mafinga pia, Ruvu ilikuwa wazalisha mpunga na ufugaji ambao ulileta faida kwa jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali kuweka uwazi katika ajira zinazotolewa ili kuondoa minong'ono iliyopo ya kuwa rushwa inatolewa ili vijana wetu kupata ajira bila usumbufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, nashauri Kiwanda cha Nyumbu kifufuliwe ili watendaji walioajiriwa kwa ajili ya kiwanda wasiligharimu Taifa bila kazi yoyote. Serikali iweze kuona kiwanda hiki kilikuwa na uwezo wa kuongeza ajira na Pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali kwamba Vituo vya Jeshi viwekwe mbali na mazingira ya wananchi ili kutoleta migongano na mazoea yaliyopitiliza kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nashauri Serikali iwapatie posho na vitendea kazi askari wetu ili kufanya kazi zao kwa urahisi zaidi.

Vilevile naishauri Serikali kulipa madeni kwa Jeshi linayodaiwa kwa kuwapa fedha zile zilizopitishwa na Bunge badala ya kusitishwa huduma muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali itoe ushawishi wa Watanzania kutumia bidhaa zao ili kuweza kuwaongezea pato.

**MHE. RASHID M. CHUACHUA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la Bima ya Afya kwa wanajeshi, kuna malalamiko ya wanajeshi kuhusu kutibiwa kwenye hospitali zao pekee bila ya kuwa na Bima ya Afya, ni lini Serikali itawapatia bima za afya wanajeshi na familia zao?

**MHE. RHODA E. KUNCHELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Kujenga Taifa kazi yake kuu ni kulinda usalama wa Taifa, wananchi na mipaka yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majukumu makubwa ya Wizara hii bajeti hii bado haitoshi ili tuendelee kuwa na amani na utulivu tulionao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu migogoro ya mipaka na Jeshi, Jeshi likiwa imara na wananchi wanakuwa salama katika Taifa. Ni lini Serikali kupitia Wizara hii itatatua mgogoro uliopo katika Kata ya Misunkumilo Manispaa ya Mpanda na Jeshi kuchukua eneo ambalo wananchi wamejenga? Ni lini Serikali itatatua mgogoro huu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi liliwakuta wananchi likaazima eneo hili, leo hii linadai eneo ni la Jeshi na wananchi wamekatazwa kujenga na kulima katika eneo hili.

Je, Serikali haioni kwamba Jeshi linataka kuwapora wananchi maeneo yao na mashamba, nani atawalipa fidia wananchi hawa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, kiusalama kuweka vifaa vya usalama vya kijeshi karibu na makazi ya watu yaliyopo katika Kata ya Mpanda Hoteli, Misunkumilo, Milala na Makanyagio; je, hamuoni huku ni kuhatarisha usalama kama ulivyotokea mlipuko wa mabomu Mbagala? Naomba majibu kuhusiana na suluhisho hili ili wananchi waondokane na unyanyasaji huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu wanajeshi kuboreshewa maslahi yao kama mshahara, pensheni na nyumba zao; kuchelewesha maslahi yao haya kunapelekea

baadhi yao kujihusisha na matukio ya ujambazi na uhalifu katika Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matukio ya uhalifu wa watu kuuawa, mauaji ya Kibiti, nini tamko la Serikali ili kuondoa na kumaliza uhalifu huu unaofanywa na baadhi ya wastaafu wanajeshi ambao siyo waaminifu. Ni aibu kuona nguo/vazi la Jeshi kutumika katika matukio ya aibu, Watanzania wana imani na Jeshi hili lakini kwa baadhi ya matukio ya kijinga yanayofanywa na baadhi ya watu yanalichafua Jeshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Paulo Makonda, alipoenda kuvamia *Clouds Radio* alikuwa na watu au wanajeshi wawili waliovaa vazi la Jeshi kwa hili lililotokea hamuoni kwamba imelichafua Jeshi hili, nini tamko la Wizara na Serikali ili kumwajibisha huyu Bashite katika tukio hili, hamuoni kwa Jeshi kukaa kimya linaonesha Jeshi linahusika kufanya haya matukio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ulinzi wa mipaka na wananchi katika maeneo yanayopakana na nchi jirani je, mkakati gani unatumika pamoja na kuwashirikisha wananchi elimu kwa raia namna ya kutoa taarifa kuhusu ulinzi na usalama wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Jeshi hili lijikite zaidi katika kulinda usalama wa Taifa na lisitumiwe na watu wenye nia mbaya kwa raia. Maonyesho ya makomando hadharani hamuoni kwamba inawapa mwanya watu waovu kujua ubora na udhaifu wa Jeshi letu. Mazoezi ya Jeshi hadharani yenye tija na sio ya kutisha wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho Jeshi la Kujenga Taifa lisitumike vibaya na utawala wa CCM kwa maslahi ya Chama Tawala, bali Jeshi hili liangalie maslahi mapana ya Taifa.

**MHE. SILAFU J. MAUFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya yote ninaunga mkono hoja kwa asilimia zote. Napenda kuwapongeza Waziri na Katibu Mkuu wake kwa kusimamia,

kuiongoza na ufuatiliaji wao wa karibu zaidi wa majukumu ya Wizara yao, pamoja na changamoto zote na ukosefu wa kupatiwa bajeti katika ukamilifu wake kama ilivyopitishwa na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikizungumza kwa uchungu kuhusu Mkoa wetu, hapo awali tulikuwa na makambi ya JKT Milundikwa na Luwa, Rukwa ambayo yalitusaidia kuwaweka vijana wetu ndani ya maadili ya uzalendo na ulinzi uliotukuka wa ushirikishwaji na wananchi wetu, sasa kama itakuwa Serikali (Hazina) haitoi fedha za kukidhi mahitaji kwa angalau asilimia 75 kwa umuhimu wa Wizara hii, kwani hawana masaa maalum ya utumishi wao, hivyo kuna umuhimu wa kupewa fedha za maendeleo kwa asilimia hiyo ili makambi haya yakarabatiwe na kuanza kutumika mapema, kwani vijana wanaongezeka mitaani/Vijijini baada ya kumaliza masomo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2016/2017 zimetolewa fedha za maendeleo shilingi 35,900,000,0000 ikiwa ni asilimia 14.5 ya bajeti iliyoidhinishwa mwaka 2017/2018. Bajeti imepungua kwa shilingi 29,000,000,000 kwa bajeti ya mwaka 2016/2018 iliyokuwa shilingi 248,000,000,000 na sasa kuwa 219,000,000,000 kwa mwaka 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni kwamba fedha za maendeleo ni vema zikatolewa kwa wakati na katika ukamilifu wake, kutokana na umuhimu wa:-

(i) Kukamilisha ukarabati wa makambi ndani ya mwaka 2017/2018, kuchelewa zaidi kutatuathiri.

(ii) Tuondokane na migogoro ya wananchi waliochukuliwa maeneo yao kwa matumizi ya Jeshi, walipwe fidia zao waweze kujiendeleza. Hizo bilioni 27 ni muhimu kwa sasa kabla ya Juni, 2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madhumuni ya kukamilisha makambi ni kuwajenga vijana wetu kiuzalendo, kiulinzi na naishauri Serikali inapohitaji kuajiri Polisi, Wanajeshi, Maafisa

Usalama wa Taifa, Uhamiaji, Jeshi la Zimamoto na Magereza usaili ufanyike kwa vijana waliopitia JKT.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa vijana wanaopitia JKT baadhi wanabaki mitaani/vijijini ni bora vijana hawa wakaunganishwa kwenye huduma za ulinzi za *SUMA Guard* badala ya kurudi kujiunga na jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. LOLESIA J. M. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kuchukua fursa hii kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa kuwasilisha hotuba vizuri juu ya maendeleo na utekelezaji kwa ujumla wa Wizara. Vilevile niwapongeze kwa dhati watumishi wote wa Wizara kwa kazi nzuri ya ulinzi wa Taifa letu. Hii imewezesha kuwepo kwa hali ya utulivu na amani ya nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuishukuru Wizara kwa mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa kwa vijana wetu kwani wanapata maarifa na ujuzi hasa katika stadi za kazi zinazowawezesha kujiajiri na kujitegemea. Hivyo, ninaomba na kuishauri Serikali kuongeza idadi ya vijana wa kujiunga na JKT kutoka 20,000 hadi 25,000 kwa mwaka 2017/2018, hii itasaidia vijana wengi zaidi kujishughulisha kutokana na ujuzi wanaoupata kutokana na mafunzo ya JKT.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo muhimu ninalopenda kuwasilisha ni juu ya wapiganaji vita vya Kagera. Wapo wanajeshi wengi nchini Tanzania wanadai mafao yao. Mwaka jana niliuliza juu ya suala hili na katika maelezo ya wanajeshi hawa ni kwamba Serikali Awamu ya Nne ya Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete waliahidiwa kulipwa mafao yao, mpaka sasa hakuna chochote. Nimeangalia kwenye bajeti iliyowasilishwa ya mwaka 2017/2018 sijaona kabisa kuzungumziwa suala hili. Ninaomba Mheshimiwa Waziri, nipate maelezo ya kina juu ya suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimelileta suala hili kutokana na wanajeshi walioko Jimboni kwangu Busanda wamekuwa wakifuatilia sana juu ya suala hili, ninaomba nipate maelezo ya kina na ufafanuzi juu ya suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo haya, naunga mkono hoja.

**MHE. ESTER M. MMASI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima na unyenyekevu mkubwa naomba niunge mkono hoja ya wasilisho la bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la kujenga Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja kwa moja niende kwenye hoja ya msingi juu ya masuala ya ulinzi na usalama wa raia na mali zao. Ni ukweli usiopingika kuwa bado tuna changamoto kubwa juu ya kukabiliana na majanga ya ujambazi kutokana na vifaa duni katika Jeshi la Kujenga Taifa na hata kwa askari wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye bajeti ya mwaka 2016/2017 hususani kwenye bajeti ya Jeshi la Askari tuliomba Serikali iidhinishe bajeti ya manunuzi ya magari mawili ya *bullet proof* ili kuweza kupambana na uhalifu nchini Tanzania, lakini cha kusikitisha hadi tunaelekea mwisho wa mwaka wa fedha 30 Juni hakuna hata gari moja lililonunuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata ninapoandika mchango wangu huu ni kweli kuwa Taifa limepoteza nguvu kazi ya Jeshi la Askari hadi sasa tuna jumla ya askari 13 -15 waliopoteza maisha kwenye uharamia wa Rufiji, lakini pia tuna takribani jumla ya wananchi 20 - 30 waliopoteza maisha kwenye sakata la ujambazi Rufiji siyo hivyo tu uharamia wa Benki Mbagala na *Dar es Salaam City Centre*, wapo wananchi wengi waliopoteza maisha pamoja na Jeshi la Wananchi na hata askari kwa ajili ya kukosa magari ya *bullet proof.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kikosi cha Jeshi la Wananchi nchini Kenya pamoja na Jeshi la Askari ni ukweli

kwa nchi ya Kenya ina hazina ya magari ya *bullet proof* zaidi ya mia mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mauaji yanayoendelea ni dhahiri kwamba kama Wizara kupitia Jeshi la Wananchi na JKT kama vile Ngome na JKT hatutajipanga vizuri ni ukweli usiopingika kwa changamoto hizi hazitafika kwenye ukomo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji Jeshi la Wananchi lipewe fedha ya kutosha ili waweze kununua vifaa vya kisasa katika kukabiliana na uhalifu nchini kwetu. Wizara ya Jeshi la Kujenga Taifa haijatengewa fedha katika kununua magari ya *bullet proof* na silaha muhimu za kijeshi katika kukabiliana na uhalifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika wasilisho la ripoti ya Kamati pia tumesikia kuwa Wizara ya Jeshi la Kujenga Taifa pia liko katika hatua za mwisho za ukamilishaji wa *National Defense Policy.* Pamoja na ukweli kuwa tumeona juhudi nzuri na utendaji kazi mzuri wa Mheshimiwa Waziri kwenye Wizara yake, lakini kwa kutokuwepo kwa sera hii muhimu ni ukweli usiopingika kuwa pengine kuna uzembe mkubwa katika kitengo cha sheria katika Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni maombi yangu kuwa Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anahitimisha hoja ya Wizara yake atuambie ni kwa nini hadi leo Sheria ya Ulinzi ya mwaka 1966 imepitwa na wakati. Je, nini tamko la Waziri mhusika kwenye changamoto hii? Naomba kuwasilisha.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujua kuna maeneo ya wananchi katika Wilaya ya Ilemela ambayo Jeshi liliyapima ili kuyachukua kwa miaka mingi bila kulipa fidia na kuwaondoa wananchi katika maeneo hayo, Mheshimiwa Waziri naomba kufahamu uthamini uliofanyika maeneo ya Nyagunguku - Ilemela, Nyanguku, Lukobe kwa miaka miwili sasa umefutwa au bado upo *valid?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama lengo la JWTZ lilikuwa kufanya uthamini na baadaye kuwaacha wananchi katika maeneo yao kwa muda mrefu bila kujua hatima yao, naomba kujua watalipwa lini au Jeshi limejiondoa kwenye nia ya kumiliki maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatana na timu za Orjoro JKT na Kanembwa JKT kushushwa daraja kwa tuhuma za rushwa ambazo zimeshindwa kuthibitishwa na chombo cha kisheria cha uchunguzi wa makosa hayo *(PCCB).* Je, ni hatua gani Wizara yako imechukua kupigania haki ya vijana wako na heshima ya vyombo hivyo nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na kudorora sana kwa michezo ya aina mbalimbali, mfano, riadha, sarakasi, ngumi, mitupo, *volleyball*, nimetaja kwa uchache tu kwa nini kuanzia sasa kipaumbele cha kijana kujiunga na JWTZ na JKT au vyombo vingine isiwe ni kipaji kimojawapo cha michezo ili kuufanya umma wa Watanzania kupenda michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili vijana hao wawe *competent* ni vizuri Wizara yako ikatafuta wabia (marafiki) kutoka nje ya nchi kusaidia kuongeza taaluma, mfano, China, Cuba, Urusi na Korea, ambapo vijana wetu waweze kupata ujuzi mpya au nyongeza ya ujuzi walionao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Wizara yako ina mpango mkakati upi wa kusaidia kuimarisha michezo nchini?

**MHE. YUSSUF HAJI KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa neema kubwa ya uhai na uzima. Ninakushukuru wewe kwa kunipatia nafasi na mimi nichangie ingawa kwa muhtasari. Nianze kwa kupongeza utamaduni mzuri wa vijana wetu wanaomaliza vyuo na wale wengine kujiunga na Jeshi la Kujenga Taifa, kwa mujibu wa sheria na wale wa kujitolea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili ni jema sana kwani vijana wetu hupata mafunzo mbalimbali yakiwemo

ya ulinzi na usalama na yale ya ujasiriamali, vijana wanaopatiwa mafunzo ya ujasiriamali katika shughuli za kilimo, ufugaji, fundi uashi, fundi uchongaji, na mengine mengi hufanikiwa vizuri wakiwa kambini, wakishaondoka kambini elimu yote waliyopata hupotea kwa sababu vijana hawawezeshwi wanabakia vijiweni tu hawajui la kufanya na elimu waliyopata inapotea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu vijana hawa wakusanywe vikundi mbalimbali, wasajiliwe kisheria, Serikali iwalee na kuwawezesha ili wajiajiri na kuendeleza elimu waliyopata kambini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa vijana wanapata mafunzo ya kijeshi na wana uwezo wa kutumia silaha mbalimbali, Serikali haiwezi kuwaajiri vijana wote, wengi wao hurudi nyumbani wakiwa hawajui la kufanya, vijana wanakuwa rahisi kujiunga na makundi ya uhalifu, hivyo ni hatari kwa Taifa na usalama kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu vijana hawa wawekwe katika orodha maalum sekta za ulinzi zinapohitaji kuajiri wafanyakazi, kwa mfano, Polisi, Magereza, Zimamoto, Usalama wa Taifa hata kampuni za ulinzi wa binafsi basi wapewe kipaumbele vijana wetu ambao wamepitia Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile wabakie kama Jeshi la Akiba hivyo wapangiwe utaratibu kila baada ya muda fulani wanakusanywa kwa kukumbushwa majukumu yao juu ya wajibu wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie muingiliano wa kambi za Jeshi na makazi ya raia. Hili ni tatizo ambalo linahitaji kuangaliwa kwa makini sana. Shughuli za kijeshi ni maalum kwa Jeshi mambo mengi ya hatari ambayo yanawahusu wenyewe, mfano maghala ya milipuko mbalimbali ambapo ikitokea bahati ambayo inasababisha maafa makubwa kwa

wote. Mfano, mkubwa na hai ni ule wa Gongo la Mboto na Mbagala taharuki kubwa kwa nchi na wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali ifanye juhudi za makusudi, kuepusha kambi zote za Jeshi zenye ghala za milipuko zitengwe na makazi ya raia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie ajira katika Jeshi na vyeti *fake.* Tatizo hili ni la Taifa zima na katika taasisi mbalimbali, lakini taasisi hii muhimu ina athari kubwa na ni hatari kuwaajiri askari na ukawapa mafunzo yote na siri zote za Jeshi wanazifahamu wamefanya kazi zaidi ya miaka 10 au 15 ndiyo unakuja kugundua vyeti vyao ni *fake* na kumfukuza kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii siyo vizuri kwa sababu hili ni kundi kubwa sana tunalolikufukuza na tunalifukuza wakiwa na taaluma. Naomba Serikali iangalie kwa umakini suala hili mwanzo wa kuajiri wabaini kasoro zote ambazo hazifai ikiwemo vyeti *fake.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho niombe usawa wa ajira kati ya pande mbili za Muungano kwa kuwa Muungano wetu ndiyo unaunda taasisi hii muhimu ya ulinzi naomba ajira zake zifanywe kwa uwazi mkubwa tena kwa uwiano mzuri. Hii itajenga heshima na uimara katika Jeshi letu na kupata ushirikiano kwa pande zote na kwa watu wote.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaanza sasa na majibu ya Serikali, tunaanza na Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsi, Wazee na Watoto dakika tano, Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki dakika tano, *AG* dakika kumi.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa fursa hii. Naomba nichangie kidogo Hoja hii ya Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitachangia kwenye maeneo mawili, eneo la kwanza linahusu hoja ambayo ipo katika kitabu cha Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani kwa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, ambapo kwenye ukurasa wa 17 na kuendelea anazungumzia kuhusu uteuzi wa wanajeshi, ama wanajeshi ambao bado ni wanajeshi au wanajeshi waliostaafu kwenye nafasi mbalimbali za kiuongozi kama wakuu wa mikoa na wakuu wa wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Msemaji huyu wa Kambi Rasmi ya Upinzani anazungumzia kwamba hii ni sawasawa na dhana ya *politicization of the Army.* Napenda kupingana naye kwa sababu *politicization of the Army* haipo katika zama hizi kwenye nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema haipo kwa sababu kinachofanyika kwa sasa kimsingi ni kwamba Mheshimiwa Rais anatumia mamlaka yake ambayo yamekuwa *provided for* kwenye Katiba yetu kuteua watu ambao anaona watafaa kwenye maeneo mbalimbali ya uongozi na kuwapa madaraka ya kumsaidia kazi ya kuongoza nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kuna maeneo yamekaa kimkakati *(strategic regions)* kama Kigoma ni mpakani, Kagera pamoja na maeneo ya Ruvuma. Maeneo ambayo yamekaa kimkakati kwa maana ya kiulinzi zaidi Mheshimiwa Rais anaona watu ambao wana *inclination* ya kijeshi aidha ni wanajeshi au ni wanajeshi wastaafu wanafaa kwenda kumsaidia kuongoza katika maeneo yale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais… *(Makofi)*

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** ...kwa kazi nzuri anayofanya...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara, hebu kaa kwanza. Jamani tusipoteze muda, hii bajeti inatakiwa iishe leo.

**T A A R I F A**

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa ndugu yangu, shemeji yangu, Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla kwamba sisi hatupingi wanajeshi kuteuliwa katika nafasi mbalimbali, tunachotaka ni kwamba wakiteuliwa wafuate utaratibu wa kawaida. Kama ameshakuwa mwanajeshi amekuwa mtumishi wa umma maadili wa kawaida yafuatwe, ndicho tunachosema sisi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla, endelea.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kitabu hakuna mahali ambapo wanaelezea mwanajeshi hata mmoja ambaye ameteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Mkuu wa Mkoa ambaye amekiuka taratibu anazozizungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi, tunachokiona ni kwamba Mheshimiwa Rais amewateua watu ambao anaona watafaa kumsaidia kutekeleza majukumu yake ya kuongoza nchi yetu na kulinda mipaka yetu na kuleta amani ndani ya nchi na kusaidia kuleta amani kwa watu ambao wanatuzunguka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa msingi huo nashindwa kuelewa wanatoa wapi dhana kwamba Jeshi letu linakuwa *politicized.* Kwa sababu hawezi leo hii Mheshimiwa Waitara kuweka Mezani hapa hata *photocopy* tu ya kadi ya

mwanajeshi hata mmoja ambaye amejiunga na CCM, hawezi kuweka Mezani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachoweza kuzungumzika ni kwamba anahisi kwa sababu kwenye Katiba ya CCM ukiwa Mkuu wa Mkoa ama Mkuu wa Wilaya unakuwa Mjumbe wa Kamati ya Siasa ya Chama cha Mapinduzi anahisi na hao wanajeshi pengine baada ya kuteuliwa kushika haya mamlaka mbalimbali kama Mkuu wa Wilaya ama Mkuu wa Mkoa basi wanaingia kwenye vikao vya Kamati ya Siasa ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna ushahidi wowote wa hilo na naweza kusema kwamba kwa sababu Ilani inayoongoza Taifa letu ya mtu ambaye amechaguliwa na wananchi, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli ni ya Chama cha Mapinduzi na ili ilani hii isimamiwe na chama ambacho kinaongoza dola ni lazima wale ambao wamepewa nafasi ya kusimamia utekelezaji wa ilani hiyo waweze kutoa taarifa ndani ya chama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama italazimika Mkuu wa Mkoa kwenda kutoa taarifa ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi kwenye Kamati ya Siasa na yeye ni mwanajeshi, atakwenda kutoa taarifa hiyo. Kwa sababu huwezi kutenganisha uongozi wa nchi hii ambao Chama cha Mapinduzi kimepewa dhamana na wananchi kupitia kura kwa kumchagua Mheshimiwa Rais anayetokana na Chama cha Mapinduzi na utendaji wa kila siku wa chama, haiwezekani, ni dhana ambayo haipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na kwamba, Chama cha Mapinduzi kilimsimamisha Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Rais akachaguliwa na wananchi na baada ya kuchaguliwa sasa anatekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama chake, watu aliowateua ni lazima waende wakakieleze chama nini wanafanya kwenye nafasi mbalimbali walizopewa kwenye maeneo yao. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Kolimba.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, lakini nitakwenda kwenye hotuba iliyotolewa na Kambi ya Upinzani katika ukurasa ule wa 14 ambapo walikuwa wanazungumzia suala la usalama wa mipaka ya nchi na hasa mgogoro wa mpaka wa Ziwa Nyasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe taarifa ifuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuanzia mwaka 2014 tarehe 20 mpaka tarehe 21 Machi, mkutano wa kwanza ambao unasimamiwa na jopo la Marais wastaafu watatu ulifanyika. Nataka tu nitoe *status* kwa sababu swali lao linaulizia *status,* lakini sitaweza kuwaambia yale ambayo yanazungumzwa ndani ya jopo lile kwa sababu bado linaendelea na linatoa taarifa kwenye ngazi maalum inayohusika lakini sio mahali ambapo ni pa wazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kulikumbusha na kuliambia Bunge lako Tukufu kwamba mahusiano ya Tanzania na Malawi yako vizuri, ninyi ni mashahidi na yako vizuri kwa ushahidi wa kwamba sisi kama Wizara ya Mambo ya Nje na kwa niaba ya Serikali tumeweza kufanya mikutano na Malawi kwa pamoja na yapo vizuri katika mahusiano ya kiuchumi na kijamii na ninyi ni mashahidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukienda katika suala la mgogoro wa mpaka wa Ziwa Nyasa, niseme tu kwamba, mgogoro ule ulisitishwa mwaka 2014 na sababu ya kusitishwa mgogoro ule ni kwamba Malawi ilikuwa unaingia kwenye uchaguzi mwezi Julai na kwa hiyo, Mwenyekiti wa jopo lile la usuluhishi akaona kwamba ni hekima Malawi wangekuwa hawana nafasi ya kuweza kuhudhuria vikao vile kwa hiyo, wakasitisha. Ilipofika mwaka 2015, Tanzania iliingia pia kwenye uchaguzi Mkuu, kwa hiyo, Mwenyekiti wa jopo pia alisitisha mazungmzo ya kujadili usuluhishi wa mgogoro huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa hivi nchi zote hizi haziko kwenye uchaguzi na utaratibu sasa hivi unafanyika ili kuweza kuendelea na mazungumzo haya katika mwaka huu. Kwa sasa hivi Mwenyekiti wa jopo hili anajaribu ku-*consult* na wadau watakaohusika katika Mkutano huu ili kuweza kuendelea na mazungumzo ya usuluhishi. Hiyo ndiyo *status* ya mgogoro huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba, naomba sana kwa Waheshimiwa Wabunge pamoja na Watanzania kwa ujumla wake, diplomasia iachwe ifanye kazi yake. Tunapokuwa tunaiingilia kwa kuangalia labda mitandao au nani kasema nini, nasema kwa niaba ya Wizara yangu kwamba jambo hili linashughulikiwa na lipo katika mikono ya jopo na tuiache diplomasia ifanye kazi yake. Hii ni kwa nia njema tu, kwa sababu tunapokuwa tunashabikia kuchukua maneno yanayosemwa huku, sisi tunasema kutoka kwenye Ofisi husika kwamba usuluhishi wa jambo hili unaendelea na hivi karibuni mtaambiwa lini watakapo-*consult* kwamba wadau watakuwa na nafasi kwa siku gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la mipaka; kuna Kamati ambayo inaendelea kufanya kazi yake, lakini kama mnavyojua kwamba mpaka wa Ziwa Nyasa bado haujaweza kupata usuluhishi wa kusema kwamba mpaka unapitia wapi mpaka hapo usuluhishi utakapokuwa umekwisha, jopo litakapomaliza kazi yake ndipo mpaka wa Ziwa Nyasa utakapokuwa umesemwa. Kwa hiyo, siwezi

kuzungumzia suala la mpaka kama lilivyoandikwa kwenye hotuba ya Kambi ya Upinzani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kwenye hotuba ile ile ya Kambi ya Upinzani, katika ule ukurasa wa 15, Kambi ya Upinzani inauliza ni nini hatima ya mgogoro huu? Hivi kweli tunaweza tukatoa jibu saa hizi, kama mgogoro huu unaendelea kujadiliwa na usuluhishi wake unaendelea! Wawe na subira, Kamati hiyo na jopo litakapomaliza kazi yake, ndipo tutakapojua kwamba lini tutapata jibu na mwisho wa mgogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, naomba kuunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa *AG.*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa nami niweze kuchangia, lakini pia namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa fursa hii. Yapo mambo kadhaa yamezungumzwa hapa ya Kikatiba na Kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwanza niseme hivi; Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 inatoa haki za msingi, lakini na wajibu. Hivi vitu vinakwenda pamoja; haki na wajibu.

Katiba hiyo hiyo ndiyo inayoipa Bunge mamlaka ya kusimamia na kuishauri Serikali. Ibara ya 100 ina vifungu viwili; cha kwanza na cha pili. Kimoja kinatoa uhuru wa majadiliano, lakini kifungu kidogo cha pili kinasema, bila kuathiri masharti ya Katiba hii na Sheria na huo ndiyo msingi wa kanuni ya 64.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge Ibara ya 29(5) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano inasema hivi;

*"Ili watu wote waweze kufaidi haki na uhuru vilivyotajwa katika Katiba hii, kila mtu ana wajibu wa kutenda*

*na kuendesha shughuli zake kwa namna ambayo hataingilia haki na uhuru wa watu wengine au maslahi ya Umma."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yamezungumzwa mambo hapa ambayo kimsingi yanawadhalilisha Wanajeshi na Jeshi la Wananchi wa Tanzania. Bunge lisiruhusu hiki kitu. Bunge limetunga Sheria; tunayo Sheria ya Usalama wa Taifa *(The National Security Act)* na sheria hii, Kifungu cha (4) inataja "Public officer" ikiwajumuisha na Wabunge. Yako mambo ambayo huwezi ukayasema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha (4) cha Sheria ya *The National Security Act;* na hata kama umeambiwa hizo habari, ndiyo maana tuna fursa hapa za kuchangia hata kwa maneno na kwa maandishi kwa sababu haya mambo yapo *protected.* Someni Kifungu cha (4) cha Sheria ya Usalama wa Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais Kikwete enzi zake aliwahi kutuambia; "akili za kuambiwa, changanya na ya kwako." Hamwezi mkazungumza mambo ambayo hata yanadhalilisha wanawake wa Wanajeshi; Hao Wanajeshi wenyewe wako humu halafu tunakaa kimya!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi nilikuwa nataka kusema hivi...

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa naomba...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *AG* hebu subiri kidogo, Mheshimiwa Lissu.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, maneno anayosema Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ni makubwa sana na ni ya hatari sana. Kusema kwamba Bunge haliwezi likazungumzia masuala ya ndani ya Ukumbi wa Bunge kwa sababu ni masuala ya usalama wa Taifa, maana yake ni kusema kwamba Bunge halina mamlaka tena ya kuisimamia Serikali. Serikali ni pamoja na Jeshi. Kwa hiyo, kauli inakwenda kinyume na msingi mkuu

wa Katiba yetu kwamba Bunge ni chombo cha kuisimamia na kuishauri Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, Bunge hili siyo tu lina mamlaka ya kuisimamia na kuishauri Serikali, lina mamlaka vile vile ya kuiwajibisha Serikali pale inapokosa. Mamlaka hayo ya kuiwajibisha Serikali ni pamoja na mamlaka ya kupitisha azimio la kutokuwa na imani na Waziri Mkuu na kusababisha Baraza zima la Mawaziri kuvunjwa. *(Makofi)*

Mwisho, Bunge hili lina mamlaka ya kumwondoa Mheshimiwa Rais madarakani kwa ku-*move a motion* of *impeachment*. Kwa hiyo, mamlaka ya Bunge ya kuisimamia Serikali ni makubwa sana, ni mamlakaya Bunge... *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lissu, ahsante. Mheshimiwa *AG.*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hii taarifa naikataa. Yeye alikusudia kueleza tu mamlaka. Nimesema hapa, Ibara ya 100(2) inasema:

*"Bila kuathiri Katiba hii au masharti ya Sheria nyingine yoyote inayohusika."*

Nimesema hivi, Katiba yetu inatoa haki na wajibu. Kwa mfano, huwezi ukapiga mtu au ukatukana mtu, ukasema nina uhuru wa hapa. Haiwezekani! Tunatambua Katiba inatoa mamlaka hayo na tumetunga sheria hizi hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami ngoja niwashauri hapa. Najua hapa wakati fulani mnapotoshwa. Uhuru huo mnaotafsiri Katiba vibaya, kuna siku nyingine mtajikuta pabaya, *that is it!* Eeh! *(Kicheko/Makofi)*

Hamuwezi, kwa sababu Katiba iko wazi, nakupeleka tu Mahakamani. *(Kicheko)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, maneno ya kwenye Ibara ya 10 ya hotuba hii, yanasema "Vinanunuliwa vifaa vibovu ambavyo havifai kutumika kwa ajili ya matumizi ya Jeshi...

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumwambia Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwamba maneno anayozungumza kwanza Spika aliyaondoa tukakubaliana hapa, lakini kwa upande wenu wa CCM mlitoa hoja tukaunga mkono. Sasa anarudia mambo ambayo tulishafunga na wewe uliagiza yakaondolewa kwenye *Hansard*. Kwa hiyo, anarudi tulikotoka. Nadhani kama amemaliza kuchangia, ampe mtu mwingine tufunge mjadala huu. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa *AG.* Mheshimiwa *AG* maneno yaliyotolewa yote yasisemwe. *(Makofi)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, aliyasema; lakini ninachotaka kusema ni hivi, Waheshimiwa Wabunge watumie uhuru wao kuishauri na kuisimamia Serikali kwa hekima. Eeh! Haya mambo yapo hapa. Siku hizi wameanzisha utaratibu...

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, yale unayoyakataa, wanaweka kwenye mitandao. Wakiweka kwenye mitandao, nitawachukulia hatua za kisheria.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rhoda, kaa chini.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hawawezi kuwa *protected.*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rhoda, kaa chini.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Naitwa Sophia, siitwi Rhoda.

**MWENYEKITI:** Kaa chini!

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naitwa Sophia.

**MWENYEKITI:** Sophia kaa chini.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Taarifa!

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nasimamia ununuzi hata Mikataba yote inapita hapa, vifaa vya kisasa wananunua; unaweka maneno hayo, una-*expose* Taifa hili kwa watu wengine kwamba Jeshi la Tanzania lina vifaa duni, kwa hiyo tunaweza tukaenda tukawavamia kule. Haiwezekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, limezungumzwa hapa na kukubali kwamba Katiba Ibara 147 imepiga marufuku Wanajeshi kujiunga na Vyama vya Siasa. Hiyo ni kweli kwa sababu ni sharti kabisa la Kikatiba lakini, Ibara ya 45, Kifungu cha 25 cha Sheria ya Ulinzi wa Taifa *(The National Defence Act)...*

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa!

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** ...kimetoa Mamlaka kwa Rais ku-*second* mtu yoyote.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sophia nimesema kaa chini.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** ...Wanajeshi na kipindi chote hicho amekuwa...

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa!

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Kuhusu utaratibu.

**MWENYEKITI:** Wewe unatafuta matatizo.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** ...kuwa ni Mwanajeshi. Kipindi chote hicho, huyo mtu anaendelea kuwa Mwenyekiti. Sasa kwa mfano, kama ameteuliwa kuwa Mkuu wa Wilaya au Mkuu wa Mkoa, tunajua yuko Mwenyekiti wa Chama wa Mkoa; Mwenyekiti wa Chama wa Wilaya ana majukumu yake, hawezi kuchukuliwa na Mkuu wa Mkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Katiba yenyewe ya Chama cha Mapinduzi imesema kwenye Ibara ya 94 na Ibara ya 80; "Mkuu wa Mkoa atakuwa Mjumbe wa hizo Kamati kama anatokana na Chama cha Siasa." Eeh, na wote tunafahamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa sababu huyu anakwenda kufanya mambo ya Serikali kule siyo ya Chama. Katiba iko wazi. Huyu anatokana na Chama cha Siasa. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa AG. Mheshimiwa Waziri.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu jioni ya leo ili niweze kuhitimisha hoja yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia katika hoja hii na michango ilikuwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, waliochangia kwa maandishi ni Waheshimiwa Wabunge 38 na waliochangia kwa kuzungumza ni Waheshimiwa Wabunge 21.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee naomba niishukuru kwa dhati Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama chini ya uongozi thabiti wa Mheshimiwa Balozi Adadi Rajabu kwa ushirikiano wao mkubwa katika kutekeleza mambo ya kikanuni kama ilivyoainishwa katika kanuni za Bunge, Toleo la Januari, 2016 kupitia masuala yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza walitembelea miradi ya maendeleo chini ya Wizara yangu; pili, walifanya tathmini ya utekelezaji wa mipango ya bajeti ya mwaka wa fedha 2016/2017, walifanya uchambuzi wa makadirio kwa mwaka wa fedha 2016/2017; na mwisho, walitoa maoni na ushauri wa Kamati ambayo yalitolewa kwa kuzingatia uchambuzi wa mambo yaliyozingatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naungana na Kamati katika maoni yake kuhusu miradi ya maendeleo kutopatiwa fedha kadri ya makadirio na hili limekuwa ni changamoto kubwa kwetu. Tunaendelea kuwasiliana na Wizara ya Fedha na Mipango ili kuona kwamba miradi hiyo inapatiwa kipaumbele kabla ya mwisho wa mwaka wa fedha 2016/2017. Tatizo kubwa kwa muda mrefu limekuwa ni ufinyu wa makusanyo

na kipaumbele kwa matumizi ya Serikali na vipaumbele mbalimbali vinavyoikabili nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama ilivyo ada, naomba nianze kujibu baadhi ya hoja ambazo zimetolewa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa kuna hoja ya kwamba Serikali iyapatie mafungu ya Ngome JKT na Wizara, fedha zote za maendeleo kwa mwaka wa 2016/2017. Kulingana na upatikanaji wa fedha zinazotokana hasa na mapato ya ndani, Serikali imekuwa ikitoa fedha za maendeleo kwa Wizara ili kuweza kutekeleza shughuli za maendeleo. Mfano, hadi kufikia mwezi Machi, 2017 Wizara ilikuwa imepokea jumla ya shilingi 35.9 bilioni sawa na asilimia 14.5 ya bajeti ya maendeleo. Kumekuwa na mawasiliano kati ya Wizara yangu na Hazina kuhusu Wizara kupatiwa fedha za maendeleo zilizobakia ili kukamilisha utekelezaji wa mipango yake ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ni Serikali itoe shilingi bilioni 27 zilizotengwa mwaka 2016/2017 kwa ajili ya kulipia maeneo yaliyochukuliwa na Jeshi kabla ya terehe 30 Juni, 2017. Katika mwaka wa fedha 2016/2017, Wizara ilitenga shilingi bilioni 27.7 kwa ajili ya kupima na kuwalipa fidia wananchi ambao maeneo yao yalitwaliwa kwa matumizi ya Jeshi. Hata hivyo, fedha hizi bado hazijatolewa hadi kufikia mwezi Machi, 2017. Wizara imekuwa ikiwasiliana na hazina kuhusu kupatiwa fedha kwa ajili ya kutekeleza shughuli za maendeleo ikiwemo fedha kwa ajili ya fidia za ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadaye nitatolea maelezo yale maeneo yote ambayo Waheshimiwa Wabunge wameyazungumza kwa uchungu kabisa kuhusu fidia kwa maeneo yaliyochukuliwa na Jeshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ni kwamba Serikali ipime ardhi inayomilikiwa na Jeshi na kuimilikisha kwa Jeshi Kisheria. Kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi Na. 4 ya mwaka

1999 na Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na. 5 ya mwaka 1999, hakuna kipengele cha utoaji wa hatimiliki kwa Taasisi za Serikali likiwemo Jeshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, mazungumzo yanaendelea kati ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la kujenga Taifa na Mamlaka husika ili hatimaye maeneo yote ya Jeshi yapewe hatimiliki bada ya kuzifanyia marekebisho Sheria hizo. Serikali kupitia Wizara husika na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, inaendelea na taratibu za kuibadilisha Sheria ya Ardhi Na. 4 na 5 ya mwaka 1999 ili kuziwezesha Taasisi za Umma likiwemo Jeshi kumilikishwa maeneo kwa hatimiliki ili kuondokana na utaratibu wa sasa wa kusajiliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo la Sera na Sheria ya Ulinzi; Kamati ilitaka Serikali ikamilishe mchakato wa kufanya marekebisho katika Sheria ya Jeshi la kujenga Taifa, Sura ya 193 na Sheria ya Ulinzi wa Taifa, Sura ya192 ili iweze kuendana na wakati, mifumo ya utawala na mahitaji ya sasa ya Kisheria katika Sekta ya Ulinzi.

Mheshimiwa mwenyekiti, kwa kuwa suala la Sera ya Ulinzi wa Taifa ni la Muungano, kukamilika kwake kunategemea ridhaa ya pande zote mbili za Muungano. Hatua iliyofikiwa kwa sasa ni kupata maoni kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, marekebisho ya Sheria ya Ulinzi wa Taifa na Sheria ya JKT yatafanyika baada ya kukamilika kwa Sera ya Ulinzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili, napenda nilieleze Bunge lako Tukufu kwamba tumefikia sehemu nzuri sana, nimefanya mazungumzo na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais anayeshughulika na vikosi vya SMZ kule Zanzibar na ameniahidi kwamba sera hii sasa inakaribia kupata maoni ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ili tuweze kukamilisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni Serikali ione muhimu wa suala la fidia kwa vijana wanaopata ulemavu wakiwa katika mafunzo ya JKT. Napenda kuliarifu Bunge lako kwamba malipo ya fidia hufanyika kwa mujibu wa Sheria ya

Ulinzi wa Taifa ya mwaka 1966 ambapo mapendekezo ya marekebisho ya Sheria tajwa yatafanyika baada ya kukamilika kwa Sera ya Ulinzi wa Taifa. Kwa sasa, kijana analipwa fidia kwa kutumia kiwango cha mshahara wa Askari wa cheo cha *Private* kwa mwaka wa kwanza. Maana yake ni kwamba vijana wanaokwenda JKT wakiumia, siyo kwamba hawalipwi fidia, wanalipwa fidia kwa kutumia kigezo hiki cha kwamba tunawalipa sawa na aliyeajiriwa katika ngazi ya *Private* anapokuwa ni mwaka wake wa kwanza Jeshini. Kwa hiyo, fedha hizi huwa wanazipata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni Serikali itoe kipaumbele kwa vijana waliopitia mafunzo ya JKT wakati wa kuajiri vijana kwa ajili ya shughuli za ulinzi katika Shirika la SUMA JKT. Hivi ndivyo hasa ilivyo. Napenda kutoa taarifa kwamba *SUMA JKT Guard Limited* linatoa kipaumbele kwa vijana waliopitia mafunzo ya JKT wakati wa kufanya ajira zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni Serikali iboreshe miundombinu ya kambi za JKT ili vijana wengi kwa mujibu wa Sheria waweze kufanya mafunzo hayo na kutenga fedha kwa ajili ya shughuli za uendeshaji wa mafunzo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inaendelea kuwasiliana na Mamlaka husika ili kuona uwezekano wa kuongeza fedha kwa mafunzo hayo kadri hali ya kifedha itakavyoruhusu. Sisi sote tunapenda kwamba vijana wote wanaokamilisha masomo yao ya kidato cha sita waweze kuingia Jeshini kwa mujibu wa sheria kabla hawajaendelea na elimu ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu eneo la madeni, Kamati imeitaka Serikali ilipe madeni ya Wazabuni na madeni ya Kimkataba. Serikali ione umuhimu wa kuongeza kasi ya kulipa madeni yote ya Wizara yaliyohakikiwa kiasi cha shilingi bilioni 212.3. Maelezo ni kwamba kiini cha madeni ya Jeshi ni ufinyu wa bajeti katika maeneo mbalimbali ya utekelezaji wa majukumu ya kijeshi. Jumla ya madeni yaliyohakikiwa na ambayo yanapaswa kulipwa ni shilingi bilioni 95.6. Mpaka

sasa Serikali imechukua hatua ya kuanza kulipa madeni hayo ambapo imetoa shilingi bilioni 5.16. Aidha, madeni ambayo hayajalipwa ni shilingi bilioni 90.4.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara katika mwaka wa fedha 2016/2017, imelipa shilingi milioni 61.2 kwa ajili ya malipo ya Wazabuni wa ndani ambao wametoa huduma mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwa upande wa Wazabuni wa nje Wizara imelipa shilingi bilioni 30. Aidha, Wizara inadaiwa deni la kimkataba, mikataba mbalimbali kiasi cha shilingi bilioni 785.2. Kwa hiyo, katika mwaka wa fedha 2017/2018 Wizara imekasimia shilingi bilioni 120.7 kwa ajili ya kulipa madeni ya kimkataba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu fungu 39 la JKT jumla ya madeni ya fungu hili hadi kufikia mwezi Aprili, 2017 ni shilingi bilioni 101 na madeni yaliyohakikiwa ni shilingi bilioni 79.8. Serikali imeweza kulipa shilingi bilioni 4.2, hivyo kufanya deni hilo lililohakikiwa kubaki shilingi bilioni 75.6.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni kuhusu *SUMA Guard* ilipwe madeni yake na wale ambao wamepewa huduma naye. Tumepokea ushauri wa Kamati kuhusiana na Kampuni ya *SUMA JKT Guard Limited*, kampuni itaendelea kufuatilia madeni kwa washitiri wake kwa kutumia Wakala wa kukusanya madeni na kuimarisha kitengo chake cha ukusanyaji madeni kwa ajili ya kufuatilia na kuwakumbusha wateja wake kulipa madeni yao.

Mheshimiwa Mwenyeki, kuhusu Mashirika ya Jeshi; Kamati imetaka Shirika la Mzinga kumilikiwa kisheria na kuwajibika chini ya mamlaka moja. Shirika la Mzinga ni Taasisi iliyo chini ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, lakini kama taasisi nyingine za Serikali au za Umma, linawajibika kuwa kwa Msajili wa Hazina vile vile. Wizara itashughulikia ushauri uliotolewa ili Shirika hili liweze kuwajibika chini ya mamlaka moja kwa kuanza utaratibu wa kubadilisha sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Serikali itenge fedha za kutosha kwa ajili ya ukarabati na ujenzi wa miundombinu ili kuongeza ufanisi wa utendaji wa Mashirika ya Nyumbu na Mzinga; Serikali katika mwaka wa fedha 2017/2018 imetenga shilingi bilioni 8.8 kwa ajili ya kufanya ukarabati wa miundombinu ya teknolojia ya Shirika la Nyumbu na shilingi bilioni 1.5 kwa ajili ya Shirika la Mzinga. Hata hivyo, mashirika haya yataendeleza juhudi za mashirika yenyewe binafsi ili waweze kuzalisha fedha zaidi ambazo zitawasaidia katika kuboresha hali ya miundombinu ya mashirika haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ilikuwa ni sehemu ya kujibu hoja zilizotolewa na Kamati na sasa naomba niingie katika hoja zilizotolewa na Kambi ya Upinzani. Kabla sijaingia kwenye hoja zenyewe naomba niseme maneno machache ya utangulizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi ni Taasisi ambayo ni tofauti sana na taasisi nyingine za kiraia hasa kutokana na majukumu yake. Kila Mwanajeshi anapoingia Jeshini anafunzwa miiko na taratibu zake ambapo kwa sehemu kubwa ni kumwezesha Mwanajeshi kutumika vyema wakati anapohitajika kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikitika kwamba sehemu kubwa ya hotuba ya Kiongozi wa Upinzani au Msemaji wa Upinzani, imetokana na hisia na baadhi ya matamshi ambayo hayana ukweli wowote au hayajafanyiwa utafiti na matokeo yake yanaweza kuzua majungu au utovu wa nidhamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikumbukwe kwamba Jeshi huendeshwa kwa kuzingatia mambo yafuatayo:-

(1) Katiba ya Nchi;

(2) Sheria ya Ulinzi wa Taifa;

(3) Kanuni ya Majeshi ya Ulinzi; na

(iv) ni *Forces Routine Orders* zinazotolewa na Mkuu wa Majeshi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, rejea zote zilizotajwa hapo juu, zinatoa utaratibu kamili wa namna ya kuendesha Jeshi kama Taasisi ya Nidhamu na Utii chini ya uongozi wa Amiri Jeshi Mkuu na pia uongozi wa Kisiasa wa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa katika uhalisia wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Ulinzi wa Taifa na Kanuni za Majeshi ya Ulinzi, *volume* ya kwanza, ya pili na ya tatu, zinatoa maelekezo ya namna Wanajeshi watakavyotenda kazi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba ya Kiongozi wa Kambi ya Upinzani inaingilia mno shughuli za uendeshaji wa jeshi. Hatari iliyopo ni kwamba Kiongozi wa Upinzani amechukua maneno kutoka kwa Askari wasiozingatia nidhamu na bila ya kufanya utafiti wa kutosha, amegeuza kuwa ndiyo taarifa yake. Ni vyema tutambue kwamba kauli kama hizi zinaweza kupelekea kuligawa jeshi bila sababu yoyote au kupandikiza mbegu za utovu wa nidhamu jeshini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanajeshi wamejiunga na jeshi kwa masharti yaliyopo na wanapaswa kuyazingatia wakati wote wa utumishi wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia kusema, nimesikitishwa sana na maneno yenye lengo la kuwagombanisha wanajeshi na Serikali yao pamoja na Wanajeshi na Uongozi wao wa juu. Hili halipaswi kuvumiliwa na ni vyema Bunge lako liangalie utaratibu wa kikanuni za kumtaka Msemaji athibitishe maelezo aliyoyatoa katika wakati muafaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, sasa naomba nizijibu hoja zilizotolewa na Msemaji wa Kambi ya Upinzani kama ifuatavyo:-

Kwanza, kuongeza muda wa kufanya kazi Jeshini baada ya muda wa kawaida kwisha. Siyo sahihi kuwa Wanajeshi hawakupewa au hawakuelezwa sababu za kuendelea kufanya kazi baada ya muda wa kazi za kawaida. Wanajeshi wote walipewa taarifa na hakuna taharuki yoyote. Muda wa kazi uliongezwa kwa ajili ya michezo na mazoezi ya viungo. Aidha, ikumbukwe kuwa wanajeshi wanaandikishwa kwa masharti ya kufanya kazi masaa 24. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la usalama wao; wanajeshi wanasafirishwa kwenda na kurudi kazini kwa kutumia mabasi maalum ya usafiri. Hapa nataka kusema kwamba, baada ya saa za kazi, ili Wanajeshi hawa wawe na utimamu wa kimwili na kiafya, wanatakiwa wafanye mazoezi ya viungo na hasa wajihusishe na michezo. Ndiyo sababu ya kuongeza muda wa kutoka kazini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zamani, ama kuna wakati pengine ilizoeleka kwamba watu wanamaliza baada ya muda wa saa za kazi wanakwenda *bar* wanakunywa pombe na kadhalika. Hii haina afya kwa jeshi letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, viongozi wanapokuja kurudisha taratibu stahili hatupaswi sisi kama viongozi kuwaona wanafanya makosa, badala yake tuwapongeze kwa hatua hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ilikuwa ni kusitisha utoaji wa fedha za likizo kwa wanajeshi. Malipo ya fedha za likizo kwa wanajeshi hayajasitishwa na ni haki kwa wanajeshi wote. Aidha, siyo kweli kwamba Mnadhimu Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, yaani *Chief of Staff* amezuia madai ya wanajeshi ya kulipwa malipo ya likizo. Mnadhimu Mkuu wa Jeshi amekuwa mstari wa mbele katika kufuatilia stahiki hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi kila mwaka wa fedha, fedha za likizo zinatengwa kutoka bajeti ya Jeshi kila mwaka wa fedha. Changamoto kubwa imekuwa ni ukomo wa

bajeti, hali inayosababisha kutokidhi kuwalipa wanajeshi wote wanaostahili kwenda likizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara itaendelea kuwasiliana na Hazina iweze kusaidia kuongeza bajeti katika eneo hili ili wanajeshi wote waweze kwenda likizo. Aidha, Wizara inajaribu kubuni njia nyingine kwa kushirikiana na Hazina ili kuhakikisha kuwa wanajeshi wote wanalipwa fedha za likizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuongezea katika eneo hili; mimi binafsi wakati nikifanya ziara zangu katika Kambi za Jeshi, napata nafasi ya kuzungumza na Wanajeshi; katika kero kubwa ambayo imekuwa ikizungumzwa na Wanajeshi, ni kero ya fedha za likizo. Nimekuwa nikiwaambia kwamba hakuna mtu, siyo Wizarani wala Jeshini ambaye angependa wasipate. Sote tunapenda wapate, tunawapigania sana na tukifanikiwa katika kupata fedha hizi tutawalipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale wote ambao hawajalipwa kwa kipindi ambacho walistahili, zinahesabiwa kama ni madeni. Fedha za madeni zikilipwa, watapewa fedha zao. Kwa hiyo, hatuoni sababu kwa nini kuja na dhana kwamba *Chief of Staff* anataka watu wasilipwe? Hili litahitaji kuthibitishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hoja nyingine iliyotolewa kwamba Wajumbe wa Bodi ya Manunuzi wanajipa safari za ununuzi wa zana nje ya nchi. Bodi ya Wazabuni ya JWTZ imeundwa kisheria kwa kuzingatia Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2011 na Kanuni zake. Bodi hiyo ina wajibu wa kutoa idhini ya manunuzi ya vifaa mbalimbali kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu zilizopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wajumbe wa Bodi hiyo hawana wajibu wa kununua vifaa na hakuna Mjumbe wa Bodi ya Manunuzi ambaye amesafiri kwenda nje ya nchi kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya JWTZ. Utaona kwamba hoja hii nayo inataka ithibitishwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani mtu mmoja barabarani akasema maneno ambayo kwa kweli yanaharibu taswira ya Jeshi zima, halafu tukayachukua tukayaweka kwenye hotuba halafu wengine tukanyamaza kimya. Kwa kweli hili litakuwa siyo jambo la busara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ilikuwa ni kuondolewa kwa maduka ya bei nafuu Jeshini, yaani *Military Duty Free Shops.* Maduka hayo yaliondolewa rasmi na Serikali tarehe 1 Julai, 2016 baada ya kuonekana kutowanufaisha Wanajeshi na pia baadhi ya wafanyabiashara wasio waaminifu kutumia mwanya wa maduka hayo kukwepa kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuondoa maduka hayo, Serikali imekuwa ikiwalipa Wanajeshi fedha za ruzuku kama sehemu ya kupunguza makali ya misamaha ya kodi iliyoondolewa. Siyo kweli kwamba fedha hizo zimetolewa mara moja tu, fedha hizo bado zimeendelea kutolewa kila baada ya miezi mitatu kama Serikali ilivyoahidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika, katika ziara zangu katika makambi ya Jeshi, ukiuliza matatizo ya Wanajeshi, wao wenyewe watakiri kwamba maduka haya yalikuwa yanawanufaisha wafanyabiashara siyo wao. Maduka mengi ya Jeshi, ilikuwa gharama wanazolipa wao ni sawa na kununua mtaani, wakati wao wametolewa ushuru. Kwa hiyo, aliyekuwa anafaidika ni wale wafanyabiashara. Serikali imegundua hili, sasa hivi wanatakiwa kulipwa; wameanza fitina na hili linaonekana kama vile Wanajeshi wanaonewa. Siyo kweli, waliokuwa wananufaika siyo Wanajeshi na tutaendelea kuwapa hiyo ruzuku ili kuweza kuwapunguzia makali ya maisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la tano, kuhusu Wanajeshi kutopandishwa vyeo. Suala la Wanajeshi kupandishwa vyeo, linazingatia sheria, kanuni na taratibu zilizopo bila ubaguzi wowote. Maafisa na Askari ambao wanastahili na wamekidhi vigezo, wamekuwa wakipandishwa vyeo mara kwa mara kwa kufuata taratibu

zilizopo. Mara ya mwisho Maafisa na Askari wamepandishwa vyeo katika ngazi mbalimbali mwezi Aprili, 2017. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii maana yake nini? Maana yake, katika Hotuba ya Kambi ya Upinzani walitaka kuashiria kwamba, kuna Mkuu wa Majeshi mpya ameacha kupandisha watu vyeo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepandisha watu vyeo. Kwanza kwa taarifa yenu, upandishwaji wa vyeo unafanywa na Kamati ya Ulinzi ya Taifa, ambayo Mwenyekiti wake ni Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Aprili mwezi uliopita tumekaa na tumepandisha vyeo Wanajeshi wote wanaostahili kupandishwa vyeo. Kwa hiyo, siyo kweli hata kidogo kwenda mitaani kuchukua maneno ambayo hayana chembe ya ukweli kuyaleta na kuyazungumza ndani ya Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, malipo ya fedha za chakula kwa Wanajeshi *(Ration Allowance);* fedha za chakula kwa Wanajeshi hulipwa kwa kuzingatia Sheria ya Ulinzi ya Taifa ya mwaka 1966; na Kanuni za Majeshi ya Ulinzi, Utawala ambapo chakula hutolewa kwa Wanajeshi kwa kuzingatia majukumu anayopewa Mwanajeshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwanajeshi anawajibika kula chakula stahiki na mahali stahiki kwa mujibu wa kanuni na taratibu zilizopo. JWTZ kwa kushirikiana na Serikali, litaendelea kuhakikisha kuwa Wanajeshi wanapewa chakula stahili kwa kuzingatia majukumu wanayopewa. Fedha za chakula anazolipwa Mwanajeshi, siyo kwa ajili ya familia yake bali ni kwa ajili yake mwenyewe ili awe na afya imara, isiyotetereka ili aweze kutekeleza majukumu ya ulinzi wa Taifa kikamilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niongezee kusema kwamba, wale ambao wapo kazini, wale ambao wapo kambini, wale ambao wana kazi maalum *(operation)*, lazima wale ndiyo wakatekeleze *operations*. Wale ambao wapo katika maeneo mengine, wanapewa fedha zao kwenye

mishahara yao. Hakuna tatizo hapa. Kwa hiyo, haya maneno pia hayana ukweli Mheshimiwa. Naomba sana siku nyingine ukipata maelezo kama haya, nione kwanza, nitakupa taarifa kabla hujaweka kwenye hotuba yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine inahusu ufinyu wa bajeti ya umeme. Suala la ufinyu wa bajeti ya umeme, linatokana na ukomo wa bajeti unayotolewa na Serikali. Tunapenda kuishukuru Serikali kwa hatua iliyochukua ya kuweza kupunguza madeni ya umeme ili JWTZ liendelee kupata huduma ya umeme katika makambi. Wizara itaendelea kuwasiliana na Hazina ili waweze kutoa fedha za kutosha, katika eneo la umeme na maeneo mengine muhimu ambayo tunadaiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo kweli kwamba Jeshi halilipi kwa kutotaka, wala siyo kweli kwamba Amiri Jeshi Mkuu ameamua hata Kambi za Jeshi zikatiwe umeme. Alichosema ni kwamba watu lazima walipe na baada ya hapo Hazina walitoa fedha na jeshi likalipa; na tutaendelea kufanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendelee na eneo lingine la utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2016/2017. Kambi ya Upinzani wanasema fedha za maendeleo zimetolewa pungufu, hili tunakiri. Fedha za Maendeleo hutolewa kila mwezi kutegemeana na mapato ya Serikali kila mwezi, Wizara inaendelea kuwasiliana na Wizara ya Fedha na Mipango ili fedha zote ambazo hazijatolewa, ziweze kutolewa katika kipindi kilichobaki ili tuweze kutimiza majukumu yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu makusanyo kidogo ya maduhuli ya JKT; maduhuli ya JKT yaani Fungu 39 yanatokana na matunzo ya mazao ya shamba darasa, uuzaji wa nyaraka za zabuni na siyo kutoka katika shughuli za uzalishaji mali za SUMA JKT. Yaani kwa maana nyingine tutofautishe kati ya SUMA JKT na Fungu 39, yaani Makao Makuu ya JKT.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii taarifa ya asilimia 31.8 ni maduhuli ya JKT, yaani Fungu 39 hadi kufikia Machi 2017. Aidha, hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2017 fedha zilizokusanywa kutokana na maduhuli zimefikia asilimia 67.5 ya lengo. Kwa hiyo, tunakwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika randama ya Fungu 57 *subvote* 1005 na *subvote* 2004 hazikutengewa fedha za mishahara. Je, vitengo hivi havina watendaji? Lilikuwa ni swali, ambalo jibu lake ni kwamba vitengo hivi kwa sasa havina watumishi wa umma ambao mishahara yao ingepaswa kuonekana hapo, bali kwa sasa wapo Wanajeshi ambao mishahara yao inalipwa kutoka Fungu 38 la Ngome.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni Uteuzi wa Wanajeshi katika nafasi za Kisiasa. Ndugu yangu Naibu Waziri wa Afya amenisaidia kujibu hili eneo, lakini niseme tu hivi kwamba, uteuzi wa viongozi unazingatia weledi na hitajio la uongozi katika eneo husika na kwa kuzingatia Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Majukumu ya Viongozi hawa siyo ya kisiasa, bali ni kutekeleza kazi za Kiserikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, uteuzi unaofanywa siyo tafauti na majukumu ambayo Serikali imekuwa mara kwa mara ikiliagiza Jeshi kusaidia mamlaka za kiraia. Kwa maana nyingine, mara kadhaa tumeshaombwa na mamlaka za kiraia kutoa msaada hususan katika maeneo ya mipakani. Kwa hiyo, inaleta mantiki unapomweka Mwanajeshi kusimamaia pale akiwa kiongozi kwa sababu atakuwa na uharaka wa kuchukua hatua kama hizi tunazozizungumzia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo baadhi ya Wanajeshi ambao wameteuliwa na Chama Tawala katika nafasi mbalimbali za uongozi. Hata hivyo, uteuzi huo hufanyika kwa makubaliano ya Chama Tawala na Wanajeshi husika baada ya kustaafu utumishi Jeshini na siyo wanapokuwa katika utumishi wa Jeshi. Mfano, uteuzi wa Kanali Lubinga kuwa Katibu wa *NEC* ya Chama Tawala, ulifanyika baada ya Afisa Mkuu huyo kustaafu rasmi utumishi Jeshini. *(Makofi)*

Wanajeshi wanateuliwa kushika nafasi za Kiserikali na siyo za kisiasa, hivyo wanaruhusiwa kuvaa sare za Kijeshi kulingana na majukumu na matukio maalum. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ushiriki wa Jeshi katika *operation* za ulinzi wa amani; napenda niseme kwamba, ushiriki wa Jeshi katika *operation* za Umoja wa Mataifa umekuwa na faida kubwa hususan kwa kuwawezesha Wanajeshi wetu kuongeza weledi, kuongeza uzoefu na *exposure,* teknolojia na kuitangaza Tanzania katika tasnia ya ulinzi na usalama duniani. Tumekuwa tukipata sifa nyingi na ni mategemeo yetu kwamba tutaendelea kutuma vijana wetu wakalinde amani katika maeneo mbalimbali duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu eneo la JKT kwamba SUMA JKT limetoa mchango gani kwa Jeshi katika kukabiliana na changamoto za bajeti? SUMA JKT linashiriki kupunguza changamoto za kibajeti kwa Jeshi kwa kuchangia katika uendeshaji wa Kambi na pia kuchangia gharama za chakula kwa vijana JKT ambapo mpaka sasa asilimia 55 ya gharama inalipwa na itaongezeka kufikia asilimia 100 siku zijazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, *SUMA JKT* kupitia kampuni yake ya ujenzi imekuwa ikishiriki ukarabati na ujenzi wa Kambi na miundombinu bila kutoza gharama ya kazi hizo. Mchango wa SUMA kuipunguzia Serikali gharama za uendeshaji, ni kwamba jukumu la SUMA ni kuipunguzia Serikali gharama za kuendesha JKT. Jukumu hilo limeanza kutekelezwa kwa kuchangia kulisha vijana na gharama za uendeshaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, idadi ya miradi ya uzalishaji wa mali wa SUMA JKT, iko mingi ikiwemo kilimo na mifugo, uhandisi wa ujenzi, kutoa huduma za ulinzi kwa jamii, uunganishaji na usambazaji wa matrekta na uzalishaji samani, kokoto na ushonaji wa nguo. Fedha zilizoingizwa kutokana na uzalishaji ni jumla ya Shilingi bilioni 7.8 na zinaonekana katika *audit report* ya SUMA JKT .

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie eneo hili la Kambi ya Upinzani kwa hoja hii ya Jeshi la Kujenga Taifa, kwamba Jeshi hili ni pamoja na kuwa na dhima ya kuwafunza vijana, kuzalisha mali ikiwemo kuzalisha chakula. Jeshi lipimwe kwa uzalishaji mali na kupunguza njaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, JKT lina *program* ya kuongeza uzalishaji mali na mafunzo ya uzalishaji mali hasa chakula kwa vijana wake kupitia mashamba darasa yaliyopo. Aidha, vijana waliopo kwenye makambi ya JKT wameanza kujitegemea kwa awamu katika gharama za chakula kutokana na chakula wanachokizalisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ni nyingi, sitoweza kuzimaliza zote, lakini nataka kuwahakikishia Waheshimiwa kwamba tutazitoa kwa maandishi kabla ya mwisho wa Bunge hili. Kuna eneo moja muhimu sana ambalo limechangiwa na Wabunge wengi, nalo ni migogoro ya ardhi na fidia kwa maeneo ambayo Jeshi limeyatwaa. Eneo hili limechangiwa na Waheshimiwa Wabunge wengi akiwemo Mheshimiwa Ester Matiko, Mheshimiwa Manyinyi, Mheshimiwa Mabula, Mheshimiwa Deo Sanga na wengi ambao orodha yao ninayo hapa.

Waheshimiwa Wabunge, ninachoweza kusema na naomba mnielewe vizuri kwamba nia ya kulipa ipo, tathmini katika baadhi ya maeneo imeshafanyika, upimaji umeshafanyika, kwa hiyo, kilichobaki ni kulipa tu hiyo fidia inayotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliweka katika bajeti yetu kama nilivyosema shilingi bilioni 27.7, bahati mbaya bado hatujapokea, lakini mazungumzo yanaendelea. Tuna mategemeo kwamba kabla ya mwisho wa mwaka huu wa bajeti, fedha zitakazopatikana tutaanza kulipa fidia zinazotakiwa katika maeneo ambayo nimeyazungumzia hapa. Kwa hiyo, kuna maeneo mengi mno na naweza nikaitoa ile orodha, lakini kwa sababu ya muda, naomba niendelee na maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa kuna hoja ya pensheni ndogo kwa wastaafu waliostaafu zamani. Tunakubaliana kabisa na hoja hii na nataka niseme kwamba Serikali imeanza kulifanyia suala hili ili hatimaye tuweze kurekebisha penisheni hizo. Ila ni lazima tuelewe kwamba wastaafu wako wengi sana na fedha zitakazohitajika ni nyingi sana. Kwa hiyo, lazima zoezi hili liende awamu kwa awamu, ndiyo maana Serikali imeanza na ngazi za juu. Imeanza kutoka cheo cha Meja Jenerali hadi Jenerali kamili na tutaendelea kwa awamu hadi hapo ambapo tutaweza kutimiza jukumu hili la Serikali la kuweza kuwatazama wale ambao wamestaafu muda mrefu uliopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hoja za Mheshimiwa Fakharia, kuhusu idadi ndogo ya wanaojiunga na JKT kutoka Zanzibar. Mpaka sasa hivi wanaojiunga na JKT kwa mwaka tunapeleka nafasi 300. Kila tukiongeza idadi ya wanaoingia JKT, pia tutaongeza idadi ya wale wanaotoka Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nawashauri tu Waheshimiwa Wabunge kwamba utaratibu ule wa ugawaji, siyo jukumu la Serikali ya Jamhuri ya Muungano wala siyo la Jeshi. Tunazikabidhi kwa Serikali ya Zanzibar na kuwataka wao wazigawe kwa kadri watakavyoona inafaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa taarifa nilizokuwanazo, kwa sasa zinagawiwa katika Wilaya na Mikoa na kama kuna matatizo huko, likiwemo lile alilozungumzia Mheshimiwa Dau kule Mafia kwamba Mshauri wa Mgambo ndio anachukua watu kutoka nje, hapa naweza kusema kwamba zoezi hili linafanywa na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya. Halipaswi kufanywa na mtu mmoja. Kwa hiyo, namshauri Mheshimiwa Dau kwamba kama ni kweli haya yanatokea, basi ahakikishe anakaa na *DC* kama Mwenyekiti ili waweze kudhibiti hii hali, kwa sababu suala hili ni jukumu la Kamati ya Ulinzi na Usalama, siyo suala la Mshauri wa Mgambo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Jasson Rweikiza alitaka kujua tuna-*ratify* lini ile *Biological Weapon Treaty*

ambayo, tumeshaisaini? Naweza kumwambia Mheshimiwa Mbunge kwamba wakati tunaleta hoja hii kwa ajili ya *ratification* tulipewa ushauri, kwamba kuna *treaties* nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna *Chemical Weapons Treaty;* kuna *Biological Weapon Treaty* kuna *Nuclear Weapon Treaty;* hizi zote ni *weapon of mass destruction*. Tukashauriwa kwamba ziwekwe kwa pamoja ili ziwe zina sheria moja. Ili ziweze kufanya hivyo, kwa hiyo, tumekubaliana kwamba zoezi hilo sasa lianze kwa haraka ili hatimaye tuweze kui-*ratify treaty* hii na tuweze kupitisha sheria ili tuweze ku- *domesticate* sheria zote hizi kwa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Masoud aliungana na Wabunge wengine kusema kwamba bajeti ya Wizara hii ni ndogo na tunakubaliana na hilo, lakini hiyo ndiyo hali ya uchumi wa nchi. Tuna uhakika kwamba kila uchumi ukikua na Wizara hii itaongezewa fedha kwa umuhimu wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *Ration Allowance* kwamba isiondolewe; tunasema kwamba *Ration Allowance* haijaondolewa; ipo na itaendelea kuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la fidia ya maeneo yaliyochukuliwa na Jeshi, nimeshalitolea taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ujenzi wa maghala kwamba hayajakamilika na yatakwisha lini? Niseme hapa kwamba maghala yako katika hatua nzuri sana, yaliyobaki ni mambo machache sana ya kuunganisha umeme hapa na pale na kadhalika, isipokuwa lile ghala la Pemba, ambapo kumetokea mgogoro na Mkandarasi. Sasa hivi utaratibu unafanywa wa kuuvunja mkataba ule ili apewe Mkandarasi mwingine mwenye uwezo alikamilishe lile ghala na silaha zetu ziweze kukaa sehemu salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya ulinzi wa Taifa nimeshalitolea taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu eneo la Hospitali za Jeshi kuwa katika mazingira ambayo hayaridhishi na kadhalika. Waheshimiwa Wabunge wengi wamechangia hili. Naweza kusema hapa kwamba tuko katika mchakato wa kuanzisha Bima ya Afya kwa Wanajeshi. Sisi tuna imani kubwa kwamba huo ndiyo utakuwa mwarobaini wa matatizo yote ya kiafya Jeshini. Tutapata fedha za kutosha kuboresha vituo vyetu, kuongeza dawa kuajiri Madaktari na kuwalipa hata wale Madaktari ambao wanakuja kufanya *part time. (Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naona muda wangu umekwisha, bado nina hoja nyingi sana ambazo sijajibu; lakini kama nilivyoahidi, tutazitoa kwa maandishi ili Waheshimiwa Wabunge wote wapate majibu ambayo tulikuwa tumeyaandaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Hoja imeungwa mkono. Katibu.

**NDG. ASIA P. MINJA – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 57 – Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa**

Kif. 1001 – *Admin. & HR Mgnt..................*Sh. 16,314,720,125/=

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nimepokea majina ya Vyama vyote. Tunaanza na Martha Mlata.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba kwanza nimshukuru Mheshimiwa Waziri, lakini nilitoa mchango wangu na kwa sababu ya muda, naamini alishindwa kujibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu Mheshimiwa Waziri anipatie ufafanuzi, nawe unatambua kwamba vijana wetu wanaofanya mtihani wa kidato cha nne, wanafanya mtihani mwezi wa Kumi lakini wanakaa miezi nane wakisubiri wale waliofaulu kwenda *form five* mwezi wa Saba. Kwa hiyo, ni kipindi kirefu sana vijana hawa wanakaa nyumbani na matokeo yake tunaweza wengine tukawapoteza njiani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa JKT wamefanya kazi kubwa sana, kwanza kwa wale wanaojitolea kwenda JKT *target* yao ilikuwa ni 10,000 lakini wamechukua 9,800. Wale wanaomaliza kidato cha sita, waliomaliza ni 65,000, lakini wakawachukua 14,000 na hawa ni sawa na wale ambao wanatakiwa kwenda kidato cha tano; kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri atusaidie kuweka ufafanuzi kwa sababu Sheria ya Mwaka 1964 inatambua mtoto wa miaka 16 kujinga na Jeshi la Kujenga Taifa. Je, isingekuwa ni sahihi, watoto hawa waweze kutumia muda huu kupata mafunzo ya Jeshi kwa maana ya JKT? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Mheshimiwa Mlata alileta hoja hiyo, kwa bahati mbaya sana sikupata muda wa kuifafanua, lakini ukweli ni kwamba Sheria ya Jeshi la Kujenga Taifa inataka vijana waliomaliza *form six* na vile vile wale waliomaliza *form four* lakini wakapata elimu ya ziada, sio *form four* peke yake, hiyo ni kwa mujibu wa Sheria. Kwa hiyo, ninachoweza kusema hapa ni kwamba hoja ya Mheshimiwa Martha ni nzuri kwa sababu ukiangalia sasa hivi

wanaomaliza *Form Six* mpaka kuanza Vyuo Vikuu muda ni mfupi mno, lakini wale wa *form four* wana muda mrefu zaidi. Kwa hiyo, tunachoweza kusema ni kwamba tutaliangalia kwa umakini kwa kushirikiana na wenzetu wa JKT lakini vilevile hata kama litaonekana linafaa litahitaji mabadiliko ya Sheria. Kwa hiyo,...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Matha.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na naunga mkono hoja kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Richard Mbogo.

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Langu ni fupi tu, nitahitaji kujua mkakati wa Serikali au mipango. Wakati Mheshimiwa Waziri anajumuisha, ameelezea migogoro mbalimbali ya maeneo na watu wanaopewa fidia, lakini tunajua kwamba maeneo ya Majeshi hasa maeneo ya Mijini yamezungukwa na raia kutokana na kuongezeka kwa idadi ya watu na kuwa karibu; na kumekuwa ni migogoro mpaka Majeshi yanakaa kwenye maeneo ya Manispaa, yaani Mijini. Sasa je, Serikali haioni haja ya kupunguza haya maeneo na ikabaki na huduma za kijamii kama vile upande wa afya, elimu na hata kuweza kupewa maeneo mengine?

Kwa mfano, Manispaa ya Mpanda waliweza kupunguza toka ekari 3,000 na kitu mpaka 1,000 na kitu. 1,100 zilienda Manispaa. Sasa je, Serikali haioni mpango wa kuondoka Mijini na kwenda sehemu nyingine kuondoa hatari kwa wananchi?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimjibu Mheshimiwa Mbogo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vema ikaeleweka kwamba Kambi za Jeshi zina madhumuni tofauti tofauti, siyo zote zenye kazi moja. Kuna kambi ambazo ni za kimapigano ambazo zinahitaji maeneo makubwa kwa sababu ya usalama wa wananchi. Kuna kambi nyingine ambazo ni za kiutawala; na kuna kambi nyingine ambazo ni za *logistics.* Kwa hiyo, kusema kwamba kambi zote ziondoke mjini, tutakwama katika upande wa *logistic*s na mambo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninachoweza kumwambia Mheshimiwa Mbogo ni kwamba tutaangalia *case by case,* hatuwezi kutoa maamuzi ya jumla ili kuona ni wapi ambapo hicho anachoshauri kinawezekana na wapi ambapo hakiwezekani?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Masoud.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nami naomba kupata maelezo ya ziada na kama sikuridhika, natoa shilingi mapema jioni ya leo. Kuna malalamiko ya muda mrefu; pamoja na maelezo ya Mheshimiwa Waziri kwamba wananchi wanachukuliwa maeneo yao, sasa ni karibu miaka 50; na maeneo haya Jeshi la Wananchi wa Tanzania ambayo wameyachukua kwa wananchi ni maeneo 262.

Mheshimiwa Mwenyekiti, waliyoyafanyia tathimini ambayo mpaka sasa hakuna fidia iliyotolewa ni maeneo 17. Sasa ndani ya miaka 50 ambapo Jeshi la Wananchi limechukua maeneo ya wananchi na wananchi wengine wameshafariki, wanaendelea kudai haki zao, Mheshimiwa Waziri anasema kwamba nia ya kulipa ipo; kama ingekuwa ni yeye binafsi Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi ningekubali, lakini siyo ni Serikali. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu mambo haya ni tangu mwaka 2006. Kuna kitabu kimeandikwa, "Taarifa ya Ahadi za Serikali," mimi nikiwa Waziri kivuli, tena kivuli cha saa 11.00 jioni, kitafika huko kivuli changu. Tangu mwaka 2006, sasa ni miaka 11, mnasema mtayatekeleza; maeneo mmeyataja; Bulombola, Mlale JKT, Turuti, maeneo ya Jeshi kibao, yote mmesema, lakini hamtoi fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara hii ya 2016/2017 shilingi bilioni 27.7 ambazo zimetengwa, hakuna hata shilingi moja. Mheshimiwa Waziri, aniambie sasa; ana lipi kubwa ambalo atafanya juu ya kukamilisha shughuli hizi?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema katika maelezo yangu, kwa kweli sina maelezo ya ziada. Fedha tulizotenga, shilingi bilioni 27.7, hili tatizo linajulikana, tumezungumza na wenzetu wa Hazina, wametuahidi kututafutia kiwango fulani cha kuweza kulipa katika bajeti ya mwaka huu; na vilevile katika bajeti ya mwakani, tumeweka fedha vilevile. Kwa hiyo tunachosema Mheshimiwa, maelezo zaidi ya hapo sitakuwanayo isipokuwa naomba mtuamini kwamba fedha hizi zitapatikana kwa awamu ili tuweze kuondoa hilo tatizo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Masoud.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na maelezo ya Mheshimiwa Waziri na amesema kwamba tuwaamini, lakini hii ni robo ya tatu ya mwaka tunamalizia; na kwa kuwa wananchi wengine wameshafariki na sisi ndio sauti zao, naomba Waheshimiwa Wabunge mniunge mkono tujadili kwa kina namna bora ya kuwapatia wananchi fedha hizi ambao wamelalamika muda mrefu, maeneo yao yamechukuliwa na mpaka sasa hakuna fidia iliyotolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba naomba kutoa hoja.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwigulu, Mheshimiwa Chegeni, Mheshimiwa Ashatu, *Chief Whip* utakuwa wa mwisho, Mheshimiwa Waitara, Mheshimiwa Matiko, Mheshimiwa Riziki, Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Halima.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa hamwezi kupata wote. Naandika tu, halafu nitakuwa nachagua hapa.

Haya, tunaanza na Mheshimiwa Matiko.

**MHE. ESTER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nimesimama kuunga hoja ya Mheshimiwa Masoud kuhusiana na maeneo ambayo Wanajeshi wameyachukua. Ni dhahiri kuwa ni takriban miaka yote tunaweka bajeti hapa, Serikali inashindwa kutoa hela. Kwa hiyo, kusema tumwamini Mheshimiwa Waziri inakuwa ni ngumu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba haya maeneo ya wananchi ambayo Wanajeshi wamechukua, kwa sababu mmeshindwa kuyalipa kwa sababu hamna hela, muwarudishie wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri leo nimekutana na wananchi wa Tarime; na kuna mmoja ni babu kabisa ana miaka karibia 80; huwezi ukajua wako pale juu. Wamemweleza na amesikia kilio chao. Kwa hiyo, naunga mkono hoja, maeneo yarudi kwa wananchi. Serikali haiwezi kulipa fidia kwa hawa wananchi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Kigwangala.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Napenda kumsihi Mheshimiwa Masoud asiichukue shilingi ya Mheshimiwa Waziri kwa hoja kwamba yeye kama Mbunge *senior* humu ndani atakuwa anafahamu changamoto ambazo Taifa letu linapitia katika kutekeleza bajeti yetu katika nyakati nyingi mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto hizi haziwezi kuwa mahsusi tu kwa Wizara hii ya Ulinzi, mambo mengi tunayapanga kama *aspiration* za nchi yetu sisi hapa Bungeni, tukiamini kwamba tutafanikiwa kukusanya pesa za kutosha kutatua changamoto zote ambazo zinatukabili; lakini hutokea mara chache, tukashindwa kufikia malengo na hii haiwezi kuwa ni sababu ya makusudi, ni sababu za kiuchumi na ziko nje ya uwezo wa binadamu.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Riziki.

**MHE. RIZIKI S. MNGWALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nami nisimame kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Masoud. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nia lazima ifuatiwe na vitendo. Nia tu, nia, hii nia mpaka lini? Miaka 50, mnasema wenyewe tunatenga shilingi bilioni 27, hata senti mbili haijapangwa; sasa nia hii itafika mwisho kweli! Hebu tufike mahali hii Serikali ione aibu kwa wananchi wake. Wananchi wanyonge walipwe pesa hizi, wanashikilia maeneo mengine wala hawana kazi nayo; Buza, sijui wapi, mengine yapo mjini kabisa, wanachukua tu maeneo ya watu, fidia hawalipi. Kwa kuwa wananchi ni wanyonge!

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa leo shilingi itaondoka. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Naunga mkono hoja ya Mheshimiwa

Masoud. Mheshimiwa Waziri anasema tangu mwanzo wa maelezo mpaka mwisho kwamba Serikali kwa sasa haitakuwa na uwezo wa kulipa watu hawa; na hawa ni Watanzania wenzetu ambao wanapata shida. Nadhani ingekuwa ni busara tu kuwaachia maeneo waendelee kujiendeleza kiuchumi; siku watakapopata fedha, wakati huo watazungumza kwa bei ya wakati huo ya soko la ardhi. Ni hivyo tu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mwigulu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niwakumbushe tu Waheshimiwa Wabunge kwamba Wizara tunayoongelea ni ya Jeshi la Wananchi. Mnaposema maeneo hayo yachukuliwe na wananchi; hili ni Jeshi la Wananchi na wananchi wanatakiwa mara zote watambue kwamba Jeshi la Wananchi liko kwa ajili ya wananchi. Kiusalama tu, hata wanapopata eneo, sisi kiraia mnaweza mkadhani halina kazi, lakini kiusalama na usalama wa wananchi wenyewe, ni vyema shughuli za kijeshi zinapoendelea zisiwe karibu sana na uraia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, Serikali inasema itayalipia yale maeneo. Kwa hiyo, linalotakiwa kufuatana na vipaumbele; na kwenye eneo hili nawaomba Waheshimiwa Wabunge, wala hatuna hata haja ya kuvutana kwa sababu ya uzito wa jambo tunaloliongelea. Hatuna haja hata ya kuvutana, tukubaliane tumpe fursa Mheshimiwa Waziri huku tukiwa tumeshaona *concerns* zenu kama Wabunge kwa sababu mnatimiza wajibu wenu wa kuielekeza Serikali.

Mheshimiwa Waziri ameshapokea, Serikali imepokea, atakwenda kulipa, lakini hatuna haja ya kuvutana kwa shilingi kwa ajili ya umuhimu wa Wizara tunayoijadili.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Chegeni.

**MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Masoud alikuwa Mjumbe

mwenzangu wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama. Tumezunguka naye katika baadhi ya maeneo na yaliyozungumzwa na Mheshimiwa Waziri nadhani ameona ni hoja ya msingi kabisa, kwa sababu Mheshimiwa Waziri ameonesha nia kama Waziri na Serikali iko tayari kujaribu kufanya fidia ya haya maeneo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri Mheshimiwa Masoud hoja yake, tulizunguka kwenye Kamati wakati ule, kwa nini asimwachie Mheshimiwa Waziri akafanye kazi na kauli ameshasema hapa sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ashatu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na napenda nimwombe tu Mheshimiwa Masoud kama alivyosema Mheshimiwa Waziri wa Wizara husika, kwamba nia ya Serikali ni njema, nasi tumejipanga kulipa fedha hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo naomba muichukue hivyo; na tulisema tangu mwanzo, tangu tumeanza kipindi hiki kwamba tulikumbana na changamoto ya kupanda kwa riba katika Soko la Dunia, lakini sasa imeshuka na sasa tuko sehemu nzuri, hizi ni pesa za maendeleo, zimepatikana na zitalipwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Masoud, nia ya Serikali yetu ni njema, na wananchi wote watalipwa, siyo ndani ya Wizara hii tu, Wizara zote ambazo tunatakiwa kulipa *compensation,* Serikali inatoa *commitment,* tutafanya malipo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Masoud amwachie Mheshimiwa Waziri shilingi yake ili tuweze kutekeleza bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri majibu yako ndiyo yale yale, huna tena la kuongezea. Au una la ziada ambalo umelipata sasa hivi?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba nashukuru *commitment* ya Serikali imepatikana na mimi mwenyewe nimewaahidi Waheshimiwa Wabunge wengi kwamba nitafika katika maeneo yao binafsi kuzungumza na wananchi wao ili nami kuweza kufikisha *commitment* hizi za Serikali kwa wananchi ili wanisikie moja kwa moja. Kwa hiyo, nitafanya hivyo baada ya kikao hiki cha Bunge. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Masoud, baada ya *commitment* ya Serikali, nafikiri ni ubinadamu tu ukubali tuwape muda na sasa hivi mambo yanakuwa mazuri na nia ya Serikali ni kulipa hizi pesa sababu ni wajibu wananchi hawa siku nyingi hawajalipwa. Kwa hiyo, *commitment* ya Waziri wa Fedha na Waziri mwenyewe...

Chief Whip nilikuwa sijakupa nafasi! Umeridhika!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, (SERA, BUNGE, AJIRA, VIJANA NA WALEMAVU):** Ndiyo.

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, nakusihi tu umrudishie pesa yake, tutashirikiana kuitafuta hiyo pesa pamoja ili wananchi walipwe hela zao.

Mheshimiwa Masoud.

**MHE. MASOUD A. SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sina pingamizi na maelezo yako, lakini mara nyingi Mawaziri wanapojibu, wanasema Serikali ya Awamu ya Tano haisemi uongo. Mimi nataka tu kusikia ni lini? Wanasema kwamba fedha inatafutwa na sasa tupo katika robo ya tatu ya mwaka; nataka mniambie tu, ni lini wananchi hawa; mniambie tu *time frame,* muda gani? Ni hiyo tu siyo kingine. Shilingi nitarudisha jioni hii sina pingamizi, sema ni lini? basi ni hilo tu.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Masoud, *commitment* imeishawekwa. Serikali ikitoa *commitment* ndiyo kauli ya Serikali. Nashukuru shilingi imerudi. *(Makofi)*

Tunaendelea. Mheshimiwa Lolesia Bukwimba *(Makofi)*

**MHE. LOLESIA J. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kutoa hoja. Sina nia ya kutoa shilingi kwa Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi, nimeulizia kwa habari ya wapiganaji wa Vita vya Kagera vya mwaka 1978/1979, ni kipindi kirefu sasa wapiganaji hawa wa vita wamekuwa wakifuatilia haki zao, mafao yao na wanahitaji kulipwa *pension.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipindi chote hicho Serikali imekuwa ikiwaahidi tu mara kwa mara lakini hakuna kinachoendelea. Vile vile katika Serikali ya Awamu ya Nne ya Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Serikali ilionesha matumaini kutaka kuwalipa mafao hawa wapiganaji wa Vita vya Kagera, lakini mpaka sasa utekelezaji bado haujaonekana.

Sasa ningependa kujua kwamba Serikali inasemaje kuhusu jambo hili? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu Mheshimiwa Bukwimba kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha anazozungumzia Mheshimiwa Mbunge ni vizuri awe amewaelewa wahusika wanazungumzia fedha gani? Kuna fedha ambazo zililipwa kama ahsante baada ya watu kurudi kutoka vitani na zililipwa kwa wote, hakuna anayedai fedha hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye suala la *pension; pension* wanapata wale ambao walikuwa ni waajiriwa wa Jeshi. Mtakumbuka wakati wa vita vile, kuna wengine walikuwa sio waajiriwa wa Jeshi. Kwa hiyo, hawa hawastahili *pension.* Sasa kama kuna ambao ni waajiriwa wa Jeshi, ambao hawana *pension,* napenda kumwambia Mheshimiwa Mbunge atuone ili tuangalie taratibu zao lakini wanastahili *pension* yao kama walikuwa ni waajiriwa wa Jeshi.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Lolesia, bado una hoja?

**MHE. LOLESIA J. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa Mheshimiwa Waziri kuonesha nia ya dhati kuweza kuwaona wale wahitaji kuweza kuwasikiliza. Kwa hiyo, nashukuru sana, nami binafsi nitawaomba wale watu waje kumwona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mathayo.

**MHE. DKT. VEDASTUS M. MANYINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Nami hoja yangu kubwa ilikuwa inahusiana na fidia ya wale wananchi walioko katika Kata ya Makoko ambapo Jeshi lilichukua nafasi yao. Sasa kama nilivyosema, bahati nzuri niliwaleta wakaonana na Mheshimiwa Waziri, naye akatoa *commitment,* lakini jambo moja kubwa ambalo limenipa faraja ni majibu ya Mheshimiwa Waziri, lakini na Serikali kwa ujumla kwa maana ya Waziri wa Fedha alivyosema kwamba ataleta fedha. Kwa hiyo, ni imani yangu kwamba hilo limeisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri.

**NDG. ASIA MINJA - KATIBU MEZANI:** Hajatoa hoja ameshukuru.

**MWENYEKITI:** Aah, wewe hukutoa hoja, siyo!

**MHE. DKT. DAVID M. DAVID:** Sikutoa hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwanza, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi. Hoja zangu zote za Upinzani amejibu ipasavyo, vizuri, hayo ndiyo niliyokuwa nataka. Ndiyo kazi ya Upinzani kuchokoza, unaleta majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili namshukuru sana Mkuu wa Majeshi kwa kuokoa maisha yangu, nimempa ng'ombe 25 kwa mke wangu kutoka Nyakabindi pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu, hoja yangu ni kuhusu wale Wateuzi wa Kisiasa; Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa ambao wanaendelea kuvaa Sare za Jeshi. Nahitaji kauli yako. Kama hakuna majibu mazuri, nakusudia kutoa shilingi ili tujadili kwa mapana yake. Kwa wale wateule ambao ni Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa ambao wameshatoka Jeshini, wanafanya kazi za Utumishi wa Umma, lakini wanaendelea kuvaa sare za Jeshi; naomba kauli yako, utaratibu ukoje Jeshini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati najibu hoja hapa, hili suala nililizungumzia, pengine Mheshimiwa Mbunge hakusikia. Nilisema hivi, Wanajeshi ambao wameshikizwa katika kazi za Kiserikali kwa maana ya Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa, bado wanaweza wakavaa *uniform* pale ambapo wanahitajika kufanya hivyo, kwa kibali cha Mkuu wa Majeshi. Sasa ukimwona *RC* au *DC* amevaa, amepata kibali cha Mkuu wa Majeshi kutokana na kazi ambayo anatakiwa kuifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, leo katika mipaka yetu kule kuna *operation* maalum ya kushughulikia labda wahamiaji haramu au wakimbizi au nani, huyu Kamanda anaamua kuvaa *uniform* ili awaongoze vijana wake kwenda kufanya kazi maalum kule. Sioni kama kuna tatizo, kwa sababu yuko katika majukumu yake ya kiulinzi. Hiyo ndiyo sababu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa kanuni na taratibu ni kwamba, kinachotakiwa ni kibali, asivae kwa maamuzi yake. Kama ameshapata kibali, nami najua kwamba Mkuu wa Majeshi alishatoa hicho kibali, kwa hiyo, hakuna tatizo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara, majibu haya ndiyo sahihi. Nafikiri Mheshimiwa Waziri amejibu vizuri sana, *professionally* kabisa. *(Makofi)*

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo kweli, kama ni kweli, sijaelewa vizuri. Kwa hiyo, naomba nitoe hoja Bunge lijadili na tupate maelezo sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**MHE. TUNDU A. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Sawa ni kwa mujibu wa Kanuni wala hata hamna taabu, lakini nami nina kitabu changu cha Kanuni hapa.

Mheshimiwa Mwigulu, Mheshimiwa Almas, Mheshimiwa Mayenga, Mheshimiwa Martha bado upo? Mheshimiwa Bilago, Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla, Mheshimiwa Frank, Mheshimiwa Marwa, Mheshimiwa Albeto, Mheshimiwa Haonga, Mheshimiwa Bashe; bado mko wengine? Haya tunaanza na Mheshimiwa Albeto.

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Leo nimepata *conflicting messages* kutoka kwa Serikali hasa wakati wa kuleta bajeti asubuhi. Kwa maana ya kwamba mimi nilifikiri nchi hii Wanajeshi lazima wakae mbali katika mambo ya kiutawala, lakini taarifa niliyopata hivi asubuhi ni kwamba hata hivi jioni tumesikia kwamba hata kuna makubaliano baina ya Serikali na Wanajeshi namna ya kuwachukua kuingia katika Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ina-*send very wrong message.* Tunaona nchi nyingine, watu waliokuwa Wanajeshi, baada ya kutoka kwenye Jeshi hakuna suala la kuvaa *uniform* kwa sababu ni vitu viwili vinavyotengana. Hatukatai nafasi yake kama Mwanajeshi, hatukatai nafasi yake, anaweza akaongoza kikosi lakini ina-*send wrong message* kwa maana kwamba kumbe Jeshi bado linahusika katika siasa. Hili ndilo tunaona kwamba halifai, litenganishwe kabisa Jeshi na siasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Albeto, mimi sio Waziri, lakini kwenye masuala mengine nyeti ya Serikali kunakuwa na *joint forces* zinaunganishwa. Ukienda Marekani utakuta Mkuu wa Majeshi **Admiro** anakuwa ni *National Security Adviser* anakuwa *incharge* wa *CIA,* anafanya uraiani lakini bado ni Mwanajeshi. Kwa hiyo, kuna vitu kwenye Serikali ili kulinda maslahi, lazima kuwe na uwiano fulani wa Kiserikali ikiamua…

*(Hapa Mheshimiwa Ally Saleh Ally alisimama)*

**MWENYEKITI:** Kaa tu, wala sikupi tena nafasi ya kusema kwa sababu muda wako umekwisha.

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Kwa sababu Waziri wa Nchi, ndio mtu wa kujibu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa kaa. Mimi ndio Mwenyekiti. Mwenyekiti anatakiwa ajue kila kitu, kaa.

Kwa hiyo hivi ni vitu vya kawaida tu. Mheshimiwa Waziri atakujibu lakini *these are normal positions* ambapo Serikali inaweza kumteua mtu wa Jeshi kufanya kazi kwenye maeneo maalum.

Baada ya maneno hayo, tunaingia kwenye *guillotine. (Makofi/Kicheko)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa uliotuteua inakuwaje?

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, huo ubabe bwana!

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa sikilizeni vifungu. Sikilizeni vifungu.

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MBUNGE FULANI:** Tunasikiliza!

**MWENYEKITI:** Katibu Soma.

**NDG. ASIA MINJA - KATIBU MEZANI:** Hawasikii, wanapiga kelele.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo umetumia Kanuni gani? Tuambie Kanuni uliyotumia.

**NDG. ASIA MINJA - KATIBU MEZANI:** Narudia Fungu 57 - Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, fedha iliyoombwa shilingi bilioni mia tisa na...

**MBUNGE FULANI:** Kuhusu utaratibu.

**MWENYEKITI:** Kaa chini.

**Fungu 57 – Wizara ya Ulinzi naJeshi la Kujenga Taifa**

Kif. 1001 – *Administration and HR Mgt*....Sh. 16,314,720,125/=
Kif. 1002 – *Finance and Accounts* ... ... ... .Sh. 265,096,300/=
Kif. 1003 – *Policy and Planning* ... ... ... ... .Sh. 405,580,000/=
Kif. 1004 – *Internal audit Unit*.. ... ... ... ... ..Sh. 154,878,000/=
Kif. 1005 – *Procurement Mgt Unit*..... ... ... Sh. 55,273,200/=
Kif. 1006 – *Legal Services Unit*.. ... ... ... ... ..Sh. 46,137,200/=
Kif. 1007 – *Govern't Comm. Unit*..... ... ... ..Sh. 49,300,000/=
Kif. 1009 – *Independent Tel. Network*. ... ... .Sh. 54,164,000/=
Kif. 2001 – *Industries, Construction& Agriculture* ........... ... ... ... ... Sh. 280,585,000/=
Kif. 2002 – *Military Research &Dev.* ... ... ... Sh. 177,362,754/=
Kif. 2003 – *Building Consulting Unit* ... ... .....Sh. 41,260,000/=
Kif. 2004 – *Estate MGT and Dev. Unit* ... ... ..Sh. 66,640,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 38 – Ngome**

Kif. 1001 – *Defence Forces Headquarters' Command*... ... ... ... ... Sh. 1,199,446,006,118/=
Kif. 1007 – *Land Forces Command* ... ... Sh. 2,087,265,726/=
Kif. 1008 – *Air Defence Command* ... ... Sh. 1,850,195,124/=
Kif. 1009 – *Navy Command*... ... ... ... ... .Sh. 815,295,195/=
Kif. 1010 – *Military Hospitals*... ... ... ... ...Sh. 1,045,527,400/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 39 – Jeshi la Kujenga Taifa**

Kif. 1001 – *The National Service Force*.. Sh. 283,362,530,783/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 38 – Ngome**

Kif. 1001 – *Defence Forces Headquarters' Command* ... ... ... ... ... .... Sh. 8,000,000,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

**Fungu 39 – Jeshi la Kujenga Taifa**

Kif. 1001 – *The National Service Force*... ..Sh. 6,000,000,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 57 – Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa**

Kif. 1003 – *Policy and Planning* .. ... ... ....... Sh. 400,000,000/=
Kif. 1009 – *Indep. Telecom. Network*.......Sh. 15,418,000,000/=
Kif. 2001 – *Industries Construction and Agriculture* ...........................Sh. 21,300,000,000/=
Kif. 2002 – *Military Research and Dev*... Sh. 147,593,180,000/=
Kif. 2003 – *Building Consulting Unit* . ... ... ...Sh. 250,000,000/=
Kif. 2004 – *Estate Mgt Dev. Unit* ..............Sh. 20,038,820,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. ASIA MINJA - KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa taarifa Kamati imemaliza kazi zake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Tukae, Mtoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa taarifa kwamba Bunge lako limekaa kama Kamati ya Matumizi na limekamilisha kazi zake. Naomba Taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Hoja imeungwa mkono, sasa nitawahoji.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2017/2018 – Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa yalipitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *Chief Whip*.

**MWONGOZO WA SPIKA**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nasimama kwa kanuni ya 68 (7) nikiomba mwongozo kuhusu jambo ambalo limetokea Bungeni mapema; na jambo hili kwa kweli limetokea mapema leo na limeendelea kuchukua nafasi mpaka tunapomaliza kuhitimisha hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja iliyotolewa leo hapa Bungeni ilikuwa inahusu Wizara ya Ulinzi na kwa mujibu wa kanuni, hoja hii ilipaswa kutolewa hotuba ya Mheshimiwa Waziri, Mwenyekiti wa Kamati inayohusika lakini na Msemaji wa Kambi ya Upinzani Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo ninaotaka kuuomba kutoka katika kiti chako ni kuhusu utaratibu wa

kikanuni ambao pia unaendana na kanuni ya 64(1)(a) ambayo inakataza Wabunge kusema uongo ndani ya Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kanuni hiyo pia inamtaka mtu ambaye anataka kuthibitisha uongo wowote unaosemwa Bungeni arudi kwenye kanuni ya 63 na kuthibitisha kwamba maneno ambayo ama Mbunge ama mtu yeyote atakayezungumza ndani Bunge anabakia katika kusema ukweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeshukuru sana Msemaji wa Kambi ya Upinzani wakati anaingia kwenye mafungu ya sera amesema kabisa hapa kwamba anamshukuru Mheshimiwa Waziri amejibu yale aliyoyachokoza kuyasema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Msemaji wa Kambi ya Upinzani alipokuwa anazungumzia eneo la fedha ya chakula, alitaka kuwathibitishia Watanzania kitu ambacho hakikuwa halisia na siyo cha ukweli. Alipokuwa anazungumza eneo la fedha za likizo kwa ajili ya wapiganaji wetu, alitaka kuwathibitishia Watanzania kupitia Bunge lako kwamba eneo hilo halikuwa likisimamiwa vizuri, lakini taarifa yake haikuwa na ukweli. Eneo la muda wa kazi za ziada katika Jeshi letu la Ulinzi wa Tanzania vivyo hivyo, eneo la manunuzi vivyo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, Mheshimiwa Waziri wakati anahitimisha hoja hii ametoa ufafanuzi na amesema ukweli wa mambo hayo jambo ambalo kanuni zetu zinatupasa, unapotaka ku-*prove* aliyesema kitu fulani amesema uongo ni lazima wewe useme ukweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi ameeleza ukweli wa maeneo hayo yote na kuonesha kwamba yale yaliyoandikwa kwenye hotuba ya Kambi ya Upinzani hayakuwa maneno ya kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba mwongozo wako, katika hali ya namna hii, hotuba hii ya Kambi ya Upinzani imeshatolewa na ni *public document* ambayo

inaweza ikasomwa na mtu yeyote, lakini ina maneno haya ambayo siyo ya ukweli. Kwa nini kiti chako kisimtake aliyeyasoma maneno haya Bungeni ayafute maeneo haya kwamba siyo maneno ya kweli na ikiwezekana awaombe radhi wapiganaji wetu kwa kusema maneno ambayo hayana ukweli, ambayo yalikuwa yanataka kuchonganisha Serikali, Jeshi na Watanzania, ama ayafute maneno hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hatayafuta, utupe mwongozo, kanuni zetu zinasema nini ili tuweze kujifunza nidhamu ndani ya Bunge ya kuandika na kusema maneno yenye ukweli ndani ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara, ni kweli mwongozo unaoombwa uko sahihi na nilitoa tahadhari wakati unasoma. Kwa hiyo, yako maneno na hasa Wizara hii, siyo jambo jema kuzungumza vitu ambavyo havina uthibitisho au vitu vya kuokotea tu mitaani.

Licha ya *sensitivity* ya Wizara yenyewe, kanuni zetu hizi haziruhusu hata kama kuna Wizara nyingine, hairuhusiwi kuzungumza vitu ambavyo siyo vya ukweli. Sasa kanuni zetu ziko *very clear, either* usimame ufute maneno uliyoyasema au kiti kikupe muda uende uthibitishe haya maneno unayoyasema. Vitu viwili tu; simama ufute maneno yako; na wahusika wenyewe wako hapa na kama unafikiri unao uthibitisho, nikupe muda wa siku mbili; Ijumaa ulete uthibitisho, kwa sababu limewagusa watu wengi sana na hasa limewagusa viongozi wenyewe wa Jeshi, kidogo wamepata shida. Kwa hiyo ni vitu viwili; futa maneno yako uliyoyasema au nikupe muda ukathibitishe. *(Makofi)*

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwanza Wanajeshi unaowasemea kwamba wamekwazika, labda kama wamekuandikia. Ninachosema, haya maneno, hii *document* ilienda kwa Ofisi ya Spika na

imesomwa hapa Bungeni. *From time to time* wakati wanasoma hatua kwa hatua, kulikuwa na mwongozo na maneno yote yaliondolewa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara...

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Waziri alipokuwa anazungumza hapa, kuna vitu amekiri kwamba vilikuwa havijalipwa. Sasa unasema nifute maneno yapi? Labda awe *specific* na neno lipi ambalo limesemwa, kwa sababu maneno yote tumeongozwa hapa, yamefutwa wakati wa mjadala.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara, ni *very simple.* Nanyi mnaompigia makofi mtamwacha peke yake hapa. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Waitara, *very simple!* Futa maneno yako, twende tukapumzike, ni hilo tu basi. Futa maneno; ni maneno machache tu; futa maneno yako uliyoyasema tuondoke.

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachosema, ni maneno yapi? Kwa sababu maneno mengine yamefutwa na Spika na mengine yamefutwa hapa. Muwe *specific* maneno yapi natakiwa nifute hapa? Ndiyo hoja yangu. Au basi nikupe nafasi wewe ambayo unaona hayafai, uyaondoe kwenye *Hansard*. Wewe unifutie kwa niaba yangu, kwa sababu siyajui ni yapi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa hebu msomee maneno yake.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namheshimu sana Mheshimiwa Waitara. Mheshimiwa Waitara ni Mbunge mahiri, mwakilishi mzuri wa wananchi wake, lakini ninachotaka kusema, niko *very specific* na nimesema hapa *very specific*.

Mheshimiwa Waitara eneo lililokuwa linazungumza kuhusu…

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mwenyekiti taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Frank, hebu kaa. Mheshimiwa Frank hebu kaa; usitake nikupe maneno mengine, kaa.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mwenyekiti kila wakati unatupa maelezo hapa ...

**MWENYEKITI:** Wewe kaa chini! Wewe kaa chini!

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Kuthibitisha anatakiwa athibitishe…

**MWENYEKITI:** Wewe kaa chini! Ukisimama tena, nitakuchukulia hatua. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wala sitaki kurudi kwa Mheshimiwa Mbunge aliyekaa, tumeshathibitisha haya yote ambayo ninayasema hapa. Eneo linalohusu manunuzi, eneo la fedha za chakula, eneo la fedha za likizo, eneo la muda wa saa za ziada; yaliyosemwa Mheshimiwa Waitara uyaondoe kwa sababu Mheshimiwa Waziri ameshatoa ufafanuzi na kutoa ukweli wa maeneo hayo. *(Makofi)*

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nawashukuru sana, mimi sina ugomvi na Jeshi la Wananchi kwanza. Nasi unajua ndio wenye Jeshi, linaitwa JWTZ, yaani Jeshi la Wakurya Tanzania. Nimesema Mheshimiwa Mabeyo ni shemeji yangu. Kwa hiyo, mimi nasema yale maelezo ya Mheshimiwa Waziri yasimame, yangu yaondolewe. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara, sema nafuta maneno yangu. Sema nafuta maneno yangu tumalizane. Hayo yote yafute, utabaki peke yako humu! Haya basi toa.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naweza nikabaki peke yangu, natosha sana, lakini kwa sababu nakuheshimu Mbunge mwenzangu kule Ilala jirani yangu na Mwenyekiti wa Kamati hii, naomba kwa heshima kubwa nifute maneno hayo, tuko pamoja na nyie. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Kwanza nakushukuru Mheshimiwa Waziri, umefanya kazi nzuri sana, uko peke yako, lakini umeweza kujibu maneno yote na umeyajibu kwa ufasaha. *(Makofi)*

Nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia, ndiyo uzuri wa Bunge hili, kanuni ni kanuni. Nimeingia kwa *guillotine* si kwa mapenzi ya mke wangu, ni kwa kanuni. *(Makofi)*

Kanuni zinanipa fursa mimi kuamua muda gani niahirishe Bunge kwa mujibu wa kanuni. Kwa hiyo, kanuni inasema, "Mwenyekiti anaweza." Nimekuona Mheshimiwa Bilago unapiga makelele, unataka nikufundishe tu. Soma kanuni ya 104 utanielewa.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya maneno hayo machache, naahirisha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 1.48 Usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumatano, Tarehe 17 Mei, 2017 Saa Tatu Asubuhi)*